3 FEBRUARI, 2015

BUNGE LA TANZANIA

_____

MAJADILIANO YA BUNGE

_____

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Saba - Tarehe 3 Februari, 2015

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

SPIKA: Hati za kuwasilisha mezani, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama au kwa niaba yake Mheshimiwa Capt. John Chiligati.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):

Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama Katika Kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015.

MHE. SELEMANI S. JAFO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):

Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA):

Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara Katika Kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumeletewa taarifa kwamba kwa sababu mgeni tulionao ndani ya nchi hii Rais wa Ujerumani vipindi vya *TBC* asubuhi hii vitakuwa kwenye *TBC 2* na siyo *TBC1,* kwa sababu kule kuna mapokezi huko uwanja wa Taifa kule.

Kwa hiyo, tutarudia tena baada ya mapokezi hayo kumalizika. Lakini pia jioni kwa sababu kutakuwa na dhifa ya kitaifa, pia matangazo hayatakuwa kwenye *TBC1* na siyo vinginevyo. Kwa hiyo, hayo ni maelezo wazi sana.

Maswali Waheshimiwa Wabunge tunaingia Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe anauliza swali hilo, kwa niaba yake Mheshimiwa Grace Kiwelu.

Na. 68

Ahadi ya Ujenzi wa Daraja la Mnepo Kijiji cha Mijongweni

MHE. GRACE S. KIWELU (K.n.y. MHE. FREEMAN A. MBOWE) aliuliza:-

Daraja la mnepo lililopo kijiji cha Mijongweni Kata ya Machame Weruweru, Wilayani Hai limekuwa kero ya muda mrefu inayohatarisha maisha na hata kufifisha uchumi na wananchi wa kata hiyo. Kwa zaidi ya miaka ishirini (20) Serikali imekuwa ikitoa ahadi mbalimbali za ujenzi wa daraja la kudumu bila utekelezaji:-

(a) Je, kwa mara nyingine tena, Serikali inatoa jibu gani la utatuzi wa tatizo hilo?

(b) Je, ni sababu gani zinazosababisha jambo hili lisitekelezwe kwa vitendo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, Mbunge wa Hai, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Halmashauri ya Wilaya Hai imeidhinishiwa shilingi bilioni 1,026,433,120.50 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali za barabara, kati ya fedha hizo shilingi milioni 353 ni kwa ajili ya utekelezaji wa ahadi ya ujenzi wa daraja la Mnepo katika kijiji cha Mijongweni.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Halmashauri ya Wilaya ya Hai ilishapelekewa shilingi milioni 266,959,192 ambapo shilingi milioni 210 zimeshatumika kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo.

Kazi ya ujenzi wa nguzo za daraja umekamilika na ujenzi wa sehemu ya juu yaani deki unaendelea. Ujenzi wa daraja umefikia asilimia 65 na kazi inategemewa kukamilika mwisho mwa mwezi Machi, 2015.

(b) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ahadi za Serikali umekuwa ukifanyika kwa awamu katika maeneo mbalimbali nchini kwa kuzingatia upatikanaji wa rasilimali fedha. Hivyo hakuna sababu za makusudi za Serikali kuchelewa kutekeleza ahadi hiyo. Azma ya Serikali ni kuhakikisha hadi zote zinazotekelezwa ili kuimarisha huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spik, Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa jimbo la Hai kuwa daraja hilo linajengwa na kukamilika ili kuondoa kero ya usafiri mahali hapo.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza nishukuru kwa niaba ya Halmashauri yetu ya Hai kwa kupokea fedha hizo lakini ningependa kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri amesema fedha zimeweza kukamilisha ujenzi wa daraja kwa asilimia 65 fedha zilizobaki zinaweza kukamilisha asilimia 35 iliyobaki?

Kwa kukizingatia tunakwenda kipindi cha mvua ambapo daraja hilo limekuwa likisababisha vifo kwa wananchi wetu wa jimbo la Hai? Nashukuru sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru ameshukuru kwa jitihada hizo ambazo zimefanyika mimi hili eneo labda ni *declare interest* Siha ile inatokana na Hai kwa hiyo, mimi nalifahamu hilo daraja linalozungumzwa na nimekwenda kule, nimeliona nafahamu kinachozungumzwa hapa. Wakati tunaanza kujenga daraja hili tuliona hilo tatizo ambalo Mheshimiwa Grace Kiwelu analizungumzia. Kwa hiyo, kazi ya kwanza inayofanyika pale ni kuhakikisha kwamba tunaanza kujenga kutoka kule chini ili kuanza kuja kutengeneza sasa hii *runway* ambapo ndipo magari yatakapopita pale.

Kwa hiyo, tatizo la kwamba mvua zitakuja zitatukuta huko tumeshapita *look at my eyes and look at my lips* nenda kaangalie kule utakuta hilo jambo linafanyika pale.

Lakini kiasi cha pesa ambacho kimebaki ni shilingi milioni 147 ambazo nataka nimthibitishie Mheshimiwa kwamba kufikia mwezi Machi tena mwezi Machi nimekwenda mbali tu najaribu kuwa mwangalifu maana yake najua watakuja kunikandamizia hapo chini.

Lakini nataka nimthibitishie kwamba kazi hii inafanyika nimezungumza mimi hapa na *engineer* wa wilaya Bwana Kweka, asubuhi hii nikamwambia una hakika mkandarasi yuko kwenye *site* na amenithibishia kwamba kazi hii inaendelea. Uwe na amani moyoni mwako na Mheshimiwa Mbowe mwambie *home boy* wangu asiwe na wasiwasi, kazi inaendelea. *(Makofi)*

SPIKA: Haya macho na lips hatuzionagi, Mheshimiwa Cynthia Ngoye swali linalofuata.

Na. 69

Uchafu Kwenye Miji Nchini

MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE aliuliza:-

Miji mingi hapa nchini ni michafu sana yakiwemo maeneo ya mitaa, Taasisi za Umma na za binafsi:-

(a) Je, ni hatua zipi za muda mfupi na za muda mrefu zimewekwa ili kuhakikisha miji yetu ina usafi endelevu?

(b) Je, ni utaratibu gani umewekwa na TAMISEMI kuhakikisha utekelezaji wa sheria, kanuni na maagizo yanayohusu uhifadhi wa mazingira yanatekelezwa kwa ukamilifu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la usafi wa miji hapa nchini linasimamiwa na sheria mbalimbali zikiwemo sheria za mazingira ya mwaka 2004, sheria ya afya ya jamii ya mwaka 2009 pamoja na sheria ndogo za Halmashauri. Serikali inazingatia sheria hii katika kuhakikisha miji inakuwa safi ili kutunza mazingira na kuepuka magonjwa yanayosababishwa na uchafu. Usimamizi wa sheria kutoka kwa wadau mbalimbali zikiwemo mamlaka za Serikali za Mitaa umekuwa siyo wa kuridhisha hali ambayo imesababisha baadhi kuwa na uchafu uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na usimamizi usioridhisha wa sheria changamoto nyingine ni uhaba wa vifaa vya kufanyia usafi pamoja na baadhi ya wananchi kutothamini vifaa vya kufanyia usafi pamoja na baadhi ya wananchi kutothamini usafi wa mazingira kama sehemu ya maisha yao. Kwa kuzingatia hali hiyo Halmashauri zimekuwa zikitenga Bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufanyia usafiri.

Mfano jiji la Mbeya, limenunua vifaa vya kuhifadhia na kusafirishia taka zinaitwa *skip containers*, magari manne ya kubeba makasha ya taka *skip loaders trucks*, makasha 83 ya kuhifadhia taka, mitambo miwili ya kuhudumia *dampo* la kisasa nak ukamilisha ujenzi wa *dampo* la kisasa yaani *Sanitary landfill.*

Kazi zote hizi zimegharimu jumla ya shilingi bilioni 3.8. Aidha, Halmashauri kupitia sheria ndogo zimeweka adhabu kwa yoyote atakayesababisha uchafu ambayo ni kati ya shilingi 10,000 hadi shilingi 50,000 kama inavyofanyika katika Jiji la Mbeya. Manispaa ya Moshi na Jiji la Dar es Salaam. Hatua nyingine zinazochukuliwa ni kushirikisha Kamati za Maendeleo za Kata na Mitaa, vikundi vya kijamii na makampuni binafsi kushiriki moja kwa moja katika kupanga na kusimamia suala la usafi wa maeneo yao.

ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imekuwa ikikumbusha Halmashauri na Mikoa kupitia vikao pamoja na kuhakikisha usimamizi wa Sheria na Kanuni za usafi unaimarishwa ili kufanya miji yake iweze kuwa safi.

Vilevile ofisi imekuwa ikifanya ufuatiliaji na kuchukua hatua kwa watendaji wanaoshindwa kusimamia usafi kwenye maeneo yao. Hivi sasa Serikali imeanzisha Idara ya Usafi na Mazingira katika Halmashauri kwa lengo la kuimarisha huduma ya usafi na usafishaji wa miji nchini.

Utaratibu mwingine unaotumika ni kushindanisha Majiji, Manispaa, Miji na Halmashauri za Wilaya kila mwaka ili kutoa motisha kwa Halmashauri zinazofanya vizuri. Serikali itaendelea kusimamia Halmashauri kupitia mikoa ili kuhakikisha kazi ya usafi inatekelezwa kikamilifu. *(Makofi)*

MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nimshukuru kwa majibu yake mazuri na fasaha. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ni kweli kwamba Serikali imekuwa ikiratibu masuala ya Usafi wa Mazingira katika Halmashauri za Wilaya na katika Miji na Majiji.

Je, Waziri anaweza kutuambia hapa Bungeni ameweka mtu maalum katika ofisi yake au dirisha maalum ambaye anashughulikia kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sheria Kanuni na Taratibu katika mikoa, wilaya na maeneo mengine hapa nchini?

Swali la pili ni kwamba Halmashauri ya Jiji la Mbeya, imejitahidi kununua vifaa vingi sana kwa ajili ya usafi wa mazingira, lakini ukipita katika maeneo mengi ni machafu pamoja na vifaa hivyo.

Je Waziri anaweza kutuambia anaweza kuiangalia Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuiongezea fedha za kutosha ili kutekeleza Sheria na Utaratibu wote wa uzoaji wa taka pamoja na kwamba wana vifaa hivyo? Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi, maana yake haya maswali yatakutia majaribu bure uanze… *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, pale utaratibu tulionao sisi tuna mtu anaitwa *Director of Local Government* huyo kwanza ambaye anashughulika na masuala haya yote tunayozungumza hapa.

Pili, kuna Director anayehusika na uendelezaji wa Miji yuko hapa ambaye pia anahusika na mambo haya. Kama namwelewa vizuri Mheshimiwa Mbunge anachozungumza hapa kwamba kuna mtu huyo ndiyo watu ambao tumewaweka pale ndiyo wana *link* na sekretarieti za Mikoa, ndiyo wana *link* moja kwa moja na Halmashauri zetu kule kwa maana ya kuratibu na kusimamia haya yote na kuhakikisha kwamba tunaunganisha na ofisi nyingine.

Kwa mfano ofisi ya Makamu wa Rais ambayo inashughulikia jambo hili na zile ofisi zingine *NEMC* na watu wengine wote wale hivyo ndivyo tunavyofanya.

Huo ndiyo utaratibu tunao na tutaangalia vizuri zaidi kama sasa tumefika mahali tunafikiri kwamba kuna haja ya kusema kabisa uwe na mtu mmoja ambaye kazi yake akiamka usiku asubuhi yeye ni Mazingira tu. *Well* mimi nieleze utaratibu ulioko na ni wazo zuri Mheshimiwa Mbunge natambua kwamba huyu alikuwa Mwenyekiti wa *NEMC*. Kwa hiyo, hainipi tabu kwamba ana uzoefu mkubwa katika suala hili analolizungumzia. *(Makofi)*

Sasa hili la pili analozungumza la Bajeti hapa nimeeleza hapa Mbeya ni Jiji lile limetumia 3.8 bilioni na ni kweli kama unavyosema nisije nikaingia majaribuni hapa. Bajeti ni mpango wa Serikali unaokuonyesha hela zitakapopatikana na namna zitakavyotumika.

Sasa Bajeti imeshapita mimi nitakwenda kuzungumza na watu wa Mbeya tuangalie tena kama kuna chochote kilichobaki huko ili tuweze kusaidia na kuweza kusaidia katika hilo eneo ambalo analizungumza.

MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Jiji la Dar es Salaam linaongoza kwa uchafu na vitongoji vyake. Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Jiji lile linakuwa safi na kwa kuzingatia sheria hizo hizo alizotaja Mheshimiwa Naibu Waziri?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Obama, kama sikusikia jina lake vizuri utanisamehe.

SPIKA: Abama siyo Obama, yeye ni Abama sasa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Habama Mrisho**.**

SPIKA: Jamani, Abama!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Basi hivyo kama alivyosema Spika. Niseme kwa kifupi hapa nazungumzia habari ya Jiji la Dar es Salaam, Waheshimiwa Wabunge na wale wengine mnakusudia kusimama kwanza kuna mradi ambao tumeuweka katika *Strategic Cities*.

Of course Dar es Salaam haikuwemo humu ukienda Arusha, Kigoma, Mtwara utaona tunavyofanya na tumeanzisha madampo mle ndani. Lakini awamu ya pili inayokuja tumeweka Halmashauri za miji 18 mle ndani ambayo pia hii Dar es Salaam haipo. Lakini kuna mradi namwona Mheshimiwa Rajab ananiangalia. Kuna mradi ule wa Dar es Salaam *Metropolitan Development Project,*

ambao jumla ya shilingi bilioni 500 zimetengwa kwa ajili ya hilo eneo. Huo mradi sasa hivi unafanyiwa maandalizi. Niko kwenye hatua sasa ya kujibu swali hilo. Hiyo ndiyo *program* ambayo tunayo, ndiyo ambayo tunategemea kwamba itatuondolea matatizo yote ambayo yanajitokeza katika Jiji la Dar es Salaam.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Moja ya tatizo ambalo liko katika mkoa wa Dar es Salaam ni kutumia *dampo* moja tu la Kinyerezi ambalo linamilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Waziri taka si uchafu, taka ni mali nilitaka kupata kauli ya Serikali. Je, ni kwanini katika Jiji la Dar es Salaam, kila Manispaa haijitegemei kwa ajili ya kutupa taka katika *dampo* lake?

SPIKA: Kama taka ni mali sasa tena watupe za nini, Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbarouk ambaye ni Mwenyekiti wa *Local Authority Accounts Committee,* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili jambo analoliuliza hili najua kwamba ni jambo tumelizungumza katika Kamati. Majukumu haya yakushughulikia taka yamewekwa katika Jiji lakini hayakuondoa kazi ile ya Manispaa kwa maana llala, Temeke pamoja na Kinondoni kushughulikia masuala haya.

Zile sheria nilizosema hapo anashughulikia, lakini *at the end of the day dampo* lenyewe kwanza liko chini ya Jiji na vile vifaa vinavyochukua zile takataka zile zote ziko pale.

Mheshimiwa Spika, nadhani kama ninakuelewa vizuri Mheshimiwa Mbarouk unachosema hapa ni kwamba kwa nini msifanye. Sasa kwa maana ya Dar es salaam kuna suala la uratibu pale na namna ya kuangalia jinsi ya kuzichukua zile taka na nini ambazo unasema ni mali na kuweza kupeleka pale.

For the time being utaratibu ni huo na nina uhakika unaufahamu. Hata hivyo, sisi tunachukua mawazo haya kuweza kuona kama Kinondoni wenyewe wanaweza wakakaa wakasomba takataka wenyewe wakashughulika wenyewe?

Je, Ilala na Temeke tutafanya hivyo.Tutakwenda kuangalia tutafanya *study* kidogo tuweze kuona, lakini kwa sasa hivi utaratibu ni huo niliouleza. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante, tuendelee na Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Desderius John Mipata, atauliza swali hilo.

Na. 70

Uwiano wa Maendeleo Nchini

MHE. DESDERIUS JOHN MIPATA aliuliza:-

Pamekuwepo na tofauti za kimaendeleo katika maeneo mbalimbali hapa nchini kiasi kwamba jambo hili lisipodhibitiwa linaweza kuwa tishio la kutoweka kwa utengamano, amani na utulivu ulioko nchini hivi sasa.

Je, Serikali ina mpango wowote mahsusi wa kuweka uwiano wa Maendeleo nchini?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tofauti za kimaendeleo katika sehemu mbalimbali nchini zina asili ya historia pamoja na uwepo wa kutokuwepo kwa rasimali asili na uwekezaji katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kihistoria ya maeneo yaliyokaliwa na kupendelewa zaidi kwa wingi wa watawala wa kikoloni ni kwa sababu ya hali ya hewa waliyoipendelea hasa sehemu za miinuko na zenye baridi.

Kwa mfano, Nyanda za Juu Kusini, Kaskazini zilikuwa na hali ya hewa waliyopendelea wakoloni na siyo Tanzania tu bali hata nchi nyingine kama Kenya na Zimbabwe. Maeneo hayo yalikuwa kati ya sehemu za kwanza kuanzishiwa shule na uendelezaji wa shughuli za kiuchumi tofauti na maeneo mengine ambayo hayakuwa na hali ya hewa kama hizi.

Mheshimiwa spika, hatua zilizochukuliwa baada ya uhuru ilikuwa ni kuendeleza elimu katika maeneo yote nchini na kusambaza huduma za afya, kujenga miundombinu ya barabara na mawasiliano, kusambaza umeme na maji mjini na vijijini, kuweka vitega uchumi mbalimbali kulingana na rasilimali asili zilizopo eneo husika na kutumia fursa za kijografia.

Hatua zote hizo zimetekelezwa kupitia mikakati na *program* mbali mbali ikiwemo Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano kama huu unaokaribia kumalizika, MKUKUTA, TASAF, MMEM, MMES na *REA*. *(Makofi)*

MHE. DESDERIUS JOHN MIPATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa katika kujibu swali Serikali imekubali kuwepo kwa tofauti katika maeneo mbalimbali ya nchi na inafanya juhudi za kusambaza huduma mbalimbali katika kuondoa changamoto hiyo. Nataka kujua ni juhudi gani au ni kwa kiasi gani wanafanya ili kusogeza maeneo ambayo yamebainishwa yako chini zaidi ili kuyasogeza juu zaidi kuliko maeneo mengine.

Swali la pili, kwa kuwa kupitia *sensa* tumeona kwamba mgawanyo wa huduma mbalimbali umekuwa ukifanyika nchini na mpaka sasa kuna tofauti kubwa.

Kwa mfano, katika usambazaji wa umeme, ipo Mikoa ya Kaskazini inatumia nishati ya umeme kama mwanga wa kuangazia kwa asilimia zaidi ya 20 (20%) lakini Mikoa kama Rukwa na Mtwara hutumia Nishati hiyo chini ya asilimia 8 (8%). Katika usambazaji wake, utaona kwamba tunasambaza kwa usawa kila mwaka tunavyofanya.

Je, Serikali haioni kwamba haina nia ya dhati ya kuondoa changamoto hiyo ya utofauti uliopo?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mipata kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kweli na nimekubali kwamba zimekuwepo tofauti za kimaendeleo baina ya maeneo na historia yake nimeieleza. Ninachoweza kusema ni kwamba zipo juhudi hasa za Serikali katika kurekebisha hali hiyo. Mpango unaokaribia kumalizika uliweka mikakati ya kuweka miundombinu ili kuweka fursa na kuondoa vikwazo kwa ajili ya maendeleo. Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na mimi kwamba maeneo ambayo tumeyapa kipaumbele ni yale ambayo kabla ya hapo miundombinu hiyo haikuwepo ukiwemo Mkoa wa Rukwa, Kigoma na Ruvuma.

Mikoa hii barabara zinaendelea kutengenezwa hivi sasa ili kutoa fursa kwa sekta ya Kilimo iweze kufanya vizuri zaidi, iwafanye wakulima wafike kwa urahisi katika masoko ya mazao yao. Hizo ni juhudi za waziwazi ambazo hata Mipata anazijua na anazikubali. Kwa hiyo, juhudi hizo zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la umeme ni kweli zipo tofauti hizo anazozisema, lakini tofauti hizi ni za mahitaji na uwezo. Kwa mfano, katika Mikoa ya Kusini ndiyo sasa tunaanza kusambaza umeme na wananchi wanaanza kutumia umeme.

Kwa hiyo, itachukua muda kabla kiwango cha mahitaji yao hakijaongezeka, lakini katika Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Kigoma sasa mipango ya kupeleka umeme wa *grid* iko katika hatua za utekelezaji. Hatua hizi zote zitasaidia katika kuleta uwiano wa maendeleo katika nchi nzima. (*Makofi*)

MHE. SAID MOHAMED MTANDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba Mikoa ya Kusini ni miongoni mwa Mikoa ambayo pengine kwa namna moja au nyingine haijafanyiwa juhudi ya kutosha ili kuweza kuleta uwiano sawa wa kimaendeleo katika nchi. Nauliza ni kwa nini sasa Mikoa ya Kusini hasa Mkoa wa Lindi umetengwa kwenye mradi ule ambao ungesaidia sana kupunguza tatizo hili la Maendeleo kupitia ule mradi wa *SAGCOT?*

Kwa nini Mikoa ya Lindi haikuingizwa, mradi ambao ungeweza kusaidia sana kunyanyua maisha ya wananchi wa Mikoa ya Kusini hasa Lindi?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mkoa wa Lindi haukutengwa, *program* zile zinaendelea na ni kweli huko nyuma Mikoa ya Kusini ilikuwa haina miundombinu. Sasa uwezekano wa kuwasiliana na Mikoa ya Kusini na Tanzania nzima ni mkubwa baada ya kuwa barabara ya kutoka Dar es salaam mpaka Lindi na Mtwara imetengenezwa, sasa Mikoa ya Kusini inaunganishwa na Ruvuma kupitia barabara inayotoka Masasi kwenda Mangaka, Tunduru mpaka Songea. Mimi naamini kabisa hali hiyo italeta mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *SAGCOT,* ile *SAGCOT* lilikuwa suala la majaribio katika maeneo maalum ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inakopita reli ya *TAZARA* na ni mawazo ya siku nyingi, lakini haikuwa kwamba itakapomaliza hapo SAGCOT itakuwa mwisho.

Tulitaka kuona *SAGCOT* inafanya namna gani na tuanzishe tena *corridor* nyingine ili tuendelee kuendeleza hivi hivi lakini ilikuwa lazima tuanzie mahali. Kwa hiyo, Kusini haikuingizwa lakini vilevile Kati haikuingizwa na vilevile Mikoa mingine ya Ziwa haikuingizwa. Tuna nchi moja hapa ambako mnaripoti hatuwezi kuanza kila kitu kila mara. *(Makofi)*

Na. 71

Kudhalilishwa na Kupigwa kwa Baadhi ya Waandishi wa Habari

MHE. ANNA MARYSTELLA JOHN MALLAC aliuliza:-

Kumekuwa na tabia ya kuwadhalilisha na kuwanyanyasa baadhi ya Waandishi wa Habari wakati wanatekeleza majukumu yao hasa wakati wa matukio ya vurugu.

Je, Serikali haioni kuwa wakati umefika kuhakikisha kuwa waandishi wanawekewa ulinzi ikiwa ni pamoja na kupewa vazi maalum la kuvaa wakati wa matukio ya hatari ili kuweza kuwatofautisha na raia wengine?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Marystella John Mallac, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Uandishi wa Habari ni taaluma kama zilivyo taaluma nyingine. Ni taaluma muhimu katika jamii kama ilivyo ualimu, udaktari, urubani, uanasheria na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwa wanahabari wanafanya kazi katika mazingira yanayohitaji ulinzi maalum pale inapolazimu. Serikali inawajibika Kikatiba kutoa Ulinzi kwa raia na mali zao wakiwemo Waandishi wa Habari. Aidha ifahamike kuwa jukumu la kwanza la ulinzi liko kwa Waandishi wa Habari wenyewe kujihami na kujilinda kwa kuyafahamu mazingira ya maeneo ya kazi husika.

Pili wazingatie miiko ya taaluma yao yaani mambo yanayotakiwa na yasiyotakiwa kutendwa katika eneo la kazi husika.

Tatu Waandishi wa Habari wakumbuke hawako juu ya Sheria nyingine za nchi hivyo, nao wazingatie sheria bila shuruti wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Nne, Wamiliki wa Vyombo vya Habari wawawezeshe watumishi wao kwakuwapatia vifaa stahiki kwa kazi zao na kwa kuwakatia Bima yaani *Risk Insurance* ili wapate fidia endapo wataumia au kufariki wakiwa kazini.

Aidha, Serikali katika matukio muhimu ya kitaifa huwa inawapatia waandishi wa habari mavazi na vitambulisho maalum kuwatofautisha na raia wengine. *(Makofi)*

MHE. ANNA MARYSTELLA JOHN MALLAC: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina swali la nyongeza lenye sehemu (a) na (b).

Kwa kuwa Uandishi wa Habari ni taaluma kama taaluma nyingine, lakini Waandishi wa Habari wanapokuwa kwenye kazi zao za matukio kutekeleza kazi zao, huwa wanafuata sheria ya kuwa na vitambulisho vyao na kufuata sheria zote. Lakini tumeshuhudia waandishi wa habari baadhi wananyanyaswa, wanapigwa wengine inapelekea mpaka kupoteza maisha.

Je, sasa Serikali imewasaidia namna gani Waandishi wa Habari ambao kwa namna moja ama nyingine wameshaumizwa na wamepoteza maisha?

(b) Napenda kujua, ni lini Serikali sasa italeta Muswada Bungeni wa Sheria za Habari?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anna Marystella Mallac, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kwamba Waandishi wa Habari taaluma yao haina tofauti na taaluma nyingine. Kuwawekea ulinzi mmoja kila mwandishi wa Habari itakuwa ni kazi ngumu sana, hata Wabunge hawana walinzi, Mawaziri hawana Walinzi na kadhalika.

Sasa leo tukisema kila Mwandishi wa habari tumpe ulinzi sijui utakuwa wa namna gani huo. Lakini pia baadhi yao Waandishi wa Habari ninaamini wengi wanazingatia sheria na maadili ya taaluma yao. Inafika wakati baadhi ya Waandishi wa habari wanakumbana na matukio ambayo pengine inaonekana kama ni kunyanyaswa, lakini ni wao wenyewe kukiuka taratibu za eneo husika.

Kwa mfano, Polisi wanapowaambia Waandishi wa Habari wasipige picha ama kufanya kazi fulani katika tukio fulani, lakini wao wanajaribu kuwa juu ya sheria, kitu ambacho kinaleta mtafaruku kati ya pande zote mbili. Ni kweli wapo Waandishi wa Habari wamepoteza maisha katika maeneo ya kazi zao, waandishi wa habari tunaita ni *sub solders*.

Kwa hiyo, unapokuwa ni *sub-solder* lazima uchukue tahadhari. Pia na hii siyo Tanzania tu, ni katika nchi nyingi Duniani. Matukio ya kuuwawa kwa Waandishi wa Habari wanapokuwa kazini yamekuwa yakiongezeka siku hata siku. Kwetu sisi tunachofanya ni kuchukua tahadhari. *(Makofi)*

(b) Lini Serikali italeta Muswada wa Sheria ya Habari? Ni wakati wowote kuanzia leo. *(Makofi)*

SPIKA: Hiyo haiwezekani. Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini. Ninyi mnaamini leo kweli? Mheshimiwa Eng. Athumani Rashid Mfutakamba. Wakati wa maswali hakuna kivuli wala nini? Mheshimiwa Mfutakamba, uko wapi?

Na. 72

Anguko la Bei ya Nishati ya Mafuta Duniani

MHE. ENG. ATHUMANI RASHID MFUTAKAMBA aliuliza:-

Anguko la bei ya Nishati ya Mafuta Duniani katika kipindi cha miaka mitano Dola 105-70 (Tshs 184,000/= - 123,000/=) kwa pipa moja limezipa hasara nchi wanachama wachimbaji Mafuta *(OPEC CARTEL)* Dola 316 (Tshs.553/= Trilioni) mwaka huu na anguko hilo lipo pia kwenye chuma ghafi *(iron/ore)* mahindi na Shaba:-

(a) Je, Serikali inaweza kutuambia sababu za anguko hili Duniani?

(b) Je, kwa nini gharama za usafirishaji, bei za bidhaa viwandani, ujenzi na vyakula hazijashuka ilihali mafuta yameshashuka bei?

(c) Je, kwa nini bei ya umeme unaozalishwa na *TANESCO, IPTL, Agreko*, *Symbion* haujashuka ilihali mafuta yameshuka bei?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES JOHN PAUL MWIJAGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba nijibu swali Namba 72 swali la Mheshimiwa Alhaji Dkt. Eng. Athumani Rashid Mfutakamba, Mbunge wa Igalula.

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali hili nitoe angalizo kwamba hili swali linahitaji semina, mjadala mkubwa sana kwa sababu maelezo yake hayawezi kujaa hapa. Naomba nijibu kama inavyofuata.

Mheshimiwa Spika, hali hii ya sasa ya kushuka kwa bei za Nishati ya Mafuta duniani imetokana na mambo yafuatayo:-

Kudorora kwa uchumi wa Bara la Ulaya katika kipindi hiki, kuwepo kwa tofauti ya mitazamo ya kisiasa (*geo-politics*) hasa kati ya Marekani na Urusi; Kuongezeka kwa matumizi ya nishati mbadala au nishati jaridifu (*renewable energy*) kuimarika kwa utumiaji mzuri wa mafuta, (*energy efficiency*) na ufanisi wa tija katika kuzalisha mafuta toka miamba ya *Shell* yaani *Shell Gas* na *Shell Oil.*

Mambo haya kwa ujumla yamechangia kupungua kwa uhitaji wa bidhaa jamii ya *petrol* ilihali ugavi wa mafuta ya gharama nafuu ukiongezeka na hivyo kusababisha kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, bei za mafuta ni sehemu tu ya viingia katika gharama za usafirishaji, uzalishaji viwandani, ujenzi na uzalishaji wa vyakula. Viingia vingine ni pamoja na gharama za vipuri, rasilimali watu, gharama za uendeshaji shughuli na thamani ya shilingi ya Tanzania inavyodhoofu kulinganisha na dola. Hivi karibuni tumeshuhudia kushuka kwa thamani ya shilingi ukilinganisha na dola.

Kudhoofu kwa shilingi yetu dhidi ya dola kuna athari kwa bei ya bidhaa na huduma inayoagizwa nje. Sababu nyingine ni suala la muda tokea anguko la bei na wakati tulipo. Kwa baadhi ya bidhaa muda zaidi unahitajika kwanza gharama mpya kuchangia gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini kwa sasa ni *Megawatt* 1,226.24. Mitambo ya kufua umeme kwa kutumia maji inazalisha *megawatt* 561.84 au 46%; gesi *megawatt* 441(36%) na mafuta *megawatt* 232.40 au 18%. Umeme wa mafuta unazalishwa na mitambo ya *TANESCO* Ubungo na Nyakato na Kampuni binafsi za *IPTL* na Aggreko.

Kampuni za *IPTL* na Aggreko zinaiuzia *TANESCO* umeme wa senti za Marekani 28 na senti 40 sawia kwa *unit* moja, wakati *TANESCO* inawauzia wananchi umeme kwa senti za Marekani 16.4 kwa unit moja. Kwa kuangalia takwimu hapo juu, ni dhahiri kuwa *TANESCO* inanunua kwa bei ya juu kuliko bei inayowauzia wananchi, hivyo kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia hakujawapa *TANESCO* unafuu wa kufanya washushe bei ya umeme.

Mheshimiwa Spika, Serikali hailifumbii macho hali hii ya kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia na imeagiza Mamlaka husika *TANESCO* na *EWURA* kuangalia inapotokea fursa hii ili wananchi wa chini waweze kunufaika. *(Makofi)*

MHE. ENG. ATHUMANI RASHID MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Madam tunahitaji Semina basi hiyo semina atuletee ili tuweze kutafakari zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kipengele chake cha jibu, kipengele cha tano amezungumzia suala a *Shell Oil* na *Shell Gas*. Nilikuwa nataka kufahamu ni mkakati gani ambao Serikali inao pengine kupitia *TPDC* kushirikiana na makampuni mengine kama Afrika ya Kusini yako Makampuni matatu sasa hivi yanazalisha mafuta na *gas* kwa kutumia huu utaratibu wa kuchoronga miamba sambamba, yaani *horizontalhydraulicfactoring* ili na sisi tuweze kupata hayo mafuta katika maeneo ya Mawembele kule Tabora, Pwani, Tanga inawezekana miamba hii ipo.

(c) Je, kuna sera pamoja na mikakati ya kutengeneza utaratibu wa kisheria kwa sababu wenzetu Afrika ya Kusini wamepata matatizo ya kutokuwa na sheria za kusimamia uchimbaji wa mafuta kupitia *Shell Oil* pamoja na *Gas*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES JOHN PAUL MWIJAGE): Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Eng. Athumani Rashid Mfutakamba, kwa kuridhishwa na majibu ya kwanza, lakini Mheshimiwa Mfutakamba tuweke wazi kwa Wabunge wenzetu kwamba mimi na wewe tumekuwa tukisimamia sekta hii.

Kuhusu hii teknolojia ya *Shell Oil* na *Shell Gas* ni kwamba hawa wenzetu ambao wamefanikiwa katika shughuli hii, Marekani, Urusi, China na kwa Afrika Kusini shughuli hii walianza zamani kutokana na nguvu yao ya kipesa.

Wanatenga pesa nyingi kwenye *RNB* sisi tumelitambua hili, tumelijua hili na nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa *TPDC*, vijana wetu wapo na mkakati nilionao wako Watanzania ambao walisomea mambo haya lakini fursa hii haikutokea wameshastaafu.

Tunapotoka Dar es Salaam na kwenda kuwaita wataalam wote wa mafuta, tukutane na vijana wapya, tuweze kuangalia ni namna gani ya kutumia fursa hii.

Swali la pili, kama nilivyosema, wakati wenzetu walianza zamani, tulidhani labda wanapoteza muda, sasa suala limeshafika na liko Afrika Kusini. Tutajiandaa kuhakikisha kwamba Sera na Sheria zinakwenda sambamba kusudi tusipate matatizo ambayo yaliyotokea na kuwapata Afrika Kusini. *(Makofi)*

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amezungumzia juu ya anguko la fedha ya Tanzania, shilingi ya Tanzania, lakini kwa mujibu wa takwimu za Benki Kuu, takribani asilimia 40 ya fedha za kigeni zinatumika katika kuagiza mafuta. Kwa hiyo, tuliotarajia kutokana na anguko la bei ya mafuta, kuwe na *reserve* ya asilimia 40 ya fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha hizi za kigeni hazihitajiki sana katika manunuzi ya nje, tulitarajia fedha ya Tanzania ipate nguvu.

Je, kwa nini mpaka sasa hatujaweza ku-*realize* kwa Tanzania juu ya anguko hili la bei ya mafuta katika mafuta tunayonunua Watanzania? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES JOHN PAUL MWIJAGE): Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, juu ya anguko la bei ya mafuta.

Siyo kweli, nafuu katika anguko la bei ya mafuta, imeshafika. Suala hapa ni kwamba tunataka nafuu kubwa sana na nimesema, ndiyo maana *EWURA* jana walikuja hapa, ndiyo maana *REA* walikuja hapa jana, tunataka nafuu zaidi. Kitu ambacho tunapashwa tuzingatie, sisi tunanunua kwa fedha za kigeni, bila kujali kwamba unanunua kiasi gani.

Kama tani moja ungenunua dola 800 ya *diesel*, wakati shilingi ya Tanzania ikiwa inalingana na dola ya Kitanzania moja kwa moja, ni tofauti ikiwa moja kwa 185. Kwa hiyo, huwezi kuepuka, hata kama unanunua 40% au 10%.

Ninachoweza kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba tutaendelea kukandamiza, kusudi tupate nafuu zaidi. Lakini jambo la kuzingatia la msingi, lazima mfahamu, kwamba tunayo *fixed cost* katika bei ya mafuta, ile ya soko la dunia. Inapofika nchini, sisi tunayo fedha ambayo lazima ikae *constant*. Kwa mfano kwenye *diesel*, tunazo fedha karibu shilingi 800, ambayo ni *service levy, fuel levy* na *company margin,* iko palepale.

Kwenye *petrol* tuna shilingi karibu 700, kwenye mafuta ya taa shilingi 700, kwa hiyo, hiyo itakufanya wewe usipate ile nafuu moja kwa moja. Ina maana kwa kila anguko la fedha ya mafuta ya dunia, utapata 40%. Mheshimiwa Mbunge, ninayo kwenye makabrasha nitakuonyesha *exactly number* mambo yanavyokwenda na hii *formula*, itabidi tui-*publish kwenye web-site* ya Bunge, kila mtu aweze kuona *structure* ya bei inavyopangwa, hakuna siri. *(Makofi)*

Na. 73

Hitaji la Umeme Mufindi Kusini

MHE. MENDRAD L. KIGOLA aliuliza:-

Mheshimiwa Rais aliahidi kupeleka umeme katika vijiji vya Malangali?

(a) Je, ni lini Serikali itaanza kazi ya kuweka nguzo za umeme katika vijiji hivyo?

(b) Je, ni kwa nini Serikali inachelewesha utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati nguzo zipo ndani ya Jimbo la Mufindi?

NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES JOHN PAUL MWIJAGE): alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali Namba 73 la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme kwenye vijiji vya Malangali, unatekelezwa na Serikali kupitia wakala wa nishati vijijini *(REA)*. Mkandarasi anayetekeleza mradi huo ni *Sengerema Engineering Group Limited*, ambaye ana uhuru wa kununua vifaa toka popote kwa mujibu wa mkataba. Utekelezaji ulianza tarehe 22 Oktoba, 2014, na inatarajiwa mradi kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2015.

Mheshimiwa Spika, kazi za mradi zinahusisha ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa *kilo vote*33 yenye urefu wa kilomita 101, ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa *kilo vote* 0.4, yenye urefu wa kilomita 40.

Ufungaji wa *transformer* 18 na kuwaunganisha umeme wateja wa awali wapatao 350. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 4.7. Hatua ya uetekelezaji iliyofikiwa katika vijiji vya Malangali ni asilimia 70 ya usimikaji wa nguzo za njia ya msongo wa *kilo vote* 33 na asilimia 30 ya usimikaji wa nguzo za njia ya msongo wa *kilovote* 0.4.

Mheshimiwa Spika, maeneo yatakayonufaika na mradi huu ni pamoja na vijiji vya Kinengambasi Moja,

Kiningambasi Mbili, Iramba Moja, Iramba Mbili, Nyingo, Indofu Moja, Indofu Mbili, Nyanyembe, Mbalamaziwa, Ibanga, Isimikinyi, Ihoanza, Kiponda na Katwanga na shule za Sekondari za Malangali, Itengule na Ihoanza. *(Makofi)*

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwamba katika *plan* ya kupeleka umeme Malangali, wameishia pale Ihoanza na katika ramani inaonyesha, hata kwenye jibu la Waziri kwamba wafikie Kiponda na Kwatwanga, lakini Kiponda na Kwatwanga bado nguzo hawajapeleka na hapa kuanzia Nyororo mpaka Maduma, wameishia Nyororo pale shuleni, bado hawajapeleka kule Maduma.

Sasa je, hivi vijiji vilivyobaki, Serikali itaanza kupeleka lini?

Swali la pili, kuna kituo kikubwa cha pale Mgololo, ambacho *transformer* imeshaungua, na *transformer* ile ilikuwa inatawanya umeme karibu kanda ya Kusini na viwanda vikubwa vilikuwa vinategemea umeme kutoka pale.

Je, Serikali itapeleka lini *transformer* ili umeme uweze kusambazwa, wananchi waweze kutumia umeme kama kawaida?

NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES JOHN PAUL MWIJAGE): Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Kuna maeneo hawajapeleka vifaa, kama iko kwenye mpango wa kazi, vifaa vitakwenda. Tunarudi palepale kwenye kitendawili, kwamba mkandarasi hatujampa fedha. Kama ni suala la usimamizi, nawaagiza tena wahusika wasimamie, kama ni suala la fedha, wawasiliane na *REA* na sisi tunaedelea kuhangaika kupata fedha za kutosha.

Transformer iliyoungua, narudia tena na Waheshimiwa Wabunge niwaambie, leo saa tano nimewaagiza watendaji wakuu wa *TANESCO*, wanakuja hapa, nitatafuta sehemu, nikikosa tutakaa pale uwanjani, njooni muwaulize maswali haya ya *transformer*, wawajibu palepale. Halafu *transformer* inapoungua, peleka *transformer* nyingine. *(Makofi)*

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nashukuru, nilikuwa naomba tu Mheshimiwa Naibu Waziri anisaidie katika wilaya mpya ya Mkalama mkoani Singida, kata ya Mwanga haipo kabisa kwenye orodha ambayo vijiji vyake kama Kidarafa na maeneo mengine kuwekewa umeme wa *REA*.

Je, ni lini Serikali itakumbuka maeneo hayo? Ahsante sana.

SPIKA: Unamtegemea Charles Mwijage kweli ajibu wewe huko ulikosema!

NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES JOHN PAUL MWIJAGE): Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili mazuri ya Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge, umeme uwe wa *REA* au wa *TANESCO*, wote ni umeme wa *TANESCO* na unakwenda kwenye makundi matatu sasa. Kuna ule umeme wa asili tulikuwa tunaujua, uliojengwa na *TANESCO*. Kuna *phase* ya kwanza, *REA* namba moja, iliyojengwa na *REA*, kuna namba mbili ambayo imejengwa na *REA*.

Maelekezo, maeneo yote ambayo hayako kwenye mipango hiyo mitatu, tumewaekeleza watendaji wa *TANESCO*, wayaainishe na tutengeneze *program* ya kuwaeleza wananchi na Wabunge, kwamba shughuli hizo zitatekelezwa lini na narudia kuagiza.

Mjibu maswali hayo moja kwa moja ni wajibu wenu kuwapigia Wabunge kuwaeleza mnafanya nini, kusudi niwaelekeze njia zipite wapi, ni Mbunge tu anayejua mahitaji ya watu wake, wengine wanajipitisha tu. *(Makofi)*

SPIKA: Naomba tuendelee na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Na. 74

Huduma Muhimu kwa Watoto Yatima

MHE. JITU V. SONI (K.n.y. MHE. NAMELOCK E. SOKOINE) aliuliza:-

Kuna vituo vingi vya watoto yatima nchini ambavyo vingine vinasimamiwa na watu binafsi:-

(a) Je, Serikali inawasaidiaje watoto hao ili waweze kupata matibabu bure?

(b) Watoto hao pia wanahitaji kwenda shule na shule hizo zina michango mingi. Je, ni nini mchango wa Serikali kwa watoto hao kielimu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA N AUSTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Namelock Edward Sokoine, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Jukumu la kusimamia na kuratibu huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi na wale wanaolelewa katika makao wa watoto nchini ni la Serikali. Aidha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii, imepewa mamlaka ya kusajili Makao ya Watoto na kutoa leseni pamoja na ufuatiliaji wa kutolewa kwa huduma za msingi kwa watoto ili uendane na viwango vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria, na kuna miongozo inayosimamia huduma hizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa sheria ya mtoto ya mwaka 2009, jukumu la utoaji wahuduma zote kwa watoto wanaolelewa katika Makao ambazo zinajumuisha chakula, matibabu, malazi, mavazi na elimu limewekwa chini ya wamiliki na wawekezaji katika Makao hayo.

Kwa mantiki hiyo, kabla ya kutolewa kwa leseni, ukaguzi ulifanyika na uchunguzi wa kina kuhakikisha wamiliki wana uwezo wa kutoa huduma zote muhimu. Pia katika uendeshaji wa makao, wizara inafanya ufuatiliaji na ukaguzi wa mara kwa mara kuhakikisha kwamba haki za mtoto ikiwemo huduma ya afya zinapatikana na kulindwa na waliopewa dhamana ya malezi na matunzo ya watoto hao.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii haina utaratibu wakutoa michango ya kugharamia elimu kwa watoto yatima wanaolelewa katika vituo hivyo ambavyo vinamilikiwa na watu binafsi.

Aidha sheria ya mtoto ya Mwaka 2012 na Kanuni zake inatoa wajibu kwa Halmashauri husika kuhakikisha watoto wote kwenye Halmashauri husika wanapata fursa sawa za kulindwa na kuendelezwa wakiwemo watoto wanaotunzwa katika Makao hayo.

Kwa kuhakikisha kwamba watoto wanaolelewa wanaondolewa vikwazo ambavyo vitaweza kusababisha kukosa haki zao za msingi ikiwemo elimu.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kutoa wito kwa wamiliki wote wa vituo vya kulelea watoto yatima na jamii ya Watanzania kuhakikisha wanakuwa na vyanzo vya mapato vya uhakika kuwezesha kutoa huduma bora kwa watoto, likiwemo suala zima la elimu.

Aidha nazipongeza Halmashauri ambazo zimeweka na kuweza kusaidia watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi kupata elimu bora bila vikwazo. Mfano wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imekuwa ikisaidia kutoa michango ya elimu kwa watoto wanaolelewa katika kituo cha Taifa cha watoto pale Kurasini. *(Makofi)*

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kutokana na vituo vingi hivi, vimeanza kuwa vingi sana na vituo vingi havina mapato ya uhakika kuwaendeleza hao watoto, kuwapa huduma zote muhimu ambazo zimetajwa.

Je, sasa tuna mpango gani au Serikali ina mfumo gani wa kuhakikisha kwamba hivi vituo vinakuwa endelevu.

Swali la pili, je, Serikali ina mpango gani ili tuweze kuwawekea Bima ya Afya hao watoto wote, lakini pamoja na hiyo, kuhakikisha kwamba wanapata, wale ambao wanamaliza Sekondari, wapate kwenda katika vyuo vya ufundi na vyuo vingine ili na wao waweze kujikimu katika maisha waweze kujiendeleza?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Sehemu (a), kwamba hakuna mapato na Serikali ina mpango gani. Napenda kutumia nafasi hii kulieleza Bunge lako Tukufu na Watanzania, hivi sasa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tunao mpango na tuko karibu kuukamilisha kwa kusaidiana na wenzetu wa *DANIDA* kuangalia hali halisi ya utoaji wa huduma ya Afya na Ustawi wa Jamii ikoje katika nchi ili kusudi maeneo yale tutakayoyabaini tuweze kupanga mpango ambao utajielekeza kujibu na kupunguza changamoto ambazo zipo.

Sehemu (b), suala la Bima ya Afya, hili ni suala ambalo ni endelevu na tunao mpango ambao tunaendelea sasa hivi kupita kwenye *Steering Committee*, ambako wizara mbalimbali ikiwemo Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kuangalia kwamba malipo ya afya yaweje kwa Watanzania na matarajio kufikia mwaka 2015/2020, angalau asilimia 75 ya Watanzania waweze kukaa katika mpango huu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa suala zima la kusaidia watoto hawa, ni katika makundi yale ambayo, kwa sera ya nchi yetu ya Mwaka 1997 ya kutoa huduma bure katika makundi maalum.

Watoto hawa ni sehemu ambayo inajumuisha, wale ambao ni mafukara, chini ya miaka mitano, akina mama wajawazito na magonjwa sugu yakiwemo magonjwa ya saratani pamoja na wazee.

Kwa hiyo, hawa wamejumuishwa katika makundi hayo kwa sera ya mwaka 1997. *(Makofi)*

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Spika, Ahsante sana na mimi naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mashirika ya Dini yamekuwa mstari wa mbele kusaidia watoto hawa na wadau wengine akiwepo Mzee Mengi na hata watoto wale kuwapeleka nje ya nchi kwa matibabu na watoto wale wenye ulemavu wa ngozi kuwasaidia.

Je, kama Serikali mnatambua mchango wa Mashirika ya Dini na watu binafsi waliojitolea kusaidia hawa watoto hawa?

Mnawasiadiaje ili kuendeleza hii shughuli ambayo wanaifanyia yaani mchango wenu mnatoa kiasi gani kusaidia Mashirika haya ya Dini na watu binafsi wanaojitokeza?

NAIBU WAZIRI WA AFYA N AUSTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maryam Msabaha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sheria namba 18 ya mwaka 2010 ambayo inahimiza suala zima la kufanya kazi kwa pamoja na wadau, yaani ile sekta binafsi na sekta ya umma.

Mheshimiwa Spika, suala la takwimu kwamba Serikali inachangia kiasi gani, sheria hii inatuhusu na tunachangia katika maeneo mbalimbali. Kwa takwimu za kifedha tutaweka mchanganuo na Mheshimiwa Mbunge ataweza kuipata.

Hata hivyo, naomba kupitia Bunge hili, nihimize sheria hii iweze kusaidia kufanya shughuli hizi kwa pamoja kwa sababu ni sehemu ya jamii. Lakini pia maendeleo yote duniani, asilimia 60 inachangiwa na *Public Private Partnership (PPP). (Makofi)*

Wawekezaji Wanaoingia na Silaha za Moto Nchini

MHE. ABDALLHAH HAJI ALI aliuliza:-

Baadhi ya wawekezaji wanakuja kuwekeza Tanzania si waaminifu na wanaingia na silaha za moto nchini kinyume na sheria za nchi.

Je, Serikali inasemaje juu ya hili.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallhah Haji Ali, Mbunge wa Kiwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, baadhi ya wawekezaji siyo waaminifu na huingia na silaha za moto nchini kinyume cha sheria. Kufanya hivi ni kinyume na sheria na kufanya hivyo ni kosa la jinai.

Mheshimiwa Spika, ziko taratibu za kisheria zinazotoa kibali kwa mwekezaji anaetaka kuingiza silaha nchini na ni vyema taratibu hizo zikafuatwa. Serikali inatoa wito kwa mtu yeyote mwenye taarifa za wageni wa aina hiyo kuziwasilisha kituo cha polisi kilicho karibu naye ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

MHE. ABDALLHAH HAJI ALI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa muda wa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Serikali imekiri juu ya uwepo wa uovu huu na mfano mzuri tu ni hivi karibuni, Zanzibar kule Paje, kuna mwekezaji mmoja aliwashambulia watu na kuwajeruhi watu wanne na baadaye siku chache tu alikamatwa na silaha nyingine nzito kuliko ile ya mwanzo.

Je, Serikali ni lini itafanya msako wa makusudi kwa wawekezaji wageni na kubaini jambo hili?

Swali la pili, kwa kuwa sheria za Zanzibar haziruhusu mtu au raia kumiliki silaha.

Je, mwekezaji huyu aliyejeruhi watu, silaha hizi alizipitisha wapi, au wawekezaji hawakaguliwi wanapoingia nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Abbdallah Haji Ali, kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kweli kwamba kulitokea matukio ya kujeruhi wananchi katika hoteli ya *Cristal Palace* kule Paje hivi karibuni na baada ya tukio hilo, jitihada zilifanywa ili kufanya msako.

Ukweli ni kwamba msako umeshafanywa katika baadhi ya hoteli ambazo pengine zina shaka kubwa na tunapanga kufanya msako wa hoteli zilizosalia. Hiyo silaha anayoizungumzia Mheshimiwa Mjumbe ambayo inatisha zaidi ilipatikana baada ya upekuzi.

Pia kuna hoteli nyingine ambazo zilipekuliwa, basi pia kulikuwa na dalili za kuvunja hii sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, silaha hii imeingizwa kimagendo. Pamoja na ulinzi ambao tutaweka kwenye vituo vya kuingia kwa maana ya *airport* na *seaport* bado kuna watu ambao wana nia mbaya wanaweza kutumia bandari ndogo ndogo ambazo ziko nyingi Zanzibar na kuingiza silaha hizi. Muhimu hapa ni wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa kwa pale ambapo wanamuona mtu na wanamtilia shaka.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Juzi kulitokea tukio la wizi hapo Darajani na ulikuwa wizi wa kutumia silaha. Je, watuhumiwa ni watu wenye asili gani? Ni Watanzania au wanatoka nje ya Tanzania? *(Kicheko)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwenye tarehe 23 kulitokea tukio hili la ujambazi pale Darajani. Kwanza niwashukuru wananchi ambao walisaidia sana kuhakikisha kwamba wahalifu hawa hawafanikiwi na tunawapata. Watu wawili walikamatwa baada ya ushiriki mkubwa wa wananchi na asili yao kwa kweli ni ya Tanzania safi. *(Kicheko)*

MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa kumekuwa kuna wimbi kubwa la kuongezeka uhalifu Zanzibar kwa miaka ya hivi karibuni ikiwemo haya matukio ambayo yamejitokeza hivi karibuni, hili la Darajani na lingine la kurusha mabomu, je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutupatia takwimu kuanzia miaka ya themanini mpaka sasa ya ongezeko la wingi wa ujambazi; na je ni jitihada gani zimechukuliwa na Serikali kuhakikisha kwamba inadhibiti mtandao huu ili matukio kama haya yasiweze kujitokeza tena.

SPIKA: Mheshimiwa jibu sehemu ya pili, la kwanza huwezi kumuuliza Waziri atatoa wapi takwimu saa hizi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimwia Spika, kitakwimu ni kwamba mwanzoni kabla ya mwaka tisini Zanzibar ilikuwa na matukio machache sana. Ilipofika miaka ya 90 yakaongezeka na yakazidi pengine kumi kwa mwaka. Hata hivyo, kutokana na mikakati mbalimbali ikiwemo Polisi Shirikishi na elimu kwa wananchi, matukio haya yamepungua na sasa hivi ni kati ya manne, matatu au moja.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, mikakati mikubwa tunayoifanya ni kuhakikisha kwamba tunaongeza doria, tunaongeza elimu kwa wananchi na vilevile kuhakikisha kwamba udhibiti katika maeneo ya kuingilia unakuwa mkubwa na mara mojamoja tunafanya operesheni.

SPIKA: Naomba tuendelee na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Christowaja Mtinda.

Na. 76

Vijiji vya Wilaya ya Ikungi Vilivyopo Kwenye Mipango ya Miradi ya Maji

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA aliuliza:-

Taarifa ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/2015 inaonyesha kuwa miradi 538 ya miundombinu ya maji vijijini itahusisha vituo 9,630 vya kuchota maji katika 587 vitakavyohudumia wanakijiji 2,040,500 na mikataba ya miradi 707 inayohusisha vituo 13,050 katika vijiji 725 yenye uwezo wa kuhudumia wanakijiji 3,262,000 imesainiwa.

Je, ni vijiji vingapi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi vipo katika miradi 538 na vingapi vipo katika miradi ya 707 iliyosainiwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Programu ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini kwenye mradi wa vijiji kumi, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi inatekelekeza miradi ya maji katika vijiji vitano na miradi mingine mitano inatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida Vijijini ambapo ndiyo Halmashauri mama iliyoandaa mpango huo hapo awali. Ni vijiji vitano vya Halmshauri ya Wilaya ya Ikungi vipo katika miradi 674 katika Mpango wa Utekelezaji wa Miradi ya Vijiji 10 nchini kote. Vijiji hivyo ni Puma, Siuyu, Mkuhi, Nkhoiree na Mgungiaa.

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Puma, Siuyu, Mkuhi, Nkhoiree ni kati ya vijiji 674 ambavyo vimekamilika nchini kote kuanzia mwezi Julai 2013 hadi Mwezi Disemba 2014…

SPIKA: Waheshimiwa, tuko ndani ya Bunge, naona wengine wameshasahau wanaongeaongea tu. Naomba uendelee kujibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, vijiji hivyo vinawanufaisha wananchi 14,471 wanaopata huduma ya maji na kijiji kimoja cha Mgungira ujenzi wa miundombinu ya maji unaendelea na ikadiriwa kuwa wananchi 3,284 watanufaika na huduma ya maji pindi mradi utakapokamilika katika kijiji hicho.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba niulize maswali mawili.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Ikungu ni mtoto wa Halmashauri

ya Singida Vijijini. Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ni Halmashauri ambayo ina Majimbo mawili na ina Wabunge wawili na ina vijiji 101. Ni Halmashauri ambayo inajitegemea, ina Mkuu wake wa Wilaya na Mkurugenzi.

Mheshimiwa Spika, swali langu, kama Halmashauri hii ya Wilaya ya Ikungi imeshakuwa na uongozi wake na imeshakuwa na bajeti yake, ni kwa nini sasa bado Halmashauri hii haipewi ruhusa ya kuandaa miradi yake; ukizingatia ina vijiji 101 na bado inategemea miradi ambayo iliandaliwa na Halmashauri mama? Ni kwa nini sasa Wizara isione umuhimu wa kuipa ruhusa Halmashauri hii mpya iandae miradi ya vijiji vyake?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Katika Jimbo ninalotoka la Singida Magharibi ambalo pia liko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, nikitoa mfano wa Kata moja tu ya Mwaru, akina mama wanatembea kutoka kijiji kinaitwa Kaugeri, kilometa 16 kwenda na kilometa 16 kurudi kufuata maji. Pia kijiji kinachoitwa Mduguyu wanawake wanatembea kilometa 10 kwenda na kilometa 10 kurudi, jumla kilometa 20 kufuata maji na maji hayo wanachangia na wanyama kama nguruwe. Waziri yuko tayari sasa kwenda kutembelea Jimbo hilo, hususan Kata hiyo ambayo nimeitaja na kuandaa upya utaratibu wa kupeleka maji katika Kata ile?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Sehemu ya kwanza watajibu TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Christowaja…

SPIKA: Unajibu sehemu ya pili, ya kwanza watajibu wenzio.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: *Okay*. Kuhusu suala la kufika katika Kata ambayo ameisema na hivyo vijiji viwili, mimi niko tayari na hapa ni karibu tu haina tatizo tutakwenda.

SPIKA: TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, miradi iliyokuwepo ambayo ilipangwa kabla Halmasauri haijagawanywa bado ilikuwa inasimamiwa na Halmashauri mama. Hata hivyo, sasa hivi kila Halmashauri inaandaa mipango yake. Kwa hiyo, Halmashauri imeruhusiwa kuandaa mipango yake.

SPIKA: Ahsante, tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona.

Na. 77

Ujenzi wa Bwawa katika Mto Songwe

MHE. ALIKO N. KIBONA aliuliza:-

Serikali iliahidi kushirikiana na nchi ya Malawi na wafadhili wa Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa kujenga bwawa katika Mto Songwe kwenye eneo la Bupigu Wilayani Ileje kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo kudhibiti Mto Songwe ambao una tabia ya kuhamahama, kufuga samaki, kufua umeme, umwagiliaji n.k:-

(a) Je, mpango huo bado upo au umekufa?

(b) Kama mpango huo bado upo, je, ni lini Serikali itaanza kulipa fidia kwa wakazi wa Bupigu na Ibungu ili kuepuka gharama za fidia zinazoongezeka kila siku?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali bado ina mpango wa kujenga bwawa katika Mto Songwe kwenye eneo la Bupigu, Wilayani Ileje kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo la kudhibiti tabia ya kuhamahama ya Mto Songwe. Kwa sasa, usanifu wa kina unaendelea na unatarajia kukamilika mwezi Aprili, 2015. Kazi ya ujenzi wa Bwawa hilo itaanza baada ya kukamilika kwa usanifu huo.

Mheshimiwa Spika, ulipaji wa fidia kwa wakazi wa vijiji vya Bupigu, Ibungu na sehemu nyingine ambazo zitaathiriwa na mradi huo, utafanyika baada ya kupata tathmini halisi ya waathirika. Kwa sasa tathmini ya mazingira na kijamii inaendelea na inatarajiwa kukamilika Februari, 2015. Tathmini hiyo inahusisha pia uandaaji wa mpango wa kuwahamisha na kuwafidia wakazi ambao wataathirika na shughuli za mradi kulingana na sheria zilizopo.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kibona swali la nyongeza.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua, tangu mradi huu umeanza mchakato wake, wananchi hawajashirikishwa kwa namna yoyote na ni muhimu sana wadau wafahamu miradi mikubwa kama hii inapofanyika. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari sasa kuandaa utaratibu ili wananchi wale wapate elimu ya nini kitafanyika katika eneo lao ili wabaki na elimu sawasawa na watu wa maeneo mengine wanaopata miradi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, siku za karibuni kumekuwa na sintofahamu kati ya Serikali ya Tanzania na Malawi hasa pale Malawi ilipotangaza kwamba asilimia mia moja ya Ziwa Nyasa ni mali ya Malawi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, kauli hii imeathiri vipi maendeleo ya kukamilika kwa mradi huu wa bwawa la Ibungu? Naomba kupata majibu.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nikubaliane naye kwamba mradi huu wananchi wanapaswa kupata elimu na moja ni kwamba una faida kwao ikiwemo umwagiliaji, kufua umeme, kilimo na mambo mengine. Kwa hiyo, niko tayari Wizara yangu kuendelea kutoa elimu na tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge na hata mmoja wetu kati ya mimi na Waziri kufika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, la pili, nimtoe wasiwasi kwamba mradi huu hautaathirika na hilo ambalo analisema. Nimhakikishie kwamba tunaendelea kuwa na mazungumzo kwa sababu mradi huu utazinufaisha nchi mbili, Tanzania na Malawi. Kwa hiyo, tutatengeneza pia Kamisheni ya pamoja ya kuendelea kumiliki miradi hii kwa pamoja.

SPIKA: Mheshimiwa Buyogera, swali la nyongeza.

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kuuliza swali humuhumu Bungeni juu ya tatizo la fedha zinazopangwa kwenda kwenye Halmashauri na kuonekana kwenye mtandao wakati kwenye Halmashauri husika hazifiki. Nauliza tena leo tatizo hilo limefikia wapi? Fedha za tangu mwaka wa jana mwezi wa tano mpaka leo hatujaziona. Mna mpango gani wa kutupelekea fedha katika miradi mikubwa mitatu kwenye Jimbo langu ambayo yote imekwama?

SPIKA: Waziri unaliweza swali hilo, siyo la Waziri wa Fedha hilo?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna hilo tatizo kwa sababu tunapotoa *exchequer* baadaye ndipo taratibu za kutoa fedha zinafuata. Hata hivyo, zile fedha zote ambazo zilikuwa zimekwama, za mwaka wa jana mpaka Desemba na Januari hii tayari tumeshazitoa, zipatazo shilingi bilioni mia tatu na tisini na nne. Nadhani kati ya fedha hizo zitakuwa zimo hizo fedha za maji. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri aendelee kufuatili na nadhani taratibu zitakapokamilika atazifuata tu hizo fedha. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, kwa niaba yake Mheshimiwa Mngodo.

Na. 78

Utoaji wa Fidia kwa Eneo Lililoachwa ili Mradi wa *EPZ* Upite

MHE. REBECCA M. MNGODO (K.n.y. MHE. JOSHUA S. NASSARI) aliuliza:-

(a) Je, ni utaratibu gani uliotumika katika kutoa fidia kwa eneo lililotengwa kwa ajili ya mradi wa *EPZ* kwa wananchi wa Malula?

(b) Je, walengwa wa fedha hizo ni akina nani na kiasi gani cha ekari kilichopangwa kulipwa kwa wahusika?

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uongozi wa Wilaya ya Arumeru kwa kushirikiana na Mamlaka ya *EPZ* ilifanya vikao mbalimbali vya makubaliano na wenye maeneo husika na mwezi Januari 2012, Kamati ya wenye maeneo hayo iliandika barua kuruhusu zoezi la upimaji na tathmini liendelee baada ya Kamati ya wenye maeneo hayo kupelekwa na Halmashauri ya Arumeru kutembelea maeneo ya *EPZ* Dar es Salaam na Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012, Halmashauri ya Arumeru ilipewa kiasi cha Sh.21,828,500 na Mamlaka ya *EPZ* kwa lengo la kufanya uthamini wa mali kwa ajili ya eneo la Malula. Aidha, baada ya fedha zilizotolewa kushindwa kukidhi majukumu yaliyokusudiwa, Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru iliandika barua yenye kumbukumbu namba L20/ MER55/19 ya tarehe 9 Julai, 2013, ikiomba fedha za ziada kwa ajili ya kuendelea kufanya tathmini kwa eneo husika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti, hadi sasa eneo la Malula bado halijakamilika kufanyiwa uthamini na hivyo fidia kwa walengwa haijatolewa. Kwa hali hiyo, naiomba Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru kuharakisha zoezi la uthamini wa mali katika eneo hilo ili kuepuka kuongezeka kwa gharama zisizo za lazima.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, jumla ya hekari 4,000 zilibainishwa katika kijiji cha Malula kwa ajili ya mradi wa *EPZ*. Orodha ya wananchi ambao ndiyo walengwa waliopisha mradi huo inashughulikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru na pindi itakapokamilika na uthamini kufanyika taarifa itatolewa.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imekuwa sasa ni tabia ya Serikali kuchukua maeneo ya wananchi kabla ya kufanya tathmini ya fidia, Serikali haioni kwamba Halmashauri ya Meru

imetumia vibaya fedha za umma jumla ya Sh.21,828,500 kufanya tathmini ambayo haikufikia mwisho au kukamilika.

Mheshimiwa Spika, katika barua ya kwanza, maana nina barua mbili zenye majibu tofauti. Barua ya kwanza inasema wanasubiri shilingi milioni nane na laki tisa. Je, fedha zitakapopatikana Halmashauri ya Meru itafanya tathmini upya, kwa sababu gharama za ardhi zitakuwa zimepanda?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, ni kwa nini sasa wananchi wanaoishi pale King'ori na Malula wasipewe ridhaa waendelee kufanya shughuli zao za kawaida za kilimo, kwa sababu ni zaidi ya miaka kumi, siyo miaka miwili kama majibu yalivyosema, ni zaidi ya miaka kumi wananchi wa pale Malula na King'ori wameshindwa kuendeleza shughuli zao za kilimo. Je, wanapewa ruhusa sasa ili waendelee na shughuli zao za kawaida kwani wana familia zao na wanahitaji kusomesha watoto na kuendesha maisha kama kawaida? *(Makofi)*

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza, suala la msingi hapa ni Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru kuona kwamba inaendeleza uthamini wa eneo lile. Kwa sababu utaratibu huu umeshaanza, sioni kwamba nguvu iliyotumika pale ni kupoteza fedha za Serikali kwa sababu tayari dalili zote zinaonekana kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru ingependa utaratibu wa mradi huu ufanyike katika eneo hili kama maeneo mengine yanavyofanya.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, kijiji cha King'ori na Malula, kwa maana ya kwamba wananchi watumie maeneo yao ambayo wamekaa kwa muda mrefu, hili ni suala ambalo Mamlaka ya *EPZ* na Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru tunaweza tukakaa tukazungumza lakini hata kama ruhusa hiyo itatolewa na kwa sababu Wilaya ya Arumeru inataka mradi huu inawezekana kabisa wakaruhusiwa kutumia maeneo yale kwa upandaji wa mazao ambayo si ya kudumu kwa sababu mchakato mzima unaendelea.

SPIKA: Ahsante, tuendelee na swali linalofuata, Mheshimiwa Selemani Said Jafo.

Na. 79

Kiwanda cha Kusindika Matunda Kisarawe

MHE. SELEMANI S. JAFO aliuliza:-

Wilaya ya Kisarawe inalima kwa wingi machungwa, embe na mananasi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kiwanda cha kusindika matunda hayo Wilayani Kisarawe?

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mbunge wa Kisarawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, malengo na mkakati wa Serikali kwa sasa ni kuhakikisha kuwa mazao ya kilimo yakiwemo matunda yanaongezwa thamani kabla ya kuuzwa. Hivyo Wizara imekuwa ikiendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda katika maeneo ambayo malighafi ya kutosha inapatika.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza malengo ya Serikali, Wizara yangu kupitia *SIDO* imekuwa ikiendesha mafunzo ya usindikaji kwa wajasiriamali wadogo ili kuwajengea uwezo wa kuanzisha viwanda vidogo vya kusindika matunda kupitia utaratibu wa Programu ya Muunganisho Ujasiriamali Vijijini *(MUVI)*. Pamoja na hayo, Wizara kupitia *SIDO* tayari imeishaingia mkataba na nchi ya Japan na imetoa kiasi cha shilingi bilioni moja kama *counter part fund* ambazo zitawekwa katika Benki ya *CRDB* kwa lengo la kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wajasiriamali wasindikaji *(agroprocessers)* kupitia *credit guarantee scheme.* Mara Mfuko huu utakapoanza kufanya

kazi, Wilaya ya Kisarawe itanufaika na Mfuko huu kwa kujenga viwanda vidogo vidogo vya kusindika matunda.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Serikali bado haijapata mwekezaji wa kujenga kiwanda cha kusindika matunda katika Wilaya ya Kisarawe, tunashauri wakulima wa Wilaya hiyo kuuza matunda kwenye kiwanda cha kusindika matunda cha Bakheresa kilichopo Mwandege, Wilaya ya Mkuranga. Pamoja na hayo, namuomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na sisi tushirikiane katika kuhamasisha wawekezaji wa nje na wa ndani ili tuwezeshe kuanzishwa kwa viwanda vya usindikaji wa matunda Wilayani Kisarawe.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa Kisarawe kuna vikundi vingi sana vya akina mama na vijana, ambao kwa sasa hivi wanaendelea na shughuli za usindikaji hasahasa wanasindika matunda na uzalishaji wa asali. Je. Serikali inatueleze nini wana Kisarawe, kwamba ikiwezekana kupitia *SIDO* na *TBS,* kuja kutoa mafunzo maalum kwa ajlili ya kuzalisha bidha ambazo zitakuwa zinakidhi ushindani?

(ii) Kwa kuwa sasa hivi Kisarawe tunaenda katika mchakato mkubwa sana wa uanzishwaji wa Mipango Miji na hali kadhalika kutenga eneo la viwanda. Hivi sasa tumetenga eneo la Visegese kwa ajili ya ujenzi wa viwanda. Je, Serikali kupitia Wizara yako Mheshimiwa Wazira, ina mpango gani kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, kuhakikisha kwamba wawekezaji wote wanaokuja nchini, wanaelekezwa Kisarawe katika eneo la Visegese ili mradi vijana wetu wapate ajira na hivyo kupunguza tatizo la ajira kwa vijana? *(Makofi)*

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, tutawaagiza Wakurugenzi wa *TBS* na *SIDO* waje

Kisarawe kukutana na vikundi hivyo vya akina mama na kutoa mafunzo haya ya kuongeza ubora katika bidhaa. Naelewa mpaka sasa tuna programu mbalimbali katika Mkoa wa Pwani, karibu wajasiriamali 1,450 wameshapta mafunzo hayo. Kwa hiyo, hilo tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili napenda sana nimpongeze Mheshimiwa Selemani Jafo, kwa jitihada zake za kuhamasisha uwekezaji katika eneo lake la Wilaya ya Kisarawe. Mfano hai ni Mradi wa Michikichi utakaogharimu zaidi ya dola milioni 400 katika eneo la Kimala Misale, ambapo pana shamba kubwa linaanzishwa pale. Kwa hiyo, nakubaliana naye kwamba tutashirikiana pamoja kuendeleza eneo la Visegese ili kupata eneo la uwekezaji na hasa ikizingatiwa kwamba Wizara yangu imeshatoa agizo kwa kila Halmashauri ya Wilaya nchini, kutenga maeneo maalum kwa ajili ya viwanda vidogo, vya kati na vikubwa kwa ajili ya wawekezaji ambao wanatarajia kuja katika maeneo hayo. *(Makofi)*

MHE. RIDHWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza hasa katika eneo lake la viwanda.

Mheshimiwa Spika, pale Bagamoyo pamekuwa na mpango wa *EPZ,* lakini kwa kipindi kirefu sana tunaona tu yale maeneo yamehodhiwa na *EPZ,* hakuna kiwanda kinachojengwa, hakuna kinachoendelea. Sasa tunataka tujue, nini mpango mlio nao juu ya eneo lile? Ahsante sana. *(Makofi)*

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunaendelea na mchakato wa kuona ni jinsi gani tunaweza kuanzisha mradi wetu mkubwa wa *EPZ* pale katika eneo la Bagamoyo. Kazi kubwa inayoendelea sasa hivi ni kuangalia taratibu za kulipa fidia kwa wananchi wanaoishi pale. Napenda kukutaarifu Mheshimiwa Ridhwani

kwamba tarehe 11 Februari, 2015, tayari zimeshatengwa shilingi bilioni 6.7 ambazo zitalipwa kwa wananchi wa vijiji vya Zinga na Kondo. Vilevile tayari tumeshapata shilingi bilioni 10 kutoka Shirika la Bandari kuwalipa wale wenye maeneo ambayo Bandari ile itajengwa. Kwa hiyo, maendeleo ya mradi huu yanaendelea vizuri. *(Makofi)*

Na. 80

Kuboresha Viwango vya Pensheni kwa Watumishi

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE aliuza:-

Viwango vya pensheni kwa wastaafu hapa nchini ni vidogo sana na huathiri uhakika wa maisha ya wastaafu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha pensheni?

(b) Je, kwa nini mtumishi asikatwe zaidi na Serikali ichangie zaidi ili viwango vya pensheni kwa wastaafu vipande?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K.A. MALIMA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha viwango vya pensheni kwa ajili ya kuwapunguzia wastaafu makali ya ongezeko la gharama za maisha. Ili kukabiliana na changamoto za ugumu wa maisha kwa wastaafu, Serikali tayari iko kwenye mchakato wa kuongeza viwango vya pensheni. Pia ongezeko hilo la viwango vya pensheni litategemea zaidi kuimarika kwa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuongeza mchango wa mwajiri unategemea pia uwezo wa mwajiri kimapato. Mfano mchango wa mwajiri ukiongezeka unaathari za moja kwa moja kwenye "*wage bill*" kwa maana ya gharama za mishahara ya Serikali au Taasisi husika. Pia mchango zaidi wa mtumishi utakuwa unaathari za moja kwa moja kwenye "*take home*" kile kiwango anachochukua nyumbani ambacho ndiyo msingi wa kuendesha maisha yake leo akiwa bado mtumishi. Viwango vya pesnsheni vinaweza kuboreshwa kwa kuangalia viashiria au vigezo vingine kama vile marekebisho ya viashiria vya umri, riba, kanuni za mafao, aina ya mafao, kama ni mafao ya lazima au hiari na kuimarisha mifumo na sheria zinatozumika kuendesha na kusimamia Mifuko ya Hifahdi ya Jamii.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri au ya Serikali lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa viwango vya mishahara kwa wafanyakazi au watumishi ambao wako kazini sasa hivi ni vidogo sana na hivyo kuwafanya wasiwe na uwezo wa kuweza kujiwekea akiba ya baadaye. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni vema ije na mpango madhubuti ambao kwa kweli utasaidia kuboresha hali halisi ya wafanyakazi hao?

(b) Viwango vya pensheni vilivyopo sasa hivi vya Sh.50,000/= na kuendelea vimekuwa ni vidogo sana na vinachukua muda mrefu sana kubadilika, kKwa nini Serikali isije na mpango ambao utasaidia labda baada ya miaka miwili au mitatu viwango hivyo viongezwe, kuliko miaka kumi au ishirini ndiyo vinapanda? Maana Sh.50,000 ya miaka mitano iliyopita haina thamani kwa leo. Kwa nini Serkali isije na mpango wa kuboresha hali hiyo? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K.A. MALIMA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa viwango vya sasa hivi mtumishi anachangia asilimia 5 ya mshahara wake na mwajiri anachingia asilimia 15. Sasa kile kiwango cha

mshahara kikiongezekana, maana yake na ile michango atakayochangia mtumishi kwa ajili ya hiyo pensheni yake ya baadaye navyo vitaongezeka. Ndiyo maana tukasema kwamba, kadri Serikali itakavyopata uwezo wa kuongeza mishahara ya watumishi, ina maana kile atakachochukua nyumbani kitaongezeka lakini na ile pensheni atakayokuwa nayo baadaye itaongezeka.

Mheshimiwa Spika, ninasema huo ndiyo utaratibu tunaokwenda nao sasa hivi, tunaangalia mchakato mzima huo wa pensheni, ndani ya Wizara ya Fedha upo mchakato unaoangalia hiyo hatua, lakini lazima tuweke tahadhari, kwamba sisi tunawalipa watumishi wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama na wale ambao wamestaafu kabla ya mwaka 2004. Wale wanaolipwa *PSPF, PPF* na *NSSF* wana utaratibu mwingine.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba sisi hatulipi viwango nje ya vitakavyolipwa na taasisi nyingine, ndiyo maana nikasema, utaratibu huu wa kufanyia tathmini ya pensheni inayowezekana kulipwa ina kazi kubwa kidogo. Itahusu mjadala kidogo mpana lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote kwamba mchakato huo unafanyiwa kazi sasa hivi ili kuangalia hatua zinazostahili na uwezo wa kuboresha pensheni kwa ajili ya wanaostahili.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, wote naomba muangalie saa.

Na. 81

Ujenzi wa Barabara Muhimu

MHE. EUGENE E. MWAIPOSA aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuruhusu kampuni za ndani na nje kuwekeza kwenye barabara ili kuharakisha maendeleo ya nchi?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kutofanya hivyo kunazinyima fursa kampuni zenye uwezo wa kuwekeza katika sekta hiyo ambayo ingesaidia kupunguza tatizo la ajira?

(c) Je, Serikali haioni kuwa kiasi cha rasilimali fedha kinachoelekezwa katika ujenzi wa miundombinu hiyo kwa kiasi kikubwa kingeweza kuelekezwa katika sekta nyingine kama afya, maji na elimu?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eugen Elishiringa Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, fursa za uwekezaji kwenye ujenzi wa Miundombinu ya barabara nchini kwa Makampuni ya watu binafsi wa ndani na nje ya nchi ziko wazi kwa kupitia Sera ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(PPP)* na kupitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka 2010 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2011. Sheria hii inainisha namna ya kupata makampuni ya ndani na nje ambayo yanaweza kuwekeza kwenye sekta ya miundombinu nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeanza kutekeleza sheria hii kwa vitendo. Daraja la Kigamboni ambalo ujenzi wake unaendelea, ni aina mojawapo ya *PPP*. Aidha, Wizara inaendelea na taratibu za kujenga barabara ya Dar es Salaam – Chalinze *Express way* kwa njia ya *PPP* baada ya Serikali kuifanyiaa marekebisho sheria hii mwaka 2014.

MHE. EUGENE E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata jibu ambalo kusema ukweli halikuwa ni jibu sahihi kwa maswali yangu haya matatu. Kwa sababu mimi nimeuliza makampuni binafsi sijauliza *PPP*. Sasa kwa sababu nimepata fursa hii, niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu hayo, naamini kabisa yapo makampuni mengi nchini ambayo yana uwezo wa kwenda na mtindo huo wa *PPP* lakini hawana elimu ya kutosha. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhamasisha makampuni ya ndani yenye uwezo huo ili kuweza kutumia mpango huo wa *PPP?*

Mheshimiwa Spika, lakini *concern* ya maswali yangu haya yalikuwa ni makampuni ya ndani na nje ambayo yenyewe tu yana uwezo bila kuingia ubia na kampuni nyingine au taasisi yoyote ile ya Kiserikali ili kuweza kujenga barabara hizi za pembezoni mwa Jiji au Miji. Kwa mfano, barabara za kilomita 3, 4, 5 zijenge kampuni zenyewe halafu baada ya barabara kukamilika sasa waweze kutoza tozo kwa ajili ya kurudisha zile fedha zao.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza jambo hili lingesaidia sana kuwapa fursa vijana za ajira lakini pia fedha nyingi za Serikali ambazo zinatumika kuwekeza kwenye barabara za vumbi, basi makampuni haya yangeweza kusaidia kutengeneza barabara za lami.

SPIKA: Swali sasa.

MHE. EUGENE E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, swali langu nauliza kwamba, je, Serikali sasa kwa nini isije na utaratibu wa kuruhusu makampuni hayo kuwekeza kwenye barabara yenyewe kama yalivyo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kwa kufikiria kwamba ujenzi wa barabara badala ya Serikali miaka yote kuwa ndiyo mjenzi tuingize na sekta binafsi. Hata hivyo, ili tuweze kufanikiwa lazima tuchukue uzoefu wa nchi nyingine wamefanya vipi mpaka wakafanikiwa kwa kutumia sekta binafsi na ndiyo maana tukaileta hii sheria ya *PPP* na Bunge mkaipitisha.

Mheshimiwa Spika, sasa nachosema ni kwamba pamoja na hayo mawazo aliyonayo kwa sababu hizi *assets* ni mali ya Serikali, ukisema mtu atajenga tu barabara bila

kufuata sheria na aanze kutoza tutakuwa na vurugu. Kwa hiyo, kwa kila kitu lazima tufuate sharia na ndiyo maana tumeweka sharia hii. Sheria yenyewe inaleta vivutio kwa sababu hakuna mtu anayeweza akawekeza fedha zake katika ujenzi wa barabara halafu asipate *return*. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na mfumo fulani ambapo kutakuwa na majukumu Serikali inafanya nini na mtu binafsi huyo atafanya kitu gani, faida yake itakuwa kitu gani. Kuna vitu vinaitwa *Built Operate and Transfer,* kwa hiyo, kwa miaka fulani lazima mpatane kwamba atajenga, ataendesha, akisharudisha fedha zake ana-*transfer* kwa Serikali.

Na. 82

Daraja la Mto Mbwemkulu

MHE. FATUMA A. MIKIDADI (K.n.y. MHE. FAITH M. MITAMBO) aliuliza:-

Daraja la Mto Mbwemkulu lililoko mpakani mwa Wilaya ya Liwale na Nachingwea lililojengwa enzi ya mkoloni liko kwenye hali mbaya:-

Je, ni lini Serikali itajenga upya daraja hilo ambalo wakati wowote linaweza kusababisha madhara?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Daraja la Mto Mbwemkulu lililo mpakani mwa Wilaya ya Liwale na Nachingwea lenye urefu wa meta 62 ni daraja la chuma au kwa lugha ya Kiingereza linaitwa *bailey bridge*. Madaraja ya aina hii huwekwa mbao *(timber deck)* ambayo ndiyo njia inayotumika kwa magari kupita. Ubovu wa madaraja haya chuma unaonekana pale mbao zinapochakaa. Mbao za daraja hili ziliondolewa na kuwekwa upya mwezi Novemba, 2014. Hivi sasa hali yake ni

nzuri. Aidha, vyuma vya daraja hili vinakaguliwa mara kwa mara na kufanyiwa matengenezo ili kufanya daraja hili libakie kwenye ubora na salama kwa kupitisha magari.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa daraja hili bado linaweza kutumika na kwa kuzingatia ufinyu wa bajeti ya Serikali, hivi sasa Serikali haina mpango wa karibuni wa kujenga daraja jipya katika Mto Mbwemkulu. Serikali itaendelea kulifanyia matengenezo muhimu daraja hili ili kuepusha madhara *(preventive maintenance)* ili liendelee kutumika wakati Serikali inatafuta fedha za kuyabadilisha madaraja hayo ya *(bailey bridge)* na kuyaajenga upya.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, madaraja haya ukiachia Mbwemkulu, madaraja tu ndani ya Mkoa wa Lindi, kwa maana Liwale, Nachingwea, Ruangwa, Kilwa na Lindi, mengi yalijengwa wakati wa mkoloni 1950 na kuendelea. Madaraja haya mengi ni mabovu. Je, Serikali itayafanyia lini ukaguzi na ukarabati?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Mkoa wa Lindi, madaraja mengi yalijengwa tulivyopata uhuru na yametumika kwa muda mrefu. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, kazi ya Mameneja wa *TANROADS* ni kuendelea kuyafanyia matengenezo ya kawaida *(preventive maintenance)* ili yaendelee kutumika. Kwa hiyo, kama kuna madaraja ambayo bado yana tatizo hilo, tutayafutilia na kuweza kuchukua hatua zinazostahili.

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Pamoja na ukarabati wa daraja hili, bado ile barabara ya Liwale – Nachingwea ambayo ndiyo kitega uchumi cha wananchi wa Liwale ni mbovu sana. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuambatana na mimi kwenda kushuhudia ubovu wa barabara hiyo ili iweze kufanyiwa matengenezo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili…

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, siyo swali lako.

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, barabara anayoitaja ya Liwale – Nachingwea ni barabara ambayo iko chini ya Wizara yangu. Niko tayari kuambatana naye, ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Faith Mitambo, aliyeuliza swali la msingi, kwenda kuiangalia na kuchukua hatua zinazostahili kwenye barabara hiyo. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda umepita. Naomba nitambue baadhi ya wageni walioko humu ndani. Kwanza kabisa katika Ukumbi wa Mheshimiwa Spika, ninao wageni, Wajumbe wa Chama cha Ushirika cha Ujenzi wa Nyumba Mwenge, yuko Mheshimiwa Walter Kiswaga - Mjumbe wa Bodi, yupo Ndugu Ramadhani Mdenho -Mjumbe wa Bodi, yupo Thomas Mosha - Menaja wa Ushirika, yupo John Phascal – mwanachama, na yupo Primy Mushi – mwanachama, kasoro tu hakuna wanawake. Wageni hawa wapo hapa Dodoma kwa ajili ya kazi. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria kutoka Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ambao ni Ndugu Albert Msangi - Kamishna, yupo kwenye *gallery* ya Spika. Pia yupo Ndugu Agness Mgeyekwa - Kaimu Katibu Mtendaji, ahsante sana tumefurahi kuwaona ninyi nyote. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wageni wa Mheshimiwa Selemeni Jafo ambao ni Ndugu zake kutoka Kisarawe wakiongozwa na Ndugu Mbegu Rwambo - Mwenyekiti wa Kitongoji cha Chambasi, Mwenyekiti

tafadhali simama na kundi lako. Kumbe wapo watu wawili, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni watatu wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ambao ni Mheshimiwa Abdallah Mwendadi Mauya Diwani Kata ya Mkange, yupo Ndugu Adam Mwandosia - Mwenyekiti wa Kijiji cha Saadani, kuna Ndugu Gensenda Mwise Mbilikimo - Mwenyekiti wa Kijiji cha Matipwili, karibuni. *(Makofi)*

Halafu tuna wageni 19 wa Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa Selemani Jafo ambao ni wafanyakazi wagonjwa wa Kampuni ya Acacia, Mgodi wa Bulyankhulu wakiongozwa na Kiongozi wa Chama cha Wafanyakazi wa Migodi na Madini, Ndugu Benjamini Daudi Doto. Naomba msimame, tumesikia habari zenu mara kwa mara, naona mmemua kuja kuwafuata wanaohusika hapahapa. *(Makofi)*

Tuna Wageni wa Mheshimiwa Juma Sururu Juma ambao ni Viongozi wa Umoja wa Vijana wa CCM kutoka Tawi la Shariff Musa ambao ni Ndugu Khamis Abdallah Ally, Ndugu Omar Salum Hamad na Ndugu Abdul-aziz Salum Mohammed, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile tuna wageni wa Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ambao ni Wajumbe watano wa Umoja wa Wanawake na Wajumbe 11 kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI. Umoja wa Wanawake, wale Wajumbe watano na watumishi 11 naomba wote wasimame, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Andrew Chenge ambaye ni Ndugu Robert Mayongera - Mwenyekiti wa SHIRECU, Mkoa wa Shinyanga. Naomba asimame Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

Pia tuna wageni wa Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola ambao ni wanafunzi 50 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, hawa wanafunzi wako wapi? Karibuni sana nategemea mnatimiza wajibu wenu kwani kusoma ndiyo

lengo, mkitaka kuingia kwenye maneno kama haya muwe mmemaliza kusoma. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Highness Kiwia ambao ni Ndugu Abubakar Mombeki Kapera, karibu Ndugu Kapera. *(Makofi)*

Wageni waliopo kwa ajili ya mafunzo Bungeni ambao ni wanachuo 10 kutoka vyuo vya afya vya Bugando, St. John na Royal ambao wapo katika mafunzo kwa vitendo katika Hospitali ya Rufaa ya Dodoma wakiongozwa na na Ndugu Saimon Gagie. Naomba hao Madaktari wetu wasimame popote walipo, tunawatakia mafunzo mema, ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna kikundi cha kwaya cha Inueni Mioyo kutoka Parishi ya Mt. Petro Chamwino. Naomba wasimame watuinulie mioyo. Ahsanteni sana mmependekeza, katika kuimba mtuombee na muiombee nchi yetu. *(Makofi)*

Matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa tano asubuhi kutakuwa na kikao kitakachofanyika katika ukumbi wa Msekwa. Kikao cha saa tano sijapata sababu kwa hiyo itakuwa saa saba, anayeomba saa tano ni mpaka atoe sababu mpaka mimi niridhike lakini hapa sijaridhika ni saa saba.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika katika ukumbi namba 231.

Katibu wa Wabunge Wanawake CHADEMA, Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, anaomba niwatangazie Wabunge wanawake wa CHADEMA kuwa leo saa saba watakuwa na kikao chao katika chumba namba 227.

Pia, Katibu wa Wabunge Wanawake Wabunge wa CCM Bungeni, Mheshimiwa Mary Chatanda anaomba niwatangazie Wabunge wote wa CCM wakutane saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Vilevile kuna tangazo la Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Charles Mwijage anasema, naomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa Wataalam wa *TANESCO*, msikilize vizuri hapo, wataalam wa *TANESCO* watakuwa katika ukumbi namba 229, ghorofa ya pili, jengo la utawala kuanzia saa sita mpaka saa nane mchana kwa ajili ya kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na miradi ya umeme katika Majimbo yao ikiwemo hoja ya Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini. Sasa chumba kimoja kitatosha hicho? Mtaangalia itakavyokuwa huko, naamini hakitoshi maana kila mtu atasogea huko.

Ofisi ya Bunge inatangaza kwamba *UTT* wanafanya maonyesho ya shughuli wanazofanya kwenye viwanja ya Bunge kwenye eneo la maegesho ya magari leo tarehe 3 Februari, 2015. Mimi sijui *UTT* ni nini, mkaangalie huko, maonyesho hayo yapo eneo la maegesho.

Ofisi pia inaomba niwatangazie kwamba Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi inatarajia kufanya marejesho ya Sheria ya Utwaaji Ardhi na Fidia. Ili kupata sheria inayokidhi mahitaji ya wananchi, Wizara inashirikisha wadau mbalimbali kutoa maoni yao. Hivyo, wameleta dodoso ambalo Wabunge wanatakiwa kulijaza. Dodoso hilo linapatikana kwenye mapokezi ya mlango wa kuingia Bungeni na wakishazijaza wazirejeshe hapohapo walipochukua. Kwa hiyo, nadhani kuna madodoso yanayopita mchukue ili muweze kushiriki katika jambo hilo linaloendelea.

Katibu!

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Katiba, Sheria na Utawala Pamoja na Maoni na Mapendekezo Yaliyomo kwenye Taarifa hiyo kama ilivyosomwa Bungeni

SPIKA: Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Rweikiza!

MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kipindi cha kuanzia Januari 2014 hadi Januari 2015.

Mheshimiwa Spika, awali kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi sote uzima na afya. Niwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi sana kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Nimshukuru na kumpongeza sana Mwenyekiti Mstaafu aliyenitangulia, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, kwa uongozi mahiri, makini na wenye ufanisi mkubwa sana wakati wa uongozi wake. Nitaendelea kujifunza kutoka kwake na kutumia uzoefu wake katika uongozi wangu. Nawashukuru pia wananchi wa Bukoba Vijijini kwa ushirikiano na msaada mkubwa wanaonipa unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya Kibunge kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa fasili ya 6(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba, Sheria na

Utawala imepewa majukumu ya kusimamia shughuli za Wizara zifuatazo:-

(i) Ofisi ya Rais (Utawala Bora);
(ii) Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma);
(iii) Ofisi ya Rais (Uhusiano na Uratibu);
(iv) Ofisi ya Rais (Tume ya Mipango);
(v) Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano);
(vi) Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge); na
(vii) Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na muundo wa shughuli za Kamati zilizotajwa katika fasili ya 6(2) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Wizara tajwa hapo juu zinajumuisha Taasisi, Idara na Wakala nyingine mbalimbali. Kamati yangu katika utekelezaji wa majukumu yake imeongozwa na mpangokazi wake wa mwaka. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Kamati yangu iliandaa mpangokazi ambao ndiyo uliotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizofanyika. Kutokana na kuwepo kwa shughuli maalum kubwa na muhimu ya utungaji wa Katiba mpya, ratiba ya vikao vya Kamati ililazimika kubadilika ili kuendana na shughuli hiyo muhimu kwa Taifa. Bunge Maalum la Katiba lilifanya vikao vyake kuanzia Februari hadi Aprili kisha kusitishwa kwa muda kabla ya kurejea tena mwezi Agosti hadi Oktoba 2014. Kwa msingi huo, baadhi ya shughuli za Kamati hazikuweza kutekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/ 2015, Kamati imetekeleza majukumu ya Kikanuni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Katika kipindi cha Januari 2014 hadi

Januari 2015, Kamati ilifanya ziara mbalimbali za ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Jengo la ofisi na makazi ya Makamu wa Rais. Kamati ilifanya ziara ya kukagua ujenzi wa jengo la ofisi na makazi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano iliyopo Tunguu, Zanzibar. Jengo hili jipya na la kisasa limejengwa kutokana na kuongezeka kwa haja na shughuli za ofisi hiyo na pia kuimarisha utekelezaji wa kazi zinazohusu mambo ya Muungano. Jengo hili limegharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa asilimia mia moja na limegharimu shilingi bilioni 10.3.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini mambo mawili muhimu yafuatayo:-

(a) Kuwepo kwa jengo la ghorofa linalomilikiwa na mtu binafsi jirani sana na ofisi na makazi ya Makamu wa Rais. Jengo hilo la ghorofa linahatarisha ulinzi na usalama wa kiongozi huyo mkuu wa nchi kwani watu wanaoishi na kutumia jengo hilo wana uwezo wa kuona kila kitu kinachoendelea katika nyumba na ofisi ya Makamu wa Rais.

(b) Matumizi ya shata za mbao katika madirisha ya nyumba ya kuishi Makamu wa Rais. Kwa kuwa eneo hili lina chumvichumvi, shata zilizotumika zilionekana kutofaa kwani zinachakaa mapema na hivyo kuhitaji matengezo ya mara kwa mara, jambo ambalo linaongeza gharama za utunzaji wa jengo hilo. Mambo hayo ni dosari kubwa zilizopaswa kurekebishwa.

(ii) Ujenzi wa jengo la ofisi na Makazi ya Waziri Mkuu Dodoma. Mnamo tarehe 7 Juni, 2014, Kamati ilitembelea mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi na makazi ya Waziri Mkuu….

SPIKA: Waheshimiwa wanaotaka kuongea wanakwenda nje lakini siyo kuleta fujo humu ndani, endelea tafadhali!

MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mnamo tarehe 7 Juni, 2014, Kamati ilitembelea mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi na makazi ya Waziri Mkuu na kupokea taarifa ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006, Ofisi ya Waziri Mkuu iliamua kuboresha mazingira ya kufanyia kazi ikiwemo kuanzisha mradi mpya wa ujenzi wa ofisi na makazi ya Waziri Mkuu Mjini Dodoma. Ujenzi huo unahusisha makazi mapya ya Waziri Mkuu, ofisi ya Waziri Mkuu, nyumba za wageni wa Kitaifa, ujenzi wa viwanja vya michezo na eneo la kutua *helicopter*. Ujenzi huu ulianza mwaka 2009 na ulitarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 12. Mradi huu unagharimiwa na Serikali ya Tanzania kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, gharama za awali za mradi zilikadiriwa kuwa shilingi bilioni sita na milioni mbili. Hata hivyo, gharama hizo zimeongezeka hadi kufikia shilingi bilioni saba na milioni mia hamsini na nne sawa na ongezeko la 16.2% kutokana na kubadilika kwa usanifu wa jengo kulikopelekea kuongezeka kwa kazi. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu, ujenzi wa majengo ya ofisi na makazi ya Waziri Mkuu ulikuwa umefikia zaidi ya 90%.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua nzuri za utekelezaji wa mradi lakini mradi huo unakabiliwa na changamoto kubwa mbili zifuatazo:-

(a) Ugumu wa kupatikana fedha za mradi kwa wakati. Mradi huu hadi sasa umechukua miaka mitano na miezi minne na bado haujakamilika badala ya miezi 12 iliyotarajiwa. Ucheleweshaji huu unatokana na mtiririko hafifu wa utoaji wa fedha kutoka Hazina. Aidha, Serikali ilikuwa ikitenga fedha kila mwaka wa bajeti lakini fedha hizo zilikuwa hazitolewi. Pale ambapo Serikali inapotoa fedha hizo, zimekuwa zikitolewa kidogo na kwa kucheleweshwa.

(b) Udhaifu wa Mtaalam Mshauri. Kutokana na dosari ya Mtaalam Mshauri kuchelewa kutoa taarifa ya ushauri wa kitaalam kila mara, mwenendo wa kukamilisha mradi huu umekuwa wa kasi isiyoridhisha. Changamoto hizo zote mbili kwa pamoja zimeathiri mradi huo.

(iii) Ukaguzi wa miradi ya Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA). Tarehe 7-15 Juni, 2014, Kamati ilitembelea na kupokea taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma. Itakumbukwa kwamba, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma ilianzishwa kwa Amri ya Uanzishwaji wa Mamlaka *(Establishment Order No.230)* ya mwaka 1973 chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Mashirika ya Umma Na.17 ya mwaka 1969. Lengo la uanzishwaji huo lilikuwa ni kutekeleza azma ya Serikali kuhamishia Makao Makuu ya nchi kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Juni, 2013 hadi Mei, 2014 Mamlaka ilitekeleza miradi ifuatayo:-

(a) Ujenzi wa miundombinu. Mamlaka imeweza kujenga barabara kwa kiwango cha lami pamoja na kuchonga barabara za vumbi katika eneo la mradi ili kufikisha huduma za jamii katika eneo la mradi.

(b) Mpango kuhusu uendelezaji wa ardhi. Katika juhudi za kuendeleza ardhi, Mamlaka imefanya mapitio ya mpango kabambe wa eneo la Mji Mkuu. Mpango huo unahusisha ujenzi wa mji wa Serikali utakaokuwa na ofisi, nyumba za viongozi na huduma muhimu za kijamii kwa viongozi na watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu yaliyotekelezwa na Mamlaka lakini ipo changamoto kubwa iliyojitokeza na changamoto hiyo; ni kukosekana na utashi wa Serikali. Uamuzi wa kuhamishia Makao Makuu Dodoma ulifanyika toka mwaka 1973 ambapo hadi sasa ni miaka 42 imepita. Kamati haioni juhudi za kutosha za Serikali za kuhamishia Makao Makuu kutoka Dar es Salaam kuja

Dodoma. Hii ni kutokana na Serikali kuendelea kujenga ofisi na nyumba nyingi za Serikali kwa gharama kubwa Jijini Dar es Salaam wakati miradi ya Ustawishaji wa Makao Makuu ikiendelea kusuasua.

Mheshimiwa Spika, miradi ya *TASAF,* Awamu ya III. Kamati yangu ilitembelea Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *TASAF* Makao Makuu mnamo mwezi Mei 2014 na kupata taarifa za utekelezaji wa miradi ya *TASAF* Awamu ya III. Katika taarifa hiyo, Kamati ilielezwa kuwa *TASAF* imeanza kutekeleza mradi wa kuinua kaya maskini sana uliozinduliwa mwaka 2013. Mradi huo unalenga kuwapatia ruzuku ya fedha kaya maskini sana ili kuziinua kiuchumi kwa lengo la kuziwezesha kumudu gharama za mahitaji muhimu ya kibinadamu kama vile chakula, afya na elimu kwa kaya hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mpango huu, kaya maskini katika mamlaka za utekelezaji 113 za Halmahauri za Jiji, Miji, Manispaa, Wilaya, Kata, Vijiji na Shehia zipatazo 7,061,630 zilitambuliwa, kuidhinishwa na kupitishwa katika mikutano mikuu maalum ya Jiji, Mitaa na Shehia kwa kuzingatia vigezo maalum vya umaskini. Baada ya utambuzi wa kaya maskini sana jumla ya shilingi bilioni 31 zimelipwa kama ruzuku kwa kaya 266,601 katika Halmashauri 41 nchini. Mchakato wa utambuzi wa kaya maskini sana unaendelea katika maeneo mengine 48 ya utekelezaji kwenye Vijiji, Mitaa, Shehia 3,160 katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Rukwa, Tabora, Kigoma, Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kunusuru kaya maskini sana unahusisha kutoa ajira ya muda kwa walengwa ambapo walengwa hufanya kazi kwa muda wa siku 15 katika kipindi chenye njaa. Kupitia ajira hizo, walengwa hulipwa kiasi cha shilingi 2,300/= kwa siku sawa na shilingi 138,000/= kwa kipindi cha miezi minne ambapo mradi umekusudiwa. Miradi ya kutoa ajira imeanza katika maeneo ya Kibaha, Chamwino, Bagamoyo, Manispaa ya Mtwara, Lindi, Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, changamoto za utekelezaji wa *TASAF* Awamu ya III. Pamoja na mafanikio ya Mradi wa *TASAF,* Mradi huu umekabiliwa na changamoto zifuatazo:-

Upungufu wa Rasilimali Fedha, ukosefu wa ofisi kwa Watumishi, vigezo vya utambuzi wa kaya maskini sana kutokueleweka vizuri miongoni mwa walengwa na baadhi ya watu wenye vigezo vya kuitwa maskini sana wameachwa katika Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa Ikulu Ndogo ya Chamwino: Mnamo tarehe 15 Juni, 2014 Kamati yangu ilitembelea Mradi wa Ukarabati wa Ikulu Ndogo ya Chamwino ili kujionea hatua iliyofikiwa katika ukarabati huo. Ikulu Ndogo ya Chamwino ilijengwa miaka ya 1970 hivyo imekuwa na majengo yaliyochakaa sana. Ikulu hii kwa mara ya mwisho ilifanyiwa ukarabati mkubwa kwa baadhi ya majengo katika Mwaka wa Fedha 2010/2011, ambayo ni Jengo la Makazi ya Rais, Jengo la Ofisi ya Rais na Jengo la Mapokezi. Majengo ambayo hayakufanyiwa ukarabati yako katika hali mbaya sana ya uchakavu na hayafai kabisa kutumika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea Ikulu Ndogo ya Chamwino ilijionea changamoto zifuatazo:-

- Ufinyu wa bajeti: Fungu linalotolewa kwa ajili ya ukarabati wa Ikulu limekuwa likitengewa fedha kidogo na isiyokidhi mahitaji ya kazi hiyo. Aidha, pale ambapo fedha ya ukarabati inakuwa imetengwa katika Mwaka husika wa bajeti, fedha hizo hazitolewi kwa wakati na wakati mwingine hazitolewi kabisa, hali inayoathiri utekelezaji wa mpango wa ukarabati wa majengo hayo.

- Upungufu wa maji: Tanki la maji lililojengwa kwa ajili ya kuhifadhia maji ni dogo sana kwani lilijengwa ili kukidhi mahitaji ya wakazi wachache waliokuwa wanazunguka eneo hilo. Aidha, kutokana na shughuli za kibinadamu, kumekuwa na uharibifu katika chanzo cha maji; hivyo, kuathiri upatikanaji wa maji kwenye chanzo hicho na

kusababisha uhaba wa maji Ikulu na wananchi wanaozunguka eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa Mahakama nchini. Mnamo mwezi Mei, 2014, Kamati yangu ilitembelea Mahakama ya Tanzania na kukutana na Jaji Mkuu wa Tanzania Mheshimiwa Othman M. Chande pamoja na Watendaji wengine wa Mahakama na kupokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Mahakama nchini. Katika taarifa hiyo, Kamati ililezwa yafuatavyo:-

Ujenzi wa Mahakama: Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Mahakama, inaendelea na mchakato wa kuanza ujenzi wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali nchini kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama Jijini Dar es Salaam, Mahakama Kuu katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Kigoma, Mara, Singida, Morogoro, Manyara, Shinyanga na Dodoma.

(ii) Ujenzi wa Mahakama za Wilaya katika Wilaya za Bunda, Bariadi, Nkasi, Bukombe, Bagamoyo na Kilindi.

(iii) Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo katika maeneo ya Buguruni, Kawe, Kigamboni, Makuyuni, Mailimoja, Songea, Mpanda, Terrati, Mtowisa, Sangabuye, Ilolanguru, Mwanga, Mangaka, Makongorosi, Itigi, Machame, Mkomazi, Gairo, Kiagata, Lukuledi, Longido, Ngorongoro, Kilekero, Maruku, Magoma na Bomang'ombe.

Uendeshaji wa shughuli za Mahakama: Kamati yangu imekuwa ikitoa ushauri kwa Serikali kuhusu kuboresha Mhimili wa Mahakama ili uweze kutekeleza jukumu lake kikamilifu. Miongoni mwa mambo ambayo Kamati yangu ilishauri ni pamoja na kuimarisha Muundo mpya wa Utawala wa Mahakama ambao utatenganisha shughuli za kiutawala na za kimahakama.

Ninafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali

ilitekeleza ushauri kwa kuanzisha Muundo Mpya wa Mahakama kupitia Sheria Na. 4 ya 2011 (*The Judicial Administration Act*).

Mheshimiwa Spika, katika Sheria hiyo, ulianzishwa Mfuko wa Mahakama wenye lengo la kuwezesha uendeshaji wa Mahakama katika ngazi zote na kuboresha mfumo wa usikilizaji wa mashauri nchini. Kutokana na kuanzishwa kwa mfumo huo, Bajeti ya Mahakama iliongezeka toka shilingi bilioni 20 kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na kufikia zaidi ya shilingi bilioni 166 kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Ongezeko hili limewezesha kuboresha utendaji wa Mahakama kwa kuongeza usikilizaji wa mashauri na idadi ya vikao vya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada nzuri ikiwemo Mipango Kabambe ya Mahakama kuboresha mfumo wa utoaji haki nchini, Mhimili huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

Ufinyu wa Bajeti: Pamoja na kutambua ongezeko kubwa la bajeti katika Mfuko wa Mahakama, kumeendelea kuwa na upungufu wa fedha kwani fedha zinazotengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha husika zimekuwa hazitolewi zote na kwa wakati.

Upungufu wa vitendea kazi na Rasilimali Watu: Katika Mhimili wa Mahakama, changamoto ya upungufu wa vitendea kazi na rasilimali watu ni kubwa hasa ukizingatia mazingira ya sasa ambapo uhalifu na uelewa wa sheria vimeongezeka miongoni mwa wananchi.

Mmomonyoko wa maadili: Katika Mhimili wa Mahakama kumekuwepo na mmomonyoko wa maadili kwa baadhi ya watumishi ambao wanaoshughulikia utoaji haki katika Mhimili huo. Baadhi ya viashiria vya mmomonyoko huo ni pamoja na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Machi hadi Juni 2014, Kamati ilikutana na Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali

za Serikali zilizo chini yake katika Ofisi Ndogo ya Bunge Dar es Salaam kwa lengo la kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na kupokea Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Baada ya kupokea taarifa za utekelezaji wa majukumu kwa Wizara zilizo chini yake, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka 2014/2015, ambapo maoni kuhusu uchambuzi wa bajeti ya Wizara, Taasisi, Idara na Wakala wa Serikali yameainishwa katika sehemu ya Taarifa ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Taasisi, Idara na Wakala hizo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015 Kamati yangu ilipata fursa ya kuchambua Miswada mitatu ya Sheria; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali *(The Written Laws Miscellaneous Amendments Act), 2014,* Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2), 2014 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.2) Act), 2014* na Muswada wa Sheria ya Maafa *(The Disaster Amendment Act), 2014*.

Katika kufanya uchambuzi wa Miswada hiyo, Kamati ilihakikisha kuwa wadau wanashirikishwa ipasavyo.

Maoni ya Kamati kuhusu wa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, 2014 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.2) Act, 2014)* iliwasilishwa katika Mkutano wa 16 na 17 wa Bunge hili Tukufu.

Taarifa kuhusu maoni ya Kamati kufuatia uchambuzi wa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2), 2014 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.2) Act)*, 2014 itawasilishwa katika Mkutano huu wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Mei, 2014 Kamati yangu ilitembelea Ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) ili kujionea utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hiyo. Katika ziara hiyo, Kamati ilielezwa kuwa Serikali imeendelea kuimarisha Taasisi hiyo ili kuimarisha Utawala Bora kwa maendeleo ya Taifa letu. Katika jitihada hizo Serikali imeweza kuiimarisha TAKUKURU kama ifuatavyo:-

- Ili kuepukana na adha ya kupanga, Serikali iliipatia TAKUKURU fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi yake iliyoko Upanga, Jijini Dar es Salaam.

- Taasisi hii imekuwa ikikabiliwa na upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali na hivyo kuathiri utendaji na ufanisi. Kupitia jitihada za Kamati yangu katika kuishauri Serikali kuboresha Taasisi hii, Serikali imetoa kibali cha kuajiri watumishi 400 katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 wa kada mbalimbali kwa lengo la kuimarisha Taasisi na watumishi hao wamekwisha anza kazi.

- Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imepatiwa vifaa vya kisasa na maabara inayowezesha kufanya uchunguzi wa tuhuma za makosa ya rushwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, TAKUKURU inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Upungufu wa Fedha: Taasisi hii imekuwa ikitengewa fedha kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi iliyonayo.

- Ulazima wa kupata kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inalazimika kuomba kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini kwa makosa yote makubwa na madogo ya rushwa.

- Jambo hili limekuwa likidhoofisha juhudi za Taasisi katika kupambana na rushwa kwani vibali huchelewa

kutolewa na wakati mwingine havitolewi kabisa. Gharama nyingi za Serikali zimekuwa zikitumika katika kufanya uchunguzi wa tuhuma za rushwa nchini, lakini majalada yanapowasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka mengi yao hayatolewi vibali na kuachwa kwa kigezo cha kutokuwa na ushahidi wa kutosha, jambo linaloisababishia hasara Serikali. Aidha, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2014 hadi Januari 2015 TAKUKURU ilichunguza majalada 3014 ya rushwa na kati ya hayo, TAKUKURU imefungua kesi 108 Mahakamani. Hii ni sawa na asilimia 3.58. Idadi hii kubwa ya majalada yanayochunguzwa ni kielelezo cha nchi yetu kuchukia rushwa na kuchukua hatua stahiki kwa wale wanaothibitika kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yako imekuwa na utaratibu wa kawaida wa kuwajengea uwezo Wabunge kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kutokana na jukumu kubwa la Kikatiba la kuwawakilisha Wananchi. Ili kufanikisha lengo hilo, Ofisi yako imekuwa ikiandaa semina, warsha, makongamano na ziara za ndani na nje ya nchi ili kutimiza azma hiyo. Katika kufanya hivyo, kati ya tarehe 8 - 15 Novemba, 2014 Kamati yangu ilifanya ziara ya kimafunzo nchini ya Uingereza kwa lengo la kuongeza ujuzi na weledi kwa Wajumbe wa Kamati kuhusiana na masuala ya kupambana na rushwa ili watumie ujuzi huo katika kuishauri Serikali namna bora ya kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa nchini.

- Mafunzo yaliyopatikana katika ziara hiyo: Katika ziara hiyo Kamati ilikutana na taasisi tatu tofauti na kujifunza mambo mbalimbali.

- Kikao na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya kupambana na Makosa ya Udanganyifu Mkubwa wa kijinai *(Serious Fraud Office)*. Kutokana na kikao na Mkurugenzi Mkuu na Watendaji wengine wa Ofisi hii, Kamati ilijifunza mambo yafuatayo:-

- Taasisi hii imepewa jukumu la kuchunguza

makosa ya udanganyifu mkubwa na yenye athari kubwa za kiuchumi na kijamii yanayofanywa na watu na makampuni.

- Taasisi ya Kupambana na Makosa ya Udanganyifu Mkubwa *(Serious Fraud Office)* ni taasisi yenye mamlaka kamili na huru inayochunguza na kuendesha mashtaka katika makosa makubwa ya udanganyifu na rushwa bila kulazimika kuomba kibali kutoka kwa Mwendesha Mashtaka wa Serikali.

- Taasisi hii imejengewa uwezo mkubwa kwa kuipa rasilimali watu, fedha na nyenzo za kisasa za kufanyia kazi ambapo ina Wafanyakazi 300 wenye ujuzi wa hali ya juu katika fani za sheria, uchunguzi na uhasibu. Katika kutekeleza majukumu yake, Taasisi ya Kupambana na Makosa ya Udanganyifu Mkubwa, inafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na taasisi zingine zinazohusika na usimamizi wa makosa ya jinai kama Ofisi ya Taasisi ya Mwendesha Mashtaka ya Umma *(The Crown Prosecution Service),* Polisi ya Uingereza *(The London Metropolitan Police)* na Polisi wa London *(The London Police)*.

- Kikao na Kamati ya Bunge ya Haki *(Justice Committee):* Kamati ya Bunge ya Haki ya Uingereza ambayo inafanya kazi sawa na Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, haiingilii utendaji wa siku hadi siku wa Taasisi za Serikali za kuzuia na kupambana na rushwa.

- Kikao na Mkurugenzi wa Taasisi ya Mwendesha Mashtaka ya Umma wa Serikali *(The Crown Prosecution Service)*. Katika Taasisi hiyo Kamati yangu ilijifunza mambo yafuatayo:-

Ofisi hii inashughulikia makosa ya rushwa ambayo hayajafikia kiwango cha kushughulikiwa na Taasisi ya Kupambana na Makosa ya Udanganyifu Mkubwa. Pamoja na Taasisi ya Kupambana na Makosa ya Udanganyifu Mkubwa na Taasisi ya Mwendesha mashtaka ya Umma zipo Ofisi nyingine zinazoshughulikia makosa ya rushwa kutegemeana na mazingira ya kosa lenyewe. Ofisi hizo ni Polisi wa London

(The London Police) na Polisi ya Uingereza (*The London Metropolitan Police)*. Taasisi hii imejengewa uwezo mkubwa kwa kuipa rasilimali watu wenye ujuzi wa hali ya juu, bajeti ya kutosha na nyenzo za kisasa za kufanyia kazi, hivyo kuifanya ofisi hii itekeleze majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(TASAF)* katika kutekeleza Mradi wake wa Awamu ya Tatu wa kutoa ruzuku kwa kaya maskini sana, iliamua kujenga uelewa wa pamoja kwa Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi kwa kuandaa ziara ya mafuzo katika nchi inayotekeleza Mradi unaofanana na huo. Katika kutekeleza uamuzi huo, mwezi Januari, 2014 Kamati ilifanya ziara ya mafunzo nchini Mexico na kujionea jinsi mradi ya kuinua Kaya Maskini Sana kupitia Mradi kama wa *TASAF* katika nchi hiyo.

Kamati ililelezwa jinsi kaya maskini sana zinavyofaidika kwa kupewa fedha za shule, matibabu na kutoa mitaji ya biashara kwa vikundi vya akina mama. Kufuatia mafunzo hayo, Kamati iliona kuwa mfumo wa uendeshaji Mradi kama huo unaofanywa na *TASAF* Awamu ya Tatu nchini Mexico ni wa kuigwa ili kuboresha utendaji wa Mfuko huo hapa nchini kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kama ifuatavyo kuhusu Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Zanzibar:-

- Serikali ya Muungano kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wafanye jitihada za kuzungumza na mmiliki wa jengo la ghorofa lililo karibu na jengo la ofisi na makazi ya Makamu wa Rais ili walinunue kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama wa Makamu wa Rais na watumiaji wengine wa jengo hilo.

- Serikali ibadilishe aina ya shata za mbazo zilizotumika katika madirisha ya nyumba ya makazi ya Makamu wa Rais na badala yake yatumike madirisha ya vioo ili kuendana na mazingira ya eneo hilo ya chumvi chumvi yanayofanya shata za mbao kuchakaa haraka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi na Makazi ya Waziri Mkuu, Dodoma, Kamati inashauri ifuatavyo:-

- Serikali itoe fedha zilizotengwa kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa jengo hili kwa wakati ili kuharakisha ukamilishwaji wake na kuepuka uwezekano wa kuongezeka kwa gharama za ujenzi kutokana na kuchukua muda mrefu wa kukamilika kwake.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma, Kamati inashauri ifuatavyo:-

- Serikali ibuni vyanzo mbadala vya mapato ili kuwezesha kutengwa kwa fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa Miradi mbalimbali ili kuiwezesha Serikali kuhama kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma.

- Serikali iangalie uwezekano wa kufuta vijiji vilivyomo ndani ya eneo la Mradi.

- Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi wakiwemo viongozi wa kisiasa;

- Serikali iboreshe Miundombinu katika eneo la Mradi.

Kutokana na utekelezaji hafifu wa Serikali kuhamishia Makao Makuu Dodoma, Kamati inaishauri Serikali itafakari upya kama kuna nia ya dhati na sababu za kutekeleza azma hiyo, kama hakuna nia hiyo na sababu hizo, mpango huo uachwe.

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kujionea changamoto zinazoikabili Ikulu ndogo ya Chamwino, inashauri kama ifuatavyo:-

Serikali ijenge utamaduni wa kukarabati majengo ya

Ikulu ndogo ya Mikoani badala ya kuziacha kwa muda mrefu bila kufanya ukarabati. Kutokana na ongezeko la watu wanaohudumiwa na maji kutoka tanki la maji la Chamwino, tanki hilo limeelemewa na kufanya maji hayo kutotosheleza mahitaji, Serikali ijenge tanki lingine na kutafuta chanzo kingine cha ziada.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi katika shughuli za uchambuzi wa Miswada, Kamati iwe inapewa muda wa kutosha wa kuchambua Miswada ili kuiwezesha kuchambua Miswada hiyo kwa kushirikiana na wadau. Kasi ya kuwajengea uwezo Wabunge juu ya mchakato wa utungaji wa sheria ikiwemo uchambuzi wa Miswada iongezwe.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni muhimu kufanya marekebisho ya sheria za nchi yetu ili ziwe nzuri na ziweze kutumika kwa ufanisi, Kamati inashauri Serikali kutoleta Miswada ya sheria inayokusudia kufanya mabadiliko makubwa na mengi ya kisera kwenye Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali, badala yake marekebisho hayo yaletwe katika sheria mahususi inayosimamia masuala husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ziara za kimafunzo nje ya nchi, Kamati inashauri kuwa Ofisi yako ifanye maandalizi mapema ikiwa ni pamoja na kufanya mawasiliano na Mabalozi wetu walioko huko ili kuepusha usumbufu kwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Serikali iimarishe TAKUKURU kwa kuipa mamlaka kamili ya kufungua mashtaka na kuyaendesha Mahakamani bila kuomba kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka. *(Makofi)*

Kutokana na kuongezeka kwa matukio ya rushwa nchini, Kamati inaona ni muda mwafaka kwa nchi yetu kuanzisha chombo kingine kipya kitakachoshughulikia makosa madogo madogo ya rushwa na TAKUKURU ishughulikie makosa makubwa makubwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha utendaji kazi wa Mfuko wa Jamii *(TASAF),* Serikali iendelee kutenga fedha za kutosha katika bajeti yake.

Kuhusu upungufu wa ofisi, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato wa kuimilikisha *TASAF* Kiwanja Na. 2454/118 ili iweze kuanza ujenzi wa jengo la ofisi zake. *TASAF* iendelee kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu vigezo vinavyotumika katika kutambua Kaya Maskini.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha Mhimili wa Mahakama, Muundo mpya wa Mahakama chini ya Sheria Namba 4 ya Mwaka 2004 uimarishwe kwa kusimamiwa kikamilifu. Serikali iendelee kutenga bajeti ya kutosha ili kuiwezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Itakumbukwa kuwa, Taarifa hii ya Kamati inahitimisha Taarifa za Mwaka za Utekelezaji wa Majukumu kuhusu Bunge la Kumi. Kwa kuwa Taarifa hii ni ya mwisho, niruhusu niseme machache kuhusu mafanikio ambayo Kamati yangu imeyapata katika kuishauri na kuisimamia Serikali hususan katika Wizara, Idara, Taasisi na Wakala wa Serikali zilizo chini yake.

Kamati imepata mafanikio makubwa tangu kuanza kwa Bunge la Kumi na baadhi ya mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:-

Ushiriki wa Kamati katika mchakato wa Katiba mpya. Mnamo tarehe 31 Disemba, 2010 Mheshimiwa Profesa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Hotuba yake ya kuuaga mwaka na kuukaribisha mwaka mpya, alitangaza kuanza kwa mchakato wa utungwaji wa Katiba mpya ambayo ingewashirikisha wananchi wengi zaidi, itakayoongoza nchi yetu kwa miaka hamsini ijayo au zaidi.

Ili kufanikisha zoezi hili, Serikali ilileta Muswada Bungeni ambao pamoja na mambo mengine, ulikuwa unakusudia

kuanzisha Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa ajili ya kuratibu na kukusanya maoni ya Wananchi kuhusu katiba mpya, kuandaa Rasimu ya Katiba kisha kuiwasilisha kwa Rais.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati yangu ilishiriki kikamilifu katika mchakato wa utungaji wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sheria Na. 8 ya Mwaka 2011. Sheria hii ndiyo iliyoweka utaratibu wa kukusanya maoni, uundwaji wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, uundwaji wa Bunge Maalum pamoja na utaratibu wa kupiga kura unaotarajiwa.

Sheria hii ilifanyiwa marekebisho mara nne kwa lengo la kuiboresha. Miswada ya Sheria zote hizo ilipita kwanza katika Kamati, ambapo Kamati ilifanya kazi ya kupokea Maoni ya Wadau, kuchambua na hatimaye kutoa maoni katika Bunge lako Tukufu ili kulisaidia Bunge namna ya kuiboresha Miswada na kupata sheria nzuri.

Kamati yangu imekuwa ikiishauri Serikali kupitia Wizara zilizo chini yake, kujenga majengo yake yenyewe ili kuepuka gharama zinazotokana na kupanga Ofisi. Ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kutokana na ushauri wa Kamati, Taasisi zifuatazo zimejenga majengo yake yenyewe:-

RITA ambao wamekamilisha ujenzi wa Jengo la Ofisi yao lenye urefu wa ghorofa 33 lililopo Mtaa wa Makunganya Jijini Dar es Salaam na TAKUKURU ambayo imejenga jengo la ofisi yake Jijini Dar es Salaam.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Kengele ya pili.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kama ilivyowasilishwa Mezani)

TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA KWA KIPINDI CHA KUANZIA JANUARI, 2014 HADI JANUARI, 2015

_____

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015. Kanuni hii inaitaka kila Kamati ya Kudumu ya Bunge kuwasilisha taarifa ya mwaka ya shughuli zake ili zijadiliwe na Bunge lako tukufu katika mkutano wa mwisho kabla ya mkutano wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ni miongoni mwa Kamati kumi na nane (18) za Bunge lako tukufu**.** Kamati hii imeundwa chini ya Kanuni ya 118 (1) & (2) ikisomwa pamoja na fasili ya 5(1) (b) na fasili ya 6(2) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge,Toleo la Aprili 2013. Kwa mujibu wa fasili ya 6(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala imepewa majukumu ya kusimamia shughuli za Wizara zifuatazo:-

(a) Ofisi ya Rais

(i) Utawala Bora;
(ii) Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
(iii) Uhusiano na Uratibu na
(iv) Tume ya Mipango

(b) Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano

(c) Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Uratibu na Bunge; na

(d) Wizara ya Katiba na Sheria

Mheshimiwa Spika, Pamoja na Muundo wa Shughuli za Kamati zilizotajwa katika fasili 6 (2) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge; Wizara tajwa hapo juu zinajumuisha taasisi, Idara na Wakala kama ifuatavyo:-

1. **Ofisi ya Rais - Utawala Bora inajumuisha;**

(i) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini (TAKUKURU).
(ii) Ofisi ya Rais Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.
(iii) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania. (MKURABITA).
(iv) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).
(v) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea.
(vi) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma
(vii) Ofisi ya Rais; Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.
(viii) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.
(ix) Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma.
(x) Ofisi ya Rais - Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma.
(xi) Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango.

2. **Ofisi ya Makamu wa Rais inajumuisha;**

(i) Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais
(ii) Ofisi ya Makamu wa Rais; Muungano

3. **Ofisi ya Waziri Mkuu iajumuisha;**

(i) Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu.
(ii) Ofisi ya Waziri Mkuu.
(iii) Tume ya Taifa ya Uchaguzi.
(iv) Msajili wa Vyama vya Siasa.
(v) Idara ya Maafa.
(vi) Mfuko wa Bunge.
(vii) Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

4. **Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha;**

(i) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
(ii) Mkurugenzi wa Mashtaka.
(iii) Tume ya Marekebisho ya Sheria.
(iv) Tume ya Utumishi wa Mahakama.
(v) Mahakama.
(vi) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.
(vii) Wakala wa Usajili, Udhamini na Ufilisi, (RITA).

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu katika kutekeleza majukumu yake imeongozwa na Mpango kazi wake wa Mwaka. Katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, Kamati yangu iliandaa mpango kazi ambao ndio uliotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizopangwa kufanywa na Kamati katika mwaka huu ni kama zifuatazo:-

(i) Kutembelea na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotengewa fedha za maendeleo;

(ii) Kupokea taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Idara, Wakala na taasisi zinazosimamiwa na Kamati;

(iii) Kufanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na Taasisi zote zinazosimamiwa na Kamati;

(iv) Kupitia na kufanya uchambuzi wa Miswada ya Sheria iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Mheshimiwa Spika;

(v) Kufanya ziara za mafunzo ndani na nje ya nchi; na

(vi) Kufanya kazi nyingine yoyote ambayo Mheshimiwa Spika ataagiza Kamati iifanye.

2.0 SHUGHULI ZILIZOFANYIKA

Mheshimiwa Spika, Kutokana na kuwepo kwa shughuli maalum, kubwa na muhimu ya utungaji wa Katiba Mpya, ratiba ya vikao vya Kamati ililazimika kubadilika ili kuendana na shughuli hiyo muhimu kwa taifa. Bunge Maalum la Katiba lilifanya vikao vyake kuanzia Februari hadi Aprili kisha kusitishwa kwa muda kabla ya kurejea tena mwezi Agosti hadi Oktoba, 2014. Kwa msingi huo baadhi ya shughuli za Kamati hazikuweza kutekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2014/2015 Kamati imetekeleza majukumu ya kikanuni kama ifuatavyo:-

2.1 Kufanya Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015, Kamati ilifanya ziara mbalimbali za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyokuwa imetengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Madhumuni ya ziara hizo yalikuwa kuangalia utekelezaji wa miradi, hatua zilizofikiwa katika utekezaji wake na changamoto zinazoikabili miradi hiyo, pamoja na kutoa ushauri juu ya namna bora ya kuendelea kukabiliana na changamoto hizo. Miradi iliyotembelewa ni kama ifuatavyo:-

2.1.1 **Jengo la Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais:**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara ya kukagua ujenzi wa jengo la Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano lililopo Tunguu, Zanzibar. Jengo hili jipya na la kisasa linajengwa kutokana na kuongezeka kwa haja na shughuli za Ofisi hiyo na pia kuimarisha utekelezaji wa kazi zinazohusu mambo ya Muungano. Jengo hili limegharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa asilimia mia moja na limegharimu jumla ya shilingi bilioni 10.3.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo kamati ilibaini mambo mawili muhimu kama ifuatavyo:-

(i) Kuwepo kwa jengo la ghorofa linalomilikiwa na mtu binafsi jirani na Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais. Jengo hilo la ghorofa linahatarisha ulinzi na usalama wa kiongozi huyo Mkuu wa Nchi, kwani watu wanaoishi au kutumia jengo hilo wana uwezo wa kuona kila kitu kinachoendelea katika nyumba na Ofisi ya Makamu wa Rais.

(ii) Matumizi ya shata za mbao katika madirisha ya nyumba ya kuishi Makamu wa Rais. Kwa kuwa eneo hili lina chumvichumvi, shata zilizotumika zilionekana kutofaa kwani zinachakaa mapema na hivyo kuhitaji matengenezo ya mara kwa mara, jambo ambalo linaloongeza gharama za utunzaji wa jengo hilo.

Mambo hayo ni dosari kubwa zinazopaswa kurekebishwa.

2.1.2 **Ujenzi wa Jengo la Ofisi na Makazi ya Waziri Mkuu, Dodoma**

Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 7 Juni, 2014 Kamati ilitembelea mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi na Makazi ya Waziri Mkuu na kupokea taarifa ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2006 Ofisi ya Waziri Mkuu iliamua kuboresha mazingira ya kufanyia kazi ikiwemo

kuanzisha mradi mpya wa ujenzi wa ofisi na makazi ya Waziri Mkuu mjini Dodoma. Ujenzi huo unahusisha makazi mapya ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, nyumba za wageni wa kitaifa, ujenzi wa viwanja vya michezo na eneo la kutua helikopta. Ujenzi huo ulianza mwaka 2009 na ulitarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 12. Mradi huu unagharimiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia miamoja.

Mheshimiwa Spika, gharama za awali za mradi zilikadiriwa kuwa shilingi 6,002,003,502.00. Hata hivyo gharama hizo ziliongezeka hadi kufikia 7,154,541,643.42 sawa na asilimia 19.2 kutokana na kubadilika kwa usanifu wa jengo kulikopelekea kuongezeka kwa kazi. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huo, ujenzi wa majengo ya ofisi na makazi ya Waziri Mkuu ulikuwa umefikia asilimia zaidi ya 90.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua nzuri za utekelezaji wa Mradi, Mradi huo unakabiliwa na changamoto kubwa mbili zifuaatazo:-

(i) **Ugumu wa kupata fedha za mradi kwa wakati**

Mradi huu hadi sasa umechukua miaka mitano na miezi minne na bado haujakamilika badala ya miezi 12 iliyotarajiwa. Ucheleweshwaji huu umetokana na mtiririko hafifu wa utoaji wa fedha kutoka Hazina. Aidha, Serikali ilikuwa ikitenga fedha kila mwaka wa bajeti lakini fedha hizo zilikuwa hazitolewi. Pale ambapo Serikali iliamua kutoa fedha hizo, zilikuwa zikitolewa kidogo na kwa kuchelewa.

(ii) **Udhaifu wa Mtaalam Mshauri**

Kutokana na dosari ya Mtaalam Mshauri ya kuchelewa kutoa taarifa na ushauri wa kitaalamu kila mara, mwenendo wa kukamilisha mradi umekuwa na kasi isiyoridhisha.

Changamoto hizo mbili kwa pamoja zimeathiri utekelezaji wa mradi na hivyo kusabisha kasoro katika utekelezaji wa bajeti.

2.2 **Ukaguzi wa miradi ya Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA)**

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 7 na 15 June, 2014 Kamati ilitembelea na kupokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma. Madhumuni ya ziara hiyo yalikuwa kujionea namna ambavyo Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma inavyotekeleza majukumu yake kwa kuzingatia malengo ya uanzishwaji wake na bajeti inayotengwa katika kila mwaka wa fedha kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu, Dodoma ilianzishwa kwa amri ya uanzishwaji wa Makao Makuu (The Capital Development Authority (Establishment) Order Na.230 ya Mwaka 1973 chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Mashirika ya Umma Na. 17 ya Mwaka, 1969. Lengo la uanzishwaji huo lilikuwa kutekeleza azma ya Serikali ya kuhamishia Makao Makuu ya nchi kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma.

Katika kutekeleza azma hiyo ya Serikali, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu ilipewa majukumu yafuatayo:-

(a) Kutekeleza uamuzi wa Serikali wa uhamishia Makao Makuu Dodoma.
(b) Kuandaa mipango ya kuendeleza Mji Mkuu na kuiwasilisha kwa Rais ili ipitishwe kwa utekelezaji.
c) Kufanya uendelezaji utakaowezesha Dodoma kuwa Mji Mkuu wa Nchi.
(d) Kushauri na kuisaidia Serikali namna nzuri ya kutekeleza azma ya kuhamia Dodoma.
(e) Kutwaa na kumiliki ardhi na mali zisizohamishika kwa maelekezo ya Rais.
(f) Kutoa huduma kwa idara na taasisi kwa kadri zitakavyohitaji katika zoezi la kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Juni, 2013 hadi Mei, 2014, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu ilitekeleza miradi ifuatayo:-

(i) **Ujenzi wa Miundombinu**

Mamlaka ya ustawishaji Makao Makuu imeweza kujenga barabara kwa kiwango cha lami pamoja na kuchonga barabara za vumbi katika eneo la mradi ili kufikisha huduma za jamii katika eneo la mradi.

(ii) **Mipango Kuhusu Uendelezaji wa Ardhi**

Katika juhudi za kuendeleza ardhi Mamlaka imefanya mapitio ya mpango kabambe wa eneo la Mji Mkuu. Mpango huo umepitishwa na Kamati Maalum ya Mipango katika eneo la Mji Mkuu na taratibu za kisheria za kutangaza katika gazeti la Serikali zinaendelea kufanyiwa kazi. Mpango huo unahusisha ujenzi wa mji wa Serikali utakaokuwa na ofisi, nyumba za viongozi na huduma muhimu za kijamii kwa viongozi na watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu yaliyotekelezwa na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu, zipo changamoto tano zilizojitokeza kama ifuatavyo:-

(i) **Kukosekana kwa utashi wa Serikali**

Uamuzi wa kuhamisha Makao Makuu toka Dar es Salaam kuja Dodoma ulifanyika toka mwaka 1973, ambapo hadi sasa ni miaka 42 imepita. Kamati haioni juhudi za kutosha za Serikali za kuhamishia Makao Makuu ya Nchi Dodoma. Hii ni kutokana na Serikali kuendelea kujenga Ofisi na Nyumba nyingi za Serikali kwa gharama kubwa Jijini Dar es Salaam wakati Miradi ya Ustawishaji Makao Makuu ikiendelea kusuasua.

(ii) **Ufinyu wa bajeti**

Mamlaka imekuwa ikitengewa fedha kidogo ikilinganishwa na fedha zinazoombwa wakati wa makadirio ya bajeti kwa mwaka husika. Aidha, fedha kidogo zinazotengwa huwa hazitolewi kwa kiasi kilichoidhinishwa jambo linaloathiri utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Mamlaka.

(iii) **Uwepo wa vijiji vilivyosajiliwa katika eneo la mpango (Capital City District**)

Katika eneo la mpango wa uendelezaji wa Makao Makuu, kuna vijiji vilivyosajiliwa na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na vina mipaka inayotambulika kisheria. Suala hili limekuwa changamoto kwa Mamlaka kwa kuwa pale inapotaka kufanya upangaji wa mji, hulazimika kuingilia mipaka ya vijiji na hivyo kuzua migogoro kati ya mamlaka na vijiji hivyo.

(iv) **Uvamizi wa maeneo**

Maeneo ya Mamlaka yaliyopimwa na yasiyopimwa yamekuwa yakivamiwa mara kwa mara na wananchi ili kuyaendeleza kwa kufanya ujenzi holela au kuyauza kwa watu wengine.

(v) **Ukosefu wa Miundombinu**

Baadhi ya maeneo ya mradi hayana miundombinu muhimu kama barabara katika maeneo yaliyopimwa.

2.3 **Utekelezaji wa TASAF awamu ya Tatu**

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilitembelea mfuko wa Hifadhi ya Jamii (TASAF) Makao Makuu mnamo mwezi Mei, 2014 na kupokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya TASAF awamu ya tatu. Katika taarifa hiyo, Kamati ilielezwa kuwa TASAF imeanza kutekeleza mradi wa kuinua kaya maskini sana uliozinduliwa mwaka 2013. Mradi huo unalenga kuwapatia ruzuku ya fedha kaya maskini sana ili kuziinua kiuchumi kwa lengo la kuziwezesha kumudu gharama za mahitaji muhimu ya kibinadamu kama vile chakula, afya na elimu kwa kaya hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mpango huu kaya maskini katika Mamlaka za Utekelezaji 113 za Halmashauri ya Jiji, Miji, Manispaa, Wilaya, Kata, Vijiji na Shehia zipatazo 761,630 zilitambuliwa, kuidhinishwa na kupitishwa katika Mikutano Mikuu Maalum ya Jiji, Mitaa, na Shehia kwa kuzingatia vigezo maalum vya umaskini. Baada ya utambuzi wa kaya maskini

sana jumla ya shilingi bilioni 31 zimelipwa kama ruzuku kwa Kaya 266,601 katika halmashauri 41 nchini.

Mheshimiwa Spika, Mchakato wa utambuzi wa kaya Maskini sana unaendelea katika maeneo mengine ya utekelezaji 48 yenye Vijiji, Mitaa, Shehia 3,160 katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Rukwa, Tabora, Kigoma, Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa kunusuru kaya maskini unahusisha pia kutoa ajira ya muda kwa walengwa ambapo walengwa hufanya kazi kwa muda wa siku 15 katika kipindi chenye njaa. Kupitia ajira hizo walengwa hulipwa kiasi cha Tshs. 2,300 kwa siku sawa na Tshs. 138,000/= kwa kipindi cha miezi minne ambayo mradi umekusudiwa. Miradi ya kutoa ajira imeanza katika maeneo ya Kibaha, Chamwino, Bagamoyo, Manispaa ya Mtwara, Lindi, Unguja na Pemba.

Changamoto za Utekelezaji wa TASAF Awamu ya III

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mafanikio ya Mradi wa TASAF, Mradi huu umekabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Upungufu wa Rasilimali Fedha.

(ii) Upungufu wa Ofisi kwa Watumishi hali ambayo imeilazimu TASAF kukarabati jengo lililokuwa linatumiwa na Kampuni ya Saruji ili litumike kama Ofisi.

(iii) Vigezo vya Utambuzi wa kaya maskini sana kutokueleweka vizuri miongoni mwa walengwa jambo linalopelekea malalamiko kwa baadhi ya wananchi kuwa baadhi ya wanufaika hawastahili kuitwa maskini sana.

(iv) Baadhi ya watu wenye vigezo vya kuitwa maskni sana wameachwa katika mradi huo.

2.4 **Ukarabati wa Ikulu Ndogo ya Chamwino**

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 15 Juni, 2014 Kamati ilitembelea mradi wa ukarabati wa Ikulu Ndogo ya Chamwino ili kujionea hatua ziliyofikiwa katika ukarabati huo. Ikulu Ndogo ya Chamwino ilijengwa miaka ya 1970's hivyo imekuwa na majengo yaliyochakaa sana. Ikulu hii inajumuisha majengo yafuatayo:-

(a) Makazi ya Mheshimiwa Rais
(b) Ofisi ya Mheshimiwa Rais
(c) Jengo la Mapokezi
(d) Majengo ya Wageni wa Ikulu (Guest Wing)
(e) Majengo ya Ofisi – House Keeper, Stores, Generator House na jengo la askari wa FFU
(f) Jengo la Auditorium na
(g) Nyumba za viongozi wanaoambatana na msafara wa Mheshimiwa Rais, (nyumba 10) na nyumba za watumishi wa Ikulu Ndogo ya Chamwino.

Mheshimiwa Spika, Ikulu hii kwa mara ya mwisho ilifanyiwa ukarabati mkubwa kwa baadhi ya majengo katika mwaka wa fedha 2010/2011 ambayo ni Jengo la makazi ya Rais, Jengo la Ofisi ya Rais na Jengo la Mapokezi. Majengo ambayo hayakufanyiwa ukarabati yako katika hali mbaya sana ya uchakavu na hayafai kabisa kutumika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea Ikulu Ndogo ya Chamwino ilijionea changamoto zifuatazo:-

(a) **Ufinyu wa bajeti**

Fungu linalotengwa kwa ajili ya ukarabati wa Ikulu limekuwa likitengewa fedha kidogo na isiyokidhi mahitaji ya kazi hiyo. Hali hiyo imepelekea baadhi ya majengo ya Ikulu yaliyopo nje ya Dar es salaam kutokarabatiwa kwa wakati ikiwemo Ikulu ndogo ya Chamwino. Ikulu Ndogo ya Chamwino ina uchakavu wa majengo unaotokana na kuwa ya muda mrefu hivyo kuyafanya yahatarishe usalama wa viongozi na kushusha hadhi na heshima ya Ofisi hiyo.

Aidha, pale ambapo fedha ya ukarabati inakuwa

imetengwa katika Mwaka husika wa bajeti, fedha hizo hazitolewi kwa wakati na wakati mwingine hazitolewi kabisa hali inayoathiri utekelezaji wa mipango ya ukarabati wa majengo hayo.

(b) **Upungufu wa maji**

Tanki la maji lililojengwa kwa ajili ya kuhifadhia maji ni dogo sana kwani lilijengwa ili kukidhi mahitaji ya wakazi wachache waliokuwa wanazunguka eneo hilo. Idadi hiyo kwa sasa imeongezeka ikilinganishwa na idadi ya wakati huo hivyo kufanya tanki hilo kutokutosheleza mahitaji.

Aidha, kutokana na shughuli za binadamu, kumekuwa na uharibifu katika chanzo cha maji hivyo, kuathiri upatikanaji wa maji kwenye chanzo hicho na kusababisha uhaba wa maji Ikulu na wananchi wanaozunguka eneo hilo.

2.5 **Uimarishaji wa Mahakama Nchini**

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Mei, 2014 Kamati yangu ilitembelea Mahakama ya Tanzania na kukutana na Jaji Mkuu wa Tanzania Mheshimiwa Othman M. Chande pamoja na watendaji wengine wa mahakama na kupokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Mahakama Nchini. Katika taarifa hiyo Kamati iliezwa yafuatavyo:-

(i) **Ujenzi wa Mahakama**

Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Mahakama inaendelea na mchakato wa kuanza ujenzi wa majengo ya mahakama katika ngazi mbalimbali nchini kama ifuatavyo:-

(a) Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama Jijini Dar es salaam.

(b) Mahakama Kuu katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Kigoma, Mara, Singida, Morogoro, Manyara, Shinyanga na Dodoma.

(c) Ujenzi wa Mahakama za Wilaya katika Wilaya za Bunda, Bariadi, Nkasi, Bukombe, Bagamoyo na Kilindi.

(d) Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo katika maeneo ya Buguruni, Kawe, Kigamboni, Makuyuni, Mailimoja, Songea, Mpanda, Terrati, Mtowisa, Sangabuye, Ilolanguru, Mwanga, Mangaka, Makongorosi, Itigi, Machame, Mkomazi, Gairo, Kiagata, Lukuledi, Longido, Ngorongoro, Kilekero, Magoma na Bomang'ombe.

(ii) **Uendeshaji wa shughuli za Mahakama**

Kamati yangu imekuwa ikitoa ushauri kwa Serikali kuhusu kuboresha Muhimili wa Mahakama ili uweze kutekeleza jukumu lake kikamilifu. Miongoni mwa mambo ambayo Kamati yangu ilishauri ni pamoja na kuimarisha muundo mpya wa Utawala wa Mahakama ambao utatenganisha shughuli za kiutawala na za kimahakama. Nafurahi kulijulisha Bunge kuwa Serikali ilitekeleza ushauri kwa kuanzisha muundo mpya wa Mahakama kupitia sheria Na. 4 ya 2011 (***The Judicial Administration Act***).

Mheshimiwa Spika, Katika sheria hiyo, ulianzishwa mfuko wa Mahakama wenye lengo la kuwezesha uendeshaji wa Mahakama katika ngazi zote na kuboresha mfumo wa usikilizaji wa mashauri nchini. Kutokana na kuanzishwa kwa mfumo huo, Bajeti ya Mahakama iliongezeka toka shilingi bilioni 20 kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 na kufikia zaidi ya shilingi bilioni 166 kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Ongezeko hili limewezesha kuboresha utendaji wa Mahakama kwa kuongeza usikilizaji wa mashauri na idadi ya vikao vya Mahakama.

Changamoto

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada nzuri ikiwemo mipango kabambe ya Mahakama kuboresha mfumo wa utoaji haki nchini, Muhimili huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(a) **Ufinyu wa Bajeti**

Pamoja na kutambua ongezeko kubwa la bajeti katika mfuko wa Mahakama, kumeendelea kuwa na upungufu wa fedha kwani fedha zinazotengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha husika zimekuwa hazitolewe zote na

kwa wakati. Hali hii inasababisha Mahakama kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(b) **Upungufu wa vitendea kazi na Rasilimali Watu.**

Mheshimiwa Spika, katika Muhimili wa Mahakama changamoto ya upungufu wa vitendea kazi na rasilimali watu ni kubwa hasa ukizingatia mazingira ya sasa ambapo uhalifu na uelewa wa sheria umeongezeka miongoni mwa wananchi hivyo, uhitaji wa matumizi ya chombo hiki nao umeongezeka. Uhitaji huo ni mkubwa kuliko idadi ya watumishi waliopo na uwepo na ubora wa vitendea kazi vilivyopo, hali inayoathiri juhudi za mahakama za kutoa haki sawa kwa wote na kwa wakati.

(c) **Mmomonyoko wa maadili**

Mheshimiwa Spika, katika Muhimili wa Mahakama kumekuwepo na mmomonyoko wa maadili kwa baadhi ya watumishi ambao wanaoshughulikia utoaji haki katika Muhimili huo. Baadhi ya viashiria vya mmomonyoko huo ni pamoja na vitendo vya rushwa.

2.6 **Upokeaji na Uchambuzi wa Bajeti**

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Machi hadi Juni 2014, Kamati ilikutana na Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali zilizo chini yake katika Ofisi Ndogo ya Bunge Dar es Salaam kwa lengo la kupokea taarifa ya utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na kupokea Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa za utekelezaji wa majukumu kwa Wizara zilizo chini yake Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka 2014/2015, ambapo maoni kuhusu Uchambuzi wa bajeti ya Wizara, Taasisi, Idara na Wakala wa Serikali yameainishwa katika sehemu za taarifa za Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Taasisi Idara na Wakala hizo kwa mwaka wa Fedha 2014/2015.

2.7 **UCHAMBUZI WA MISWADA YA SHERIA**

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015 Kamati yangu ilipata fursa ya kuchambua Miswada mitatu ya Sheria ya Serikali ambayo Mheshimiwa Spika ulielekeza ifanyiwe kazi na Kamati kama ifuatayo**:-**

(a) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (The Written Laws Miscellaneous Amendments Act), 2014.

(b) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.2) Act), 2014.

(c) Muswada wa sheria ya Maafa. (The Disaster Management Act), 2014

Mheshimiwa Spika, Katika kufanya uchambuzi wa miswada hiyo Kamati ilihakikisha kuwa wadau wanashirikishwa ipasavyo ili kuhakikisha kuwa maoni yao yanazingatiwa ipasavyo katika mchakato wa utungaji wa sheria. Maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali (The written Laws Miscellaneous Amendments Act, 2014 yaliwasilishwa katika mkutano wa 16 na 17 ya bunge lako tukufu

(d) Taarifa kuhusu maoni ya Kamati kufuatia uchambuzi wa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.2) Act), 2014 utawasilishwa katika mkutano huu wa Bunge lako tukufu.

2.8 **Mapambano dhidi ya Rushwa Nchini**

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Mei, 2014 Kamati yangu ilitembelea Ofisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini ili kujionea utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hiyo. Katika ziara hiyo Kamati ilielezwa kuwa Serikali imeendelea kuimarisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini ili kuimarisha Utawala Bora kwa maendeleo ya Taifa letu.

Katika jitihada hizo Serikali imeweza kuiimarisha Taasisi kama ifuatavyo:-

(i) **Ujenzi wa Jengo la Ofisi.**

Ili kuepukana na adha ya kupanga, Serikali iliipatia fedha Taasisi hii kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi yake iliyoko Upanga, Jijini Dar es Salaam.

(ii) **Rasilimali Watu**

Taasisi hii imekuwa ikikabiliwa na upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali na hivyo kuathiri utendaji na ufanisi. Kupitia jitihada za Kamati yangu katika kuishauri Serikali kuboresha Taasisi hii, Serikali ilitoa kibali cha kuajiri watumishi 400 katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 wa kada mbalimbali kwa lengo la kuimarisha Taasisi na watumishi hao wamekwisha anza kazi.

(iii) **Vitendea Kazi**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imepatiwa vifaa vya kisasa na maabara inayowezesha kufanya uchunguzi wa tuhuma za makosa ya Rushwa kwa urahisi.

Changamoto

Katika kutekeleza Majukumu yake, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) **Upungufu wa Fedha**

Taasisi hii imekuwa ikitengewa fedha kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi iliyonayo. Hali ya ufinyu wa bajeti inaathiri utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi hii muhimu kwa nchi yetu katika kuimarisha utawala bora.

(ii) **Ulazima wa kupata kibali kutoka kwa Mwendesha Mashaka Nchini**.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inalazimika kuomba kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini kwa makosa yote makubwa ya Rushwa.

Jambo hili limekuwa likidhohofisha juhudi za Taasisi katika mapambano ya Rushwa kwani vibali huchelewa kutolewa na wakati mwingine havitolewi kabisa. Gharama nyingi za Serikali zimekuwa zikitumika katika kufanya uchunguzi wa tuhuma za rushwa lakini majalada yanapowasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini mengi yao hayatolewi vibali na kuachwa kwa kigezo cha kutokuwa na ushahidi wa kutosha jambo linaloisababishia hasara Serikali.

Aidha katika kipindi cha kuanzia julai 2014 hadi Januari 2015 taasisi hii imechunguza majalada 3014 ya rushwa na kati ya hayo, Takukuru imefungua kesi 108 Mahakamani.

Idadi hii kubwa ya majalada yanayochunguzwa ni kielelezo cha nchi yetu kuchukia rushwa na kuchukua hatua stahiki kwa wale wanaothibitika kujihusisha na vitendo vya rushwa.

2.9 **ZIARA YA KIMAFUNZO NCHINI UINGEREZA**

Mheshimiwa Spika, Ofisi yako imekuwa na utaratibu wa kawaida wa kuwajengea uwezo wabunge kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kutokana na jukumu kubwa la kikatiba la kuwawakilisha Wananchi. Ili kufanikisha lengo hilo, Ofisi yako imekuwa ikiandaa semina, Warsha, Makongamano na Ziara za ndani na nje ya nchi ili kutimiza azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya hivyo, kati ya tarehe 8-15 Novemba, 2014 Kamati yangu ilifanya ziara ya kimafunzo nje ya nchi ambapo ilitembelea nchi ya Uingereza kwa lengo la kuongeza ujuzi na weledi kwa wajumbe wa Kamati kuhusiana na masuala ya kupambana na rushwa ili watumie ujuzi huo katika kuishauri Serikali namna bora ya kuimarisha mapambano ya Rushwa nchini ikiwemo kuimarisha Taasisi ya kuzuia na kupambana na Rushwa Nchini.

Mheshimiwa Spika, ziara ya Kamati nchini Uingereza iligharamiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (**PCCB**) ambayo inasimamiwa na Kamati yangu kwa

kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Uingereza Tawi la Tanzania (DFID).

Mheshimiwa Spika, Kamati ikiwa Nchini Uingereza ilitembelea ofisi ya Mamlaka ya Mwendesha Mashtaka wa umma (The Crown Prosecution Service) na taasisi ya Kupambana na Makosa ya Udanganyifu mkubwa (Serious Fraud Office) pamoja na kukutana na Kamati ya Haki (Justice Committee) ya Bunge la Uingereza inayofanya kazi zinazofanana na kazi za Kamati yangu.

2.9.1 **MAFUNZO AMBAYO KAMATI ILIYOPATA KATIKA ZIARA**

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo kamati ilikutana na taasisi tatu tofauti na kujifunza mambo mbalimbali. Taasisi na mafunzo hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) **Kikao na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya kupambana na Makosa ya Udanganyifu Mkubwa (Serious Fraud Office)**

kutokana na kikao na Mkurugenzi Mkuu na Watendaji wengine wa ofisi hii, Kamati ilijifunza mambo yafuatayo:-

(i) Taasisi hii imepewa jukumu la kuchunguza makosa ya udanganyifu mkubwa na yenye athari kubwa za kiuchumi na kijamii yanayofanywa na watu au kampuni za kiingereza katika mahusiano ya kibiashara baina ya kampuni moja na nyingine nchini au kampuni ya Uiingereza inayofanya biashara zake katika nchi nyingine tofauti na nchini kwetu ambapo taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inachunguza makosa yote ya Rushwa yaani makubwa na madogo.

(ii) Taasisi ya Kupambana na Makosa ya udanganyifu Mkubwa (Serious Fraud Office) ni taasisi yenye mamlaka kamili na huru inayochunguza na kuendesha Mashtaka katika makosa makubwa ya udanganyifu na Rushwa bila kulazimika kuomba kibali kutoka kwa Mwendesha Mashtaka wa Serikali, tofauti na mfumo wa nchi yetu ambapo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inalazimika kuomba kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka nchini pale ambapo inahitaji kufungua mashtaka dhidi ya watuhumiwa wa makosa makubwa ya rushwa.

(iii) Taasisi hii imejengewa uwezo mkubwa kwa kuipa rasilimali watu, fedha na nyenzo za kisasa za kufanyia kazi ambapo ina Wafanyakazi 300 wenye ujuzi wa hali ya juu katika fani za Sheria, uchunguzi, na uhasibu. Aidha, taasisi ina Ofisi za kisasa zenye nyenzo za kisasa zinaiwezesha ofisi kufanya uchunguzi wa tuhuma mbalimbali kuhusu makosa ya jinai mapema na kufungua mashtaka mahakamani.

(iv) Katika kutekeleza majukumu yake, Taasisi ya kupambana na Makosa ya Udanganyifu Mkubwa inafanya kazi kwa ushirikiano Mkubwa na taasisi zingine zinazohusika na usimamizi wa makosa ya jinai kama Ofisi ya taasisi ya Mwendesha Mashtaka ya umma (The National prosecution Service), Polisi ya Uingereza (The London Metropolitan Police) na Polisi wa London (The London Police)

(b) **Kikao na Kamati ya Bunge ya Haki (Justice Committee)**

Kamati ya Bunge ya Haki ya Uingereza ambayo inafanya kazi sawa na Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala haiingilii utendaji wa siku kwa siku wa Taasisi za kiserikali za kuzuia na kupambana na Rushwa badala yake inaweza kumuuliza maswali Mwanasheria Mkuu wa serikali Bungeni kuhusiana na utendaji wa taasisi hizo.

(c) **Kikao na Mkurugenzi wa Taasisi, Ofisi ya mwendesha mashtaka ya umma wa Serikali (The Crown Prosecution Service)**

Mheshimiwa Spika, Katika taasisi hiyo Kamati yangu ilijifunza mambo yafuatayo:-

(i) Ofisi hii inashughulikia makosa ya rushwa ambayo hayajafikia kiwango cha kushughulikiwa na taasisi ya kupambana na makosa ya udanganyifu mkubwa tofauti na mfumo wa Nchi yetu ambapo makosa yote ya rushwa bila kujali ukubwa wa kosa yanashughulikiwa na Taasisi ya kuzuia na Kupambana na rushwa (TAKUKURU).

(ii) Pamoja na taasisi ya Kupambana na makosa

ya udanganyifu mkubwa na taasisi ya Mwendesha mashtaka ya umma zipo Ofisi nyingine zinazoshughulikia makosa ya rushwa kutegemeana na mazingira ya kosa lenyewe. Ofisi hizo ni: polisi wa London (The London Police) na Polisi ya Uingereza (The London Metropolitan Police).

(iii) Taasisi hii imejengewa uwezo mkubwa kwa kuipa rasilimali watu wenye ujuzi wa hali ya juu, bajeti ya kutosha na nyenzo za kisasa za kufanyia kazi, hivyo kuifanya Ofisi hii itekeleze majukumu yake kikamilifu.

2.10 **ZIARA YA KAMATI NCHINI MEXICO**

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (TASAF) katika kutekeleza mradi wake wa awamu ya tatu wa kutoa ruzuku kwa kaya maskini sana, iliamua kujenga uelewa wa pamoja kwa wabunge ambao ni wawakilishi wa wanchi kwa kuandaa ziara ya mafuzo katika nchi inayotekeleza mradi unaofanana na huo. Katika kutekeleza uamuzi huo mwezi januari, 2014 Kamati ilifanya ziara ya mafunzo nje ya nchi ambapo ilitembelea nchi ya Mexico kwa ufadhili wa TASAF na kujiona jinsi ya mradi wa kuinua Kaya maskini sana kupitia mradi kama wa TASAF katika nchi hiyo. Kamati ililelezwa jinsi kaya maskini sana zilivyofaidika kwa kupewa fedha za shule, matibabu na kutoa mitaji ya biashara kwa vikundi vya kina mama.

Kufuatia mafunzo hayo Kamati inaona kuwa mfumo wa uendeshaji mradi kama unaofanywa na TASAF awamu ya tatu nchini Mexico ni wa kuigwa ili kuboresha utendaji wa mfuko huo hapa nchini kwa usatawi wa taifa letu.

3.0 **MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

3.1 Ziara za ukaguzi wa miradi ya Maendeleo

(a) **Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Waziri Mkuu Dodoma**

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi na makazi ya Waziri Mkuu, Dodoma, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali itoe fedha zilizotengwa kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa jengo hili kwa wakati ili kuharakisha ukamilishwaji wake na kuepuka uwezekano wa kuongezeka kwa gharama za ujenzi kutokana na kuchukua muda mrefu wa kukamilika kwake.

(b) **Utekelezaji wa miradi ya Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma**

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ibuni vyanzo mbadala vya mapato ili kuwezesha kutengwa kwa fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa miradi mbalimbali inayotekelezwa na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu ili kufikia azma ya Kuhamisha Makao Makuu kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma.

(ii) Serikali iangalie uwezekano wa kufuta vijiji vilivyomo ndani ya eneo la mradi bila kuathiri haki za wananchi wanaomiliki maeneo hayo ili kuepusha migongano na migogoro inayojitokeza katika kuendeleza Makao Makuu Dodoma.

(iii) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi wakiwemo viongozi wa kisiasa juu ya umuhimu wa mipango miji na taratibu za umiliki wa ardhi. Elimu hiyo itasaidia kupunguza matatizo ya uvamizi wa maeneo unaofanywa na wananchi katika eneo la mradi.

(iv) Serikali iboreshe Miundombinu katika eneo la mradi ili kurahisisha upelekaji wa huduma katika maeneo ya mradi kwani baadhi ya maeneo hayafikiki kirahisi kutokana kukosekana kwa miundombinu.

(v) Kutokana na utekelezaji hafifu wa Serikali kuhamishia Makao Makuu, Dodoma Kamati ilishauri serikali itafakari upya kama kuna nia ya dhati ya kutekeleza azma hiyo.

(c) **Ukarabati wa Ikulu ndogo ya Chamwino**

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kujionea changamoto zinazoikabili Ikulu Ndogo ya Chamwino, inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ijenge utamaduni wa kukarabati majengo ya Ikulu Ndogo za Mikoani badala ya kuziacha kwa muda mrefu bila kufanya ukarabati jambo ambalo linafanya Majengo ya Ikulu hizo kuchakaa vibaya na baadhi ya majengo hayo kutishia usalama wa viongozi na watumiaji wengine wa majengo. Aidha, Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa majengo hayo. Pia fedha zinazotengwa zitolewe kwa wakati ili kuwezesha mipango ya ukarabati kutekelezwa kama inavyokuwa imekusudiwa.

(ii) Kutokana na ongezeko la watu wanaohudumiwa na maji kutoka tanki la maji la Ikulu Ndogo ya Chamwino, tanki hilo limeelemewa na kufanya maji hayo kutotosheleza mahitaji hivyo, Serikali ijenge tanki jingine jipya litakalokidhi mahitaji ya ongezeko kubwa la watu. Aidha, Serikali itafute chanzo kipya cha maji sanjari na kutunza chanzo cha maji kilichopo ili kuzuia uharibifu wa chanzo hicho unaotokana na shughuli za binadamu.

(d) **Uchambuzi wa Miswada**

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi katika shughuli za uchambuzi wa miswada, Kamati inashauri kama ifuatayo:-

(i) Kamati iwe inapewa muda wa kutosha wa kuchambua miswada ili kuiwezesha kuchambua miswada hiyo kwa kina na kuwashirikisha wadau vya kutosha kwa lengo la kutunga sheria bora.

(ii) Kasi ya kuwajengea uwezo Wabunge juu ya mchakato wa utungaji wa sheria ikiwemo uchambuzi wa Miswada iongezwe ili kuwawezesha kutekeleza jukumu hili kwa ufanisi.

(iii) Kwa kuwa ni muhimu kufanya marekebisho ya sheria za nchi yetu ili ziwe nzuri na ziweze kutumika kwa

ufanisi, Kamati inashauri serikali kutoleta sheria zinazokusudia kufanya mabadiliko makubwa ya kisera kwenye muswada wa marekebisho ya sheria mbalimbali badala yake marekebisho hayo yaletwe katika sheria mahususi inayosimamia masuala husika.

(e) **Ziara nje ya Nchi**

Mheshimiwa Spika, kuhusu ziara za kimafunzo nje ya nchi, Kamati inashauri kuwa Ofisi yako ifanye maandalizi mapema ikiwa ni pamoja na kufanya mawasiliano na balozi zetu katika nchi husika ili kuepusha usumbufu kwa Kamati na Wabunge wanapokuwa wanasafiri kwenda nje ya nchi.

(f) **Mapambano dhidi ya Rushwa Nchini**

Mheshimiwa Spika, Ili kuimarisha taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iimarishe Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa iimarishwe kwa kuipa mamlaka kamili ya kufungua mashtaka na kuyaendesha mahakamani bila kuomba kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka nchini. Taasisi hii kwa sasa ina uwezo wa kutosha kujisimamia kwa kuwa na rasilimali watu na nyenzo za kazi tofauti na ilivyokuwa awali ambapo ilikuwa na upungufu wa rasilimali watu, ililazimu shughuli za kufungua na kuendesha mashitaka mahakamani kukasimiwa kwa Kurugenzi ya Mashitaka. Aidha kitendo cha kuomba kibali kwa Kurugenzi ya Mashitaka kinaathiri utendaji wa Taasisi kwani Taasisi inapeleleza tuhuma nyingi ambazo hatimaye hukosa kibali cha DPP kwa kigezo cha kukosa ushahidi.

(ii) Kutokana na kuongezeka kwa matukio ya rushwa nchini, Kamati inaona ni muda muafaka kwa nchi yetu kuanzisha chombo kingine kipya kitakachoshughulikia makosa madogo ya rushwa na kuachia TAKUKURU kushughulikia rushwa kubwa zenye athari kubwa za kiuchumi na kijamii.

(g) **Mfuko wa Hifadhi ya Jamii - TASAF**

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha utendaji kazi na ufanisi katika Mfuko wa Jamii TASAF, Kamati yangu inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iendelee kutenga fedha za kutosha kupitia bajeti yake ya ndani ili kufikia azma ya Mfuko huo ya kupunguza umaskini uliokithiri kwa Kaya zilizotambuliwa badala ya kutegemea fedha za wahisani ambazo hazina uhakika wa kutolewa.

(ii) Kuhusu upungufu wa Ofisi, Kamati inishauri Serikali kukamilisha mchakato wa kuimilikisha TASAF kiwanja Na. 2454/118 ili kuiwezesha TASAF kuanza ujenzi wa Ofisi zake kwa lengo la kuondokana na uhaba wa Ofisi za Watumishi.

(iii) TASAF iendelee kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu vigezo vinavyotumika katika kutambua Kaya Maskini sana na kuziidhinisha kuwa wanufaika wa mradi huo ili kuepuka malalamiko yasiyo ya lazima kutoka kwa baadhi ya wananchi.

(h) **Uimarishaji wa mahakama Nchini**

Mheshimiwa Spika, Ili kumarisha Muhimili wa mahakama Kamati inaendelea kushauri kama ifuayavyo:-

(i) Muundo mpya wa Mahakama ulioanzishwa chini ya sheria Namba 4 ya mwaka 2011(The Judicial Administration Act No.4 of 2011) uimarishwe kwa kusimamiwa kikamilifu kwa kuwa umeonyesha kuwa na tija katika utekelezaji wa majukumu ya mahakama nchini

(ii) Serikali iendelee kutenga bajeti ya kutosha ili kuiwezesha mahakama kutekeleza mipango yake kwa lengo la kuimarisha mfumo wa utoaji haki sawa kwa wote na kwa wakati nchini maslahi ya Taifa letu

4.0 **MAFANIKIO YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YAKE**

Mheshimiwa Spika, Itakumbukwa kuwa taarifa hii ya kamati inahitimisha taarifa za mwaka za utekelezaji wa majukumu kuhusu Bunge la kumi. Kwa kuwa hii ni taarifa yetu ya mwisho, niruhusu niseme machache kuhusu mafanikio

ambayo Kamati yangu imeyapata katika kuishauri na kuisimamia Serikali hususan katika Wizara, Idara,Taasisi na wakala wa Serikali zilizo chini ya Kamati. Kamati imepata mafanikio makubwa tangu kuanza kwa Bunge la kumi na baadhi ya mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) **Ushiriki wa Kamati katika mchakato wa Katiba mpya**

Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 31 Disemba, 2010 Mhemshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hotuba yake ya kuuaga mwaka na kuukaribisha mwaka mpya, alitangaza kuanza kwa mchakato wa utungwaji wa katiba mpya ambayo ingewashirikisha wananchi wengi zaidi itakayoongoza nchi yetu kwa miaka hamsini ijayo au zaidi. Ili kufanikisha zoezi hili Serikali ilileta muswada Bungeni ambao pamoja na mambo mengine ulikuwa unakusudia kuanzisha Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa ajili ya kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi kuhusu katiba mpya, kuanda rasimu ya katiba kisha kuiwasilisha kwa Rais.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Kamati yangu ilishiriki kikamilifu katika mchakato wa utungaji sheria ya mabadiliko ya Katiba, Sheria namba 8 ya mwaka 2011, sheria hii ndiyo iliyoweka utaratibu wa ukusanyaji na Uundwaji wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Ukusanyaji wa Maoni ya Wananchi, Uudwaji wa Bunge Maalum pamoja na utaratibu wa kupigia kuwa Katiba inayoependekezwa ndani ya Bunge Maalum.

Sheria hii ilifanyiwa marekebisho mara nne kwa lengo la kuiboresha ili ikidhi mahitaji. Kupitia marekebisho hayo, Sheria zifuatazo zilitungwa;

- Sheria ya Marekebisho ya Mabadilko ya Katiba Na. 2,2012
- Sheria ya Marekebisho ya Mabadilko ya Katiba Na. 7,2013
- Sheria ya Marekebisho ya Mabadilko ya Katiba Na. 9,2013
- Sheria ya Marekebisho ya Mabadilko ya Katiba

Miswada ya Sheria zote hizo ilipita kwanza katika kamati yangu ambapo Kamati ilifanya kazi ya kupokea maoni ya Wadau, kuchambua na hatimaye kutoa maoni katika Bunge lako tukufu ili kulisaidia Bunge namna ya kuiboresha miswada husika ili kupata Sheria nzuri. Ni kupitia Sheria nilizotajwa ndizo zilizotumika kuliongoza Bunge Maalum la Katiba ambalo limetupatia Katiba Inayopendekezwa na inayosubiri hatua ya Mwisho ya kupigiwa kura ya maoni ifikapo Aprili 30, 2015.

(b) **Serikali kuondokana na utaratibu wa kupanga Ofisi**

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imekuwa ikiishauri Serikali kupitia Wizara zilizo chini yake kujenga majengo yake yenyewe ili kuepuka gharama zinazotokana na kupanga Ofisi. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kutokana na Ushauri wa Kamati, taasisi zifuatazo zimejenga ofisi zake na hivyo kuondokana na utaratibu wa kupanga

(i) Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Registration, Insolvency and Trusteeship) ambao wamekamilisha ujenzi wa Jengo la Ofisi yao lenye urefu wa ghorofa 33 lililopo Mtaa wa Makunganya Jijini Dar es Salaam.

(ii) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini (The Prevention and Combating of Corruption Bureau) imejenga jengo la Ofisi yake Upanga Jijini Dar es Salaam.

(iii) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaendelea na Ujenzi wa Jengo lake la Ofisi Kanda ya Mtwara

5.0 **HITIMISHO**

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha taarifa ya Mwaka ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Napenda nitumie nafasi hii pia kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu. Napenda kukiri kuwa katika kipindi chote cha uongozi wako umekuwa imara kuhakikisha

kuwa misingi ya uongozi na utawala bora inafuatwa katika taasisi ya Bunge ili kulifanya litekeleze kikamilifu jukumu lake la msingi la kuwawakilisha wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Napenda kumpongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukupa ushirikiano wa dhati katika kutekeleza majukumu yako ya kuliongoza Bunge hili. Aidha, nawashukuru wenyeweviti wote wa Bunge kwa ushirikiano mzuri walioutoa kwa Bunge na kipekee kwa Kamati yangu ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nawashukuru wajumbe wa Kamati, kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuisimamia na kuishauri Serikali katika maeneo mbalimbali ya kiutekelezaji katika taasisi za Serikali. Ushauri ambao wamekuwa wakiutoa umekuwa na manufaa makubwa kwa Bunge lako tukufu na kwa taifa kwa ujumla. Umahiri na uzoefu wa muda mrefu katika masuala ya sheria, utawala na sekta nyingine mbalimbali ndio uliofanikisha kazi hii. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

(i) Mhe. Jasson S. Rweikiza, Mb - Mwenyekiti
(ii) Mhe.Gosbert B.Blandes, Mb - M/Mwenyekiti
(iii) Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu, Mb - Mjumbe
(iv) Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb - Mjumbe
(v) Mhe. Nimrod Elirehema Mkono, Mb- Mjumbe
(vi) Mhe. Halima J. Mdee, Mb - Mjumbe
(vii) Mhe. Fakharia K. Shomar, Mb - Mjumbe
(viii) Mhe. Rukia Kassim Ahmed, Mb - Mjumbe
(ix) Mhe. Ali Khamis Seif, Mb - Mjumbe
(x) Mhe. Felix Francis Mkosamali, Mb - Mjumbe
(xi) Mhe.Abdallah Sharia Ameir, Mb - Mjumbe
(xii) Mhe. Mustapha B. Akunaay, Mb - Mjumbe
(xiii) Mhe. Mariam Reuben Kasembe, Mb- Mjumbe
(xiv) Mhe. Tundu A. Mughwai Lissu, Mb- Mjumbe
(xv) Mhe. Deogratias A. Ntukamazina, Mb- Mjumbe
(xvi) Mhe. William M. Ngeleja, Mb - Mjumbe
(xvii) Mhe. Nyambari C. M. Nyangwine, Mb- Mjumbe
(xviii) Mhe. Ramadhan Haji Saleh, Mb - Mjumbe

(xix) Mhe. Zahra Ali Hamad, Mb - Mjumbe
(xx) Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb - Mjumbe
(xxi) Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mb - Mjumbe

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru ndugu Charles Mloka Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndugu Athumani Hussein, Naibu Mkurugenzi, Ndugu Maria Mdulugu na Matamus Fungo, Makatibu wa Kamati kwa kuratibu vyema kazi za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba kutoa hoja.

Mhe. Jasson S. Rweikiza, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA
FEBRUARI, 2015

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa au Mwakilishi wake. *What is it;* hakuna Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo? AAh, mnatakiwa muwe mnasogea huku bwana kusiwe na *wastage of time*. Wote wanaowasilisha wasogee huku.

(Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kama ilivyosomwa Bungeni)

MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuanzia Janauri 2014 hadi Januari 2015.

Kwanza, ninampa pole Dkt. Kigwangalla, kwa kumpeleka kwenye matibabu mzee wetu kule India,

Mwenyezi Mungu ampe afueni warudi salama.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 na kwa niaba ya Wajumbe 17 nikiwemo mimi Injinia Mfutakamba, Mbunge wa Igalula, wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati kwa kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari 2015.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ninaomba iingizwe yote kwenye kumbukumbu za Bunge, yaani Hansard.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kama ilivyo kwa Kamati nyingine za Bunge, imeundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 116 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Ninaomba kuchukua fursa hii pia kwa unyenyekevu, kuwashukuru Wajumbe wenzangu kwa kuniamini kuisoma Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, misingi ya majukumu ya Kamati hii inatokana na Ibara ya 63(2) na (3) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inayotoa madaraka kwa Bunge kuwa Chombo Kikuu cha Jamhuri ya Muungano chenye madaraka kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya TAMISEMI, ikiwa ni moja kati ya Kamati za Bunge za Kisekta, ina majukumu yafuatayo kwa mujibu wa Kanuni ya 7(1) katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 7(2)(c)(ii) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati hii imepewa jukumu mahususi la kuchambua Sheria Ndogo zilizotungwa na Halmashauri za Miji, Wilaya, Manispaa na Majiji ili kujiridhisha iwapo sheria ndogo hizo zimekidhi matakwa ya masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria

nyingine za nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii pia ina jukumu la usimamizi wa kiutendaji kwa Taasisi zifuatazo zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

(a) Shirika la Elimu Kibaha.

(b) Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa *(LAPF)*.

(c) Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa.

(d) Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo *(LGTI)*.

(e) Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (*DART*).

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Kamati kuanzia Januari 2014 hadi Januari 2015; Kamati ya Bunge ya TAMISEMI, kwa kuzingatia msingi wa majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni na kwa kuzingatia namna bora ya uendeshaji wa Bunge na Kamati zake, iliazimia kutekeleza shughuli zifuatazo kati ya Januari, 2014 na Januari, 2015:-

(a) Kushiriki semina za ndani na nje kwa madhumuni ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi;

(b) Kushughulikia Bajeti ya Serikali;

(c) Kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo;

(d) Kupokea taarifa mbalimbali za utekelezaji kutoka OWM (TAMISEMI) na taasisi zilizo chini yake;

(e) Kufanya ziara ya mafunzo nje ya nchi; na

(f) Kufanya ziara za ukaguzi na tathmini ya Miradi

mbalimbali iliyotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Taasisi zake, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mwaka huu Wabunge walikuwa sehemu ya Bunge Maalum la Katiba pamoja na sababu nyingine, baadhi ya shughuli zilizoainishwa hapo juu hazikuweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, shughuli zifuatazo zilitekelezwa na Kamati kuanzia Januari, 2014 hadi Januari 2015:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari 2014 hadi Januari 2015, Kamati yangu ilipokea na kufanya uchambuzi wa taarifa zifuatazo:-

Taarifa ya Utekelezaji ya Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa *(LGRP II D By D)* kwa Kipindi cha 2009 – 2014. Tarehe 30 Oktoba, 2014, Kamati yangu ilipokea taarifa ya Utekelezaji wa Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa *(LGRP II D By D)* kwa Kipindi cha 2009 – 2014. Kamati ilielezwa kwamba, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, imekuwa ikitekeleza Sera ya Kupeleka Madaraka kwa Wananchi *(Decentralization by Devolution),* maarufu kama *D by D* kupitia Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Programu hii ambayo imekuwa ikipata fedha kutoka kwa Wadau wa Maendeleo, pamoja na kwamba ni muhimu kwa madhumuni ya kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa, bado haijakidhi kiu ya Watanzania wa kawaida kuona umuhimu wa Serikali za Mitaa katika kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam *(DART)*.

Tarehe 31 Aprili, 2014, Kamati hii ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka *(DART)* kutoka kwa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka *(DART)*. Katika Taarifa hiyo, Kamati ilitaarifiwa kwamba Mradi

umesanifiwa kujengwa katika awamu sita zenye urefu wa takribani kilometa 130.3 katika barabara za Morogoro, Kilwa, Nyerere, Bagamoyo, Mandela, Mwai Kibaki na barabara nyingine zitakazochaguliwa baadaye.

Taarifa hiyo ilieleza kwamba, Wakala unatarajia kujenga vituo vikuu 18 na vituo vidogo 228 katika awamu zote sita. Hadi kufikia wakati taarifa hiyo inawasilishwa kwa Kamati, awamu ya kwanza ilikuwa katika hatua za mwisho za ujenzi na kwamba kufikia Disemba, 2014, usanifu wa awamu ya pili na ya tatu ungekuwa umekamilika.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika kwa Serikali kuhakikisha kuwa, changamoto ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam, hususan kwa makundi ya wakazi wa Jiji hilo wenye kipato cha chini na cha kati, inapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Aidha, msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam ni kero kubwa kwa wakazi na wageni wa Jiji hilo na kwa sehemu kubwa unakwamisha maendeleo na upatikanaji wa huduma muhimu.

Taifa linapata hasara kubwa kiuchumi ambapo inakadiriwa kwamba, kiasi cha shilingi bilioni nne hupotea kwa siku kutokana na msongamano huo kwa sababu ya hasara itokanayo na upotevu wa mafuta ya magari yanayotumia muda mrefu katika foleni na kupotea kwa muda unaoweza kutumika kwa nguvu kazi (*loss of man hours*). Aidha, magari ambayo yanakaa muda mrefu katika foleni za Dar es Salaam, hutoa hewa ukaa kwa wingi (*emission of toxic gases*) ambazo athari yake ya hewa na afya za watu kwa ujumla ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kupongeza jitihada za Serikali kubuni Mradi huu ili kupata ufumbuzi wa changamoto ya usafiri kwa Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na Vitongoji vyake, pamoja na kupunguza msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam. Inatarajiwa kwamba, Mradi utakapokamilika, utakuwa umetatua tatizo la usafiri wa umma katika Jiji la Dar es Salaam na pia kupunguza msongamano wa magari jijini humo mpaka kufikia miaka

ya 2030/31.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya kifedha katika ujenzi wa miundombinu, ambapo inasemekana kwamba, kumekuwepo kwa ongezeko la mahitaji ya fedha za kukamilisha ujenzi huo kiasi cha shilingi bilioni 64.7. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 20.6 ni ongezeko la mishahara na shilingi bilioni 44.1 ni ongezeko la kazi na madai mengineyo. Inadaiwa kwamba, ongezeko hilo limemfanya mkandarasi kutoonesha utayari wa kuanza kazi katika Barabara ya Msimbazi kwa hofu ya kutokuwepo kwa fedha za kumlipa. Aidha, Mradi unakabiliwa na changamoto nyingine ya uharibifu wa miundombinu (*vandalism*), ambapo baadhi ya wananchi na wafanyabiashara ndogondogo huvamia maeneo ya ujenzi yanayoendelea kujengwa. Vile vile, kumekuwepo na tabia ya wizi wa samani za barabara, mifuniko ya maji ya mvua, maji taka na hujuma nyinginezo.

Kamati inaishauri Serikali kufanya jitihada za makusudi kuhakikisha kuwa Mradi huu unaendelea kutekelezwa kama ilivyopangwa na fedha yote inayohitajika kukamilisha hatua mbalimbali za Mradi huu inatengwa na kupelekwa ili kutatua hizo changamoto ili Mradi ukamilike kwa wakati. Aidha, kwa umuhimu wa Mradi huu na kwa kuzingatia ukweli kuwa Mradi huu ni kwa ajili ya matumizi ya wananchi wenyewe na pia gharama kubwa za kutekeleza Miradi ya aina hii, Kamati inawataka Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na Vitongoji vyake, kuonesha uzalendo, ustaarabu na u-Dar es Salaam wao, kwa kutambua kuwa Mradi huu ni wao, kwa matumizi yao na kwa faida yao; na hivyo basi, kutoa ushirikiano kwa Wakala, Serikali, Wanausalama na Wajenzi, ili kulinda miundombinu ya Mradi na kuwezesha miundo mbinu hii muhimu na ya gharama kubwa kudumu kwa miaka mingi na kuhudumia vizazi vijavyo. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Vyombo vya Usalama, itoe elimu na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kutunza na kulinda miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba,

Serikali iandae Mpango wa Usanifu Maalum ambao utazingatia utatuzi wa tatizo hili kwa miaka 50 hadi miaka 100 ijayo kwa kutazama maoteo ya idadi ya watu katika kukidhi mahitaji mapana ya baadaye. Sanifu za mpango huo, zizingatie uwepo wa mfumo wa njia mchanganyiko jijini (*multi-modal city transit systems*) za kutatua tatizo hili, hata kama kwa sasa tuna uwezo wa kujenga miundombinu ya mabasi yaendayo haraka tu. Aidha, kwa kuzingatia jiografia ya Jiji la Dar es Salaam, sanifu mipango hiyo iende kwa kuzingatia uwepo wa mifumo ifuatayo ya usafiri:-

(a) Usafiri wa mabasi yaendayo juu ya maji, yaani *sea buses*;

(b) Usafiri wa treni chini ya ardhi maarufu kama *Metro*;

(c) Barabara za juu katika makutano, yaani *flyovers;*

(d) Reli za umeme aina ya *trams* pamoja na nguzo zake katika miundombinu ya barabara za mjini; na

(e) Njia nyingine yoyote ya usafiri ambayo inaweza kuwemo katika mifumo hiyo.

Mheshimiwa Spika, hatua ya usanifu wa namna hii ikichukuliwa sasa, itatuokolea pesa nyingi huko mbeleni na pia itatoa fursa kwa Serikali kuongeza njia moja baada ya nyingine kwa kadiri ambavyo pesa itakuwa inapatikana na pia gesi itakuwepo gharama za usafirishaji itakuwa rahisi na bila kuathiri bajeti za fidia au kubomoa bomoa miundombinu mipya na imara inayojengwa sasa na zaidi bila kuongeza msongamano katika kipindi chote cha Mradi.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 4,978,576,426,00. Kati ya fedha hizo, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Taasisi zilizo chini yake ilipangiwa kiasi cha Shilingi 479,224,062,000

ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi 273,065,895,000 ziliombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi Mengineyo) na Shilingi bilioni 206.2 kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo.

Tawala za Mikoa na Halmashauri zake kiasi cha Shilingi Trilioni 4.2 kiliombwa ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi 3.3 ziliombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi Mengineyo), Shilingi Bilioni 458.5 ikiwa ni Mapato yatokanayo na Makusanyo na Shilingi Bilioni 748.2 ikiwa ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Tathmini pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu masuala ya Bajeti. Uandaaji wa bajeti ni sehemu muhimu katika mchakato wa kuandaa Mipango, kudhibiti na kutathmini hali ya fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa uhalisia wake, ni nia ya kugawa rasilimali ili kufikia malengo yaliyowekwa. Bajeti ni chombo kinachosaidia viongozi kupanga pamoja na kudhibiti fedha ili kuhakikisha kwamba, kwa kadiri inavyowezekana, malengo yaliyopangwa yanafikiwa.

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Bajeti; kwa wastani katika miaka michache ambayo Kamati ya Bunge ya TAMISEMI imekuwa ikichambua bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na hususan bajeti inayotengwa kwa Serikali za Mitaa, kwa sehemu kubwa kiwango kilichotengwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo kimekuwa kidogo ukilinganisha na fedha inayotengwa kwa matumizi mengineyo. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 kwa wastani asilimia 17.68 tu ndiyo ilitengwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa, fedha za Miradi ya Maendeleo zinatokana na vyanzo mbalimbali mfano Ruzuku ya Serikali Kuu, Fedha za Wahisani na pia Mapato ya Ndani ya Halmashauri husika *(Own Source)*.

Mapato ya ndani kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa

ni kiasi cha fedha ambacho kimekadiriwa na kukusanywa na Halmashauri husika kutoka katika vyanzo vyake vya ndani vilivyoainishwa ambavyo havikusanywi na Serikali Kuu. Mapato yatokanayo na vyanzo hivi ni kama ushuru wa huduma *(service levy),* ada za leseni na vibali (*fees for licences and permits)* na kodi mbalimbali. Fedha hizi hukusanywa kutoka kwa wananchi wa kawaida kabisa na makampuni yanayofanya biashara katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba, Halmashauri zote zihakikishe katika bajeti zake asilimia isiyopungua sitini itokanayo na makusanyo ya ndani *(own source),* itengwe mahususi kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwa wananchi. Msingi wa pendekezo hili ni katika kuhakikisha kuwa, mapato yatokanayo na fedha zinazokusanywa kutoka kwa wananchi wanaolipa ushuru na tozo mbalimbali, fedha hiyo ionekane kutekeleza Miradi ya Maendeleo ili kuchochea uzalishaji na kuwafanya waendelee kulipa tozo hizo bila manung'uniko.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, kwa kipindi kirefu katika Halmashauri nyingi nchini, kumekuwepo na makusanyo hafifu ya mapato ukilinganisha na bajeti iliyoidhishwa au/na makusanyo yanayoakisi uhalisia wa mapato yatokanayo na vyanzo vilivyopo katika Halmashauri hizo ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa katika vyanzo hivyo kwa sababu zifuatazo:-

(i) kukosekana kwa ufanisi wa mikakati ya ukusanyaji wa mapato kutokana na vyanzo vilivyopo;

(ii) tabia sugu ya udanganyifu katika makusanyo yanayopatikana;

(iii) makisio ya chini katika bajeti ya makusanyo ya ndani *(underbudgetting);* na

(iv) Halmashauri kutokuwa na seti kamili ya Sheria Ndogo kwa vyanzo vyote vya mapato au sheria zilizopo

kupitwa na wakati.

Halmashauri nyingi bado zinategemea vyanzo vile vile vya mapato mwaka hadi mwaka ambapo linapotokea jambo linaloathiri chanzo kimojawapo, makusanyo ya Halmashauri husika hushuka. Kwa mfano, Halmashauri ambazo zimetegemea mapato yatokanayo na kilimo, pale ambapo wakulima wanapokosa mazao ya kutosha kutokana na uharibifu utokanao na majanga kama mafuriko, mabadiliko ya tabianchi, Halmashauri hizo pia hutetereka kwa kukosa mapato.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa, ihakikishe inazisimamia kikamilifu Halmashauri ili kudhibiti na kuzuia udanganyifu katika makusanyo. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote, ifanye tathmini na upembuzi yakinifu kutambua uwepo wa vyanzo vipya vya mapato ili Halmashauri hizo ziweze kuandaa makadirio kulingana na uwezo wa ukusanyaji, lakini pia kuhakikisha kuwa, mikakati madhubuti inawekwa ili kukusanya mapato kwa ufanisi na kufikia malengo yatakayowekwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba, Halmashauri zote ambazo hazina seti kamili za sheria ndogo za ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani, watunge na kupitisha sheria hizo kwenye utaratibu uliopo na kuhakikisha zinasimamiwa kikamilifu na Halmashuri ambazo sheria zilizopo zimepitwa na wakati. Marekebisho ya sheria hizo yafanyike kulingana na hali ya kiuchumi ya eneo husika.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya Mwaka 1982 *(The Local Government Finances Act No. 9 1982)*, ikisomwa pamoja na Marekebisho yake, inazipa Halmashauri mamlaka ya kukusanya kodi ya ushuru wa huduma *(service levy)* katika maeneo yake ya kiutawala. Kiwango cha kisheria cha kodi hiyo *(statutory tax rate)* ni asilimia isiyozidi nukta tatu (0.3%) ya mapato ya

mwaka, yaani *net turnover*. Kamati inatoa mapendekezo kwamba, Halmashauri zote nchini zihakikishe zinakusanya kodi hii kikamilifu kutoka kwa makampuni na mashirika yote *(corporate entities),* ambayo yanafanya shughuli zake ndani ya Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba, Halmashauri zote nchini kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa, zihakikishe zinawashirikisha wananchi kikamilifu katika maandalizi ya bajeti zao hususan katika mipango ya maendeleo, katika kubuni vyanzo vya mapato na pia katika utungaji wa sheria ndogo za ukusanyaji wa mapato ili kurahisisha zoezi la ukusanyaji bila manung'uniko. Ushiriki wa wananchi husaidia zoezi zima la kuchangia ujenzi wa Miradi ya Maendeleo hasa pale ambapo Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa zinapokuwa zimetoa mchango wake kikamilifu katika Miradi husika.

Mapato na Matumizi ya Fedha za Ruzuku Katika Miradi ya Maendeleo: Kamati inatambua kwamba utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri zetu hauwezi kutegemea kwa asilimia kubwa vyanzo vya mapato ya ndani tu. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, baadhi ya Halmashauri zina vyanzo vichache vya mapato ukilinganisha na nyingine. Kwa sababu hiyo, Serikali Kuu hutoa ruzuku hii kuzisaidia Halmashauri katika kujenga au kukarabati miundombinu iliyopo kwa madhumuni ya kusogeza huduma kwa wananchi kama afya, elimu, maji, barabara na miundombinu hata madawa baadhi ya maeneo bado ni duni pamoja na wataalamu, ikiwepo kilimo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingine zimekuwa zikilalamika kwamba, Miradi mingi inashindwa kutekelezwa au kuchelewa kutekelezwa kwa sababu fedha iliyoidhinishwa kutekeleza Miradi hiyo huchelewa kufika katika akaunti za Halmashauri hizo kutoka Serikali Kuu (Hazina). Kamati imebaini kwamba, kumekuwepo na mwenendo unaoonesha kuwepo kwa fedha isiyotumika katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwa sababu ya ucheleweshwaji huo na wakati mwingine fedha iliyoidhinishwa hufika ikiwa pungufu au

kutofika kabisa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetoa mapendekezo mahususi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa kuimarisha mfumo wa uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya Miradi kuendelea kusimamiwa na Halmashauri ili kuhakikisha kuwa, fedha za Miradi ya Maendeleo zitokanazo na makusanyo ya ndani pamoja na zile ambazo zinatoka nje, zinatumika kuwaletea wananchi maendeleo kwa wakati na kwa viwango stahiki ili thamani ya fedha iongezeke na masuala ya *reallocation,* kubadili matumizi ya fedha, lazima utaratibu wa kifedha ufuatwe, badala ya kubadilisha matumizi kiholela tu.

Mheshimiwa Spika, tulifanya Ziara Mikoa ya Mwanza, Pwani, Lindi na Kigoma na tuliyoyabaini kule, tumeeleza kwenye taarifa yetu. Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo tumezungumzia katika Taarifa hii, katika maeneo yote tuliyotembelea, katika kipindi chote cha mwaka mzima huu, pamoja na Mwanza, Shinyanga na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa ufinyu wa muda, ninaomba maelezo yangu yote haya yawepo kwenye *Hansard*. Tumeandaa pia utaratibu wa taarifa fupi fupi. Haya ni mapendekezo ya Kamati, ambayo naamini yameshafika katika Meza yako ili yafanyiwe kazi na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya

3 FEBRUARI, 2015

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA JANUARI, 2014 HADI JANUARI, 2015

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la April, 2013 na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati kwa kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari 2015.

1.1 MUUNDO WA KAMATI

1.1.1 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kama ilivyo kwa Kamati nyingine za Bunge, imeundwa kwa mujibu wa kanuni ya 116 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, kwa kutumia mamlaka uliyopewa kwa kanuni ya 116 (3), uliwateua Wabunge wafuatao kuwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa:-

(i) Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mb – Mwenyekiti

(ii) Mhe. John Paul Lwanji, Mb – M/Mwenyekiti

(iii) Mhe. Highness Samson Kiwia, Mb – Mjumbe

(iv) Mhe. Benardetha Kasabago Mushashu, Mb – Mjumbe

(v) Mhe. Rashid Ali Abdallah, Mb - Mjumbe

(vi) Mhe. Asha Mohamed Omari, Mb – Mjumbe

(vii) Mhe. Rosweeter Faustine Kasikila, Mb – Mjumbe

(viii) Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mb – Mjumbe

(ix) Mhe. Eugen Elishiringa Mwaiposa, Mb – Mjumbe

(x) Mhe. Sabreena Hamza Sungura, Mb – Mjumbe

(xi) Mhe. Eng. Dkt. Athuman Rashid Mfutakamba, Mb – Mjumbe

(xii) Mhe. Mkiwa Adam Kimwanga, Mb – Mjumbe

(xiii) Mhe. Moses Joseph Machali, Mb - Mjumbe

(xiv) Mhe. Sylvester Masele Mabumba, Mb - Mjumbe

(xv) Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza, Mb - Mjumbe

(xvi) Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb - Mjumbe

(xvii) Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb – Mjumbe

1.1.2 **Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii, kwa unyenyekevu na kwa moyo wa dhati kabisa, kuwashukuru Wabunge hawa kwa kuniamini na kunipa dhamana kubwa ya kuiongoza Kamati hii na kwa kunipa ushirikiano stahiki katika kipindi chote ambacho nimefanya nao kazi.

1.2 MAJUKUMU YA KAMATI

1.2.1 Mheshimiwa Spika, misingi ya majukumu ya Kamati hii inatokana na ibara ya 63 (2) na (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, inayotoa madaraka kwa Bunge kuwa chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano chenye madaraka kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba.

1.2.2 Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya TAMISEMI, ikiwa ni moja kati ya Kamati za Bunge za Kisekta, ina majukumu yafuatayo kwa mujibu wa kanuni ya 7 (1) katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge:-

(a) Kushughulikia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), pamoja na mikoa yote ya Tanzania bara;

(b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI);

(c) Kufuatilia utendaji wa Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI);

(d) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI); na

(e) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa mujibu wa ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1.2.3 Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya TAMISEMI pia ina jukumu la kufuatilia utekelezaji wa shughuli za kisera zinazotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Tawala za Mikoa pamoja na halmashauri zote nchini katika masuala yote yanayohusu utawala, elimu ya msingi na sekondari, utoaji wa huduma za afya ya msingi, miundombinu ya barabara iliyo chini ya mamlaka ya Serikali za Mitaa, masuala ya ardhi, miundombinu ya maji, mazingira, maliasili, kilimo na ufugaji.

1.2.4 Mheshimiwa Spika, aidha kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane kanuni ya 7 (2) (c) (ii) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati hii imepewa jukumu mahsusi la kuchambua Sheria Ndogo zilizotungwa na Halmashauri za Miji, Wilaya, Manispaa na Majiji ili

kujiridhisha iwapo sheria ndogo hizo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

1.2.5 Kwa mujibu wa ibara ya 64 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, Bunge limepewa mamlaka ya kutunga sheria zote za nchi juu ya mambo yote yahusuyo Tanzania Bara na yale yanayohusu Muungano. Hata hivyo, ili kuweza kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Serikali, Bunge limekasimisha madaraka ya kutunga Sheria Ndogo kwa mamlaka mbalimbali za Serikali kwa madhumuni ya kurahisisha utekelezaji wa sheria zilizotungwa na Bunge lenyewe.

1.2.6 Kwa muktadha huo, kila sheria ndogo inayotungwa na mamlaka hizo, inatungwa kwa niaba ya Bunge na kwa madhumuni hayo, kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri za Sheria, Sura ya Kwanza (Interpretation of Laws Act, CAP 1) kinaweka masharti juu ya utaratibu kwa mamlaka zilizotunga sheria ndogo hizo (Serikali), baada ya sheria zilizotungwa nao kutangazwa katika Gazeti la Serikali na kuanza kutumika, kuziwasilisha mezani sheria ndogo hizo Bungeni (Laying of regulations before the National Assembly).

1.2.7 Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huu wa kisheria, Bunge kupitia Kamati yake ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, linakuwa na mamlaka, pale linapoona inafaa, kuzipitia na kuzichambua sheria ndogo zilizotungwa na halmashauri zote nchini chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa madhumuni ya kanuni tajwa hapo juu pamoja na kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri za Sheria, Sura ya Kwanza.

1.2.8 Mheshimiwa Spika, Kamati hii pia ina jukumu la usimamizi wa kiutendaji kwa taasisi zifuatazo zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

(a) Shirika la Elimu Kibaha

(b) Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF)

(c) Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

(d) Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo (LGTI)

(e) Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART)

1.3 SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA NA KAMATI KUANZIA JANUARI, 2014 HADI JANUARI, 2015

1.3.1 Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya TAMISEMI, kwa kuzingatia msingi wa majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni na kwa kuzingatia namna bora ya uendeshaji wa Bunge na Kamati zake, iliazimia kutekeleza shughuli zifuatazo kati ya Januari, 2014 na Januari, 2015:-

(a) Kushiriki semina za ndani na nje kwa madhumuni ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi;

(b) Kushughulikia Bajeti ya Serikali;

(c) Kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo;

(d) Kupokea taarifa mbalimbali za utekelezaji kutoka OWM (TAMISEMI) na taasisi zilizo chini yake;

(e) Kufanya ziara ya mafunzo nje ya nchi; na

(f) Kufanya ziara za ukaguzi na tathmini ya miradi mbalimbali inayotekelezwa na Ofisi ya Waziri

Mkuu-TAMISEMI na taasisi zake, Tawala za Mikoa, na Serikali za Mitaa.

1.3.2 Mheshimiwa Spika, kwa sababu mwaka huu Wabunge walikuwa sehemu ya Bunge Maalum la Katiba pamoja na sababu nyingine, baadhi ya shughuli zilizoainishwa hapo juu hazikuweza kutekelezwa.

2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI KUANZIA JANUARI, 2014 HADI JANUARI, 2015

2.1 SEMINA NA MAFUNZO

2.1.1 Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imekuwa ikialikwa kushiriki semina mbalimbali zilizoandaliwa na Ofisi ya Bunge kupitia programu ijulikanayo kama Legislative Support Program ya Shirika la UNDP, ambapo Wajumbe wa Kamati wamekuwa wakijifunza masuala mbalimbali yanayohusu uchambuzi wa bajeti, uchambuzi wa miswada ya sheria pamoja na namna bora ya usimamizi wa kibunge katika matumizi ya Serikali.

2.1.2 Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru waandaaji na watoa mada mbalimbali katika semina hizi kwa sababu kwa namna moja au nyingine zimekuwa zikiwasadia Wabunge kuwa wawakilishi bora zaidi wa Wananchi katika masuala yanayohusu maendeleo yao.

2.2 UCHAMBUZI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI

2.2.1 Mheshimiwa Spika, kwa nyakati tofauti na kwa kuzingatia Mpango Kazi wake, Kamati ya Bunge ya TAMISEMI imekuwa ikipokea taarifa mbalimbali za utekelezaji wa sera, mipango, programu na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na taasisi zake kwa malengo ya kupata taarifa muhimu kuhusu maendeleo yake. Kamati imekuwa ikitumia fursa hiyo, kutoa maoni na

mapendekezo mbalimbali katika kuhakikisha kuwa Serikali inafanya kazi kwa ufanisi katika kuwaletea wananchi huduma muhimu.

2.2.2 Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015, Kamati yangu lipokea na kufanya uchambuzi wa taarifa zifuatazo:-

(a) Taarifa ya Utekelezaji ya Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa (LGRP II D By D) Kwa Kipindi Cha 2009 – 2014

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Oktoba, 2014, Kamati yangu ilipokea taarifa ya Utekelezaji wa Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa (LGRP II D BY D) Kwa Kipindi cha 2009 – 2014. Kamati ilielezwa kwamba, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, imekuwa ikitekeleza Sera ya Kupeleka Madaraka kwa Wananchi (Decentralization by Devolution) maarufu kama D by D kupitia Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa.

Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ilianzishwa kwa lengo la kusaidia na kuwezesha mamlaka za serikali za mitaa, kama taasisi za msingi zinazowajibika na maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kupunguza umaskini katika maeneo yao. Programu hii ilitekelezwa kwa awamu mbili, ya kwanza kuanzia mwaka 1998 – 2008 na ya pili ilianza mwaka 2010 katika maeneo manne ya utekelezaji ambayo ni:-

(i) Kuwezesha mazingira ya sera ya kupeleka madaraka kwa wananchi (Enabling Environment for D by D)

(ii) Kujenga uwezo wa mamlaka za Serikali za mitaa (Capacity Development of LGA's)

iii) Kuhuisha ushiriki na uwajibikaji wa Wananchi katika maendeleo (Enhanced Citizen Participation and Accountability)

iv) Kuendesha Programu (Program Management)

Tathmini na Maoni ya Kamati kuhusu Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa (LGRP II D BY D) Kwa Kipindi cha 2009 – 2014

2.2.3 Mheshimiwa Spika, programu hii, ambayo imekuwa ikipata fedha kutoka kwa Wadau wa Maendeleo, pamoja na kwamba ni muhimu kwa madhumuni ya kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa, bado haijakidhi kiu ya watanzania wa kawaida kuona umuhimu wa Serikali za Mitaa katika kuwaletea maendeleo.

2.2.4 Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zilizobainishwa, lakini kwa umuhimu wa programu hii, Kamati inashauri kwamba, katika kipindi cha programu cha 2014-2019, Serikali ianze kujiweka sawa ili kuja na mpango madhubuti ambao utawezesha programu kuwa endelevu hata kama Wadau wa Maendeleo watapunguza fedha au kutotoa fedha kabisa. Sera ya Ugatuaji Madaraka kwa Umma (D by D) ni msingi mkuu wa kuziwezesha halmashauri kujitegemea na kuwaletea wananchi maendeleo.

b) Taarifa ya Utekelezaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar Es Salaam (DART)

2.2.5 Mheshimiwa Spika, tarehe 31 Aprili, 2014, Kamati hii ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) kutoka kwa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART). Katika taarifa hiyo, Kamati ilitaarifiwa kwamba mradi umesanifiwa kujengwa katika awamu sita (6) zenye urefu wa takriban kilometa 130.3 katika barabara za Morogoro, Kilwa, Nyerere, Bagamoyo, Mandela, Mwai Kibaki na barabara nyingine zitakazochaguliwa baadaye.

2.2.6 Taarifa hiyo ilieleza kwamba, wakala unatarajia kujenga vituo vikuu 18 na vituo vidogo 228 katika awamu zote sita. Hadi kufikia wakati taarifa hiyo

inawasilishwa kwa Kamati, awamu ya kwanza ilikuwa katika hatua za mwisho za ujenzi na kwamba kufikia Disemba, 2014, usanifu wa awamu ya pili na ya tatu ungekuwa umekamilika.

2.2.7 Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi, Kamati ilielezwa kwamba, Wakala umetekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Ujenzi wa miundombinu

(ii) Kufanya Maandalizi ya uendeshaji wa Mfumo

(iii) Kuhamasisha Ushiriki wa Watoa Huduma ya Usafiri

(iv) Kufanyika kwa Mkutano wa Mashauriano ya Wawekezaji

(v) Kuandaliwa kwa Mfumo wa Manunuzi Chini ya Sheria ya PPP – Tanzania

(vi) Kufanya Maandalizi ya Kuitisha Zabuni

(vii) Kuandaa mpango mkakati wa uendeshaji wa Majaribio/Mpito (interim operations plan)

Tathmmini na Maoni ya Kamati kuhusu Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar Es Salaam (DART)

2.2.8 Mheshimiwa Spika, wakati umefika, kwa Serikali kuhakiskisha kuwa changamoto ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam, hususan kwa makundi ya wakazi wa Jiji hilo wenye kipato cha chini na cha kati, inapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Aidha, msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam ni kero kubwa kwa wakazi na wageni wa Jiji hilo na kwa sehemu kubwa unakwamisha maendeleo na upatikanaji wa huduma muhimu. Taifa linapata hasara kubwa kiuchumi ambapo inakadiriwa kwamba, kiasi cha Shilingi Bilioni 4 hupotea kwa siku

kutokana na msongamano huo kwa sababu ya hasara itokanayo na upotevu wa mafuta kwa magari yanayotumia muda mrefu katika foleni na kupotea kwa muda unaoweza kutumika kwa nguvu kazi (loss of man hours). Aidha, magari ambayo yanakaa muda mrefu katika foleni za Dar es Salaam, hutoa hewa ukaa kwa wingi (emissions of toxic gases) ambazo huathiri hali ya hewa na afya za watu kwa ujumla.

2.2.9 Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kupongeza jitihada za Serikali kubuni mradi huu ili kupata ufumbuzi wa changamoto ya usafiri kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na vitongoji vyake, pamoja na kupunguza msongamano wa magari jijini Dar es salaam. Inatarajiwa kwamba, mradi utakapokamilika, utakuwa umetatua tatizo la usafiri wa umma katika jiji la Dar es salaam na pia kupunguza msongamano wa magari jijini humo mpaka kufikia miaka ya 2030/31.

2.2.10 Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya kifedha katika ujenzi wa miundombinu ambapo inasemekana kwamba kumekuwepo kwa ongezeko la mahitaji ya fedha za kukamilisha ujenzi huo kiasi cha shilingi bilioni 64.7. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 20.6 ni ongezeko la mishahara na shilingi bilioni 44.1 ni ongezeko la kazi na madai mengineyo. Inadaiwa kwamba, ongezeko hili limemfanya mkandarasi kutoonesha utayari wa kuanza kazi katika barabara ya Msimbazi kwa hofu ya kutokuwepo kwa fedha za kumlipa. Aidha, mradi unakabiliwa na changamoto nyingine ya uharibifu wa miundombinu (vandalism) ambapo baadhi ya wananchi na wafanyabiashara ndogondogo huvamia maeneo ya ujenzi yanayoendelea kujengwa. Vile vile, kumekuwepo na tabia ya wizi wa samani za barabara, mifuniko ya maji ya mvua, maji taka na huduma nyinginezo.

2.2.11 Mheshimiwa Spika, ili kupata suluhisho la kudumu kuondokana na tatizo la usafiri na msongamano wa magari jijini humo, Kamati inaishauri Serikali kufanya jitihada za makusudi kuhakikisha kuwa mradi huu unaendelea kutekelezwa kama ilivyopangwa na fedha yote inayohitajika kukamilisha hatua mbalimbali za mradi huu, itengwe na kupelekwa ili hatua hizo zikamilike kwa wakati.

2.2.12 Aidha, kwa umuhimu wa mradi huu, na kwa kuzingatia ukweli kuwa mradi huu ni kwa ajili ya matumizi ya wananchi wenyewe, na pia gharama kubwa za kutekeleza miradi ya aina hii, Kamati inawataka wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na vitongoji vyake, kuonesha uzalendo, ustaarabu na uDaressalaam wao, kwa kutambua kuwa mradi huu ni wao, kwa matumizi yao, na kwa faida yao, na hivyo basi, kutoa ushirikiano kwa wakala, serikali, wana usalama na wajenzi, ili kulinda miundombinu ya mradi na kuwezesha miuondo mbinu hii muhimu na ya gharama kubwa kudumu kwa miaka mingi na kuhudumia vizazi vijavyo. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kushirikiana na vyombo vya usalama, itoe elimu na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kutunza na kulinda miundombinu hiyo.

2.2.13 Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba, Serikali iandae Mpango na Usanifu Maalum ambao utazingatia utatuzi wa tatizo hili kwa miaka 50 hadi miaka 100 ijayo kwa kutazama maoteo ya idadi ya watu katika kukidhi mahitaji mapana ya baadaye. Sanifu za mpango huo, zizingatie uwepo wa mfumo wa njia mchanganyiko jijini (multi-modal city transit systems) za kutatua tatizo hili, hata kama kwa sasa tuna uwezo wa kujenga miundombinu ya mabasi yaendayo haraka tu.

2.2.14 Aidha kwa kuzingatia jiografia ya Jiji la Dar es Salaam, sanifu mipango hiyo iende kwa kuzingatia uwepo wa mifumo ifuatayo ya usafiri:-

(a) Usafiri wa mabasi yaendayo juu ya maji yaani seabuses;

(b) Usafiri wa treni chini ya ardhi maarufu kama Metro;

(c) Barabara za juu katika makutano yaani flyovers;

(d) Reli za umeme aina ya trams (pamoja na nguzo zake) katika miundombinu ya barabara za mjini; na

(e) Njia nyingine yoyote ya usafiri ambayo inaweza kuwemo katika mifumo hiyo.

2.2.15 Mheshimiwa Spika, hatua ya usanifu wa namna hii ikichukuliwa sasa, itaokoa pesa nyingi huko mbeleni na pia itatoa fursa kwa Serikali kuongeza njia moja baada ya nyingine kwa kadri ambavyo pesa itakuwa inapatikana bila kuathiri bajeti za fidia au kubomoa bomoa miundombinu mipya na imara inayojengwa sasa, na zaidi bila kuongeza msongamano katika kipindi chote cha mradi.

2.2.16 Mheshimiwa Spika, katika nchi ya Uturuki, usanifu na ujenzi wa miundombinu ya treni za chini ya ardhi katika Jiji la Istanbul ulianza mnamo mwaka 1992 takriban miaka 23 tu iliyopita. Miaka 18 baadaye, yaani mwaka 2000, huduma ya usafiri wa treni hizo kwenda vitongoji mbalimbali vya jiji hilo ulianza rasmi. Kamati inaamini kwamba, kwa kuweka malengo yanayotekelezeka kwa kuzingatia mazingira yetu, ujenzi wa miundombinu kama hii unawezekena kwa Jiji la Dar es Salaam na miji mingine inayokuwa kwa kasi.

2.2.17 Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa Mpango wa Usanifu unaojumuisha mifumo mchanganyiko ya usafiri, utekelezaji wake unaweza kuangukia katika mamlaka tofauti za kiutawala. Kuna miradi ambayo

inaweza kuangukia moja kwa moja katika Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), mingine chini ya Wizara ya Uchukuzi na mingine chini ya Wizara ya Ujenzi. Hivyo basi, Kamati inaiagiza Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kushirikisha Wizara zote za kisekta kuandaa mpango maalum kutekeleza mapendekezo yaliyoainishwa.

2.3 UCHAMBUZI WA BAJETI KWA MWAKA FEDHA 2013/2014 PAMOJA NA BAJETI YA OFISI HIYO KWA MWAKA 2014/2015

(a) Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2013/2014

Makusanyo ya Maduhuli

2.3.1 Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Mwaka 2013/2014 Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ilikadiriwa kukusanya maduhuli ya Sh. 10,500,000 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2014 jumla ya Sh. 39,197,800 zilikusanywa ikiwa ni sawa na asilimia mia tatu sabini na tatu (373%) ya makadirio. Kamati ilielezwa kwamba sababu ya kuvukwa kwa lengo la ukusanyaji katika Ofisi hii ilikuwa ni mauzo ya zabuni za vitabu na madawati kutokana na fedha za BAE ambazo hazikuwemo katika makisio ya awali.

2.3.2 Mheshimiwa Spika, kwa upande wa taasisi zilizo chini ya Fungu 56 – Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ilikadiriwa kuwa zingekusanya maduhuli ya jumla ya Sh. 10,190,381,355 ambapo hadi kufikia Machi, 2014 taasisi hizo zilikuwa zimekusanya kiasi cha Sh. 5,091,410,695 ikiwa ni sawa na asilimia hamsini (50%) ya makisio.

Matumizi

2.3.3 Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Fungu 56 - Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) pamoja na taasisi zilizo chini yake, ambazo ni Shirika la Elimu

Kibaha, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF), Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo (LGTI) na Wakala wa Usafiri wa Haraka Dar es Salaam (DART) ziliidhinishiwa na Bunge lako tukufu jumla ya Shilingi Bilioni 278,686,064,802. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 194,359,133,000.000 ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Reccurent Budget) na Shilingi Bilioni 84,326,931,802 ziliidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo (Development Budget).

2.3.4 Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2014, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) pamoja na taasisi zilizo chini yake ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi Bilioni 176, 628,908,702 sawa na asilimia sitini na tatu nukta nne (63.4%) ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza shughuli zake.

2.3.5 Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ujumla wake ziliidhinishiwa kiasi cha Shilingi Trilioni 4,079,140,624,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, miradi ya maendeleo na makusanyo. Hadi kufikia Machi, 2014, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zilipokea na kukusanya kiasi kisichozidi asilimia sitini (60%) kwa wastani katika bajeti iliyoidhinishwa.

(b) Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2014/2015

2.3.6 Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/ 2015, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi Trilioni 4,978,576,426,00. Kati ya fedha hizo, wizara ya OWM (TAMISEMI) na Taasisi zilizo chini yake ilipangiwa kiasi cha Shilingi Bilioni 479,224,062,000 ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 273,065,895,000 ziliombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi Mengineyo) na Shilingi Bilioni 206,158,167,000 kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo

2.3.7 Tawala za Mikoa na Halmashauri zake kiasi cha Shilingi Trilioni 4,231,442,974,000 kiliombwa ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi Trilioni 3,292,680,594,000 ziliombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi Mengineyo), Shilingi Bilioni 458,470,622,000 ikiwa ni Mapato yatokanayo na Makusanyo, na Shilingi Bilioni 748,201,148,000 ikiwa ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

(c) Tathmini Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Masuala ya Bajeti

2.3.8 Mheshimwa Spika, uandaaji wa bajeti ni sehemu muhimu katika mchakato wa kuandaa mipango, kudhibiti na kutathmini hali ya fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa uhalisia wake, ni nia ya kugawa rasilimali ili kufikia malengo yaliyowekwa. Bajeti ni chombo kinachosaidia viongozi kupanga pamoja na kudhibiti fedha ili kuhakikisha kwamba, kwa kadri inavyowezekana, malengo yaliyopangwa yanafikiwa.

Muundo wa Bajeti

2.3.9 Mheshimiwa Spika, kwa wastani katika miaka michache ambayo Kamati ya Bunge ya TAMISEMI imekuwa ikichambua bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na hususan bajeti inayotengwa kwa Serikali za Mitaa, kwa sehemu kubwa kiwango kinachotengwa kutekeleza miradi ya maendeleo kimekuwa kidogo ukilinganisha na fedha inayotengwa kwa matumizi mengineyo. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 kwa wastani asilimia 17.68 tu ndiyo ilitengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

2.3.10 Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa, fedha za miradi ya maendeleo zinatokana na vyanzo mbalimbali mfano Ruzuku ya Serikali Kuu, Fedha za Wahisani na pia Mapato ya Ndani ya Halmashauri husika (Own Source). Mapato ya ndani kwa Mamlaka

ya Serikali za Mitaa ni kiasi cha fedha ambacho kimekadiriwa na kukusanywa na halmashauri husika kutoka katika vyanzo vyake vya ndani vilivyoainishwa ambavyo havikusanywi na Serikali Kuu. Mapato yatokanayo na vyanzo hivi ni kama, ushuru wa huduma (service levy), ada za leseni na vibali (fees for licences and permits) na kodi mbalimbali. Fedha hizi hukusanywa kutoka kwa wananchi wa kawaida kabisa na makampuni yanayofanya biashara katika halmashauri husika.

2.3.11 Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba, halmashauri zote zihakikshe kuwa, katika bajeti zake, asilimia isiyopungua sitini (60%) itokanayo na makusanyo ya ndani (own source) inatengwa mahsusi kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi. Msingi wa pendekezo hili ni katika kuhakikisha kuwa, mapato yatokanayo na fedha inayokusanywa kutoka kwa wananchi wanaolipa ushuru na tozo mbalimbali, fedha hiyo ionekane kutekeleza miradi ya maendeleo ili kuchochea uzalishaji na kuwafanya waendelee kulipa tozo hizo bila manung'uniko.

Hali ya Makusanyo Katika Vyanzo Vya Halmashauri

2.3.12 Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, kwa kipindi kirefu, katika halmashauri nyingi nchini, kumekuwepo na makusanyo hafifu ya mapato ukilinganisha na bajeti iliyoidhishwa au/na makusanyo yasiyoakisi uhalisia wa mapato yatokanayo na vyanzo vilivyopo katika halmashauri hizo ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa katika vyanzo hivyo kwa sababu zifuatazo:-

(i) kukosekana kwa ufanisi wa mikakati ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vilivyopo;

(ii) tabia sugu ya udanganyifu katika makusanyo yanayopatikana;

(iii) makisio ya chini katika bajeti ya makusanyo ya ndani (underbudgetting); na

(iv) halmashauri kutokuwa na seti kamili ya Sheria Ndogo kwa vyanzo vyote vya mapato au sheria zilizopo kupitwa na wakati;

2.3.13 Aidha, halmashauri nyingi bado zinategemea vyanzo vile vile vya mapato mwaka hadi mwaka ambapo linapotokea jambo linaloathiri chanzo kimojawapo, makusanyo ya halmashauri husika hushuka. Kwa mfano, halmashauri ambazo zinategemea mapato yatokanayo na kilimo, pale ambapo wakulima wanapokosa mazao ya kutosha kutokana na uharibifu utokanao na majanga kama mafuriko, halmashauri hizo pia hutetereka kwa kukosa mapato.

2.3.14 Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa ihakikishe kwamba, inazisimamia kikamilifu halmashauri ili kudhibiti na kuzuia udanganyifu katika makusanyo. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na halmashauri zote, ifanye tathmini na upembuzi yakinifu kutambua uwepo wa vyanzo vipya vya mapato ili halmashauri hizo ziweze kuandaa makadirio kulingana na uwezo wa ukusanyaji lakini pia kuhakikisha kuwa mikakati madhubuti inawekwa kukusanya mapato kwa ufanisi na kufikia malengo yatakayowekwa.

2.3.15 Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba halmashauri zote ambazo hazina seti kamili za sheria ndogo za ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani, watunge na kupitisha sheria hizo na kuhakikisha zinasimamiwa kikamilifu, na halmashuri ambazo sheria zilizopo zimepitwa na wakati, marekebisho ya sheria hizo yafanyike kulingana na hali ya kiuchumi ya eneo husika.

2.3.16 Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa pendekezo kwamba, Serikali za Mitaa ziweke mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato ya majengo (property tax) katika majiji, manispaa, miji na miji midogo kwani fedha nyingi zinapotea kwa kutokusanywa kwa kodi hii. Kamati inatambua kuwa agizo hili limeshaanza kutekelezwa na Serikali, hata hivyo kwa yale maeneo ambayo yameainishwa kufanyiwa tathmini kuhusu thamani halisi ya majengo hayo kwa ajili ya kutozwa kodi ya majengo, Kamati inapendekeza kwamba, fedha maalum itengwe ili kuwezesha tathmini hiyo kukamilika kwa haraka ikiwa sahihi ili kodi hiyo ikusanywe katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 na miaka itakayofuata.

2.3.17 Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya Mwaka 1982 (The Local Government Finances Act No. 9 1982) ikisomwa pamoja na marekebisho yake, inazipa halmashauri mamlaka ya kukusanya kodi ya ushuru wa huduma (service levy) katika maeneo yake ya kiutawala. Kiwango cha kisheria cha kodi hiyo (statutory tax rate) ni asilimia isiyozidi nukta tatu (0.3%) ya mapato ya mwaka yaani net turnover. Kamati inatoa mapendekezo kwamba, halmashauri zote nchini zihakikishe zinakusanya kodi hii kikamilifu kutoka kwa kampuni na mashirika yote (corporate entities) ambayo yanafanya shughuli zake ndani ya halmashauri husika.

2.3.18 Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba, halmashauri zote nchini kwa kushirikiana na Sekretarieti za mikoa zihakikishe kwamba zinawashirikisha wananchi kikamilifu katika maandalizi ya bajeti zao hususan katika mipango ya maendeleo, katika kubuni vyanzo vya mapato na pia katika utungaji wa sheria ndogo za ukusanyaji wa mapato ili kurahisisha zoezi la makusanyo bila manung'uniko. Ushiriki wa wananchi husaidia zoezi zima la kuchangia ujenzi wa miradi ya maendeleo

hasa pale ambapo Serikali kuu pamoja na Serikali za Mitaa zinapokuwa zimetoa mchango wake kikamilifu katika miradi husika.

Mapato na Matumizi ya Fedha za Ruzuku Katika Miradi ya Maendeleo

2.3.19 Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kwamba utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri zetu hauwezi kutegemea kwa asilimia kubwa vyanzo vya mapato ya ndani tu. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, baadhi ya halmashauri zina vyanzo vichache vya mapato ukilinganisha na vingine. Kwa sababu hiyo, Serikali kuu hutoa ruzuku ili kuzisaidia halmashauri katika kujenga au kukarabati miundombinu iliyopo kwa madhumuni ya kusogeza huduma kwa wananchi kama afya, elimu, maji, barabara na miundombinu inayowezesha kilimo.

2.3.20 Mheshimiwa Spika, halmashauri nyingi zimekuwa zikilalamika kwamba miradi mingi inashindwa kutekelezwa au kuchelewa kutekelezwa kwa sababu fedha iliyodhinishwa kutekeleza miradi hiyo huchelewa kufika katika akaunti za halmashauri hizo kutoka Serikali Kuu (Hazina). Kamati imebaini kwamba, kumekuwepo na mwenendo unaoonesha kuwepo kwa fedha isiyotumika katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa sababu ya ucheleweshwaji huo na wakati mwingine, fedha iliyoidhinishwa kufika ikiwa pungufu au kutofika kabisa.

2.3.21 Mheshimiwa Spika, kwa mwenendo huu, miradi mingi ya maendeleo haikuweza kutekelezwa kikamilifu kama ilivyopangwa au kutotekelezwa kabisa na hivyo kusababisha huduma muhimu kutowafikia wananchi. Mwenendo huu unaweza kusababisha mabadiliko ya bajeti ili kufidia athari zinazoweza kutokea kwa sababu ya mfumuko wa bei.

2.3.22 Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Kamati imebaini kwamba, kumekuwepo na matumizi holela, yasiyozingatia utaratibu au yasiyosimamiwa kikamilifu na Menejimenti za Halmashauri katika fedha inayopatikana wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

2.3.23 Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali Kuu kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI ihakikishe kwamba fedha za matumizi ya kawaida na za miradi ya maendeleo zinawasilishwa kwa Serikali za Mitaa kwa wakati. Aidha, halmashauri zenyewe zinapaswa kufuatilia kwa karibu.

2.3.24 Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa mapendekezo kwa halmashauri zote kwamba, zihakikishe zinaomba vibali kwa Mamlaka husika kwa ajili ya kubadilisha mgawanyo wa fedha kama inavyoelekezwa katika Agizo 22 (1) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 bila kuathiri utoaji wa huduma kwenye jamii iliyokusudiwa.

2.3.25 Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa mapendekezo mahsusi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kwa kushirikiana na sekretarieti za mikoa kuimarisha mfumo wa uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo na kuzisimamia halmashauri kuhakikisha kuwa fedha za miradi ya maendeleo zitokanazo na makusanyo ya ndani pamoja na zile ambazo zinatoka nje zinatumika kuwaletea wananchi maendeleo kwa wakati na kwa viwango stahiki ili thamani ya fedha iweze kuonekana.

2.4 ZIARA ZA UKAGUZI WA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI NA MIRADI INAYOTEKELEZWA NA OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)

2.4.1 Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mpango kazi wake, Kamati ilijiwekea utaratibu wa kufanya ziara katika mikoa mbalimbali kwa lengo la kujionea

shughuli mbalimbali za utekelezaji wa sera, sheria na bajeti zilizoidhinishwa na Bunge hususan katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya Januari 2014 na Januari, 2015, kamati ilifanya ziara katika mikoa ifuatayo na kutembelea baadhi ya halmashauri:-

(a) Mkoa wa Mwanza:- Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi;

(b) Mkoa Pwani:- Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo;

(c) Mkoa wa Lindi:- Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea;

(d) Mkoa wa Kigoma:- Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji, Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu.

2.4.2 Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu ambao imejiwekea, Kamati inapokuwa katika ziara mikoani, hupokea taarifa kwanza kutoka kwa Sekretarieti ya Mkoa, muhtasari wa shughuli za miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika mkoa huo na halmashauri zake. Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kamati hupokea taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayobainisha makisio ya bajeti, mapokezi ya fedha na matumizi ya fedha zilizopokelewa na pia kufanya ziara za ukaguzi katika miradi itakayopendekezwa au kuchaguliwa na Wajumbe wa Kamati. Katika ziara zilizofanywa na Kamati, Kamati ilibaini masuala mbalimbali kama ambavyo yamefafanuliwa katika aya zinazofuata.

Taarifa za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

2.4.3 Mheshimiwa Spika, katika ziara ya Kamati katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kamati ilibaini kwamba

taarifa za halmashauri nyingi kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilikuwa na mapungufu ya kimantiki, kiuchapaji, kisarufi, kimahesabu na kimchanganuo wa matumizi ya fedha zizilizoidhinishwa.

2.4.4 Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya taarifa, Kamati ilibaini kwamba, baadhi ya miradi ya maendeleo katika halmashauri ilitengewa fedha nyingi, ikapokea fedha kidogo, fedha zilizopokelewa zikatumika zote, na maelezo yakawa kwamba utekelezaji wa miradi hiyo ulikamilika. Kamati ilishindwa kuelewa iwapo maelezo hayo yanaashiria udhaifu wa kubajeti kuzidi kiwango (overbudgeting).

2.4.5 Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilibaini katika baadhi ya taarifa zilizowasilishwa hazikubainisha mchanganuo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mapato ya fedha za ndani (own source) na pia kutowekwa wazi kiasi cha fedha za bakaa kutokana na bajeti za miaka iliyotangulia hali inayotia wasiwasi ya uwepo wa mazingira ya ubadhirifu wa fedha za umma.

2.4.6 Mheshimiwa Spika, Kamati ilihoji iwapo mapungufu hayo yalikuwa ya makusudi, ya bahati mbaya au yalisababishwa na uwezo mdogo wa kiutendaji katika kuandaa taarifa au ni juhudi za makusudi zilizofanywa kwa madhumuni ya kuficha ukweli.

2.4.7 Mheshimiwa Spika, tatizo hili lilibainika katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji, Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa na Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

Maoni na Mapendekezo ya Kamati

2.4.8 Mheshimiwa Spika, tatizo la halmashauri nyingi kutoandaa taarifa ambazo zinazingatia viwango stahiki, ni tatizo ambalo hata Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekuwa akilizungumzia katika taarifa mbambali za mwaka.

2.4.9 Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia madhumuni mapana ya ukweli, uwazi na uwajibikaji wa Serikali za Mitaa na kwa kuzingatia agizo la Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Kamati inatoa mapendekezo kwamba, halmashauri zote nchini, ziwe zinaandaa taarifa zake za fedha na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia maagizo ambayo Bunge imekuwa ikiyatoa na pia kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Sekta za Umma (IPSAs).

2.4.10 Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kuzisaidia halmashauri ambazo zina uhitaji maalum wa taaluma ya uandishi wa taarifa mbalimbali, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali izijengee uwezo halmashauri nchini katika uandaaji wa taarifa hizo. Aidha, taasisi hizo, zihakikishe kwamba zinaweka mfumo thabiti wa ufuatiliaji wa halmashauri ili kuhakikisha na kujiridhisha kuwa halmashauri zote nchini zinajiunga katika mfumo wa kuandaa taarifa za fedha kwa kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha za Sekta za Umma (IPSAs).

Utekelezaji wa Miradi

2.4.11 Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inapofanya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo, hufanya tathmini ya kina katika kuangalia matumizi ya fedha iliyoidhinishwa, ubora wa mradi husika kulingana na thamani ya fedha (value for money) na muda uliotumika kutekeleza mradi husika. Pamoja na

kwamba katika baadhi ya halmashauri Kamati iliridhika kikamilifu na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini kwamba, kwa sehemu kubwa, miradi inayotekelezwa na halmashauri nyingi nchini ina mapungufu/changamoto zifuatazo:-

(a) Miradi kutotelekezwa kwa wakati

2.4.12 Mheshimiwa Spika, kamati imebaini kwamba miradi ya halmashauri nyingi huchelewa kutekelezwa kwa sababu mbalimbali. Moja kati ya sababu hizo ni kuchelewa au kutofika kabisa kwa fedha kutoka Hazina na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi hiyo.

2.4.13 Mheshimiwa Spika, katika Mradi wa Ujenzi wa Jengo Jipya katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani, Tumbi Kibaha, Kamati ilibaini kwamba, jengo hilo lilikuwa linahitaji takriban Shilingi Bilioni Sita ili kukamilika. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Moja zingetosha kujenga chumba cha upasuaji (theatre) na njia za kupanda katika ghorofa za jengo hilo (ramps) na hivyo kuanza kutumika kwa huduma muhimu ya upasuaji.

2.4.14 Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba, majadiliano yafanyike baina ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Wizara ya Fedha na Uongozi wa Mkoa wa Pwani ili kupata fedha za kutosha ili kuinusuru Miradi inayohusu Upanuzi wa Hospitali ya Tumbi kwa sababu hospitali hii ni muhimu sana kwa wakazi na wageni wa Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Dar es Salaam. Kamati inaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), itimize ahadi yake ya kupeleka Shilingi Bilioni Moja ili kuboresha huduma Hospitalini Tumbi.

2.4.15 Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuu kuhakikisha kuwa inatoa upendeleo maalum kwa halmashauri zenye miradi ambayo inatoa huduma muhimu kwa wananchi hususan huduma za afya na kuhakikisha kuwa fedha zinafika kwa wakati na zikiwa kamili.

2.4.16 Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine baadhi ya halmashauri zimekuwa hazitekelezi miradi husika kwa wakati kwa sababu ya uzembe tu wa watendaji wa halmashauri hizo katika kufanya tathmini na ufuatiliaji wa karibu katika utekelezaji wa miradi husika, hata kama fedha iliyoidhinishwa imefika.

2.4.17 Mheshimiwa, katika Mradi wa Ujenzi wa Soko la Sofya katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma, makubaliano baina ya halmashauri hiyo na wananchi na wafanyabiashara wanaotumia soko hilo ilikuwa ni kwamba wafanyabishara wakisha kamilisha ujenzi wa vibanda vyao, halmashauri iweke miundombinu muhimu kama vile mabomba ya maji, vyoo, kituo kidogo cha polisi, madampo ya kukusanyia taka n.k. Hata hivyo, Kamati ilisikitishwa kushuhudia kuwa wafanyabiashara wengi walikuwa wamekwisha kamilisha ujenzi wa vibanda vyao, lakini halmashauri haijajenga miundombinu hiyo muhimu.

2.4.18 Mheshimiwa Spika, kukosekana mwa miundombinu hiyo muhimu katika soko hilo, sio tu kunaashiria ukosefu wa uaminifu kwa halmashauri ambayo iliahidi kuijenga, lakini pia kunahatarisha usalama wa watumiaji wa soko hilo dhidi ya uhalifu na magonjwa ya mlipuko.

2.4.19 Mheshimiwa Spika, Katika Mradi wa Ujenzi wa Choo cha Matundu 8 Shule ya Msingi Mwenda, shule yenye wanafunzi zaidi ya mia sita (600), katika Kata ya Nyumbigwa, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Mkoani Kigoma, Wajumbe walisikitishwa kuona kuwa fedha zilizotengwa kutekeleza mradi huo kiasi cha Tshs 4,625,000/= zilishawawekwa katika akaunti ya Kata ya Nyumbigwa tarehe 22 Juni, 2012 lakini mpaka wakati Kamati inafanya ziara hiyo, ujenzi wa vyoo hivyo haukuwa umekamilika pamoja na kuwepo kwa nguvu ya wananchi kuchimba shimo moja kwa ajili ya choo cha wasichana.

2.4.20 Mheshimiwa Spika, jambo hili linasikitisha, sio tu kwa sababu linaonesha uzembe wa hali ya juu katika ufuatiliaji wa ujenzi wa mradi husika, lakini hali hii inahatarisha afya za wanafunzi ambao, kwa maelezo tuliyopata, wanalazimika kujisaidia vichakani.

2.4.21 Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa mapendekezo mahsusi kuhusu miradi hiyo na kwa madhumuni ya kufikiwa kwa azimio la Bunge, Kamati inapendekeza tena kwamba, watu wote waliohusika na uzembe huo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu wachukuliwe hatua za kinidhamu au/na za kisheria na pia halmashahuri ihakikishe kuwa ujenzi wa miundombinu yote inayopaswa kuwepo katika Soko la Sofya unakamilika haraka; na pia ujenzi wa choo katika Shule ya Msingi Mwenda unakamilika mapema na taarifa ya utekelezaji wa agizo hili iwasilishwe Bungeni kabla ya Mkutano wa 20 wa Bunge hili.

2.4.22 Aidha, kwa upande mwingine, katika halmashauri zilizotembelewa, Kamati imebaini kuwepo kwa tuhuma kwamba baadhi ya madiwani katika baadhi ya halmashauri, ama moja kwa moja au vinginevyo, wamekuwa wakipata zabuni katika kutekeleza miradi hiyo. Kitendo hicho, ni kinyume cha sheria za maadili ya viongozi wa umma kwa sababu ya mgongano wa kimaslahi, na kinachangia miradi kutotekelezwa kwa wakati kwa sababu usimamizi wake unakosa ufanisi.

2.4.23 Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba, Serikali kuu kwa kutumia vyombo vya ulinzi na usalama, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, na taasisi zake nyingine ianze kufanya uchunguzi ili kubaini na kisha kuchukua hatua kali za kisheria kwa madiwani wote ambao kwa namna moja au nyingine wanahusika katika kukwamisha miradi ya maendeleo kwa kujihusisha na biashara na halmashauri bila kuweka wazi maslahi yao.

b) Miradi kutokuwa na ubora stahiki

2.4.24 Mheshimiwa Spika, hili limekuwa ni tatizo sugu katika utekelezaji wa miradi mingi katika halmashauri zetu. Tatizo hili linasababishwa na kukosekana kwa uaminifu kwa baadhi ya wataalam wa halmashauri hasa wahandisi na watu wa ugavi, lakini pia kutokana na zabuni za kutekeleza miradi husika kutolewa kwa wakandarasi wasio na uwezo kukamilisha miradi husika. Aidha, katika mazingira kama haya, Kamati inaamini kuna viashiria vya kuwepo kwa rushwa au/na matumizi mabaya ya madaraka katika kugawa zabuni kwa makandarasi.

2.4.25 Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, naomba nilitaarifu Bunge lako kwamba katika utekelezaji wa miradi, suala la kukosekana kwa ubora wa miradi bado ni tatizo sugu ambalo linapaswa kutolewa maazimio yanayotekelezeka ili Serikali ichukue hatua kali za kisheria na kinidhamu kuondokana na kadhia hii.

2.4.26 Mheshimiwa Spika, katika Mradi wa Ujenzi wa Kliniki ya Mama na Mtoto eneo la Utemini katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Kamati ilibaini kwamba, kiasi cha Shilingi Milioni 853,568,493 kilitengwa na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kutekeleza mradi huu. Kiasi hicho cha fedha kilikuwa ni sehemu ya malipo ya fedha ambazo halmashauri ya Jiji la Mwanza ilipokea kutoka Benki Kuu ya Tanzania iliponunua kiwanja kilichokuwa kinamilikiwa na halmashauri eneo la Makongoro kwa Shilingi Bilioni 3.1.

2.4.27 Mheshimiwa Spika, wakati wa ukaguzi wa jengo hilo, Kamati ilisikitishwa sana kuona ujenzi ambao hauna viwango stahiki kwa matumizi ya kituo cha afya, kwa kukosa mifumo stahiki ya kuingia na kutoka (entry and exit ways), mifumo madhubuti ya kupitisha hewa (ventilation systems) na mfumo stahiki wa kupitisha

mwanga na mapungufu mengineyo mengi. Kwa kifupi, matumizi ya Shilingi Milioni 853 katika ujenzi wa kliniki hiyo hayakuwashawishi Wajumbe wa Kamati yangu, na kamwe hayawezi kuwa toshelevu kuonesha thamani ya pesa (no value for money at all) na vilevile ni kiashiria cha tatizo lingine la ubadhirifu wa fedha za umma.

2.4.28 Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa uchunguzi kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Kliniki ya Mama na Mtoto, Eneo la Utemini katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza ulikuwa ukiendelea kufanywa na vyombo husika, Kamati inaitaka Serikali, kuwasilisha Bungeni taarifa kuhusu matokeo ya uchunguzi huo, ili Bunge lako litoe mapendekezo ya ziada.

2.4.29 Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na Serikali kwa ujumla ichukue hatua za makusudi na za lazima kuhakikisha kuwa utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo unazingatia viwango stahiki ili kuonesha thamani ya fedha (value for money).

(c) Matumizi Mabaya ya Fedha

2.4.30 Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, katika utekelzaji wa miradi katika baadhi ya halmashauri, kumekuwepo tatizo la matumizi mabaya ya fedha za miradi ya maendeleo na matumizi hayo yamekuwa yakijirudia rudia. Kuendelea kuwepo kwa tatizo hili kunaashiria udhibiti dhaifu wa ndani katika usimamizi wa fedha za umma lakini pia kunatoa taswira ya kwamba, kwa sehemu kubwa, watumishi wa umma waliopewa dhamana na wenye mamlaka ya matumizi ya fedha hizo katika kuwaletea Watanzania wenzao huduma muhimu, hawana uzalendo wala utu na kutojali kabisa thamani ya kodi za wananchi.

2.4.31 Aidha, Kamati imebaini kuwa, baadhi ya halmashauri zimekuwa na matumizi mabaya ya fedha kwa kuwa na mazoea yasiyoridhisha ya uhamishaji holela wa fedha kutoka mradi mmoja kwenda mradi mwingine. Uhamishaji huu mara nyingine umekuwa hauzingatii kabisa taratibu za uhamishaji fedha (re-allocation procedure)

2.4.32 Mheshimiwa Spika, Kamati ikiwa ziarani katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela katika Mkoa wa Mwanza ilibaini kuwa, Mradi wa Ujenzi wa Zahanati ya Kitangiri, Kata ya Kirumba haukuwa umeanza wakati fedha za utekelezaji wa mradi huo zilikuwa zimeshafika katika akaunti ya Kata husika. Ujenzi huo haukufanyika kwa sababu fedha zilizopokelewa zilitumika kujenga miundombinu ya barabara (madaraja) kwa makubaliano ya vikao vya Kata. Kamati ilishangazwa na uamuzi huo kwa sababu ulionesha wazi kwamba halmashauri hiyo haikuwa inazingatia vipaumbele na mahitaji halisi ya wananchi katika maeneo yao na katika kupanga bajeti zake.

2.4.33 Mheshimiwa Spika, Kamati ikiwa ziarani katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma, ilibaini kwamba, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2012/2013, halmashuri hiyo ilipeleka maombi maalum ya Tshs 300,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji Kasulu Mjini. Mnamo tarehe 22 Agosti, 2012 kwa Stakabadhi Na. 30901 halmashauri ilipokea jumla ya Tshs 471,932,500 ambazo zilitumika mara moja kutekeleza miradi mbalimbali inayotajwa kuwa ya maendeleo. Kwa taarifa ambazo Kamati inazo, Hazina ilitoa maelezo kwamba kati ya fedha zilizotumwa, Tshs 300,000,000/= zilikuwa ni fedha za Maombi Maalum kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji Kasulu Mjini kama ambavyo halmashuri hiyo ilivyoomba. Hata hivyo kwa maelezo ambayo Kamati iliyapata kutoka kwa halmashauri hiyo, maelekezo hayo yalikuja wakati fedha hizo zimekwisha tumika.

Kamati ilihoji, lakini bila kupata maelezo ya kuridhisha, kuhusu matumizi ya kiasi hicho cha fedha bila kuzingatia au kabla ya kupokea maelekezo kutoka Hazina.

2.4.34 Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Mwaka wa Fedha uliofuata 2013/2014 Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, ilipokea kiasi cha fedha Tshs 315,528,000 ikiwa ni ruzuku ya maendeleo (CDG). Hata hivyo halmashauri inadai kwamba fedha hizo zilitambuliwa kuwa zilikuwa zimetumwa kama ruzuku ya maendeleo (CDG) kwa Stakabadhi Na. 57415 ya tarehe 19 Februari, 2014, wakati halmashauri ikiwa imeshazitumia fedha hizo kulipia ukamilishaji wa miradi ya viporo vya Mwaka 2012/2013 na matumizi mengineyo. Kamati inashangazwa na utamaduni wa halmashauri hii kutumia fedha zinazoingia katika akaunti ya maendeleo bila kujiridhisha kutoka Hazina fedha zilizowasilishwa zimetumwa kwa malengo gani.

2.4.35 Mheshimiwa Spika, Kamati inaiagiza Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya Ukaguzi Maalum (Special Audit) katika idara zote katika halmashauri hii ili kuweza kutoa mapendekezo ambayo yatafanyiwa kazi na Bunge lako tukufu. Aidha, baada ya uchunguzi huo kufanyika, na ikabainika kuwepo na matumizi mabaya ya fedha za maendeleo, watendaji wote ambao watabainika kuhusika moja kwa moja au vinginevyo na matumizi mabaya ya fedha hizo, wachukuliwe hatua stahiki za kisheria na kinidhamu.

2.4.36 Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Kamati yangu imebaini kuwepo na matumizi mabaya ya fedha, ni kutumia fedha ambazo zinapaswa

kutekeleza agizo la Serikali kwa Sheria ya Bunge, kutenga kiasi cha asilimia 10 ya fedha zitokanazo na makusanyo ya ndani (own source) kwa madhumuni ya kuwawezesha vijana na wanawake kukopa ili kujikwamua kichumi. Kwa maneno mengine ni kwamba halmashauri hizo hazitengi fedha hizo kwa ajili ya Mifuko ya Maendeleo ya Wanawake na Vijana.

2.4.37 Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2012/2013, kiasi cha Jumla ya Shilingi Bilioni 10,905,858,533 hakikutengwa kabisa kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake na Vijana katika halmashauri 68. Kamati inashindwa kuelewa, inawezekanaje Serikali ambayo imepewa dhamana ya kutekeleza sheria zilizotungwa na Bunge ikashindwa kutekeleza agizo lenye tija kwa makundi hayo.

2.4.38 Kamati inatoa pendekezo kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ichukue hatua za kisheria na kinidhamu kwa watumishi wote ambao kwa namna moja au nyingine walihusika na kutotekelezwa kwa agizo hili la kisheria. Aidha, taarifa ya utekelezaji wa pendekezo hili, iwasilishwe katika Bunge lako, kabla ya kuisha kwa Mkutano wa 20 wa Bunge hili.

2.4.39 Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Kamati imebaini kwamba matumizi mabaya ya fedha yanatokana na baadhi ya watendaji wasio waaminifu, kutumia fedha zilizoidhinishwa kutekeleza miradi ya maendeleo katika masuala yasiyo na tija sana kama mafunzo, ufuatiliaji na uthamini kuliko shughuli halisi (core activities) zinazowagusa moja kwa moja waliokusudiwa/walengwa.

2.4.40 kwa mfano, katika utekelezaji wa Mradi wa Mpango wa Kudhibiti Ukimwi, Kamati inashauri na kupendekeza kwa halmashauri zote nchini kutozitumia fedha zinazopokelewa kufanya mafunzo, uratibu na usimamizi peke yake; ni vyema asilimia kubwa ya fedha hizo itumike kuwanufaisha waathirika wa virusi vya UKIMWI na watoto yatima (Impact Mitigation).

2.5 MASUALA MENGINE YALIYOSHUGHULIKIWA NA KAMATI

2.5.1 Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ikitekeleza majukumu yake ya msingi ambayo ilijipangia kutekeleza katika mwaka huu, yalijitokeza masuala mbalimbali yenye viashiria vya migogoro ambayo kwa namna moja au nyingine yanaathiri utendaji wa halmashauri zetu au/na kukwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

2.5.2 Mheshimiwa Spika, mara zote ambazo Kamati imekuwa ikishughulikia masuala yenye asili hii, Wajumbe walilazimika kutumia muda mwingi kufanya kazi ya usuluhishi ilipobidi, kufanya kazi ya uchunguzi ilipostahili na kutumia mamlaka kamili ya kibunge katika kutaka vielelezo muhimu ili kutoa mapendekezo stahiki.

2.5.3 Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ukweli kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ikiongozwa na Waziri au Naibu Mawaziri, imekuwa ikihakikisha kuwa inakuwepo wakati wote kuhakikisha kuwa inazingatia na kutekeleza maagizo ya Kamati yanayotolewa na pia kutoa ufafanuzi wa kisera na kisheria pale inapohitajika kufanya hivyo, Kamati imekuwa ikifikia maamuzi ambayo kwa sehemu kubwa yameonekana kuwa yanazisaidia halmashauri hizo kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

2.5.4 Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maagizo mengi kuhusu masuala hayo yaliyoshughulikiwa na Kamati yalishatolewa, na kwa mengine taarifa za awali za utekelezaji zilishawasilishwa mbele ya Kamati, naomba Bunge lako tukufu liniruhusu kwa muhtasari kuyataja tu masuala/mashauri hayo bila kufafanua masuala ya kiuchunguzi na kiuchambuzi yaliyofanywa na kama ifuatavyo:-

a) Mgogoro Baina ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela

2.5.5 Mheshimiwa Spika, mgogoro huu ulikuwa unahusu mamlaka ya kiutawala (jurisdiction) hasa kuhusu usimamizi, umiliki na uendeshaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ya iliyokuwa Halmashauri ya Jiji la Mwanza kabla ya kugawanywa na kuundwa upya kwa Halmashauri ya Jiji la Mwanza (Yenye mipaka ya iliyokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Nyamagana) na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela (Yenye mipaka ya iliyokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela). Miradi ambayo ilisababisha kuwepo kwa mgogoro huu ni ifuatayo:-

(i) Mradi wa Mwanza City Commercial Complex

(ii) Mradi wa Makazi Maalum Mhonze

(b) Mgogoro Baina ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi na Wakazi wa Eneo la Mmongo na Mabano, Kata ya Rasbura, Manispaa ya Lindi

2.5.6 Mheshimiwa Spika, mgogoro huu ulikuwa wa maslahi hasa yatokanayo na Mradi wa Ubia Baina ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi na Mfuko wa Dhamana wa Uwekezaji (UTT-PID) Kupima Viwanja katika eneo la Mmongo na Mabano, Kata ya Rasbura.

2.5.7 Mheshimiwa Spika, chanzo cha mgogoro huu, ni kuwepo kwa malalamiko kutoka kwa wananchi

wakazi wa maeneo hayo, ambao walipaswa kuhama kupisha upimaji na ugawaji wa viwanja katika mradi huo, kwamba fidia iliyokuwa imekadiriwa kulipwa ilikuwa ndogo, ukilinganisha na thamani ya ardhi yao iliyo katika fukwe za Bahari ya Hindi (beach plots).

2.5.8 Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ihakikishe inatekeleza kwa ukamilifu maazimio yote yaliyofikiwa na Kamati na taarifa za utekelezaji wa maazimio hayo ziwasilishwe mbele ya Kamati kabla ya Bunge la Bajeti ya Mwaka 2015/2016.

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA

3.1.1 Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa mapendekezo kwamba, Serikali itafute namna ya kuachana na utegemezi wa misaada ya wafadhili kutekeleza miradi ya maendeleo na hatimaye kuwa na ubunifu wa kupanga miradi ya maendeleo kwa asilimia mia kutegemea fedha za ndani ya nchi zenye uhakika wa kupatikana, na mikopo yenye masharti nafuu (concessional loans) tunayoweza kupanga kuchukua na tukawa na uhakika wa kupata. Fedha za wafadhili ziwe nyongeza tu na zisionekane kwenye umbile la bajeti kama chanzo mahsusi cha fedha; ikibidi kwamba tunapokea fedha za msaada kutoka kwa wafadhili, basi ziandikwe kwenye kitabu cha nyongeza (addendum). Kamati yetu inaitaka Serikali kutoa tamko kwamba mwaka wa fedha ujao, yaani bajeti ya 2015/16, hakutokuwa na mchango wa wahisani/wafadhili kwenye umbile la bajeti yetu ili kuonesha dalili ya uwajibikaji wa serikali kwa umma kwa mujibu wa mkataba wa miaka mitano tuliyopewa kushika dola.

3.1.2 Aidha katika kupunguza matumizi ya serikali, kamati inaishauri, isijitwishe jukumu la kuwa ndiye muajiri mkuu, ijibadilishe, 'kwa vitendo na uhalisia', kuwa ni

muwezeshaji, mtunga sera na muangalizi wa namna bora ya kutia chachu ukuaji wa uchumi kwenye sekta zinazotoa ajira kwa wingi kama kwenye kilimo na viwanda vyenye 'backward linkage' na kilimo na biashara inayohusisha bidhaa za kilimo.

3.1.3 Mheshimiwa Spika, aidha Serikali ipunguze ukubwa wa majukumu yake kwa kupunguza idadi ya wizara, tume na wakala mbalimbali, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kama semina, warsha na makongamano ya kupanga bajeti; kuandaa mipango ya maendeleo ambayo haitekelezeki kirahisi; kukata matumizi ya manunuzi ya magari na matumizi ya magari yanayozidi ujazo wa injini wa CC 3000 maarufu kama "mashangingi", na kupunguza matumizi ya mafuta ya magari.

3.1.4 Mheshimiwa Spika, Kamati bado inasisitiza kuwepo na mfumo madhubuti wa kisheria na kiutawala kwa kila halmashauri katika kuhakikisha kunakuwepo usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji, ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato na hatimaye kukusanya kodi kikamilfu. Sekretarieti za Mikoa zihakikishe zinabainisha na kutunza orodha na kumbukumbu muhimu za miradi yote katika halmashauri, iliyotekelezwa, inayotekelezwa na ile inayopendekezwa.

3.1.5 Mheshimiwa Spika, hakuna nchi iliwahi kuendelea bila kukusanya mapato. Vile vile, hakuna halmashauri itatekeleza miradi yake ya maendeleo kwa wananchi bila kukusanya mapato. Kamati yetu imetoa maelekezo mahsusi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuielekeza mikoa yote kusimamia zoezi jipya na mahsusi la kuchambua, kutathmini na kuhakiki vyanzo vya mapato na namna ya kutengeneza mfumo madhubuti wa kukusanya mapato kwa tija na ufanisi na kuziba mianya yote ya uvujaji wa mapato kwa kutumia teknolojia za kisasa za kupiga picha za 'satellite' na 'Geographical

information systems (GIS)'. Eneo moja mahsusi ambalo ni roho ya halmashauri nyingi duniani ni lile la kodi ya majumba (property tax); litazamwe kwa ukaribu zaidi.

3.1.6 Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri serikali kutengeneza Mpango wa dharura wa motisha kwa wafanyakazi wa mstari wa mbele unaozingatia jiografia (Essential frontline workers' differential incentive package), kwenye vijiji vya mbali (remote areas). Mpango huu ni lazima utekelezwe kwa kutoa kipaumbele kwa wananchi kushirikiana na serikali yao kujenga nyumba za watumishi hawa wa idara muhimu za huduma ya jamii kama afya, elimu, kilimo na utawala vijijini, posho mbalimbali (mfano, posho za mazingira hatarishi, kazi maalum kama kufundisha masomo ya hisabati na sayansi ama kufanya operesheni za akinamama wajawazito vijijini, mazingira magumu ya kazi, masaa ya ziada, na ujuzi maalum), pia kuhakikisha huduma za mawasiliano vijijini, umeme vijijini na za kibenki zinapatikana kwa urahisi.

3.1.7 Mheshimiwa Spika, Kamati inaiagiza serikali kuunganisha wizara zote zinazohusika na ardhi, kupitia uongozi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kukaa kwa pamoja, kutathmini mapungufu ya kisheria yanayosababisha migogoro ya ardhi nchini na kupendekeza mabadiliko ya Sheria mbali mbali (zikiwemo za uchimbaji madini, umiliki wa ardhi yenye madini, za ujenzi na uendelezaji ardhi, za fidia ya ardhi na mali iliyowekwa juu ya ardhi, za ardhi ya hifadhi na mgawanyo wa ardhi kwa matumizi mbalimbali). Wachimbaji wadogo wadogo nao ni binadamu, nao ni watanzania, nao wanatamani kutajirika na urithi wan chi yao; mabadiliko ya sheria yaende sambamba na kuwatengea maeneo mahsusi ya wao kuchimba madini. Migogoro baina ya wakulima na wafugaji imezidi na haikubaliki; wakati umefika tuipatie suluhu ya kudumu. Mabadiliko haya yaletwe mapema kabla mwaka 2015 haujaisha ili yatusaidie kuondoa

migogoro ya ardhi nchini. Agizo hili tumelitoa miaka miwili iliyopita mfululizo. Ni matumaini yetu kuwa litafanyiwa kazi na mapendekezo ya sheria yataletwa Bungeni kabla ya mwaka huu kuisha.

3.1.8 Mheshimiwa Spika, jambo jingine la kisera na kimkakati ambalo tumeona ni vema likatazamwa ni namna ugatuaji wetu kwenye sekta ya afya haujatusaidia kuboresha huduma hii nyeti. Kamati inaishauri serikali kutazama namna ya kuzipa mamlaka kamili hospitali za wilaya, mikoa na rufaa, na pia zahanati na vituo vya afya nchini, ili vijiendeshe kibiashara (fiscal decentralization). Mpango huu uende sambamba na kuanza kutoza gharama za afya kwa wateja wote wa huduma ukitoa makundi maalum yanayopewa msamaha na sera na sheria zetu, kuboresha na kuhamasisha wananchi kuingia kwenye mfuko wa afya ya jamii ama mifuko mbalimbali ya hifadhi ya jamii au bima ya afya na kuanzisha mpango maalum wa serikali kuu kupeleka pesa zake za ruzuku kwa kupima utendaji wa kituo husika (pay for performance). Wananchi wako tayari kulipia gharama zao za afya, lakini wanataka ubora wa huduma (quality of healthcare) na uhakika wa vipimo na upatikanaji wa madawa ama tiba stahiki kwa maradhi yao. Hatuwezi kufikia ubora kama tunaendelea kutegemea zaidi ya asilimia 65 ya fedha za bajeti yetu ya afya kutoka kwa wahisani.

3.1.9 Mheshimiwa Spika, ili kuhamasisha uwajibikaji wa halmashauri zetu, Kamati yetu inaishauri serikali itazame upya dhana ya ugatuaji wa madaraka na utaratibu wa kupeleka fedha kutekeleza miradi kutoka serikali kuu kupeleka chini bila kuwapa malengo mahsusi (targets), na iweke mpango kazi mahsusi wa kukamilisha ugatuaji wa madaraka kamili kwenye halmashauri zetu ili zijitegemee. Mpango wa kupeleka fedha kutokana na malengo (targets) na upimaji wa matokeo ya utekelezaji wa malengo (pay-for-performance) unaweza kutazamwa kwa kuanzia,

kwenye sekta za afya, elimu, barabara, kilimo na uwezeshaji wananchi. Hii itahamasisha ushindani baina ya halmashauri na nyingine, baina ya kijiji na kingine, baina ya mkoa mmoja na mwingine, na hatimaye kuleta tija na ufanisi wa hali ya juu zaidi ya ilivyo sasa, ambapo kila mkoa, kila halmashauri inajua itapata tu pesa kutoka serikali kuu.

3.1.10 Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaishauri serikali kubuni mradi wa kuboresha makazi ya wananchi waishio vijijini kwa kuanzisha mpango wa uendelezaji ardhi vijijini. Mradi huu uje na jitihada za kuwawezesha wananchi kujenga nyumba za kudumu na za kisasa, kuwapa ushauri wa kilimo cha kisasa, utunzaji wa mazingira na ushiriki wa pamoja kwenye ujenzi wa uchumi. Vijiji vya Tanzania mpya haviwezi kuwa vya kizamani na visivyopangwa. Viongozi wa zama hizi tunapaswa kuja na mawazo mapya na ya kisasa yanayoongeza ubora wa maisha ya wananchi wenzetu vijijini. Mradi wa kujenga vijiji vya kisasa uje na mpango kabambe wa serikali kuu kutengeneza sera na mpango mkakati wa namna ya kujenga nyumba za kisasa, za kudumu na za gharama nafuu vijijini sambamba na mambo mtambuka niliyotaja hapo juu, na serikali za mitaa husika kwa upande wake, ziajiri waratibu wa mradi huu ili wasimamie zoezi hili. Serikali inaweza ikabuni namna ya kutoa motisha kwa kuwachangia wananchi ruzuku ya kutekeleza miradi ya namna hii, na wananchi nao watapaswa kuanzisha 'ushirika wa kujengeana nyumba za kisasa'. Kila mtanzania ana haki ya kumiliki na kuishi kwenye nyumba bora na ya kisasa, tuwawezeshe.

3.1.11 Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri serikali kutazama uwezekano wa kuibua mpango wa dharura wa kuzalisha ajira nyingi kwa haraka kupitia uwezekezaji mkubwa kwenye kilimo, viwanda vidogo vidogo na biashara za mazao ya kilimo. Mpango huu uende sambamba na mpango mpya na wa haraka wa

kuanzisha shule za ufundi stadi (VETA) kwenye kila wilaya kwa kufikiria kupunguza idadi ya shule za sekondari kwa kuzigeuza baadhi ya shule zilizopo kuwa VETA kule vijijini na ku-'concentrate' jitihada zote kwenye ubora zaidi wa shule zetu kwa kujenga mabweni, maabara, nyumba za kutosha za walimu, kupeleka umeme na maji na kujenga na kuimarisha maktaba. Mfano kwenye eneo lenye shule tano, mbili zaweza kugeuzwa kuwa VETA na nyingine zikaimarishwa na kuboreshwa kuendelea kuwa shule za sekondari. Vituo vya VETA vina faida kubwa na za haraka sana kwenye uchumi wa watu binafsi, jamii na Taifa kwa ujumla, maana kila mhitimu anaweza kujiajiri ama kuajiriwa kwenye mfumo usio rasmi, na hata rasmi, na tayari kwa sasa serikali ina sera nzuri ya kuendeleza watoto watakaopitia mfumo huu wa elimu ya ustadi wa kazi. Aidha mfumo huu unachukua waliofeli darasa la saba, na waliofeli kidato cha nne na cha sita na kuwapa fursa ya pili (second chance) katika maisha tofauti na mfumo wa elimu wa kisekula.

3.1.12 Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaiagiza serikali kuhakikisha inakamilisha uchambuzi na uhakiki wa madeni ya watumishi kwenye sekta mbalimbali ili walipwe stahili zao. Taarifa ya utekelezaji iletwe mbele ya Kamati kabla ya mwaka huu wa fedha kumalizika. Madeni ya walimu na watumishi wa kwenye sekta ya afya, ambayo yamekuwa ya muda mrefu sasa, yalipwe mara moja bila kuchelewa. Taarifa mahsusi ya utekelezaji wa agizo hili iletwe mbele ya Kamati wakati wa Bunge la bajeti, kwamba kulikuwa na walimu/whudumu wa afya wangapi wenye madeni, kiasi gani, na wamelipwa ama hawajalipwa. Jambo moja ni la uhakika, kwamba, Kamati haitoridhika na utekelezaji wa shughuli za serikali kwenye sekta hii kama hakutokuwa na taarifa ya madeni haya sugu ya watumishi wetu.

3.1.13 Mheshimiwa Spika, Pamoja na kuzingatia umuhimu wa usafi wa mazingira ya maeneo tunayoishi,

kuzingatia uwezekano wa kukusanya mapato kutoka kwa wafanyabiashara hawa na kuzingatia uendelezaji wa maeneo kwa kufuata ramani za mipango miji, kasumba ya kuwakimbiza wafanyabiashara ndogo ndogo kama wanyama bila kuwatengenezea maeneo yenye vivuli na huduma mbali mbali za kibinadam imetamalaki nchini. Kamati imekuwa ikikataza tabia endelevu ya migambo wa halmashauri zetu nchini, hususan wale wa kwenye majiji, manispaa na miji, kuwanyanyasa na kuwaonea, kumwaga vyakula vya mama ntilie, kuwanyang'anya wamachinga bidhaa zao na kuwapiga kama watumwa. Naomba habari hii iwafikie wote kuwa, ndani ya Tanzania huru na ya kizazi cha kuhoji, mambo ya namna hii hayakubaliki! Sisi viongozi wa zama hizi za mabadiliko hatuko tayari kuvumilia mambo ya namna hii. Hivyo basi, Kamati inawaagiza wakuu wote wa mikoa na wilaya nchini kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria wakurugenzi wote wa halmashauri ambazo zitabainika kuendelea kufanya hivyo, na Mkuu wa Mkoa ama wa Wilaya yoyote nchini atakayeshindwa kusimamia agizo hili, mamlaka yake ya uteuzi ifikirie upya uhalali wa yeye kuendelea kuwepo kwenye nafasi aliyopewa.

3.1.14 Mheshimiwa Spika, Kamati inaiagiza serikali kuangalia uwezekano wa kuanzisha makampuni ya ujenzi ya mkoa na mabenki ya kijamii ya kimikoa. Makampuni haya yamilikiwe na halmashauri za mkoa husika na wananchi kupitia ushirika wao, SACCOS zao na taasisi mbalimbali za kifedha na za kijamii. Makampuni ya ujenzi yajihusishe na ujenzi wa mabarabara vijijini na mitaani na kuchimba visima, wakati yale ya kibenki yasaidie kufikisha huduma za kifedha na za kibenki vijijini kwa wananchi ikiwemo mikopo ya wafanyabiashara ndogo ndogo na wakulima.

3.1.15 Mheshimiwa Spika, Wabunge wamekuwa wakitoa maoni yao mara kwa mara katika mijadala

mbalimbali kuhusu suala la watendaji wengi wa halmashauri kukaimu nafasi mbalimbali kwa muda mrefu. Kamati inatoa mapendekezo kwa Serikali, hususan Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Menejimeni ya Utumishi wa Umma, ihakikishe kwamba, katika muda mfupi ujao, mabadiliko ya kiutumishi katika halmashauri zote ambazo zimekuwa na watendaji wanaokaimu kwa muda mrefu ili idara ziwe na watumishi wenye uwezo wa kufanya maamuzi yote kwa utimilifu.

3.1.16 Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu na msisitizo wa kipekee, Kamati inatoa wito kwa Madiwani na Wabunge kama viongozi na wawakilishi wa wananchi, kwa kuwa tunao uwezo na dhamana ya kuwasimamia watendaji wasiotekeleza majukumu yao kwa maendeleo ya Wananchi, tuhakikishe kuwa tunashiriki kikamilifu katika vikao mbalimbali vya halmashauri zetu, hasa vile vya Kamati za Fedha (Finance Committees) na pia Baraza la Madiwani (Full Council) ili kuwa wasimamizi wa mwanzo wa utekelezaji wa halmashauri zetu. Aidha wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya, kamwe tusiache au kupuuzia kutekeleza jukumu la usimamizi thabiti unaochochea maendeleo.

4.0 HITIMISHO

4.1 Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya TAMISEMI itaendelea kuwa mstari wa mbele kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, kutekeleza jukumu la kiusimamizi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kuwa, bajeti inatengwa kuzingatia vipaumbele vinavyowaletea wananchi huduma

muhimu lakini muhimu zaidi, kuhakikisha kuwa bajeti hiyo inatekeleza malengo yaliyowekwa kwa ufanisi.

4.2 Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa napenda kumshukuru Mhe. John Paul Lwanji (Mb) Makamu Mwenyekiti wa Kamati, kwa msaada anaonipa kuiongoza Kamati wakati ninapokuwa natekeleza majukumu mengine ya kitaifa. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah kwa uratibu wa shughuli mbalimbali za Kamati.

4.3 Mheshimiwa Spika, kipekee nitoe shukrani kwa Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akisaidiwa na Mhe. Aggrey Deaisile Joshua Mwanri (Mb) na Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb), Naibu Mawaziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Watendaji wa Ofisi hiyo wakiongozwa na Ndg. Jumanne A. Sagini, kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake.

4.4 Mwisho lakini sio kwa umuhimu, naomba niwatambue makatibu wa Kamati ya Bunge ya TAMISEMI Ndg. Yona P. Kirumbi, Ndg. Mwajuma N. Ramadhan, Ndg. Mossy Lukuvi wakisaidiwa na Ndg. Cletty Urassa kwa utumishi wao katika kipindi chote ambacho Kamati hii imekuwa ikitekeleza wajibu wake na hatimaye kuandikwa kwa taarifa hii.

4.5 Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa naliomba Bunge liipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kuyakubali maoni na mapendekezo ya

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili yaweze kuwa sehemu ya Maazimio ya Bunge kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA

02 Februari, 2015

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mfutakamba unaweza kuchukua maji ukaenda nayo tu. *(Kicheko)*

(Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kama ilivyosomwa Bungeni)

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O - MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa ya shughuli za Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kwa kipindi cha Februari, 2014, hadi Januari, 2015. Kabla sijaanza, ninaomba Taarifa yote iingizwe kwenye *Hansard,* kwa sababu ya muda sitaweza kusoma yote.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu shughuli zake kwa kipindi cha Februari, 2014 hadi Januari, 2015 kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Kamati. Kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2013, Kamati ya Masuala ya UKIMWI ina jukumu ya kushughulikia mambo yafuatayo:-

(i) Kuratibu masuala yanayohusu UKIMWI katika sekta zote;

(ii) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na Udhibiti wa Dawa za kulevya;

(iii) Kujadili na kutoa mapendekezo na ushauri kuhusu hatua za kudhibiti madawa ya kulevya; na

(iv) Kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelezwa na Kamati ni kama iifuatavyo:-

(i) Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Kamati pamoja na kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na dawa za kulevya;

(ii) kushughulikia Bajeti za Taasisi hizo;

(iii) kushiriki kwenye mikutano na wadau;

(iv) ziara za mafunzo;

(v) kushiriki semina ili kujielimisha mambo muhimu; na

(vi) kupitia na kuchambua Miswada miwili ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 hadi 25 Julai, 2014, Kamati ilipata fursa ya kuhudhuria Mkutano wa 20 wa Kimataifa wa UKIMWI, uliofanyika nchini Australia katika Jiji la Melborne. Mkutano huo ni wa 20 tangu kuanzishwa kwake na umekuwa ukifanyika kila baada ya miaka miwili. Aidha, katika semina hiyo, kulikuwa na semina iliyoandaliwa na *IPU* kwa Wabunge wote waliohudhuria Mkutano huo wa Dunia, iliyofanyika katika Bunge la Victoria. Bunge la Tanzania lilipongezwa kwa kuwa mfano wa kuigwa Duniani na Mabunge mengine kwa jinsi linavyoshughulikia masuala ya UKIMWI ikiwa ni pamoja na kuanzisha Kamati ya kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI na Chama cha Wabunge cha Kupambana na UKIMWI *(TAPAC)*. Aidha, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alipongezwa kwa juhudi zake katika kupunguza vifo vya akina mama na Watoto wachanga. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huo, Kamati ilijifunza mambo yafuatayo:-

(i) umuhimu wa kuwashirikisha Wabunge katika kutokomeza UKIMWI na kufikia sifuri tatu *(Engaging Parliamentarians to get to three zeros);*

(ii) umuhimu wa kutenga rasilimali fedha za kutosha za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI;

(iii) mkanganyiko uliopo kati ya Janga la UKIMWI na Haki za Binadamu;

(iv) mahusiano yaliyopo baina ya unyanyasaji wa kijinsia na UKIMWI; na

(v) uhusiano uliopo baina na UKIMWI na tohara kwa wanaume.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara kukutana na shirika lisilokuwa la kiserikali la *Pili Missanah Foundation,* lililoko Kigamboni, ambalo linasimamia na kutoa huduma kwa watumiaji wa dawa za kulevya *(Sober House),* mbili ambazo ziko huko Kigamboni. Ziara hiyo ilikuwa na nia ya kupokea taarifa ya namna shirika hilo linavyopambana na dawa za kulevya na namna linavyojitahidi kuwaokoa waathirika wa dawa hizo hususan vijana ambao ni wengi wamethirika na matumizi ya dawa hizi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Kituo cha SAADA kilichopo chini ya Kituo cha Polisi Mkoa wa Dodoma. Kikundi hiki cha *Small Axe Against Drugs (SAADA)* kilianzishwa tarehe 20 Oktoba, 2009, kina vijana 26. Tangu kuanzishwa kwake Kituo hiki kimekwishahudumia vijana 156 na kuwaondoa katika utumiaji wa dawa za kulevya na hivyo kwa kiasi kikubwa kupunguza matendo mengi ya kihalifu. Huduma mbalimbali kama ushauri, matibabu na huduma za elimu hutolewa katika Kituo hiki.

Pamoja na mambo mazuri yanayofanywa na Kituo hiki, bado kinakabiliwa na changamoto mbalimbali, miongoni mwake ni pamoja na ukosefu wa jingo na ufinyu wa bajeti. Aidha, gharama kubwa za kuwapeleka waathirika *Sober House* Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kituo hiki kikabidhiwe jengo ambalo lipo jirani na kituo hiki ili kiweze kutumiwa na vijana. Jengo hili ni mali ya Wizara ya Kazi na Ajira na halijaendelezwa muda mrefu. Kamanda wa Polisi Dodoma, alishaandika barua ya kuliomba jengo hili.

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa kipindi cha mwaka uliopita, imechambua Miswada miwili ya Sheria zifuatazo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria ya Tume ya Kuthibiti UKIMWI (The Tanzania Commission for AIDS (Amendment) Bill, 2014); na

(ii) Muswada wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Dawa za Kulevya (The Drug Control and Enforcement Bill, 2014).

Mheshimiwa Spika, Kamati inachukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati wadau wote walioitikia wito wa kushiriki katika Mkutano wa Kamati hii na wadau kwa ajili ya *public hearing*. Hakika mawazo yao kwa kiasi kikubwa yamesaidia uboreshwaji wa Miswada yote miwili. Mahudhurio yao na ushiriki katika Mikutano ya Kamati imeonesha wananchi walivyo makini na walivyo tayari kufanya kazi na Bunge lao Tukufu kwa masilahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwitikio wa Taifa umelenga kufikia malengo yaliyowekwa Kimataifa 90-90-90, yaani 90% kwa waliopima afya zao na kutambua hali yao ya maambukizi, 90% wanaostahili kupata tiba na 90% ya waliopo kwenye tiba wenye kiwango kidogo cha Virusi vya UKIMWI kwenye damu ifikapo mwaka 2020. Lengo likiwa ni kufuta UKIMWI ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, itakuwa ni vigumu kwa Tanzania kufikia lengo hili kama hakutakuwa na rasilimali endelevu, kwani asilimia 97 ya fedha zote za mapambano dhidi ya UKIMWI zinategemea Wadau wa Maendeleo ambao ni Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa Dharura wa Rais *(PEPFAR)*, Mfuko wa Dunia wa Kifua Kikuu, Malaria na UKIMWI na wengineo.

Kwa kuwa baadhi ya wafadhili wamejitoa na wengine wanafikiria kujitoa kufadhili suala hili la kupambana na UKIMWI, kuna hatari kubwa sana inakuja siku za usoni kama hatutakuwa na jitihada za makusudi za kubuni vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinatisha. Kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo hili na kwa kuzingatia ukweli kwamba, wadau wanajitoa kufadhili masuala haya ya UKIMWI, Kamati inashauri kwamba ni wakati mwafaka wa Tanzania kuwa na Mfuko wa Taifa wa Kupambana na UKIMWI, ili kuwa na rasilimali endelevu.

Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwani mchakato wa kuanzisha Mfuko huu umeashaanza; hivyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono uanzishwaji wa Mfuko huu na upitishwaji wa sheria husika katika Mkutano wa Bunge lijalo. Aidha, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Wadau wa Maendeleo kwamba, rasilimali chache zilizopo za mapambanao dhidi ya UKIMWI zielekezwe kwenye maeneo yenye maambukizi makubwa ya UKIMWI ili kutoa matokeo ya haraka.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Wizara ya fedha na kuelezwa kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, kiasi cha shilingi bilioni 6.22 zilitengwa kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kupitia bajeti ya matumizi ya kawaida kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 140.24 kilitengwa kupitia bajeti ya maendeleo. Kati ya hizo, shilingi bilioni 3.0 ni fedha za maendeleo ya ndani na shilingi bilioni 137.24 ni fedha za maendeleo kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, hadi Januari, 2015 kiasi cha shilingi bilioni 2.00 tu cha fedha za maendeleo zilikuwa zimetolewa na wafadhili, fedha za ndani hazikutolewa. Aidha, katika Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, ilitengwa jumla ya shilingi bilioni 10.54 kupitia bajeti ya maendeleo ya fedha za nje, kwa ajili ya Mikoa na Halmashauri nchini. Kati ya hizo, shilingi bilioni 9.01 zilitengwa kwa ajili ya Halmashauri na shilingi bilioni 1.53 ni kwa ajili ya Sekretarieti za Mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa hakuna hata shilingi moja iliyotolewa kwenye Mkoa na hata kwenye Mikoa yenye maambukizi makubwa zaidi kama Njombe, Iringa, Mbeya na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kupambana na UKIMWI hazijapelekwa, Kamati inaomba Bunge hili kuitaka Serikali, kama kweli ina dhamira na utashi wa kuwalinda Watanzania na maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI, ambao wengi wao ni vijana na wanawake, fedha hizi zipelekwe mara moja na Bunge lako Tukufu lielezwe sababu ya kutopeleka fedha hata kwa Mikoa yenye maambukizi makubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa unyanyapaa na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto ni tatizo kubwa na ni moja ya vyanzo vya maambukizi mapya ya UKIMWI kutokana na mila potofu katika jamii zetu, Kamati inaishauri Serikali, wanawake wawezeshwe kwa kuandaliwa programu maalum za kuwajengea uwezo, ikiwa ni pamoja na Halmashauri kuendelea kutenga fedha, asilimia kumi ya mapato yao kwa ajili ya wanawake na vijana.

Kamati inatambua mchango mkubwa wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwani amefanya mambo mengi mazuri ya kuigwa katika suala mapambano dhidi ya UKIMWI, ikiwa ni pamoja na kuwaongoza Watanzania kupima ili kujua afya zao tarehe 14 Julai, 2007, hali iliyochangia Watanzania wengi kupima na kuondoa unyanyapaa miongoni mwa jamii.

Kamati inashauri kwamba, ile siku aliyopima Mheshimiwa Rais, iwe ni Siku ya Upimaji wa UKIMWI nchini ili iwe ni kumbukumbu ya kuhamasisha Watanzania ili kujua afya zao. Aidha, siku hii pia iwe ndiyo Siku ya Uzinduzi wa UKIMWI Duniani ambayo kilele chake huwa ni tarehe 1 Desemba ya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inalipongeza Baraza la Waishio na Virusi vya Ukimwi (WAVIU), kwa kuweza kuanzisha konga katika Halmashauri za Wilaya 135 nchini. Hii itasaidia watu waishio na Virusi vya UKIMWI kuwa na sauti moja. Hata hivyo, Baraza la WAVIU linakabiliwa na ukata, hali inayosababisha kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kamati inaendelea kuishauri Serikali, kutenga bajeti ambayo itasaidia Baraza hili kujiendesha na kupunguza utegemezi ukizingatia umuhimu wa Baraza lenyewe katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Bila kujitoa kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI vita hii ya kupambana na janga la UKIMWI ingekuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, ili majukumu muhimu ya Tume ya kudhibiti UKIMWI yatekelezwe kwa ufanisi, Kamati inashauri:-

(i) Serikali iongeze kasi ya maboresho ya Sera ya Taifa ya UKIMWI;

(ii) Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ishirikiane na Sekretatieti za Mikoa na Wilaya kwa kuandaa Programu za Kazi na Mpango Kazi wa Kupambana na UKIMWI katika ngazi zote;

(iii) Kamati inaitaka Serikali kupitia Tume kuanzisha programu maalum zitakazosaidia tatizo la ukatili wa kijinsia; na

(iv) Kamati inaitaka Serikali na Tume ya Kudhibiti UKIMWI kuhakikisha fedha za UKIMWI zinazotolewa zinakwenda kwa walengwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hakuna takwimu sahihi za watu watumiaji dawa za kulevya kwa njia ya kunusa, kuvuta, kupangusa au kupaka. Takwimu za watu wanaotumia dawa za kulevya hapa nchini wanazidi kuongezeka siku hadi siku na kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu *(UNODC)* inakadiriwa Watanzania kati ya 25 na 50, hutumia dawa hizo kwa njia ya kujidunga sindano.

Kamati inashauri kwamba, watumiaji hao wawekewe programu maalumu ya kuwaelimisha juu ya athari ya dawa za kulevya. Aidha, Elimu hii ni vyema kuwekwa katika mitaala na kuanza kufundishwa kuanzia Shule za Msingi hadi Vyuo Vikuu na jamii kwa ujumla ili kuokoa kizazi chetu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa watu wanaojidunga kuhusu huduma za afya hali inayochangia ongezeko kubwa la UKIMWI kwa watumiaji wa dawa za kulevya. Kamati inashauri kwamba, watoaji huduma katika Sekta ya Afya wapewe mafunzo maalumu ya namna ya kuhudumia watu walioathirika na dawa za kulevya ili wapatiwe matibabu stahili wanayohitaji na hivyo kwa kiasi kikubwa kupunguza ongezeko la maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea *Sober House* ya Kigamboni zinazoendeshwa na Taasisi ya Pili Missana. Kamati inapongeza juhudi kubwa zinazofanywa na taasisi hii na mfadhili wake Zakaria HansPope. Kamati iligundua kwamba huduma za afya ni duni. Kamati inashauri Manispaa ya Temeke kutembelea vituo hivi na kuweza kuangalia ili kuona namna wanavyoweza kusaidia kuwapatia huduma bora za afya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliwaahidi kuwapatia kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Kituo, kwani walipo wamepanga. Kamati inaishauri Halmashauri ya Temeke iwape kiwanja ili kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais na kuomba wadau mbalimbali wajitolee kujenga kituo hicho kwa manufaa ya vijana wetu. Pia Halmashauri iwasaidie

vijana hao mikopo kupitia fedha zinazotengwa kwa ajili ya wanawake ili waanzishe shughuli za kiuchumi ili kupunguza utegemezi kwani baadhi yao wana taaluma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wapo wafungwa wengi Magereza ambao walikuwa wakitumia dawa za kulevya, lakini kwa bahati mbaya Magerezani hakuna huduma ya tiba kwa watu wanaotumia dawa za kulevya. Tiba kwa watumiao dawa za kulevya kama *Methadone* hutolewa katika Hospitali tatu, yaani Hospitali ya Muhimbili, Mwananyamala na Temeke. Kamati inatoa ushauri kwamba, wafungwa walio Magerezani, wapewe *program* ya *Methadone* wakiwa katika Magereza na pia wawe na vituo vya ushauri na huduma kama ilivyo kwa Polisi ili wakitoka Magerezani wawe wameacha matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa kwamba, katika kipindi cha kuanzia Januari mwaka 2013 hadi Agosti, 2014, Kikosi Kazi kimeweza kukamata dawa za kulevya kama mchanganuo unavyoonesha katika jedwali tuliloambatanisha.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ukamataji huo, jumla ya ekari 536.5 za mashamba ya bangi ziliteketezwa pamoja na kilo 3,445 za mbegu za bangi ziliharibiwa. Katika kipindi hicho hicho, jumla ya mashauri 27 ya kesi kubwa ya dawa za kulevya yalisajiliwa katika Mahakama Kuu ambapo mashauri 26 yamesajiliwa kanda ya Dar es Salaam, manne Kanda ya Kilimanjaro, moja Pwani, moja Tanga na moja Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali katika vita hii ngumu na pia kwa kukamilisha ujenzi wa ghala la kuhifadhi vielelezo. Pia tunakipongeza Kikosi Kazi kwa kushirikiana na Tume ya Uthibiti wa Dawa za Kulevya kwa kupambana na tatizo hili kubwa kwa mustakabali wa nchi yetu kwani linaangamiza nguvu kazi ya Taifa. Hata hivyo, Kamati inasikitishwa kwa utoaji wa fedha kidogo kwa Tume kwani fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2014/2015 zilikuwa Shilingi bilioni 4.42 fedha

za matumizi ya kawaida, lakini hadi Januari, 2015 ni Shilingi bilioni moja tu zilizotolewa.

Aidha, kwa fedha za maendeleo, kiasi cha Shilingi bilioni 3.43 zilitengwa lakini hadi kufikia Januari, 2015 ni kiasi cha Shilingi milioni 150 tu kilichotolewa. Kamati inashauri Serikali kutoa fedha tena kwa wakati kwa Tume hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ukizingatia nguvu ya fedha walizonazo wafanyabiashara wa dawa hizi za kulevya.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya kudhibiti biashara haramu ya dawa za kulevya inatumika katika kutoa adhabu kwa makosa yanayohusiana na biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Hata hivyo, sheria hiyo ina upungufu ufuatao:-

(i) Sheria haijakataza kumiliki, kuuza na kusambaza mbegu za bangi au mbegu za aina yoyote ya dawa za kulevya;

(ii) Sheria haitoi adhabu kwa watu watakaokutwa na maabara au mitambo kwa ajili ya kutengeneza dawa za kulevya;

(iii) Sheria imeweka dhamana kwa kigezo cha thamani ya dawa hizo;

(iv) Sheria haikuipa Tume mamlaka ya kupekua na kukamata wafanyabiashara wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, kufuatia upungufu huo, sheria mpya ambayo itarekebisha upungufu inahitajika kwa haraka. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya ili kuwa na sheria itakayokuwa na meno. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mchakato wa Sheria mpya unaendelea vizuri, kwani tayari Muswada wa Sheria umeshafika na kuvuka katika ngazi ya Kamati na huenda ukajadiliwa katika Mkutano wa Bunge lijalo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kwamba, pamoja na ujio wa sheria tajwa, ni vema pia ikatumia uzoefu wa nchi nyingine zilizofanikiwa katika mapambano dhiti ya udhibiti wa dawa za kulevya kama Bangladesh na India.

Mheshimiwa Spika, pamoja na tatizo la dawa za kulevya kuwa kubwa, hakuna Sera ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya hapa nchini. Hata hivyo, Kamati iliarifiwa kwamba, Rasimu ya Sera ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya imeshapitiwa na Sekreatrieti ya Baraza la Mawaziri na inasubiri kupitiwa na kikao cha pamoja baina ya Makatibu Wakuu na Baraza la Mawaziri.

Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba, mchakato wa uandaaji wa Sera hiyo ya Taifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya hasa ikizingatiwa kwamba sera ndiyo hutangulia kuweka misingi ya uundwaji wa sheria, mchakato uanzishwe haraka.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza vema majukumu ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya**,** Kamati inashauri**:-**

(i) Kuharakishwa kwa mchakato wa Sera na Sheria ya Kudhibiti Dawa za Kulevya;

(ii) Kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016 Tume ijipange kuanzisha vituo vya kutosha (*sober houses*) kuhudumia waathirika wa dawa za kulevya kwa kushirikiana na wadau;

(iii) Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa Tume ya Uratibu wa Dawa za Kulevya kwani tatizo ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kabla sijamalizia, napenda niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, Hivyo, Kamati inatoa ushauri kwa vyama vyote vya siasa na wagombea watakao jitokeza, wajitokeze kulifanya suala la UKIMWI na Dawa za Kulevya kuwa ni moja ya ajenda katika kampeni zao.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Mwezi Februari, 2015. Tunaamini kwamba fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117, Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Uongozi kwa ushirikiano wao katika uendeshaji wa Bunge letu. Pia nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya masuala ya UKIMWI kwa ushirikiano wao mkubwa uliowawezesha kutekeleza majukumu ya Kamati. Nawashukuru kwa moyo wao wa kujitolea na michango waliyoitoa kwa vijana wetu wenye matatizo sehemu zote ambazo Kamati ilitembelea.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge - Mheshimiwa William Lukuvi, Mbunge, kwa ushirikiano mkubwa alioutoa kwa Kamati. Tunampongeza sana kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi. Tunamwombea Mwenyezi Mungu amwongoze katika utekelezaji wa majukumu yake mapya.

Kamati pia inampongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. Kamati ina imani kubwa na wewe kwani tunafahamu ulivyo imara katika vita hii ukiwa mwanachama mwanzilishi wa *TAPAC,* Kamati inakuahidi ushirikiano mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mwenyekiti Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI, Kamishna wa Tume ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya pamoja na Watendaji wa Taasisi mbalimbali za Serikali kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati wote wa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, naishukuru Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah kwa kuiwezesha Kamati wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati, Ndugu Abdallah Hancha na Ndugu

Mossy Lukuvi kwa kuratibu vema shughuli za Kamati kwa kipindi chote na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa, naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kuyakubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

Taarifa ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kama ilivyowasilishwa Mezani

RASIMU YA TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA MASWALA YA UKIMWI KWA KIPINDI CHA FEBRUARI 2014 HADI JANUARI, 2015

SEHEMU YA KWANZA

MAELEZO YA JUMLA

1.0 UTANGULIZI:

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maswala ya UKIMWI kuhusu shughuli zake kwa kipindi cha Februari, 2014 hadi Januari, 2015 kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013.

1.1 WAJUMBE WA KAMATI:

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati hii waliteuliwa Mwezi Machi, 2013 kwa mujibu wa Kanuni ya 116 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013. Naomba kuwatambua wajumbe hao kwa kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

(i)	Mhe. Lediana Mafuru Mng'ong'o, Mb -	Mwenyekiti
(ii)	Mhe. Diana Mkumbo Chilolo, Mb -	M/Mwenyekiti
(iii)	Mhe. Maida Hamad Abdallah, Mb-	Mjumbe
(iv)	Mhe. Chiku Aflah Abwao, Mb	"
(v)	Mhe. Said Suleiman Said, Mb	"
(vi)	Mhe. Omary Ahmed Badwel, Mb	"
(vii)	Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb	"
(viii)	Mhe. Anna M. John Mallack, Mb	"
(ix)	Mhe. Maria Ibeshi Hewa, Mb	"
(x)	Mhe. Rashid Ali Omar, Mb	"
(xi)	Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb	"
(xii)	Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb	"
(xiii)	Mhe. Mch. Luckson N. Mwanjale, Mb	"
(xiv)	Mhe. Mwanamrisho Taratibu Abama, Mb	"
(xv)	Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mb	"
(xvi)	Mhe. Ignus Aloyce Malocha, Mb	"
(xvii)	Mhe. Selemani Said Bungara, Mb	"
(xviii)	Mhe. Neema Mgaya Hamid, Mb	"
(xix)	Mhe. Sara Msafiri Ally, Mb	"
(xx)	Mhe.Maulida Anna Valerian Komu,Mb	"
(xxi)	Mhe. Ahmed Ali Salum, Mb	"

1.2 MAJUKUMU YA KAMATI:

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la mwaka 2013, Kamati ya Masuala ya UKIMWI ina jukumu la kushughulikia mambo yafuatayo:-

(i) Kuratibu Maswala yanayohusu UKIMWI katika sekta zote;

(ii) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na Udhibiti wa Dawa za kulevya;

(iii) Kujadili na kutoa mapendekezo na ushauri kuhusu hatua za kudhibiti madawa ya kulevya; na

(iv) Kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

SEHEMU YA PILI

MAELEZO YA KAZI ZILIZOTEKELEZWA

2.0 KAZI ZILIZOTEKELEZWA;

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia Kamati ya UKIMWI ni Kamati mtambuka, Katika kipindi cha Mwaka uliopita, Kamati ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kusimamia na kufuatilia Utekelezaji wa majukumu ya taasisi zilizochini ya Kamati pamoja na kufuatilia utekelezaji wa sera namipango ya serikali kuhsu UKIMWI na dawa za kulevya;

(ii) Kushughulikia Bajeti za Taasisi hizo;

(iii) Kushiriki kwenye mikutano na wadau;

(iv) Ziara za Mafunzo;

(v) Kushiriki Semina ili kujielimisha mambo muhimu; na

(vi) Kupitia na kuchambua miswada miwili ya sheria

2.1 KUSIMAMIA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia mpango kazi wa Kamati wa mwaka 2014/15 ulioandaliwa kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la mwaka 2013 ikiwemo Kanuni ya 117 inayohusu utaratibu katika Kamati za Kudumu za Bunge, Kamati ilisimamia Tume mbili zilizo chini yake yaani Tume ya Taifa ya Kupambana na UKIMWI

(TACAIDS), Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya pamoja na kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na Udhibiti wa Dawa za kulevya nchini.

2.2 KUSHUGHULIKIA BAJETI YA TAASISI

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu la Kamati la kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Tume ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya kama zilivyoainishwa katika Kifungu cha 7, Fasili ya 1(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Aprili, 2013, Kamati ilitekeleza Jukumu hili mwezi Aprili, 2014 kwa kuchambua Makadiirio ya Mapato na Matumizi ya Tume hizo.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kutekeleza jukumu hilo Kamati ilipokea maelezo kutoka kwa kila Tume kwa wakati tofauti na kutaka ufafanuzi katika maeneo mbalimbali pale ilipobidi. Baada ya Kuridhika na ufafanuzi uliotolewa, Kamati iliridhia Makadirio ya Tume zote na kuwasilisha maoni yake Bungeni ikiwa ni pamoja na kuliomba Bunge lipitishe makadirio ya na Matumizi ya Tume hizo kama tulivyoshuhudia katika Mkutano wa Bunge wa Mwezi Aprili hadi Juni, 2014

2.3 KUSHIRIKI KWENYE MIKUTANO NA WADAU

Katika mikutano yake ya kawaida na kwa kuzingatia suala la UKIMWI ni suala mtambuka Kamati ilikutana na Wizara na taasisi mbalimbali za serikali ili kuona namna zinavyozingatia na kuratibu masuala ya UKIMWI katika sehemu za kazi. Kamati pia ilikutana na asasi za kiraia ikiwa ni pamoja na Baraza la Watu waishio na Virusi vya UKIMWI (NACOPHA), Mashirika ya kitaifa na wadau wa maendeleo (DPs) ili kupokea taarifa ya jinsi asasi na Wadau wa Maendeleo wanavyoshiriki katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

Aidha, Kamati ilikutana na mashirikia ya Kimataifa ili pia kupokea na kujadili utekelezaji wa mapambano dhidi ya

UKIMWI na Dawa za kulevya. Miongoni mwa mashirika hayo ni pamoja na UNAIDS,Elizabeth Glaser, FHI 360, HelpAge International, Delloitte, PSI, DSI, Africare, ICAP, UNODC na kikundi cha wadau wa maendeleo wa masuala ya UKIMWI chini ya uenyekiti wa USAID. Kutokana na vikao hivyo Kamati ilijifunza mambo mengi muhimu yahusuyo UKIMWI na Dawa za Kulevya na changamoto zilizopo.

Aidha, Kamati pia ilipata fursa ya kukutana na ujumbe kutoka Mfuko wa Dunia wa kupambana na Kifua kikuu , Malaria na UKIMWI (Global Fund for HIV/Malaria and Tuberclosis.), USAID na Benki ya Dunia kuzungumzia uhamasishaji wa rasilimali za ndani ili kuboresha afya na uanzishwaji wa Mfuko wa Taifa wa kupambana na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 hadi 25 Julai 2014, Kamati ilipata fursa ya kuhudhuria Mkutano wa 20 wa Kimataifa wa UKIMWI uliofanyika nchini Australia katika jiji la Melborne. Mkutano huo ni wa 20 tangu kuanzishwa kwake na umekuwa ukifanyika kila baada ya miaka miwili. Mkutano huo uliazimia kwamba, wadau wote wa masuala ya UKIMWI kuhakikisha janga la UKIMWI linatokomezwa kabisa ifikapo mwaka 2030.

Mkazo mkubwa uliwekwa katika kuondoa unyanyapaa wa aina yoyote ile, ukatili wa kijinsia, ukandamizaji pamoja na kuachana na mila, desturi, sheria na sera mbaya ambazo zimekuwa zikikwamisha mapambano dhidi ya UKIMWI.

Aidha, katika semina iliyoandalia na IPU kwa Wabunge wote waliohudhuria mkutano huu wa dunia, iliyofanyika katika Bunge la Victoria, Bunge la Tanzania lilipongezwa kwa kuwa mfano wa kuigwa Duniani na Mabunge mengine kwa jinsi linavyoshughulikia masuala ya UKIMWI ikiwa ni pamoja na kuanzisha Kamati ya kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI na Chama cha Wabunge cha Kupambana na UkIMWI (TAPAC).Aidha Rais Jakaya Mrisho Kikwete alipongezwa kwa juhudi zake katika kupunguza vifo vya mama na Watoto wachanga..

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huo, Kamati ilijifunza mambo mbalimbali yafuatayo:-

(i) Umuhimu wa kuwashirikisha wabunge katika kutokomeza UKIMWI na kufikia sifuri 3 (Engaging Parliamentarians to get to 3 zeros)
(ii) Umuhimu wa kutenga rasilimali fedha za kutosha za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI
(iii) Mkanganyiko uliopo kati ya janga la UKIMWI na Haki za Binadamu.
(iv) Uhusiano uliopo baina ya unyanyasaji wa kijinsia na UKIMWI.
(v) Uhusiano uliopo baina na UKIMWI na tohara kwa wanaume.

2.4 ZIARA

Mheshimiwa Spika, tarehe 29/10/2014 Kamati ilifanya ziara kukutana na shirika lisilo la kiserikali linaloitwa Pili Missanah Foundation lililoko Kigamboni ambao linasimamia na kutoa huduma kwa watumiaji wa dawa za kulevya (Sober House) mbili zote zikiwa huko Kigamboni. Ziara hiyo ilikuwa na nia ya kupokea taarifa ya namna shirika hilo linavyopambana na dawa za kulevya na namna linavyojitahidi kuwaokoa waathirika wa dawa hizo hususan vijana ambao ni wengi waliothirika na matumizi ya dawa hizi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa kwamba, kituo hiki ambacho kilichoanzishwa mwaka 2011, kina jumla ya vijana 173 ambao miongoni mwao wapo waliohitimu taaluma mbalimmbali. Ziko changamoto nyingi wanazokutana nazo ikiwa ni pamoja kutopatiwa huduma za afya ijapokuwa waliwahi kukutana na Mhe Rais na kuahidiwa kupatiwa huduma hiyo. Hata hivyo, madaktari walifika kwa muda mfupi na baadaye kutoweka. Pia waliahidiwa na Mheshiumiwa Rais Kupatiwa kiwanja ambacho hadi sasa hawajapata.

Mheshimiwa Spika, kamati inashauri halmashauri ya wilaya ya Temeke kutekeleza ahadi ya Rais kwa kuwapatia

kiwanja taasisi hii kwani wanaopata huduma katika vituo hivi ni vijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kamati pia inashauri Halmashauri ya wilaya ya Temeke , taasisi mbalimbali kutoa mikopo kwa vijana hawa ili waweze kuanzisha shughuli za kiuchumi waweze kujitegemea na kufanya taasisi kuwa na program endelevu.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 21/11/2014 Kamati ilitembelea kituo cha SAADA kilicho chini ya Kituo cha Polisi Mkoa wa Dodoma. Kikundi hiki cha Small Axe Against Drugs (SAADA) kilianzishwa tarehe 23/10/2009 kikiwa na vijana 26 waathirika wa matumizi wa Dawa za Kulevya ambacho kwa hivi sasa ina vijana 43 kati ya hao 7 ni wasichana.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwake kituo hiki kimekwisha wahudumia vijana 156 na kuwaondoa katika utumiaji wa dawa za kulevya na hivyo kwa kiasi kikubwa kupunguza matendo mengi ya kihalifu. Huduma mbalimbali kama ushauri, matibabu, huduma za elimu hutolewa,kituo kimesaidia kutoa elimu ya sekondari na na kwa bahati nzuri kituo kimesaidia baadhi ya vijana waliosaidiwa na wameweza kuhitimu masomo katika ngazi mbalimbali hadi ngazi ya shahada.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mambo mazuri ynayofanywa na kituo hiki, bado kinakabiliwa na changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na ukosefu wa jengo, ufinyu wa bajeti na ukosefu wa fedha, gharama kubwa za kuwapeleka waathirika Sober House Zanzibar na huduma kwa waathrika wanawake kwani wana mahitaji maalum na wengine wana watoto wachanga.

Mheshimiwa Spika, kamati inashauri kituo hiki kikabidhiwe jengo ambalo lipo jirani na kituo hiki ili kiweze kutumiwa na vijana. Jengo hili ni mali ya wizara ya Kazi na ajira na halijaendelezwa muda mrefu, na kamanda wa Polisi Dodoma alishaandika andika kuomba jengo hili.

2.5 SEMINA

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka uliopita, Kamati ilishiriki jumla ya semina tano ambazo kwa kiasi kikubwa ziliongeza ufahamu na kuwajengea uwezo Waheshimiwa wa Wabunge katika kusimamia vyema kazi za Kamati lakini pia ufahamu wa mambo mbalimbali yahusuyo masuala ya UKIMWI. Semina hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Semina iliyohusu namna bora ya uchambuzi wa muswada wa sheria. Katika semina hiyo, pamoja na mambo mengine, Wajumbe waliweza kufahamu hatua za kutunga sheria, umuhimu wa kushirikisha wadau katika kutunga sheria, na changamoto zitokanazo na Miswada inayoletwa Bungeni au kwenye Kamati kwa Hati ya Dharura.

(ii) Semina iliyohusu Sheria ya UKIMWI na Mfuko wa UKIMWI. Semina hiyo iliandaliwa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania. Semina hii ilifanyika tarehe 30 Augosti, 2014. Jambo muhimu lililojadiliwa katika semina hiyo lilihusu umuhimu wa kuifanyia marekebisho sheria ya UKIMWI ili iweze kuendana na Mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa pamoja na kuoanisha sheria za nchi na masharti ya mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine muhimu lililojadiliwa lilikuwa ni umuhimu wa kuanzishwa kwa Mfuko wa UKIMWI. Uanzishwaji wa mfuko wa UKIMWI unalenga kuondoa upungufu wa rasilimali katika maeneo mbalimbali ili kuboresha afua za UKIMWI nchini. Aidha, Wajumbe walijifunza vyanzo vya mapato ya Mfuko wa UKIMWI, pamoja na hatua iliyofikiwa ya uanzishwaji wa mfuko.

(iii) Semina (round table discussion) baina Kamati na jumuiya inayoitwa Women Creative Solutions Association (WCSA) Chini ya mradi wao uitwao "sauti yetu" ambao wanauendesha kwa ushirikiano na Baraza la Watu waishio na UKIMWI (NACOPHA) wenye lengo la kuimarisha sauti za waviu ili kushiriki na kushirikishwa katika maeneo yanayo wagusa. Dhumuni la semina hii lilikuwa ni kujadiliana kuhusu VVU na magonjwa ambukizi ikiwa ni pamoja na kujadili

namna bora ya kuanzisha mfumo wa kitaifa (National Framework) kwa ajili ya WAVIU. Semina hii ilifanyika tarehe 26/11/2014.

(iv) Semina baina Kamati na waratibu wa UKIMWI kutoka sekta ya umma na sekta binafsi. Dhumuni la Mkutano huu lilikuwa ni kujadiliana kuhusu hali ilivyo hivi sasa katika suala zima la mapambano dhidi ya UKIMWI, changamoto, mafanikio na matarajio kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, semina hii iliwapa elimu na ufahamu mpana waheshimiwa wabunge juu ya mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na namna suala la UKIMWI linavyotakiwa kuzingatiwa katika sehemu za kazi kutokana na miongozo mipya kwa taasisi za serikali. Aidha, wajumbe walielimishwa namna ya kufuatilia shughuli za UKIMWI katika sekta ya umma na hasa katika Halmashauri zetu ikizingatiwa Waheshimiwa Wabunge ni Madiwani. Tume ya Utumishi wa umma ikisaidiana na Tume ya kudhibiti UKIMWI imeandaa orodha (check list) ya namna ya kufuatilia fedha za miradi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa tayari wakaguzi (inspectors) kutoka sekta ya umma wamepatiwa mafunzo kuhusu namna ya ufuatiliaji na wataanza kazi hii mwaka huu wa fedha wa 2014/15. Kamati inatoa pongezi kuhusu jambo hili kwani litaokoa fedha nyingi zilizokuwa zikitumika kwa malengo tofauti. Semina hii ilifanyika Tarehe 23 -24/11/2014 .

(v) Semina iliyoandaliwa na National Food Fortification Alliance (NFFA). Lengo la semina hii lilikuwa kuwapa uelewa Waheshimiwa Wabunge kuhusu umuhimu wa lishe kwa kuzingatia programu ya taifa ya uongezaji virutubishi vya vitamini na madini kwenye vyakula. Wajumbe walielezwa kwamba upungufu wa virutubishi vya vitamin na madini ndiyo unaathiri zaidi sehemu kubwa ya jamii na waathirika wakubwa ni watoto walio katika umri wa chini ya miaka mitano na wanawake walio katika umri wa uzazi.

Mheshimi Spika, Kamati iliarifiwa kuwa, pamoja na athari nyinginezo nyingi, ukosefu wa virutubishi hivi mwilini husababisha njaa iliyofichika (hidden hunger) na huchangia kwa kiwango kikubwa magonjwa na vifo hususan kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano na akina mama walio katika umri wa kuzaa**.** Semina hii ilifanyika Tarehe 18/11/2014.

2.6 UCHAMBUZI WA MISWADA

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa kipindi cha Mwaka uliopita, ilipitia na kuchambua miswada miwili ya sheria. Miswada hiyo ni:-

(i) Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria ya Tume ya Kuthibiti UKIMWI (***The Tanzania Commission fo AIDS (Amendment) Bill, 2014***);

(ii) Muswada wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Dawa za Kulevya (***The Drug Control and Enforcement Bill, 2014***).

Mheshimiwa Spika, Kamati inachukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati wadau wote walioitikia mwito wa kushiriki katika Mkutano wa Kamati hii na wadau (Public Hearing). Hakika mawazo yao kwa kiasi kikubwa yamesaidia uboreshwaji wa miswada yote miwili. Mahudhurio yao na ushiriki katika mikutano ya Kamati imeonesha namna wananchi walivyo na utayari wa kufanya kazi na Bunge lao Tukufu kwa maslahi ya Taifa.

SEHEMU YA TATU

MAONI NA USHAURI UNAOTOLEWA NA KAMATI

3.0 MAONI NA USHAURI

Mheshimiwa Spika, kutokana na kazi ambazo Kamati yangu ilizitekeleza kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita, mambo mbalimbali yaliyojitokeza ambayo yalihitaji maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

3.1 MASUALA YAHUSUYO UKIMWI

3.1.1 RASILIMALI ZA UKIMWI

Mheshimiwa Spika, Mwitikio wa Taifa umelenga kufikia malengo yaliwekwa kimataifa 90-90-90 yaani 90% kwa waliopima afya zao na kutambua hali yao ya maambukizi, 90% wanaostahili kupata tiba na 90% ya waliopo kwenye tiba wawe na kiwango kidogo cha virusi kwenye damu ifikapo mwaka 2020. Lengo likiwa ni kufuta kabisa UKIMWI ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, itakuwa ni vigumu kwa Tanzania kufikia lengo hili kama hatutakuwa na rasilimali endelevu kwani asilimia 97% ya fedha zote za mapambano dhidi ya UKIMWI zinategemea Wadau wa Maendeleo ambao ni serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa Dharura wa Rais (PEPFAR), Mfuko wa Dunia wa Kifua kiuu, Malaria na UKIMWI na wengineo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baadhi ya wafadhili wamejitoa na wengine wanafikiria kujitoa kufadhili suala hili la kupambana na UKIMWI, kuna hatari kubwa sana inakuja siku za usoni ikiwa hatutakuwa na jitihada za makusudi za kubuni vyanzo vya mapato. Kwa mujibu wa Takwimu zilizopo nchi yetu inakadiriwa kuwa ni nchi ya **4** Duniani kwa vifo vitokanavyo na UKIMWI na pia ni nchi ya **7** Duniani kwa watu waishio na VVU kwani inakadiriwa kuwa na WAVIU takribani milioni moja na laki nne (**1,400,000**). Aidha nchi yetu ni nchi ya **8** kwa kuwa na maambukizi mapya ya UKIMWI Duniani na inakadiriwa kuwa na yatima (Miaka 0 – 17) **1,300,000** kutokana na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinatisha. Kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo hili na kwa kuzingatia ukweli kwamba, wadau wanajitoa kufadhili masuala haya ya UKIMWI, Kamati inashauri kwamba, huu ni wakati muafaka wa Tanzania kuwa na Mfuko wa Taifa wa Kupambana na UKIMWI ili kuwa na rasilimali endelevu. Kamati inapenda kuipongeza serikali kwani mchakato wa kuanzisha Mfuko huu

umeashaanza hivyo tunaomba Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono uanzishwaji wa Mfuko huu na upitishwaji wa sheria husika katika mkutano wa Bunge lijalo. Aidha, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Wadau wa Maendeleo kwamba, rasilimali chache zilizopo za mapambanao dhidi ya UKIMWI zielekezwe kwenye maeneo yenye maambukizi makubwa ya UKIMWI ili kutoa matokeo ya haraka.

Mheshimiwa Spika, Sambamba na hili, Kamati inashauri mkazo katika mapambano uwekwe katika kuzuia maambukizi mapya nchini kwani kinga ni bora kuliko tiba. lakini pia elimu sahihi kwa makundi maalumu hasa wanafunzi kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu itolewe ili kukabiliana na janga hili la kitaifa.

3.1.2 FEDHA ZILIZOTENGWA KWA AJILI YA UKIMWI

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Wizara ya fedha na kuelezwa kwamba, katika mwaka wa fedha 2014/ 15 kiasi cha shilingi bilioni 6.22 zilitengwa kwa wizara, idara na taasisi za serikali zinazojitegemea. (MDAs) kupitia bajeti ya matumizi ya kawaida (OC) kwa ajili ya kupambana na UKIMWI na virusi vya UKIMWI. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 140.24 zilitengwa kupitia bajeti ya maendeleo. Kati ya hizo shilingi bilioni 3.0 ni fedha za maendeleo ya ndani na shilingi bilioni 137.24 ni fedha za maendeleo kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, hadi januari 2015 kiasi cha shilingi bilioni 2.00 tu cha fedha za maendeleo zilikuwa zimetolewa na wafadhili, fedha za ndani hazikutolewa.

Mheshimiwa Spika, Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2014/15 serikali ilitengwa fedha ya jumla ya shilingi bilioni 10.54 kupitia bajeti ya maendeleo ya fedha za nje kwa ajili ya Mikoa na Halmashauri nchini. Kati ya hizo, shilingi bilioni 9.01 zilitengwa kwa ajili ya Halmashauri na shilingi bilioni1.53ni kwa ajili ya sekretariet za Mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa hakuna hata shilingi moja iliyopelekwa hata kwenye Mikoa yenye maambukizi makubwa zaidi kama Njombe, Iringa, mbeya na Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kupambana na UKIMWI hazijapelekwa. Kamati inaomba Bunge hili kuitaka serikali kama kweli ina dhamira na utashi wa kuwalinda watanzania na maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI ambao wengi wao ni vijana na wanawake fedha hizi zipelekwe mara moja na Bunge lako tukufu lielezwe sababu ya kutopeleka fedha hata kwa Mikoa yenye maambukizi makubwa kama Njombe, Iringa , Mbeya na Dar es Salaam.

3.1.3 UKIMWI NA UMASIKINI

Mheshimiwa Spika, tafiti zinaonesha kwamba, kuna uhusiano mkubwa kati ya maendeleo ya kiuchumi, jamii na athari za UKIMWI. Kadri athari za UKIMWI zinavyoongezeka, shughuli za kiuchumi zinapungua kwani UKIMWI umeongeza hali ya umasikini katika kaya. Familia zilizoathiriwa zinatumia sehemu kubwa ya mapato yao katika kuhudumia WAVIU na watoto yatima.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kwamba, serikali imeliweka suala la UKIMWI katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini awamu ya pili 2011/15 kwani UKIMWI ni moja ya sababu kubwa ya umasikini. Malengo yakiwa ni kupunguza maambukizi kwa watu wenye umri kati ya 15 – 24 kutoka 2,4% mwaka 2010 hadi 1.2% mwaka 2015. Malengo mengine ni kuhakikisha upatikanaji wa ARVs na lishe kwa WAVIU bila malipo.

Mheshimiwa Spika, serikali imeweza kuongeza vituo vya kutoa huduma kwa watu waishio na virusi vya UKIMWI katika vituo vya afya. Hata hivyo huduma hizi hazikufika katika vijiji vingi na hivyo kufanya wagonjwa kukosa nauli kwenda vituo vya mbali na kuamua kuacha kutumia dawa. Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri serikali kuendelea

kuongeza utoaji wa huduma za ARVkatika vijiji na ikibidi kutumia Mobile Services (Mkoba).

3.1.4 MWONGOZO KUHUSU DAWA ZA UKIMWI

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mabadiliko ya miongozo ya kutumia dawa za UKIMWI (ARVs) kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) na hivyo kuongeza wigo wa watumiaji wa dawa hizo. Hivi sasa, inatakiwa WAVIU wenye CD4 kuanzia mia tano (500), aanze kutumia dawa hizi kwa maisha yake yote. Hii ina maana kwamba, mzigo kwa nchi unazidi kuwa mkubwa lakini pia umuhimu wa kuhakikisha dawa zinapatikana tena kwa wakati kwa watumiaji unazingatiwa. Kamati inashauri serikali kupitia Bohari ya Dawa (MSD) kuhakikisha dawa za kutosha zinapatikana na zinasambazwa kuwafikia walengwa kwa wakati. Tunashukuru Mfuko wa Dunia kwa kupambana na Kifua kikuu, Malaria na UKIMWI (Global Fund) kwa kuanzisha mfumo wa ununuzi wa dawa wa pamoja.

3.1.5 UZINGATIAJI WA SUALA LA UKIMWI KWA WAWEKEZAJI

Mheshimiwa Spika, wawekezaji hapa nchini hutakiwa kuwekeza kwa kuzingatia uhakiki wa mazingira kwa maeneo wanayowekeza (Environmental Impact Assessment) hasa katika maeneo ya uchimbaji madini. Kwa kuwa janga la UKIMWI ni kubwa na hasa katika maeneo kama ya migodi, Kamati inashauri kwamba, pamoja na uhakiki wa mazingira, suala la UKIMWI Kifua Kikuu yawe ni miongozi mwa mambo ya kuzinghatiwa katika tathmini zinazofanywa kabla ya miradi hiyo kuanza. Na masuala haya yawekwe katika mkataba kuwabana wawekezaji ili wasione kama ni sual la hiyari kutoa huduma kwa vijiji vinavyozunguka, wafanyakazi na familia zao kama wavyofanya Afrika Kusini.

3.1.6 UKATILI WA KIJINSIA

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa unyanyapaa na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto ni tatizo kubwa na ni

moja ya vyanzo vya maambukizi mapya ya UKIMWI kutokana na mila potofu katika jamii zetu, Kamati inaishauri serikali wanawake wawezeshwe kwa kuandaliwa program maalum za kuwajengea uwezo ikiwa ni pamoja na Halmashauri kuendelea kutenga fedha 10% ya mapato yao kwa ajili ya wanawake na vijana.

3.1.7 URATIBU WA TAASISI ZA KITAIFA NA KIMATAIFA

Mheshimiwa Spika, kamati ilifahamishwa na wadau kwamba, kuna udhaifu katika uratibu wa taasisi zisizo kuwa za kiserikali za kitaifa na kimataifa zinazo jishuhulisha na mapambano dhidi ya UKIMWI. Kamati imeshauri serikali kupitia Tume ya Kudhibiti UKIMWI kwamba, uwepo uratibu makini na ufuatiliaji wa karibu kwa taasisi au mashirika haya ili yaratibiwe vyema katika kazi hii ngumu inayohitaji umoja na ushirikiano na serikali ili kupambana vyema na janga hili la UKIMWI.

3.1.8 WAFUNGWA NA UKIMWI

Mheshimiwa Spika, wafungwa wanakabiliwa na hatari kubwa sana ya kuambukizwa ukimwi, kifua kikuu na homa ya ini kutokana na msongamano mkubwa katika magereza yetu nchini. Kamati inatoa ushauri kwamba kuwe na adhabu mbadala zinazotolewa na mahakama badala ya kuwaweka magerezani hasa kwa makosa ambayo si lazima mtu kufungwa badala yake kuwe na adhabu ya kifungo cha nje.

3.1.9 SIKU YA UPIMAJI TANZANIA

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua mchango mkubwa wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwani amefanya mambo mengi mazuri ya kuigwa katika suala hili la kupambana na UKIMWI, ikiwa ni pamoja na kuwaongoza watanzania kupima ili kujua afya zao tarehe **14/7/2007**, hali iliyochangia wananchi wengi kupima na kuondoa unyanyapaa miongoni mwa jamii. Kamati inashauri kwamba, ile siku aliyopima Mheshimiwa Rais iwe ni siku ya upimaji

UKIMWI nchini ili iwe ni kumbukumbu ya kuhamasisha watanzania ili kujua afya zao. Aidha, Siku hii pia ndiyo iwe siku ya uzinduzi na muendelezo wa siku ya UKIMWI Duniani ambayo kilele chake huwa ni tarehe 1/12/ ya kila mwaka.

3.1.10 UELEWA MDOGO WA NAMNA YA KUJIKINGA

Mheshimiwa Spika, kwa baadhi ya maeneo ambayo Kamati imetembelea kumekuwa na malalamiko kwamba kuna watu wanawaambukiza wenzao UKIMWI kwa makusudi, Kamati inashauri kuwa, ibuniwe mbinu nzuri ya kuelimisha watu ambao wameathirika ili wasiendelee kuambukiza wenzao kwa makusudi bali wawe na mioyo ya imani, upendo na huruma kwa kutofanya tendo la ngono bila kinga akijua kufanya hivyo kutamuathiri mwingine.

3.1.11 WATOTO NA UKIMWI

Mheshimiwa spika, katika jitihada zetu za kukabiliana na janga la UKIMWI, watoto wameachwa nyuma. Karibu zaidi ya watoto 16,000 wamepata maambukizi kutoka kwa mama zao. Watoto hawa wanahitaji zaidi ya miaka kumi na tano (15) kufikia umri mkubwa ikiwa watapona katika umri walionao hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, bila kupatiwa matibabu sahihi ya VVU nusu ya watoto hawa watafariki wakiwa ndani ya miaka miwili kutokana na magonjwa yatokanayo na VVU na zaidi ya 80% watafariki kabla ya kufikia umri wa miaka 5. Kulingana na taarifa ya UKIMWI Duniani kwa mwaka 2013, Tanzania ilikuwa ya pili kwa idadi kubwa ya maambukizi mapya kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, Hali hii ni mbaya na inatishia kizazi cha Tanzania, Kamati inatoa ushauri kwamba, serikali ifanye jitihada mahususi kuokoa kizazi cha Taifa hili kwani pamoja na kupewa sifa kama nchi kwa kweza kuingiza watoto mara mbili zaidi katika huduma za dawa za kupunguza makali ya VVU, bado idadi ni ndogo kwani ni asilimia 26% tu ya wahitaji. Hivyo ni muhimu serikali kuongeza juhudi hasa katika suala

zima la huduma za afya na vifaa tiba kwa watoto wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Huduma ziboreshwe na ziwe karibu na jamii kwani upimaji kwa watoto imekuwa ni tatizo kubwa kwa kuwa vipimo huchukua muda mrefu kufika sehemu zinazohotajika kwani vipimo vinapatikana katika Hospitali mbili tu ambazo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Bugando.

3.1.12 UMUHIMU WA LISHE

Mheshimiwa Spika, lishe ni muhimu kwa afya za watanzania na hasa kwa WAVIU. Hii ni kwa sababu kuna uhusiano mkubwa kati ya lishe na virusi vya UKIMWI. Ni dhahiri kwamba virusi vya UKIMWI husababisha kupungua kwa kinga ya mwili na hivyo husababisha ongezeko la mahitaji ya baadhi ya virutubishi mwilini. Ongezeko hilo linaposhindwa kukidhiwa huweza kusababisha madhara makubwa kwa WAVIU kama utapiamlo ambao nao hupunguza kinga ya mwili na magonjwa mengine nyemelezi. Hali hii husababisha hali ya afya na lishe ya mtu anayeishi na virusi vya UKIMWI kuwa mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa pongezi kwa serikali kufanya makubaliano na wadau na wafanyabiashara wenye viwanda nchini kuweka virutubisho katika chakula ili watanzania wawe na afya njema na hivyo kuokoa maisha yao kwani upungufu wa lishe na virutunishi hivi husababisha vifo. Aidha, Kamati inaishauri serikali kuhakikisha kwamba, makubaliano ya uwekaji virutubisho katika chakula yawe ni endelevu. Aida elimu ya lishe iendelee kutolewa kwa jamii kwani 42% ya watoto wamedumaa (stunted). Serikali itenge fedha kwa ajili ya shughuli na zitolewe kwa wakati.

3.1.13 SHERIA YA UKIMWI NA HAKI ZA BINADAMU

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa ikiridhia na kusaini mikataba au Itifaki mbalimbali ya kimataifa bila kuoanisha na sharia za nchi. Hali hii husababisha ukinzani kati ya Sheria zetu na sheria za Kimataifa. Kwa mfano nchi yetu imesaini Mkataba wa Kimataifa wa kulinda Haki za Binadamu.

Kwa kusaini mkataba huo, vifungu vya 15, 21, na 47 vya sheria ya UKIMWI (2008) vinakinzana na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kuridhia mkataba huo wa Kimataifa juu ya Haki za Binadamu, Kamati inaendelea kuishauri serikali ni vyema sheria ya UKIMWI ya Mwaka 2008 ikafanyiwa marekebisho ili kuakisi Mkataba wa kulinda Haki za Binadamu. Aidha, Kamati imebaini uelewa mdogo wa sheria ya UKIMWI kwa jamii jambo linalo kwamisha juhudi za mapambano dhidi ya UKIMWI. Hivyo, Kamati inashauri elimu zaidi iiendelee kutolewa.

3.1.14 BARAZA LA WAVIU

Mheshimiwa Spika, Kamati inalipongeza Baraza la WAVIU kwa kuweza kuanzisha konga katika Halmashauri za wilaya 135 nchini. Hii itasadia WAVIU kuwa na sauti moja. Hata hivyo, Baraza la WAVIU linakabiliwa na ukata hali inayosababisha kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kamati inaendelea kuishauri serikali kutenga bajeti ambayo itasaidia baraza hili kujiendesha na kupunguza utegemezi ukizingatia umuhimu wa Baraza lenyewe katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Bila kujitoa kwa WAVIU vita hii ya kupambana na janga la UKIMWI ingekuwa ngumu sana**.**

3.1.15 UKIMWI MAHALA PA KAZI

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokutana na Ofisi ya Raisi Menejiment ya Utumishi wa Umma, iliarifiwa kwamba, kuna muungozo mpya kuhusu masuala ya UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa mahala pa kazi katika sekta ya umma. Aidha, Kamati ilifahamishwa kwamba, kumekuwa na ongezeko la VVU/UKIMWI kwa watumishi wa umma pamoja na magonjwa mengine yasiyoambukizwa kama Kisukari na presha.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza serikali kuhusu muungozo huo mpya, na inatoa ushauri kwamba, elimu itolekwe kwa watumishi wa umma kuhusu muongoz huo ili

watumishi waweze kuufahamu vyema na kwa maana hiyo kuuzingatia katika sehemu zao za kazi.

3.1.16 TUME YA KUDHIBITI UKIMWI

Mheshimiwa Spika, ili majukumu muhimu ya Tume hii yatekelezwe kwa ufanisi, Kamati inashauri:-

(i) Serikali iongeze kasi ya maboresho ya sera ya Taifa ya UKIMWI;

(ii) Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ishirikiane na na sekretatiet za mikoa na wilaya na kuandaa Mpango Kazi wa kupambana na UKIMWI katika ngazi zote;

(iii) Kamati inaitaka Serikali kupitia Tume kuanzisha program maalum zitakazosaidia kupunguza tatizo la ukatili wa kijinsia; na

(iv) Kamati inaitaka Serikali na Tume ya kudhibiti UKIMWI kuhakikisha zinatoa fedha za UKIMWI kwa walengwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ili Tume hii iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Kamati inashauri iongezewe fedha na pia kupewa fedha zilizotengwa katika bajeti kwa wakati.

3.2 MASUALA YAHUSUYO DAWA ZA KULEVYA

3.2.1 WATUMIAJI WA DAWA ZA KULEVYA

Mheshimiwa Spika, ijapokuwa hakuna takwimu sahihi za watu watumiao dawa za kulevya kwa njia ya kunusa, kuvuta na kupangusa au kupaka, takwimu za watu wanaotumia dawa za kulevya hapa nchini wanazidi kuongezeka siku hadi siku na kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC) inakadiriwa watanzania kati ya 25,000 hadi 50,000 hutumia dawa hizo kwa njia ya kujidunga. Kamati inashauri

kwamba, watumiaji hawa wawekewe programu maalumu ya kuwaelimishwa juu ya athari ya dawa za kulevya. Aidha Elimu hii ni vyema ikawekwa katika mtalaa na kuanza kufundishwa kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu na jamii kwa ujumla ili kuviokoa vizazi vyetu.

3.2.2 HUDUMA ZA AFYA KWA WAATHIRIKA WA DAWA

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka wakujidunga kuhusu huduma za afya hali inayochangia ongezeko kubwa la UKIMWI kwa watumiaji wa dawa za kulevya, Kamati inashauri kwamba, watoaji huduma katika sekta ya afya wapewe mafunzo maalumu ya namna ya kuwahudumia watu walioathiriwa na Dawa za Kulevya ili wapatiwe matibabu stahili wanayohitaji na hivyo kwa kiasi kikubwa kupunguza ongezeko la maambukizi mapya.

3.2.3 HUDUMA YA KUPATA NAFUU KWA WATUMIAJI WA DAWA ZA KULEVYA (SOBER HOUSE)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea Sober House Kigamboni zinazoendeshwa na taasisi ya Pili Missana Foundation na kuongea na vijana imegundua kwamba, vijana wanaweza kuacha dawa za kulevya bila kutumia dawa kwa kupona taratibu. Kamati inaipongeza juhudi kubwa zinazofanywa na taasisi hii na mfadhili wake Zakaria HansPope**.** Kamati iligundua kwamba huduma za afya ni duni, Kamati inashauri Manispaa ya Temeke kutembelea vituo hivi na kuweza kuangalia ili kuona namna wanavyoweza kusaidia kuwapatia huduma bora za afya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliwaahidi kuwapatia kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa kituo kwani walipo wamepanga, Kamati inashauri Halmashauri ya Temeke iwape Kiwanja ili kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais na kuomba wadau mbalimbali wajitolee kujenga kituo hicho kwa manufaa ya vijana wetu. Pia Halmashauri iwasaidie vijana hao mikopo kupitia fedha zinazotengwa kwa ajili ya wanawake na vijana ili waanzishe shughuli za kiuchumi ili

kupunguza utegemezi kwani baadhi yao wanataaluma mbalimbali..

Mheshimiwa Spika,. Aidha, Kamati inalipongeza jeshi la polisi kwa kuamua kuanzisha kituo cha SAADA hapa Dodoma ambacho kinawapa ushauri na huduma mbalimbali vijana na wazee walioathirika na dawa za kulevya na wengi wao wameacha kutumia dawa hizo na hivyo kupunguza vitendo vya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, kwa wa upande wa kituo cha SAADA kilicho chini ya Polisi Dodoma, Kamati inaiomba Serikali iipatie Polisi Mkoa jengo linalomilikiwa na wizara ya kazi na ajira ambalo limekaa muda mrefu bila kutumiwa na ambalo liko na kituo hicho na tayari Polisi Mkoa walisha tuma maombi kwa wizara hiyo husika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio ya Sober House, kituo cha SAADA cha Polisi Dodoma, kituo cha MdM , Vituo vilivyoko Hospitali ya Mwananyamala na Muhimbili, Kamati inaishauri serikali kuanzisha vituo kama hivi angalau kimoja kwa kila Mkoa ili kuwaokoa vijana wetu na kizazi kijacho cha Taifa hili.

3.2.4 WAFUNGWA NA DAWA ZA KULEVYA

Mheshimiwa Spika, wapo wafungwa wengi magerezaani ambao walikuwa wakitumia dawa za kulevya lakini kwa bahati mbaya magerezani hakuna huduma ya kitiba kwa watu wanaotumia dawa za kulevya. Tiba kwa watumiao dawa za kulevya kama methadone hutolewa katika Hospitali tatu yaani Hospitali ya Muhimbili, Hospitali ya Mwananyamala na Hospitali ya Temeke.

Kamati inatoa ushauri kwamba, wafungwa walio magerezani wapewe program ya methadone wakiwa katika magereza na pia wawe na vituo vya ushauri na huduma kama ilivyo kwa polisi ili wakitoka magerezani wawe wameacha matumizi ya dawa za kulevya.

3.2.5 UKAMATAJI WA DAWA ZA KULEVYA

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahammishwa kwamba, katika kipindi cha kuanzia januari mwaka 2013 hadi Agosti 2014 Kikosi Kazi kimeweza kukamata dawa za kulevya kama mchanganuo unavyojionesha katika jedwali.

AINA YA DAWA	KIASI(KG)	THAMANI YA DAWA(Tsh.)	IDADI YA WATUHUMIWA
Cocaine	56,775	5,109,705.000	562
Heroin	381.35	22,881,000,000	761
Bangi	127.680.306	12,768,030,600	18,119
Mirungi	21,151.35	1,057,567,500	2,601
		41,816,303,100	

Mheshimiwa Spika, sambamba na ukamataji huo jumla ya ekari 536.5 za mashamba ya bangi ziliteketezwa pamoja na kilo 3445 za mbegu za bangi ziliharibiwa. Aidha, kilo 12,285 za Heroin na kilo 5584 za Cocaine ziliteketezwa katika kiwanda cha saruji cha Wazo Hill kilichopo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hichohicho, jumla ya mashauri 27 ya kesi kubwa ya dawa za kulevya yalisajiliwa katika Mahakama Kuu ambapo mashauri 20 yamesajiliwa kanda ya Dar es Salaam, manne kanda ya Kilimanjaro, moja Pwani, moja Tanga na moja Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza sana juhudi kubwa zinazofanywa na serikali katika vita hii ngumu na pia kwa kukamilisha ujenzi wa ghala la kuhifadhi vielelezo. Pia tunakipongeza Kikosi Kazi kwa kushirikiana na Tume ya Uthibiti wa Dawa za Kulevya kwa kupambana na tatizo hili kubwa kwa mustakabali wa nchi yetu kwani linaliangamiza nguvu kazi ya taifa.

Hata hivyo, Kamati inasikitishwa kwa utoaji wa fedha kidogo kwa Tume kwani fedha zilizo tengwa katika mwaka wa fedha 2014/15 zilikuwa shilling. Bilioni 4.42 fedha za

matumizi ya kawaida lakini hadi January 2015 ni shilingi 1.1 tu zilizotolewa. Aidha, kwa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 3.43 kilitengwa lakini hadi kufikia Januari 2015 ni kiasi cha shilingi milioni 150 tu kilichotolewa. Kamati inashauri serikali kutoa fedha tena kwa wakati kwa Tume hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ukizingatia nguvu ya fedha waliyonayo wafanyabiashara wa dawa hizi za kulevya.

3.2.6 SHERIA INAYOTUMIKA NA UPUNGUFU WAKE

Mheshimiwa Spika, sheria ya kudhibiti biashara haramu ya dawa za kulevya hutumika katika kutoa adhabu kwa makosa yanayohusiana na biashara pamoja na matumizi ya dawa za kulevya. Hata hivyo sheria hiyo ina upungufu ufuatao:-

(i) Sheria haijakataza kumiliki kuuza au kusambaza mbegu za bangi au mbegu za aina yoyote ya dawa za kulevya;

(ii) Sheria haitoi adhabu kwa watu watakaokutwa na maabara au mitambo kwa ajili ya kutengeneza dawa za kulevya;

(iii) Sheria imeweka dhamana kwa kigezo cha thamani ya dawa hizo; na

(iv) Sheria haikuipa Tume mamlaka ya kupekua na kukamata wafanyabiashara wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, Kufuatia upungufu huo, sheria mpya ambayo itarekebisha upungufu huu inahitajika tena kwa haraka. Kamati inaipongeza serikali kwa kuleta muswada wa sheria ya udhibiti wa dawa za kulevya ili kuwa na sheria itakayo kuwa na meno. Inafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba, mchakato wa Sheria mpya unaendelea vizuri kwani tayari muswada wa sheria hii umeshafika na kuvuka katika ngazi ya Kamati na huenda ukajadiliwa katika Mkutano ujao wa Bunge. Kamati inaishauri serikali kwamba, pamoja na ujio wa sheria tajwa, ni vyema pia ikatumia uzoefu wa nchi

nyingine zilizofanikiwa katika mapambano dhiti ya udhibiti wa dawa za kulevya kama Bangladeshi na India.

3.2.7 SERA YA TAIFA YA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Mheshimiwa Spika, pamoja na tatizo la dawa za kulevya kuwa kubwa, hakuna Sera ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya hapa nchini. Hata hivyo, Kamati iliarifiwa kwamba, rasimu ya sera ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya imeshapitiwa na sekreatrieti ya Baraza la Mawaziri na inasubiri kupitiwa na kikao cha pamoja baina ya Makatibu Wakuu na Baraza la Mawaziri. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba, serikali iharakishe mchakato wa uandaaji wa sera hiyo ya Taifa ya Kupambana na dawa za Kulevya hasa ikizingatiwa sera ndiyo huitangulia kuweka misingi ya uundwaji wa sheria.

3.2.8. TUME YA KURATIBU UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Mheshimiwa Spika,ili kutekeleza vema majukumu ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Kamati inashauri yafuatayo:-

i) Kuharakiswa kwa mchakato wa Sera na Sheria ya Kudhibiti Dawa za Kulevya;

ii) Kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016 Tume ijipange kuanzisha vituo vya kutosha (sober houses) kuhudumia waathirika wa dawa za kulevya kwa kushirikiana na wadau;

iii) Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwani tatizo ni kubwa.

248.0 SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kabla sijamalizia, napenda niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe kwamba mwaka huu

ni mwaka wa uchaguzi, Hivyo, Kamati inatoa ushauri kwa vyama vyote vya siasa na wagombea watakao jitokeza kulifanya suala la UKIMWI na Dawa za Kulevya kuwa ni moja ya ajenda katika kampeni zao.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Mwezi Februari, 2015. Tunaamini kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117(15), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, itasaidia kuliwezesha Bunge lako tukufu kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Aidha, napenda kuwashukuru wenzangu wa Kamati ya Uongozi kwa ushirikiano wao katika uendeshaji wa Bunge letu na pia nawashukuru wajumbe wote wa kamati ya masuala ya UKIMWI kwa ushirikiano wao mkubwa uliouwezesha kutekeleza majukumu ya Kamati. Pia nawashukuru kwa moyo wao wa kujitolea na michango waliyoitoa kwa vijana wetu wenye matatizo sehemu zote ambazo Kamati ilipotembelea.

Mheshimiwa Spika, Napenda kumshukuru aliyekuwa Waziri wa nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge Mheshimiwa William Lukuvi, Mb., kwa ushirikiano mkubwa alioutoa kwa Kamati. Tunampongeza sana kwa kuteuliwa kuwa waziri wa Ardhi, nyumba na makazi. Tunamuombea Mwenyezi mungu amuongoze katika utekelezaji wa majukumu yake mapya. Kamati pia inampongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mb., kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wan chi Ofisi ya Waziri Mkuu sera, uratibu na Bunge. Kamati ina imani kubwa na wewe kwani tunafahamu ulivyo imara katika vita hii ukiwa mwanachama mwanzilishi wa TAPAC. Kamati inakuahidi ushirikiano mzuri.

Mheshimiwa Spika, Namshukuru Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mwenyekiti mtendaji wa TACAIDS, Kamishina wa Tume ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya pamoja na watendaji wa taasisi mbalimbali

za serikali kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati wa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Mwisho, lakini si kwa umuhimu naishukuru Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah kwa kuiwezesha kamati wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu Abdallah Hancha na Ndugu Mossy Lukuvi kwa kuratibu vema shughuli za Kamati kwa kipindi chote na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati. yake.

Mheshimiwa Spiaka, baada ya kusema hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kuyakubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya maswala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

.....
Lediana Mafuru Mng'ong'o, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
MASUALA YA UKIMWI

03 FEBRUARI, 2015

SPIKA: Ahsante Waheshimiwa Wenyeviti wote kwa taarifa zenu. Ukiangalia muda hapa, saa hizi naweza kupata wachangiaji watano tu. Kama kawaida muda siyo wa kutosha, mpaka mwisho wa safari nitakuwa na wachangiaji labda 16. Kwa hiyo, wengine wote waliochangia kwenye hotuba nyingine wasitegemee majina yao kuitwa hapa. Kwa hiyo, namwita kama yupo Mheshimiwa Diana Chilolo, atafuatiwa na Mheshimiwa David Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustine Masele, atafuatiwa na Mheshimiwa Kayombo na Mheshimiwa Desderius Mipata. Hawa ndio watachangia asubuhi hii. Mheshimiwa Diana Chilolo!

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa napenda nitumie nafasi kumpongeza sana Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI na Madawa ya Kulevya kwa jinsi alivyowasilisha taarifa yetu kwa ufasaha wa hali ya juu sana. Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Lukuvi kwa jinsi ambavyo tumeshirikiana naye vizuri kwenye Kamati yetu pamoja na Mwenyekiti Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Kwa kweli wametoa mchango mkubwa sana katika Kamati yetu kuweza kufanya kazi vizuri na kufikia hatua tuliyofikia. Baada ya pongezi hizi, naomba sasa nianze kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naanza na suala la Mfuko wa Madawa ya Kulevya. Naishukuru sana Serikali kwa kupokea suala hili kwa moyo mkunjufu kabisa, suala ambalo limeshapitiwa na Baraza la Mawaziri na Bunge lijalo Serikali italeta Muswada huo wa kupitisha Mfuko wa Madawa ya Kulevya.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuliomba Bunge lako Tukufu, Muswada huu utakapoingia hapa Bungeni wa kuanzisha Mfuko wa Masuala ya UKIMWI naomba Wabunge wote tuunge mkono ili Taifa letu hili ambalo limekumbwa na janga hili kubwa la ugonjwa wa UKIMWI, liweze kuwa na mfuko ambao utahudumia masuala ya kupambana na UKIMWI kiasi ambacho kitasaidia hali ambayo inatupata kushindwa kuendelea kupambana na masuala ya UKIMWI kwa sababu fedha nyingi tunategemea wahisani na wahisani wengi sasa hivi wameanza kusitisha misaada yao. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Muswada huu utakapofikishwa Bungeni katika Bunge lijalo basi tuunge mkono wote kwa pamoja ili Serikali yetu iweze kuanzisha mfuko wa kupambana na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kama Mwenyekiti wangu alivyoeleza kwenye taarifa yake, vilevile tunategemea kuletwa Muswada wa kuanzisha Sera ya Madawa ya Kulevya.

Vile vile nalo ni janga kubwa na ninapanda mjue Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba madawa ya kulevya yana uhusiano wa karibu sana na janga hili la UKIMWI. Kwa hiyo, tukipitisha Sera ya Madawa ya Kulevya hapa, nina hakika tutakuwa tumeongeza nguvu kubwa ya Taifa hili kuweza kupambana na UKIMWI ambapo wakati mwingine unapitia kwenye madawa ya kulevya.

Kumbukeni kwamba hawa wanaotumia madawa ya kulevya, hao wanaotumia, hutumia sindano kujidunga na mambo mbalimbali, kujamiiana kwa sababu wanakuwa hawana akili za kawaida. Kwa hiyo, kuambukizana ugonjwa wa UKIMWI ni rahisi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukipitisha sera hiyo itakuwa imetusaidia sana pia kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI kupitia njia za kujidunga sindano kwa wale wanaotumia madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo naomba sasa nichangie kuhusu swali ambalo limeulizwa asubuhi kuhusu Serikali sasa kuanza kusaidia watoto yatima na watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu. Nimefurahishwa sana na Mheshimiwa Dkt. Kebwe kwa majibu yake aliyoyaeleza kwamba sasa hivi Serikali itakuwa inahudumia watoto yatima na wale wa mazingira magumu.

Pia kwenye taarifa iliyosomwa imeonesha wazi kwamba Kamati imeshauri watoto hawa wapate huduma za aina hiyo, lakini kitu ambacho kinapungua, hakuna sensa iliyofanywa ya kutambua watoto yatima pamoja na watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, kama kweli ina nia thabiti ya kutaka kuwasaidia watoto yatima na watoto wa mazingira magumu, naomba sasa Serikali itakapokuwa inajibu hoja za Kamati kuwatangazia Wakurugenzi nchi nzima kuhakikisha imefanya sensa ya kuwatambua watoto yatima pamoja na watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu ili tuweze kuwapata na waweze kupata huduma hizi ambazo Serikali

imeainisha kupitia majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Kebwe.

Mheshimiwa Spika, itakuwa ni vizuri sana kama Wakurugenzi nchi nzima watafanya kazi hiyo kupitia Watendaji wao wa ngazi ya chini, kufanya sensa ya kutambua watoto yatima pamoja na watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu kwa lengo la kuweza kuwapatia huduma ambazo zimeainishwa na Serikali kwa maana ya matibabu, elimu na mambo kadha wa kadha.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati imeeleza kuhusu ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye Halmashauri zetu. Ni ukweli usiofichika kwamba miradi ya maendeleo kwa kweli inatekelezwa kwa kusuasua ama mingine haitekelezwi kabisa, mpaka sasa hivi haijaanza kutekelezwa wakati imo kwenye mpango wa ahadi za Serikali na mwaka wa fedha unaisha kwa maana ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, naungana na Kamati ya Tawala za Mikoa kuiomba Serikali kuhakikisha kwamba ile miradi ambayo imeainishwa, tufanye kila linalowezekana kuhakikisha kwamba ahadi ya Serikali isiangushwe itekelezwe kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha.

Mheshimiwa Spika, vilevile nizungumzie kuhusu suala la Wakuu wa Idara kwenye Halmashauri kukaimu. Kamati imetoa maelezo hapa kwamba Halmashauri nyingi sana zinakuwa na Makaimu Wakuu wa Idara. Kuwa na Makaimu mara nyingi ufanisi unakuwa duni sana.

Naiomba sana Serikali, kama kweli wale Makaimu tunawaona wanatosha na wana sifa za kutosha, hakuna sababu za kuendelea kuwa na Makaimu Wakuu wa Idara.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iwe inawathibitisha mara wanapoona kwamba hapa panakuwa na ukosefu wa Wakuu wa Idara, basi wale watu wanaokaimu wathibitishwe, au kama wanaokaimu mnaona hawana sifa,

mbona wasomi tunao wengi sana; kwanini mapengo haya yasiwe yanazibwa mara kwa mara pale wanapokosekana Wakuu wa Idara?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kuendesha Halmashauri na Wakuu wa Idara, kwanza tunapoteza sifa ya Halmashauri zetu kupata hati safi. Siyo hivyo tu, tunapunguza ufanisi wa kazi. Siku zote Makaimu Wakuu wa Idara hawajiamini. Utendaji wao wa kazi, huwa wanafanya wakijua kwamba pale wamekaa mguu mmoja ndani na mguu moja nje. Naomba sana, kama ilivyoshauri Kamati, nami naungana nayo, tufike mahali tuondokane na Makaimu Wakuu wa Idara.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwenye taarifa ya Kamati ya Sheria na Katiba imeongelea kuhusu Mahakimu wetu jinsi ambavyo wanafanya kazi kwenye mazingira magumu. Kama nilivyouliza swali langu la nyongeza jana kwamba kuna Wilaya nyingi hazina mahakama za Wilaya, utakuta Mkoa mzima Mahakama za Wilaya ziko mbili, Mahakamu wa Wilaya wanafanya kazi hata Rufaa za kutoka Wilaya nyingine, kazi ambazo zinakuwa ni ngumu na ni nyingi, zinawafanya Mahakimu hawa washindwe kumaliza kesi kwa wakati muafaka na kuwafanya watu wenye kesi waendelee kusumbuka na kesi hizo kwa muda mrefu sana.

Naomba sana Serikali wasomi tunao, vyuo tunavyo, hebu tupate wataalam wa kutosha tuhakikishe kwamba tunakuwa na Mahakimu kwenye Wilaya zote na Mahakimu hao wanatengewa maeneo ya kufanyia kazi. Tunakaribia kutengeneza bajeti mpya; katika kutengeneza bajeti, tuhakikishe tunatenga bajeti ya kujenga Mahakama za Wilaya kwa nchi nzima. Ni vizuri sana kama kila Wilaya itakuwa na Mahakama. Kama bajeti haitatosha, basi tutengeneze mpango wa mpito kuweka hata Mahakama za Mwanzo kuwa na Mahakama za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Silinde, anafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Masele.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii nami nichangie Taarifa za Kamati zetu tatu. Jambo la kwanza ambalo nitaanza nalo ni hili linalotokana na Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Spika, kwenye ukurasa wa tisa wa Taarifa ya Kamati umejaribu kujadili jambo moja la msingi ambalo linaitwa Utekelezaji wa *TASAF* Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Spika, lengo la utekelezaji wa *TASAF* awamu ya tatu ni kuhakikisha kwamba wanakuja na mradi wa kuinua kaya masikini na mradi huu lengo lake ambalo limeandikwa moja kwa moja unalenga kuwapatia wananchi ruzuku ya pesa moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa *TASAF* wameeleza kwa undani zaidi kwamba mpango huu unalenga kuhakikisha kwamba kaya masikini katika Halmashauri 113 za Majiji, Miji, Manispaa na Wilaya ndizo ambazo zitapitiwa na mradi huu. Katika awamu ya kwanza ya mradi huu, Halmashauri 41 zimefikiwa na fedha zilizotumika mpaka muda huu ni Shilingi bilioni 31. Hazijatajwa Halmashauri, lakini Shilingi bilioni 31 zimegawiwa fedha, yaani wamegawa kwa watu masikini.

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu ambaye anapenda umasikini. Sisi wote kama Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge tunapinga umasikini. Lakini unapogawa fedha moja kwa moja Sh. 2,300/= na ukienda mbali zaidi, malengo ya mradi huu ni kwamba tunataka kuwawezesha watu wapate hela ya chakula, pamoja na malazi. Ndicho kilichoandikwa! Sasa ukiangalia mradi umeandikwa zaidi, unasema mradi huu utafanyika kwa kipindi cha miezi minne.

Mheshimiwa Spika, nina hofu. Hofu yangu ni kwamba mradi huu unatakiwa ufanyike sasa, kwa sababu ukishindwa kufanyika sasa hivi, tusubiri bajeti ambayo inakuja ya mwaka

2015/2016 itakuwa ni rushwa itakayotumika wakati wa uchaguzi. Sasa ni lazima tuonyeshe hii hofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki kitu nimekiona kwa sababu ukienda kwa watu masikini, unasema unamlipa sh. 2,300/= kwa siku, mara siku 15 ambayo ni sawa sawa na Sh. 34,500/= kwa miezi minne mfululizo. Maana yake unaweza ukaamua sasa, inapoanza wakati wa uchaguzi, unaanza mwezi wa Sita kugawa hizo hela mpaka mwezi wa Kumi. Hii inaweza ikaonekana kama ni rushwa.

Sasa Serikali kama ina malengo hayo mema ya kuwainua watu kwenye umasikini na kuwatoa watu katika huo umasikini, hizi fedha kwanza tunataka zitumike sasa. Lakini tunawaambia kila siku, Taifa letu lina shida ya ajira,Tuna wasomi wengi hawana ajira, tuna lundo la watu wanalalamika kila siku kukosa ajira. Watu hawataki fedha, hata Biblia inasema usimpe mtu samaki, mfundishe mtu namna ya kuvua samaki. Ndiyo jambo ambalo tunataka hapa na kuliona.

Sasa hizi fedha wananchi wote wajue kabisa kwamba kuna mgawo wa fedha unakuja kutoka *TASAF III,* watu wajue, na ni fedha za wananchi. Kwa sababu kule vijijini Mtendaji anapokwenda kutambua mtu, mengine huwa wanatumia hii kama Vyama vya Siasa kwamba tutagawa katika Chama chetu, Chama cha Mapinduzi ama watu fulani. Hizi ni fedha za wananchi ambazo watagawiwa wote bure, lakini tunataka hizo fedha zigawiwe sasa na wala siyo kipindi cha uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na yote, hao *TASAF* tunaomba basi muwape wasomi mikopo waweze kufanya kazi za ujasiriamali. Wapate fedha ambayo itawasaidia maisha yao yote. Mimi *I am not happy with this system,* ukiiangalia ina lengo zuri, fedha ya chakula, lakini siyo fedha ya kudumu ya kumsaidia mtu kumwondoa katika maisha yake ya kila siku. Jambo linguine, hizi fedha zinazogawiwa huko, mtashindwa kwa sababu unajua katika kaya 761,000 Serikali kusema katika kaya hizo mwende

mkafanye *accountability* m-*cross check,* kutakuwa na wizi mkubwa sana wa fedha katika hili jambo.

Kwa hiyo, naiasa Serikali ijaribu kuliangalia upya, tunataka fedha ziwafikie wananchi lakini katika utaratibu utakaowawezesha wananchi kupata fedha zitakazowasaidia maisha yao yote na wala siyo katika kipindi kifupi ambacho kimeainishwa katika mradi huu.

Mheshimiwa Spika, naomba utekelezaji wake ufanyike sasa na wananchi watambulishwe kwamba hizi fedha ni za wananchi na wala siyo za Chama chochote cha Siasa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nilitaka nilijadili ni Daftari la Kudumu la kuipigia Kura. Sheria ya uchaguzi inataka Daftari la Kupigia kura liwe linaboreshwa kila baada ya miaka miwili na nusu mara baada ya Uchaguzi Mkuu. Sasa leo tuko katika mwaka wa mwisho wa uchaguzi.

Serikali mpaka saa hivi haijaandikisha wananchi na sasa hivi mmekuja na utaratibu mpya wa *BVR* ambao bado wananchi wa kawaida hawajauelewa, na watu wanahitaji kuandikishwa katika hili daftari. Hii tafsiri yake ni nini? Ni hofu ya Serikali, kwa sababu unapokuwa na Serikali ambayo miaka miwili mara mbili haijaandikisha maana yake mnawaogopa wananchi wenyewe kwamba tukiwaandikisha kwa sababu hatujatekeleza ahadi, watashindwa kutuchagua. Hii ni hofu ya moja kwa moja ya Serikali.

Sasa mmeahidi kwamba litafanyika katika mwezi huu wa Pili kwamba kuanzia tarehe 15 litaanza, bado maandalizi. Tulimsikia Waziri Mkuu hapa juzi wakati anaeleza, maandalizi tu yenyewe kwa ajili ya kuandikisha hili daftari, hayapo. Bado kunakuwa na utata na sisi tunataka twende katika uchaguzi huu tukiwa na daftari.

Mheshimiwa Spika, hili tulikuwa tunawaambia kila siku kwamba unapokuwa na Serikali ambayo imekuwa na vipaumbele vingi, kwa sababu ukiangalia kuanzia mwaka

wa fedha huu mpaka tunakwenda kumaliza, tunahitaji daftari, tunahitaji kwenda kwenye kura ya maoni, tumetoka kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kunahitajika vitambulisho vya uraia, tunakwenda kwenye Uchaguzi Mkuu, yaani tuna mlundikano wa mambo, hatuna kipaumbele nini kifanyike, kwa nini kifanyike ili tuweze kufikia yale malengo ambayo tunahitaji.

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo siku zote tunaita ni uzembe wa Viongozi wa Serikali ama kushindwa kufanya kazi ama watu hawajui majukumu na vipaumbele vya wakati. Sasa haya, ndiyo siku zote tumekuwa tukiwaleza kwamba jamani, kama majukumu yanawashinda, ni vizuri watu wakachukua hatua na wengine tukawachukulia hatua.

Mheshimiwa Spika, sasa tumeona, kwenye Daftari la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, wakazi wamejiandikisha na tuna idadi kubwa; na tumekwenda kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kuna mambo mengine mimi nilishakaa na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, nilikuwa namwuliza: kwa nini uliwafukuza Wakurugenzi wa TAMISEMI kwa makosa ambayo nahisi yalitokana na Wizara yako wewe mwenyewe? Kwamba mtu ambaye ameshindwa tu kusimamia Uchaguzi Mdogo wa Serikali za Mitaa amefukuzwa, lakini wale watu walioiba fedha nyingi ikiwemo zile za *Escrow,* wanashindwa kufukuzwa ama kuchukuliwa hatua? Maana yake hapo Serikali imekuwa na *double standard*. Maana yake wanawatisha Wakurugenzi ili hata tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu watu wajue kwamba usipokisaidia Chama cha Mapinduzi, utafukuzwa kazi. Haya ndiyo matokeo ambayo tunayaona na ndivyo ambavyo tunatafsiri na wananchi wa kawaida ndivyo ambavyo tunatafsiri.

Mheshimiwa Spika, sasa hili tunataka vile vile Serikali ije baadaye ilitolee ufafanuzi ni kwa nini Wakurugenzi walifukuzwa? Maana yake zile sababu nyingine zilikuwa hazijitoshelezi na mpaka sasa hivi katika maeneo mengine, maana yake siyo wale tu wachache, kuna maeneo mengi kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, mambo mengi yalifanyika kwa uovu na ninyi mna taarifa na yote hii ni kwa

sababu tu ya uzembe tu wa kawaida ambapo tumekuwa na mazoea ya kila siku kushindwa kutekeleza wajibu ambao tunautaka.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi ambayo tunaongoza. Ukipitia ripoti ya *Transparent International* ya mwaka huu ni kwamba Tanzania inaongoza sana kupeleka hela chini kwa wananchi, lakini ndiyo hiyo hiyo inayoongoza kwenye wizi na ufisadi mkubwa wa hizo fedha zinazoshuka chini kwa wananchi. Yaani sisi ni wa kwanza kwenye kushusha hela kwa wananchi, hiyo tunaita *D by D* lakini sisi ndio wa kwanza wa kula fedha za wananchi chini.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu tumekuwa na mazoea, yaani sisi kama Viongozi tunapokuwa hatuonyeshi ama hatuongozi kwa mfano, matokeo yake yake hata wa chini wanafanya hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi, ahsante.

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Augustine Massele. anafuatiwa na Mheshimiwa Kayombo naye ajiandaye.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa mchango wangu katika Kamati zetu hizi za Kudumu za Bunge tatu ambazo zimewasilisha Taarifa zao mchana huu.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu ambayo napenda kujikita kwayo ni katika masuala ya utawala kwa maana ya Serikali za Mitaa. Mimi natoka katika Mkoa mpya na Wilaya mpya ambayo kimsingi iko chini ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, napenda kuishauri tu Serikali kwa kweli iziangalie kwa makini sehemu za Mikoa mipya na Wilaya mpya kwa maana ya majengo ya utawala na nyumba za watumishi

wanaosimamia maeneo haya mapya. Maeneo haya mapya ya utawala kwa kweli yako katika mazingira magumu na hasa ikizingatiwa sasa hivi ambapo tuna ukata wa bajeti, Serikalihaitoi pesa. Matokeo yake ni kwamba sasa watumishi hawa hawaoni mbele kuna nini, kwa sababu wao wameajiriwa ili kuwasaidia wananchi katika maeneo wanayoyaongoza kuweza kupiga hatua za kimaendeleo. Lakini kwa bahati mbaya sasa watumishi hao wanajikuta katika mazingira kana kwamba wameadhibiwa kwa kupelekwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, nikianzia katika Wilaya yetu Mbogwe mpaka sasa hivi hakuna shughuli za ujenzi zinazoendelea za maofisi na nyumba za watumishi kutokana na kwamba *TBA* ambao wamepewa kazi ya kuweza kuzijenga hizi nyumba hawajapewa pesa na hasa hata katika Ofisi za Mkuu wa Mkoa na Wasaidizi wake, shughuli hizi hazifanyiki. Kwa hiyo, nahimiza Serikali kuweza kuzitoa hizi pesa kwa wakati ili kwamba shughuli hizi ziweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningeweza kutoa kama mchango ni kuhusiana na watumishi kwa maana ya Watendaji hao wa ngazi za chini. Wengi wanakaimu kwa maana ya Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji.

Naiomba tu Serikali iharakishe huu mchakato wa kuajiri Watendaji wa Kata na Vijiji ili kusudi usimamizi wa shughuli za maendeleo katika ngazi hizi za chini ambako pesa nyingi zinakwenda, basi watumishi hao wawe ni watumishi wa Serikali na ambao wanakuwa na dhamana kwa kazi zao. Vinginevyo, mpaka sasa hivi wakati mwingine unakuta miradi mingi ya maendeleo inakuwa inasuasua kutokana na kwamba watumishi hao wanakuwa ni watumishi wa muda kwa maana ya kwamba wanakaimu nafasi zao, hawajui nini kitatokea kesho.

Matokeo sasa pesa zinapokwenda pale inakuwa ni rahisi kwao kushawishika kwamba labda pengine waweze kuchukua pesa mapema ili wakati utakapotimia wa kuweza

kuletwa mtu anayehusika, basi wakute na wao wameshatoa kitu kidogo katika maeneo hayo. Matokeo yake sasa mwananchi wa kawaida ndiye anaweza kupata shida.

Mheshimiwa Spika, nije katika suala la Sheria ndogo ndogo ndizo ambazo kimsingi ni mwongozo wa kuweza kusaidia shughuli za maendeleo katika Halmashauri. Sasa hizi Sheria ndogo ndogo zinapokuwa zimepitishwa katika Halmashauri upitishwaji wake katika Ofisi ya Waziri Mkuu unachukua muda mrefu, matokeo yake, Sheria ndogo hizi ambazo zinaziwezesha Halmashauri kujiendesha zenyewe, zinapokuwa hazipo, basi Halmashauri inafanya kazi kwa kusuasua sana kwa kuhofu kwamba labda pengine wanaweza wakafanya jambo ambalo liko kinyume cha utaratibu kwa maana ya kwamba Sheria ndogo ndogo hizo zinapokuwa hazipo, mtu anaweza akatumia kigezo hicho kwenda kuwashitaki kwamba hawakumtendea haki.

Mheshimiwa Spika, nije katika suala la mapato na matumizi katika ngazi hizi za Vijiji. Tunalo tatizo kubwa la matumizi mabovu ya hela za Serikali na hata michango ya wananchi wanaokuwa wanachangishwa katika maeneo yao. Matokeo yake, unakuta kwamba wananchi wanakatishwa tamaa sana hasa wanapoona kwamba michango inachangiwa, lakini matokeo ya kazi za hizo pesa ambazo wamechangia zinakuwa hazionekani na matokeo yake wananchi wanakata tamaa na kwa maana hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba tu kwamba Serikali iwe na utaratibu na itoe mwongozo kwa Watendaji wa Kata na Vijiji wa kuwataka kwamba kila baada ya miezi hiyo mitatu au minne wawe na utaratibu wa kusoma mapato na matumizi ili kuonyesha uwazi wa matumizi ya pesa ambazo zinachangiwa katika maeno yao.

Mheshimiwa Spika, nije katika suala la Katiba na Sheria. Nchi yetu kama yalivyo Mataifa mengine, suala la Katiba na Sheria ni mambo ambayo ndiyo yanayosimamia miongozo mbalimbali ya nchi. Kwa maana hiyo, kuwepo kwa Watendaji wazuri na weledi ni jambo ambalo haliepukiki na

kwa maana hiyo sasa na mazingira ya kazi pia yanatakiwa kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu kwamba Mahakama iwezeshwe ili iweze kujenga majengo yanayoeleweka, kuwe na Mahakama za Mwanzo na Wilaya pamoja na Mahakama nyingine za Mahakimu ili kuhakikisha kwamba hii huduma muhimu inakuwa karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, tuko katika kipindi cha kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu, basi ni vizuri kwa kweli taratibu nyingine zote ambazo zinahitajika, maandalizi yake yafanywe kwa weledi ili kuhakikisha kwamba Daftari la Wapiga kura linaandaliwa mapema ili kuepusha migongano isiyokuwa na sababu.

Suala la mwisho ambalo ningependa kulifanyia rejea ni suala la upimaji wa maeneo kwa maana ya Mipango Miji. Eneo hili kimsingi linakuwa na tatizo kubwa sana. Wananchi wengi wanajenga nyumba zao katika maeneo ambayo ni *squatters*. Kwa maana hiyo, nashauri kwamba TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, wawe na mpango mkakati endelevu wa kuhakikisha kwamba maeneo mbalimbali ya Wilaya na Halmashauri yanapimwa na wananchi wanamilikishwa maeneo yao kisheria, kwa maana ya kwamba mtu anapokuwa amejenga katika eneo ambalo limepimwa, kwanza anakuwa na uhakika wa eneo lake kwamba hawezi kuja kubugudhiwa kwa maana ya bomoa bomoa ili kuweza kupisha ule upimaji wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Gaudence Kayombo, atafuatwa na Mheshimiwa Mipata.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya leo kuzungumza kuhusu mawasilisho ya Wenyeviti hawa watatu ya Kamati zao na nawapongeza kwa

kazi zao nzuri. *Comments* zangu zitajikita zaidi katika Kamati ile ya TAMISEMI na nikipata muda, ile ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, nachukua muda huu pia kwanza kuunga mkono hoja zote hizo, lakini pia kuwapongeza Wana-Ruvuma kwa kusherehekea vizuri sana maadhimisho ya miaka 38 ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Ahsante kwa makofi hayo kwa wana-CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kwa kuikopesha Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga na kuiwezesha kujenga Stendi ya kisasa kabisa na hakuna mfano wake katika nchi ya Tanzania. Lakini pia nampongeza sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwa kazi nzuri anazozifanya katika Mkoa wetu; nampongeza *DC* na Mkurugenzi wangu katika Halmashauri ya Mbinga na Madiwani wa Mbinga kwa kazi nzuri wanazofanya na wananchi wa Mbinga kwa kazi wanazofanya kwa juhudi sana.

Mheshimiwa Spika, pia kipindi cha mwaka jana, Halmashauri yetu kwa kushirikiana na Vyama vya Msingi vya Ngaka, Mahilo, Ngima na Pilikano, vilipata mkopo kutoka Shirika la *NSSF* wa Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kukusanyia kahawa. Mkopo huu umevunja rekodi kwa sababu umelipwa katika muda wa siku 90 toka ulipokopwa. Wakulima wale wamepata faida ya Sh. 1,000,800,000/= na hizi fedha zimekwenda kwa wakulima. Halmashauri imefanya kazi kubwa ya kusimamia toka kupata mkopo huu na namna ya kuwapa fedha hizi wakulima na namna ya kurudisha.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nasema, tunapopata Viongozi wazuri, Mkurugenzi na wafanyakazi wenzake, kwa kweli maendeleo katika eneo husika yanajitokeza. Mfano mzuri ni Mbinga na hasa kupitia mikopo hii iliyokwenda kwa wakulima. Ni matumaini yangu kwamba, juhudi hizi hawa Viongozi wa Halmashauri wataziendeleza ili kuleta maendeleo zaidi kwa hawa wananchi wa Mbinga.

Mheshimiwa Spika, nawapongeze *NSSF* kwa kuondoka kabisa katika utamaduni wa kawaida wa kukopesha wafanyabiashara wakubwa na kuingia kwa wakulima hawa. Huu ni ukombozi dhahiri sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Daou na Wakurugenzi wote katika Shirika la *NSSF*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya *TAMISEMI* katika uchambuzi wake ukurasa wa 13, moja ya jambo kubwa linalojitokeza pale ni kwamba hela zinachelewa kutoka Hazina, hazifiki kwenye Halmashauri zetu kwa wakati. Sasa hivi barabara zetu ni mbaya, lakini hela hazijapatikana! Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba, Serikali ilete fedha hizi kama ambavyo tumeidhinisha kwenye bajeti zetu. Hii itatusaidia sana kuleta maendeleo katika maeneo yetu na ugatuaji wa madaraka Mikoani utaonekana dhahiri tunapoleta hizi fedha. Tusigatue tu madaraka, lakini fedha zinachelewa kufika.

Mheshimiwa Spika, pia katika taarifa yake kwenye utekelezaji wa miradi ukurasa wa 24, imeonesha kuna matatizo makubwa matatu. Kwanza, miradi haitekelezwi kwa wakati na sababu mojawapo ni ucheleweshwaji wa fedha; pili, miradi hiyo haikamiliki kwa viwango vile vinavyotakiwa. Hili ni tatizo zaidi la baadhi ya watumishi katika Halmashauri yetu. Nami naomba sana msaada kwa Mheshimiwa Waziri anayehusika, kwa kweli naye nimpongeze anafanya kazi nzuri na Manaibu wake na Wakurugenzi wake katika *TAMISEMI*. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika maeneo mengine, kuna matumizi mabaya ya fedha ambayo ningependa kuona hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa. Zimechukuliwa, lakini tunadhani zikiwa zinachukuliwa kila wakati itatusaidia sana kuwakumbusha hawa wafanyakazi kwamba kazi walizopewa ni dhamana na wanapaswa kufanya kazi kama wanavyoelekezwa.

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la *own source funds.* Hapa kuna matatizo, nami ningependa sana kuomba msaada wa Wizara pamoja na Mikoa kuhakikisha wanakuja

katika Halmashauri zetu kuzungumza nasi katika Halmashauri, kwa sababu wao wana utaalamu wa kifedha, wangeweza pengine kutuonesha, katika eneo hili mnaweza mkapata fedha na katika eneo hili mnaweza kupata fedha. Hili tukishirikiana na Madiwani, tunaweza tukaweka utaratibu mzuri zaidi, kama ni Sheria ndogo ndogo zinatakiwa kuwekwa, ili ili tuweze kukusanya hizo fedha.

Kwa hiyo, mngeweza kutusaidia hizi, nami naomba mtusaidie kuleta hao Wataalamu kule Mbinga ili tuweze kushirikiananao tuoneshane maeneo yetu na uwezo tulionao ili waweze kutushauri vizuri na kupanga vizuri zaidi namna ya kupata fedha kutokana na vyanzo vyetu vya ndani, maana tumeona kutegemea zaidi Serikali Kuu kunatuumiza zaidi.

Mheshimiwa Spika, la pili, nataka kuongelea juu ya maeneo mapya. Mwaka 2014 tumeingia katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, wakati huo tulikuwa tumeomba maeneo mengi sana ya Vijiji na Vitongoji, tumepata vichache, vingi hatukupata. Kwa vile vichache, tunawashukuruni sana, kwa Kata tisa ambazo Mbinga tulipata tunawashukuruni sana. Lakini katika uchaguzi ule ni dhahiri wengine walitaka kususia ule uchaguzi kwa kusema kwamba sisi tulitegemea tupate Kijiji, sasa hatujapata.

Kwa hiyo, napenda kuona kwamba yale maombi ambayo tumeleta ya kufikiriwa tena, muweze kuyafikiria ili hivyo vijiji vinavyostahili, niko tayari kukaa na Mheshimiwa Waziri kuzungumzia juu ya jambo hili ili wale wanaostahili waweze kupata. Nami nakubaliana na Wizara kwamba siyo maombi yote tuliyoleta ya vijiji kwa kweli yanastahili, lakini bado katika baadhi ya vile vijiji vinastahili kupewa hiyo hadhi ya kuwa Kijiji au hadhi ya kuwa Kitongoji.

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia pia juu ya maeneo mapya hasa kwa namna ya kugawana mali. Mimi nina uzoefu, tulikuwa tunagawana mali na Wilaya ya Nyasa, yalitokea mabishano ambayo pengine hayana msingi. Laiti kama Wizara ikituelekeza vizuri zaidi na itajipanga kuelekeza vizuri zaidi itakuwa vizuri.

Kwa mfano, tunalazimika kugawana viti ambavyo vimechakaa. Vinakwenda kwenye Halmashauri mpya! Mimi sidhani kama ile Halmashauri inasaidiwa vizuri zaidi. Nilifikiri Halmashauri inayoanza, ianze na *furniture* mpya, itapata majengo mapya baadaye. Mambo kama haya yanaweza kusaidia sana kujenga msingi bora wa mahusiano katika Wilaya mpya na Wilaya ya zamani kwa sababu, bado hizi Wilaya zitaendelea kushirikiana kwa muda mrefu na kwa kweli zinahitaji kushirikiana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nikumbushe tu, pale Mbinga tuna nyumba ya *DC* ina miaka mitano sasa, karibu inakamilika. Ikipewa hela kidogo tu kama Shilingi milioni 100/ 150 itakuwa imekwisha.

Mheshimiwa Spika, niingie kwenye hotuba ya Mwenyekiti wa masuala ya *UKIMWI.* Hapa nilitaka kuongelea jambo moja tu kwamba mambo yote katika ulimwengu huu yanaanzia katika ulimwengu wa kiroho. *UKIMWI* maana yake ni Upungufu wa Kinga Mwilini, lakini kuna ugonjwa unaoitwa *UKIRO* – Upungufu wa Kinga Rohoni. Huu kuna watu maalum wanaoushughulikia na hawa aghalabu tunawa-*engage* katika vita hii. Nami nazungumzia hapa Viongozi wa Dini, wao ndio wanaweza wakatibu huu *UKIRO*. Nami ningependa sana Viongozi wa Dini wawe *involved* kwa kiwango kikubwa ili watu waweze kubadilisha mienendo yao na waweze kuokoka na janga hili la *UKIMWI.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

SPIKA: Ahsante sana, nashukuru kwa kuniokolea muda.

Sasa namwita Mheshimiwa Mipata, na kutokana na hiyo nafikiri, hebu azungumze kwanza Mheshimiwa Mipata.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia. Nitakuwa na nafasi ya kuchangia katika maeneo matatu;

mojawapo ni Tawala za Mikoa na Kamati pia ya Katiba na Sheria na vilevile nikiweza masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, nikianza na hiyo ya kwanza; Halmashauri zetu ili ziweze kufanya vizuri zinahitaji kupata mapato. Mapato ya Halmashauri yanaainishwa katika vyanzo vitatu, yaani yanaweza kupatikana katika maeneo matatu; ya kwanza ni ruzuku, ya pili ni maeneo wanayojitafutia wenyewe *(own sources),* eneo la tatu ni misaada kutoka kwa wadau mbalimbali. Lakini kwa sasa Halmashauri zetu zinategemea zaidi ruzuku na ruzuku hii inatufanya tuchelewe hasa kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nikianzia na ruzuku inayotolewa kwenye barabara, mtandao wa Halmashauri wa barabara ni zaidi ya kilometa 108,000 kwa Halmashauri zetu. Ile mitandao ya barabara inayoshughulikiwa na Serikali Kuu ni 35,000 *kilometres,* lakini mgawanyo unaoenda kuhudumia kutoka kwenye ruzuku ya Serikali ni *vice versa,* Halmashauri zenye mtandao mkubwa zinapata 30% tu kutoka Serikalini na Serikali inabaki na asilimia 70. Huko ndiko kunakaa wananchi wengi, hii ni changamoto inatakiwa kushughulikiwa. *Formula* hii haifai kwa sasa, itazamwe upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo yake ni nini? Naanza katika Jimbo langu. Matokeo yake barabara nyingine kwenye Halmashauri zinafunga kabisa. Nina barabara moja inaitwa Nkhanakala ina kilometa 68. Sasa hivi ninavyosema, itafunga baada ya siku chache. Yote hii ni kutokana na ukosefu wa pesa, kutegemea ruzuku ambayo inaweza isipatikane.

Mheshimiwa Spika, nawaomba wahusika wote barabara hii wainusuru, ina hali mbaya sana. Mimi kama Mbunge wa Jimbo linalohusika, nimejitahidi kuwaona wahusika wote wa nchi hii wanaohusika na barabara. Nimemwona Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, nimemwona Mkurugenzi wa Barabara Nchini na kumpelekea picha, nimemwona Katibu Mkuu, nashukuru alinikaribisha vizuri;

nimemwona Mkurugenzi wa Barabara *TAMISEMI,* nikaelezea kwamba siyo muda sasa tutapata aibu! Wananchi wapatao 14,000 wanaoishi kwenye Kata ya Kala wanaotegemea barabara moja tu kuingia na kutoka, sasa baada ya wiki mbili tatu na kwa mvua hizi zilizopo, watakuwa hawawezi kupata huduma yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013 ilitokea tukapoteza watoto wengi sana katika Vijiji vya Kata ya Kala kwa namna ambayo haikutangazwa. Hawana mawasiliano yoyote ya simu na barabara ndiyo changamoto kiasi hicho. Huduma zenyewe za afya hazipo kule. Kwa hiyo, naomba hii niiwasilishe rasmi kwa wahusika wote waichukulie kama hali ya tahadhari! Siyo hali ya kawaida, hapana! Hali ya tahadhari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo, ili wananchi hawa waweze kuchangia Halmashauri na Serikali iweze kupata mapato, wanatakiwa wasiwe na kero. Wananchi wa Chala wana kero kubwa. Nashukuru leo Mheshimiwa Magufuli yuko kule! Wanahitaji fidia ya mahali barabara inapita, Chala.

Mheshimiwa Spika, barabara yote hii inayojengwa kutoka Sumbawanga kwenda Namanyere mpaka Kibaoni, watu wote wamefidiwa tena vizuri, Chala peke yake wamebaki! Mwisho wanaweza kusema Mbunge hatusemei vizuri, mara wanasema sisi hatupendwi hapa Chala. Ni wapiga kura hawa, wanatuchangia vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iwe na masikio, itoe uamuzi wa haraka katika jambo hili. Ni kero na tunaenda kwenye uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala la barabara iko barabara nyingine inayotoka Kasu – Katani kwenda Myula. Ni eneo linalounganisha wakulima wazuri ambao wangeweza kuichangia Serikali vizuri kwa kodi, kwa ushuru na vinginevyo. Halijashughulikiwa vizuri na linaunganisha wakulima wengi sana. Naiomba Serikali iliwekee mkono wa

baraka liweze kupata pesa, tuwe na barabara nzuri katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala la mawasiliano ya simu. Sasa hivi mawasiliano ya simu yana mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa, mtu binafsi na Kaya, lakini kuhimili tahadhari mbalimbali za kiusalama. Nina Kata tatu; Kata ya Kala, Wampembe, Ninde pamoja na Kata yenye Makao Makuu ya Jimbo. Mawasiliano hamna! Ahadi za mara kwa mara zipo! Sasa hivi *Viatel* ndiyo wanaonesha nia kule. Naomba wanaohusika wapeleke msukumo wa kutosha ili tuweze kuondoa kadhia hii ambayo ni mbaya.

Ndugu zangu hali iliyoko kwenye Jimbo la Nkasi Kusini ni tofauti na Majimbo mengine, hatuna mawasiliano kabisa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la maji. Wananchi wanahitaji kuwa na afya ili wachangie mapato ya Serikali. Kuna mradi uko King'ombe unatakelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, tumetumia zaidi ya Shilingi milioni 500, hakuna maji hata tone yanayotoka pale. Ni aibu tunapoingia kwenye uchaguzi leo, wananchi tutawajibu nini?

Mheshimiwa Spika, nimemtembelea Waziri wa Maji mara kwa mara na kumweleza jambo hili aliangalie, ni aibu! Shilingi milioni 500 zimetumika kwa makosa yoyote yatakavyokuwa, kama ni ya Mhandisi Mshauri au vyovyote vile, lakini lazima wananchi hawa watatupa maswali ambayo tutashindwa kuyajibu. Yapo maeneo mengine yenye changamoto kubwa sana ambayo usipowasaidia wananchi, wanapata kadhia kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upo mradi mwingine wa maji wa Bwawa la Kawa. Mkandarasi sasa anajenga vizuri na Halmashauri imesimamia vizuri sana eneo hili. Vijiji vya Hundi, Kalundi, wamejengewa hata miundombinu. Kinachosubiriwa ni kutengeneza *treatment plant* ambayo mpaka sasa inategemewa itekelezwe na Wizara yenyewe. Kwa hiyo, naomba kwa namna yoyote ile Wizara itusaidie kuhakikisha

kwamba *treatment plant* inayotakiwa iweze kutekelezwa na hiyo itatusaidia.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni suala la Kilimo. Mmetuzoeza katika kilimo kutupa mbolea, mwaka huu hamkutupatia. Licha ya utaratibu uliobuniwa ambao haukufanikiwa sana, lakini mbolea pia haikupatikana kwa wakati, mnatuangusha. Hakuna!

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Malocha hapa alizungumza vizuri jana kuonesha takwimu za kilimo zilivyokuwa mwaka 2014, hasa Mkoa wa Rukwa. Lakini sasa wakulima saa hizi hawana pesa na tunaidai Serikali. Naomba mbuni utaratibu utakaowawezesha mbaki rafiki kwa wakulima na huku mambo yao muwe mnayashughulikia.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna uadui mkubwa zaidi, wakulima hawatupigii kura. Sababu kubwa ni hii, mbolea mlizowazoeza kuwapa hatuwapi, mazao tunayowakopa, hatuwalipi kwa wakati!

Mheshimiwa Spika, kwa sababu zozote zinazoweza kuzungumzwa na Serikali, haziwezi kueleweka kwa mwananchi ambaye ni mkulima. Anaugua, hana namna ya kumpeleka mtoto hospitalini. Mtoto anakufa, halafu kesho unakwenda kumwomba kura, anakupa kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ni za msingi kabisa, tuziangalie kwa makini. Tuwapelekee pesa zao na tuweke mfumo ambao utafanya tubaki marafiki na wananchi wetu, lakini tuwe tunawahudumia kwa kutafuta masoko, kwa kuunda taasisi au mashirika ambayo yatashughulika na masoko ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni kuhusu Mahakama. Sasa hivi kunatokea mauaji katika maeneo mbalimbali tena ya kutisha, watu wanachomwa moto, tunawaona kwenye mitandao. Tujiulize kuna nini hapa? Kuna jambo ambalo siyo kawaida limetokea! Katika mfumo wetu

wa utendaji haki, tunatenda sawa sawa? Kwa nini haya mambo yanatokea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama yanatokea namna hii kwa vyovyote kuna jambo tumekosea. Tujisahihishe katika hilo, kama siyo kumrudia Mwenyezi Mungu, vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tutakaporudi, wafuatao wawe wamejiandaa na wengine muwahi kuja. Atakuwa Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina, Mheshimiwa Wenje, Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale, Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mheshimiwa Gosbert Blandes na Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Wengine tutawataja baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa hivi Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu na Makamu wao wote wa Kamati za Kudumu, tuna Kikao sasa hivi Kamati ya Uongozi. Mkitoka hapa tuna Kikao Kamati ya Uongozi sasa hivi, msiende kwingineko, twende tukafanye hicho Kikao katika Ukumbi wa Mheshimiwa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 655 mchana, Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujasitisha shughuli za Bunge mchana niliwaita wafuatao waweze kuanza kujadili; Mheshimiwa Deogratias Ntukamazima, Mheshimiwa Wenje, Mchungaji Mwanjale na Mheshimiwa Agripina. Mheshimiwa Deograsias Ntukamazina!

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza mchana huu ili nitoe mchango kuhusu taarifa hizi ambazo zinajadiliwa.

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na nitazungumzia mambo matatu tu. Moja, nitazungumzia hali ya utawala na utawala bora nchini; pili nitazungumzia wazo hili la kuhamisha Makao Makuu ya Serikali kuyaleta Dodoma na kuishauri Serikali kuachana na ndoto hii; ya tatu, Serikali kuona umuhimu wa kutekeleza miradi miwili muhimu ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wa kawaida ambayo ni Mkurabita na *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inasimamia Ofisi nyeti ambazo zinatakiwa kutoa dira na kuhakikisha ustawi wa wananchi. Ofisi hizo kama zilizotajwa kwenye taarifa, ni Ofisi ya Rais Utawala Bora, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi, Ofisi ya Rais Tume ya Mipango na Ofisi ya Makamu wa Rais, Sera, Uratibu na Bunge lenyewe, pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, hizi taarifa ni muhimu sana, ingawa ni za mwaka mmoja lakini tukumbuke kwamba Bunge letu la miaka mitano linaelekea ukingoni. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati mbalimbali wajiulize maswali yafuatayo kwa sababu karibu tunamaliza kipindi chetu. Swali la kwanza je, sisi katika Kamati mbalimbali tumesimamia ipasavyo sekta ambazo ziliwekwa chini yetu? Tumezisimamia kikamilifu? Je, Serikali imetekeleza ushauri wetu? Je, tumekuwa na *impact* yoyote?

Mheshimiwa Spika, *impact* maana yake ni kwamba tumefanya mambo muhimu ambayo yanabadilisha maisha ya wananchi. Mwisho, tunaacha *legacy* gani? Ni mambo gani mazuri ambayo tutakuwa tumeyafanya ambayo wananchi watatukumbuka?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwenye Ofisi zote hizi nitazungumzia Ofisi ya Rais, Utwala bora. Sisi katika Kamati

yetu ya Katiba na Sheria kwa miaka minne tumekuwa tukiishauri Serikali pamoja na TAKUKURU izidishe mapambano dhidi ya rushwa, lakini naona aibu kwamba rushwa inazidi kupamba moto, nchi inanuka rushwa, *the country has gone to the dogs.* Tafsiri ya kwanza ya utawala bora ni kutokuwepo na rushwa katika jamii, mengine ni *rule of law,* yaani utawala wa sheria; *transparency* lakini mimi nitazungumzia utawala bora.

Mheshimiwa Spika, Serikali yangu ya mapinduzi ni sikivu, lakini kwa hili la rushwa, naomba niipeleke Serikali yangu kwa *Doctor* wa *ENT (Ear, Norse and Throat),* yaani kwa maneno mengine niipeleke Serikali yangu kwa Daktari wa Masikio. Naomba kabisa Serikali iwe sikivu kwa upande huu wa utawala bora.

Rafiki yangu, Mheshimiwa George Mkuchika, hayupo, ndiye anasimamia sekta hii. Mheshimiwa George Mkuchika *is a gentleman,* ni mwadilifu sana. Lakini kuwa mwadilifu haitoshi, *you have to provide a leadership,* kusimamia vyombo vile tunavyosimamia au rushwa. Lakini nitakuwa namwonea kwa sababu kazi hii ni ngumu sana, hawezi kupiga vita peke yake, hawezi ku-*provide leadership* peke yake na wala sio *number one,* ni *team work* ambayo Mawaziri wote wanatakiwa kuhusika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mkuchika, hayupo, kila ninapokutana naye ananisalimu anasema, *how are you senior citizen?* Namwambia, *I am fine!* Kuanzia kesho atakaponiambia *how are you senior citizen,* nitamwuliza swali moja tu; kila siku nitakuwa namwuliza George, *why are you still on the Government payroll?* Kwa nini wewe George bado unalipwa mshahara na Serikali wakati nchi inanuka rushwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye *Escrow*. Kwenye *Escrow* tumeambiwa upande mmoja tu. Tumeambiwa juu ya viongozi wachache ambao walipewa zawadi na rafiki yao anaitwa James Rugemalira. Mimi naita ni zawadi kwa sababu Rugemalira hakutoa rushwa, kama angekuwa ametoa

rushwa, angekuwa ameshakamatwa na kupelekwa Mahakamani. Anayetoa rushwa na anayepokea rushwa wote ni wahalifu.

Kwa hiyo, tumeambiwa upande mmoja. Mimi naomba, kama Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, tumeshamwomba Mheshimiwa George Mkuchika amwambie Ndugu Edward Hosea afanye uchunguzi kuhusu haya majina tunayoyaona kwenye mitandao na minong'ono kwamba kuna Viongozi vigogo, *senior Ministers* wamechota fedha nyingi kutoka *Stanbic* kwa upande wa yule *PAP*. Tunataka katika *transparency* na utawala bora watu hawa wajulikane na wawajibishwe, siyo kuwawajibisha Mawaziri wawili tu na wengine wanaendelea kudunda wakati ipo minong'ono na ipo kwenye mitandao.

Mheshimiwa Spika, nimemaliza kuhusu utawala bora, lakini rushwa ndiyo inaikosesha Wilaya yangu ya Ngara barabara nzuri, elimu nzuri, maji safi na huduma mbalimbali, vile vile na katika Wilaya mbalimbali. Inanikumbusha Rais Mobutu Sese Seko wa Zaire alikuwa ni Rais ambaye aliibia nchi yake sana. Kwa hiyo, unapokuwa *corrupt* mambo mengine unayaacha.

Kwa mfano, wakati *RPF* akina Kagame wanatoka Uganda kuja ku-*attack* Rwanda, alikuwa anatawala Marehemu Habyarimana. Habyarimana alijaribu kumpigia simu Mobutu, akasema naomba unisaidie, *RPF* anakuja. Akamjibu usiku, akamwambia, nilikwambia usitengeneze barabara. Sasa umetengeneza barabara, wanakuja kwa urahisi, sitakusaidia chochote. Ukishakuwa na *corruption,* mambo mengine yanapotea.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la pili, kuhamisha Makao Makuu kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma. Naomba Serikali iachane na ndoto hiyo. Imepita miaka 42, hatujafanya lolote, Wizara ya TAMISEMI ndiyo iko Dodoma peke yake, katika hii miaka iliyobaki hatuwezi na hasa ukijua kwamba nchi imeingia ufisadi sana, nchi haina hela, *Chancellor of the Exchequer* wetu juzi ametuambia (*Chancellor of the*

Exchequer maana yake ni Waziri wa Fedha) Serikali haina fedha. Kwa hiyo, tuachane na ndoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza tusije tukatoa kisikinzio kwamba hatuwezi kukinzana na ndoto ya Baba wa Taifa. Tulishaachana na falsafa yake nzuri ya Azimio la Arusha, haya mambo mengine ni madogo, tunaweza kuachana nayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali yangu ya CCM, iwe *in the driving seat,* yaani iongoze nchi vizuri, tupambane na rushwa na tuweze kuwa na ustawi wa wananchi.

Jambo la tatu ambalo napenda kulizungumzia ni ile ya kuihimiza Serikali kuhakikisha kwamba inazingatia hii miradi miwili ambayo ni ukombozi kwa wananchi wa kawaida, yaani MKURABITA, yaani kurasimisha biashara na mali za wanyonge; unapima mashamba ya kaya; unawapa hati miliki za kimila; wanaweza kwenda Benki wakapata hela; inakuwa ni dhamana au *collateral*.

Mheshimiwa Spika, pia namkumbusha Waziri mpya ambaye sasa hivi anasimamia MKURABITA, kwamba Serikali ilishatoa ahadi kwa Wilaya ya Ngara pamoja na Karagwe, kwa kuwa tuna wahamiaji haramu wanapora ardhi yetu, aliagiza Mheshimiwa Wasira na nikaenda kule MKURABITA, wakakubali kwamba watafute fedha wapime mashamba ya kaya zote za Ngara ambazo ni nyingi sana, halafu wawape hatimiliki za kimila, hivyo hivyo pamoja na Karagwe. Naomba jambo hilo lifanyike. MKURABITA ni mradi mzuri sana, naomba Serikali iuzingatie.

Mradi mwingine ni ule wa *TASAF*. Tunayo *TASAF* namba tatu ambayo lengo lake ni kusaidia kuinua hali za kaya masikini sana.

Naomba *TASAF* iwafikie wale walengwa, kaya maskini sana, wasije wakapotoshwa na viongozi wa huku chini kwenye Kata na kwenye vijiji wakaziendea kaya ambazo siyo masikini naomba wafike kwenye lengo hilo.

Mheshimiwa Spika, hili wazo la kuhamia Dodoma siyo lazima Makao Makuu ya Serikali yawe pamoja na Bunge. Hata kule Malawi na Nigeria tulikuwa na wazo hilo moja, wao walishafanikiwa. Nigeria walihamisha Serikali kutoka Lagos wakaenda Abuja; Malawi ambayo ni nchi masikini sana, kwa sababu ya utashi wa kisiasa, walihamisha Makao Makuu ya Serikali kutoka Blantyre kwenda Lilongwe.

Sasa sisi tunahitaji utashi wa kisiasa. Kama haupo, naomba Serikali itafakari upya jambo hili na iachane na mradi huu, iachane na mradi wa kuleta Makao Makuu hapa Dodoma. Waache Mabalozi wakae karibu na Bahari, wakae karibu na Serikali, wafanyabiashara wako wengi, siku hizi tunazungumzia mambo ya *Partnership* kati ya Serikali na *private sector,* acha Makao Makuu yakae Dar es Salaam na *Parliament* ikae hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii nami pia niweze kuchangia kuhusu mijadala hii ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika kuwasilisha hizi hoja ndani ya Bunge, katika Kamati iliyopita ya *LAAC* walizungumza sana suala la ufisadi uliokithiri ndani ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Katika Kamati tena ya TAMISEMI katika kitabu chao ukurasa wa nane, pia wamezungumza sana suala la ufisadi wa kutisha kwenye Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Lakini pia hapa nina *special audit,* ukaguzi maalum uliofanyika katika Jiji la Mwanza, pia wamezungumza sana kuhusu ufisadi mkubwa uliofanyika katika Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze kwa usemi maarufu wa Chinua Achebe, Mwandishi maarufu aliyewahi kusema kwamba ukitaka kukumbuka au ukitaka kujua umenyeshewa mvua kiasi gani, ukumbuke lile tone la kwanza lilikuanzia wapi. *If you want to know how much it has rained on you, you should remember where the first drop got you.*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivi? Nataka nirudi kwenye *genesis,* mwanzo kabisa, chimbuko la ufisadi hili linalozungumzwa hapa la Jiji la Mwanza na sura yake kubwa imekuja kwenye ujenzi wa *clinic* ambayo ilitengwa *almost* Shilingi milioni 800 ya kujenga *clinic* ambayo jengo lililojengwa hata godauni bora kuliko hilo jengo lililojengwa. Kuna *special auditor* hapa imetoa hiyo ripoti, kamati ya *LAAC* imetoa hiyo ripoti lakini pia Kamati ya TAMISEMI imezungumzia. Sasa tulianza kunyeshewa mvua wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba kumbukumbu ikae wazi kwamba mtu wa kwanza aliyekuwa dalali wa kwanza wa kuuza eneo maarufu Mwanza iliyokuwa eneo la *clinic,* Halmashauri ilishinikizwa kuuzia *BOT.* Dalali wa mauzo haya alikuwa ni Mheshimiwa Aggrey Mwanri, ndiye katika kila kikao kilichohusisha Madiwani wetu wa Jiji la Mwanza na watu wa *BOT,* Mheshimiwa Aggrey Mwanri alikuwa anachukua ndege kila wakati anaruka kutoka Dar es Salaam kuja Mwanza kushiriki kwenye hivi vikao, kuwa dalali kwenye mauzo haya. Sasa naomba kwanza ieleweke, nami nahoji, nataka kujua Mheshimiwa Mwanri alikuwa anatumwa na nani kuja kuwa dalali wa mauzo haya?

Mheshimiwa Spika, *it is true,* ni kweli kabisa kwamba eneo la *clinic* wananchi wote wa Mwanza wanajua pale Makongoro, lile eneo *value* yake ni kubwa kuliko Shilingi bilioni tatu. Tayari tulikuwa na watu wa *Shoprite investors* waliokuwa tayari kununua lile eneo kwa Shilingi bilioni sita, Mheshimiwa Mwanri aliambiwa. Hivyo vikao vyote vilikuwa vinafanyika mimi Mbunge nikiwa ndani ya Bunge. Jibu alilotoa, alisema kwamba haya siyo mauzo ya kibiashara, ni mauzo ya Serikali na Serikali, siyo kutafuta faida.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nauliza na naomba mjue, huu ufisadi wa mabilioni kadhaa ikiwemo na ujenzi wa *clinic* Mwanza, nataka *record* ziwe *clear,* tulianza kunyeshewa mvua wapi? *That is where it started raining on us.* Mheshimiwa Mwanri alipoamua kuwa wakala wa *BOT* kwenye manunuzi ya kiwanja kile na sijui nani alikuwa anamtuma.

Mheshimiwa Spika, baada ya mauzo haya kufanyika, Madiwani wa Mwanza pamoja na Mbunge mimi, sisi siyo Wajumbe wa *Tender Board, it should be very clear,* kuna mtu nchi hii anaitwa Wilson Kabwe, aliyekuwa MKurugenzi wa Jiji la Mwanza; kipindi hiki katika mwaka wa fedha kuanzia 2010/2011, 2011/2012 hata kipindi *CAG* wamekuja, kipindi ambacho hii *special audit* sasa inafanyika katika huo mwaka, mauzo haya yalivyofanyika, huyu Kabwe na timu yake ya Halmashauri, hawa watu ndio waliokaa wakamtafuta Mkandarasi, wakaingia naye kwenye mkataba. Tukaletewa picha ya jengo kubwa ambalo ni tofauti na jengo la *clinic actual* iliyojengwa pale.

Mheshimiwa Spika, *Special audit* imefanyika, watu wote wamesema katika Kamati hizi zote kwamba jengo la *clinic* lililojengwa Mwanza, haliendani na thamani halisi ya fedha iliyotumika. Haipo! Wamejenga choo, siyo *clinic*.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiangalia ripoti ya *CAG* ametoa *recommendation* kabisa, anasema, huyu Kabwe achukuliwe hatua za kinidhamu. Madudu ya Kabwe ni mengi aliyofanya Mwanza! Ukisoma hii *special audit report,* yamejaa ujinga mtulpu! Madudu matupu! Wizi mtupu, aliofanya Bwana Kabwe. Lakini cha ajabu, huyu Kabwe, *same* Kabwe amekuwa *promoted,* leo ndio Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam. Pamoja na kwamba *CAG* ametoa ripoti kwamba huyu mtu achukuliwe hatua, watu wote aliofanya nao kazi Mwanza wote wamekuwa *promoted.* Aliyekuwa Mkuu wa Manunuzi Bwana Titto bado yuko Mwanza, leo ndio Mkuu wa *Procurement*. Walioingia kwenye *contract* chafu ya kujenga *clinic* isiyo na tija ambayo mpaka leo haiwezi ikafanya kazi, kwa sababu iko chini ya thamani na chini ya kiwango, hawa watu wapo.

Mheshimiwa Spika, wametumia mabilioni ya fedha zetu kujenga vitu ambavyo haviwezi vikatumika. Kabwe yupo, *he is living large,* Titto yupo, ndiyo bado Mkuu wa *Procurement* pale, yupo mwingine anaitwa Bwana Wanga, aliyekuwa Mwanasheria wa Jiji kipindi hicho aliyeingia kwenye mikataba hii na hao Wakandarasi, naye yupo, leo amerudishwa tena

Mwanza kwenda kuwa Mkurugenzi Ilemela. *We are living in a country where we are glorifying thieves.* Hawa watu wapo na wanajulikana.

SPIKA: Mheshimiwa kwa sababu wewe ni Diwani, nawe iliponyeshewa mvua, ulikuwepo. *(Makofi)*

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, nimetoa *background* nimesema, kipindi mkataba huu wote unafanyika, vikao vyote Mheshimiwa Mwanri *was flying to Dar es Salaam and I was in the Parliament*. Hakuna hata kikao kimoja kilichofanywa kipindi tukiwa huku kama Wabunge na hata Mheshimiwa Kiwia tulikuwa naye. Mheshimiwa Mwanri alisema, alitumwa kwa niaba ya Serikali kwenda kusimamia mauzo.

I just want to know, kwenye Serikali nani aliyemtuma kwenda kusimamia mauzo ya Shilingi bilioni tatu wakati sisi tulikuwa na *investors* ambao walikuwa tayari kutupa Shilingi bilioni sita? *This is what I am talking about!*

Mheshimiwa Spika, huyu Bwana Kabwe ninayemsema, ukisoma hii *special audit report* iliyotolewa na *CAG* ambayo Serikali mpaka leo haiwezi ikachukua hatua, katika Jiji la Mwanza, siyo tatizo la *clinic* tu. Ukisoma ripoti ya *LAAC,* kuna miradi ya maji hewa. Maeneo ya Nyashana, imekuwa *reported.*

Kuna risiti zimewekwa humu, risiti walizokuwa wanatumia kukusanya mapato, risiti hewa. Ukisoma hii ripoti ya *CAG* huyu mtu anaitwa Kabwe ameisababishia Serikali hasara ya fedha zinazoweza zikafika Shilingi bilioni 15, ukisoma hii *special audit report* na huyu mtu yupo. Kabwe ndiye aliyetusababishia hasara na mgogoro wa wananchi kwenye viwanja vinaitwa vya Bugarika. Akachukua pesa za *NSSF* zaidi ya bilioni kwamba anaenda kulipa fidia, hawakulipa fidia, wakaenda kujenga Hoteli maeneo ya Luchelele Mwanza. Huyu mtu bado yupo! Badala ya kuchukuliwa hatua, angekuwa Gerezani, huyu mtu ndio leo pia bado ni Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka *speech* ya *P. L. O.* Lumumba, *speech* yake moja alisema: " if Mwalimu *were to wake up today*, na mimi nashangaa *if* Mwalimu *were to wake up today, what kind of* Tanzania *would be confronted with*? Angekuwa *confronted* na Tanzania ambayo *we glorify thieves, we take thieves from one station to another* hatuwachukulii hatua.

Mheshimiwa Spika, akina Mtemvu wamelalamika hapa kila siku kuhusu wizi wa Kabwe, hivi tunalipeleka Taifa wapi? Kila Mbunge akisimama hapa, ripoti zote mlizoleta ndani ya Bunge, yote yamejaa ufisadi, yananuka rushwa, *we are authors of our own problems,* wakati tunabaki tunalalamika; *we are the creators of our own problems.*

Mheshimiwa Spika, haya nasema na tunasema kila siku, Kabwe ni jangili amesababisha hasara kubwa na ripoti…

SPIKA: Haya, tunashukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, anafuatia na Mheshimiwa Agripina baada ya hapo.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu katika hotuba hizi tatu. Naomba nianze kwa kuzungumzia suala la lishe, ukisoma katika taarifa ya Kamati ya UKIMWI, kipengele cha 12 kinazungumzia mambo ya lishe. Lishe katika nchi yetu imekuwa ni tatizo kubwa sana na juzi uko Mbeya kulifanyika mkutano wa wataalam mambo ya lishe Tanzania na wakaeleza wazi kwamba katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe ni kati ya Mikoa ambayo inaongoza kuwa na lishe duni kwa nchi hii ya Tanzania na Mbeya ni ya kwanza. Asilimia 50 ya watoto chini ya miaka mitano wamedumaa wako *stranted* ni hatari kubwa kweli kweli.

Kwa hiyo, tunapozungumzia masuala haya ya UKIMWI tunaona jinsi ambavyo na kwa kweli bahati mbaya mikoa hiyo ndiyo ambayo inaongoza kwa maambukizi ya UKIMWI Tanzania. Maana yake Mbeya, Iringa, Njombe na Dar es Salaam, lakini ndiyo mikoa ambayo lishe imekuwa ni duni,

fifty percent ya watoto chini ya miaka mitano wakiwa wamedumaa, maana yake tutakuwa na jamii ambayo kwa kweli sijui tutaita jamii ipi, watoto watakuwa wamedumaa hawawezi kusoma, hata masuala haya tunayozungumza ya kuboresha elimu yatakuwa hayana maana kama hatutaanza kwanza kuangalia lishe ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwamba suala la lishe ndiyo lingekuwa jambo la kwanza kabisa kulishughulikia, watu wapate elimu wajue ni kitu gani na wengine lishe inakosekana kwa sababu ya maandalizi, matayarisho ya vyakula. Inawezekana lishe zipo katika baadhi ya vyakula lakini matayarisho ya vyakula, hili linahitaji elimu na ndiyo maana nasisitiza kwa uhakika kwa sababu Mbeya, Iringa na Njombe ni mikoa ambayo inaongoza kwa UKIMWI Tanzania. Kwa hiyo, kama lishe yake itakuwa ni ndogo maana yake watu hawa watakuwa katika hatari ya kufa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie suala hili. Lishe ni tatizo kubwa, tatizo ambalo kwa kweli limeikumbuka nchi yetu, wanasema Tanzania tuna asilimia 42 ya watoto chini ya miaka mitano wako *stranted* wanadumaa. Kwa hiyo, ndani ya miaka kumi inayokuja, miaka ishirini inayokuja maana yake tutakuwa na jamii ambayo itakuwa haina maana hata ukiwapeleka shule watakuwa hawana uwezo wa kufikiri. Sasa kwa nini Serikali inyamaze kimya kwa suala hili. Nafikiria kwamba ingekuwa ni busara sasa kuanza kufikiria namna ya kukomesha tatizo hili ili hii jamii ambayo inaishi kwa kweli iishi kwa amani.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kusema baada ya lishe ni dawa za kulevya. Dawa za kulevya limekuwa ni tatizo kubwa sana kwa nchi yetu, limekuwa ni tatizo kwa sababu dawa za kulevya zimezidi kuongezeka nchini kwetu. Nataka nitoe ushauri tu kwa Serikali tuna Sheria ya Kudhibiti Dawa za Kulevya na Sheria hiyo inatumika hapa Tanzania, lakini majirani zetu nchi kama Kenya, maana hapa tumetaja, ukisoma katika vipengele hivi imetaja kuna *cocaine*, mirungi, bangi, kuna kila kitu hicho.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo mirungi ukienda Kenya inalimwa, iko wazi, wanauza sokoni, lakini Sheria hapa Tanzania sisi tunadhibiti tunazuia na mtu akikamatwa na mirungi maana yake anawekwa ndani kwa nini Wizara hii ya *East Africa* isiwe na mahusiano mazuri na kulizungumzia suala hili kwa pamoja ili tuwe na udhibiti wa pamoja. Mirungi inapolimwa Kenya na hapa isilimwe na hapa kama Kenya wanakula basi na kule itumike.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri kwamba Serikali ingekuwa makini kuangalia sheria ambayo au Wizara hii kujaribu kukutana na wenzao wa Kenya na Uganda waweke suala hili kwa pamoja ili Sheria hii ya Kudhibiti Dawa hizi za Kulevya iwe ni kitu kimoja. Tunapozungumzia dawa za kulevya ukienda Kenya iwe ni hiyo hiyo moja na hasa kwa mirungi. Kwa hiyo, naomba sana lazima tufikirie.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kusema ni suala la bajeti ya UKIMWI, nilikuwa kwenye Halmashauri yangu kule naangalia, Serikali ilikuwa imeahidi ingetoa hela kule karibu milioni 60 kwa ajili ya Halmashauri ya Mbeya Vijijini, lakini katika milioni 60 hata senti tano haikwenda kule kusaidia kushughulikia masuala ya UKIMWI hata senti tano haikwenda, tunategemea nini? Je, tuna dhamira ya kweli kwamba kweli tunahitaji tufikie *zero* inapofikia 2030 au tunaona basi, hatuna dhamira ya hakika na ya ukweli. Naomba Serikali ingejaribu kufikiria suala hili maana kwa kweli ni gumu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naomba nichangie, kama hela haziwezi kwenda kwenye Halmashauri maana yake vitu vingi sana vitasimama. Kwa mfano, ujenzi wa zahanati nyingi sana za vijijini, namwomba Waziri wa TAMISEMI kama atakuwa na nafasi, aje kule Mbeya nimpeleke nimwonyeshe zahanati zaidi ya 70 zimekwisha wananchi walishahamasishwa, wamejenga lakini wanasubiri Serikali ahadi yake iweze kukamilisha zahanati hizo, lakini mpaka sasa hakuna. Tunategemeaje kwamba suala hili la UKIMWI litapungua wakati huko vijijini wanakwenda mbali kufuata dawa?

Mheshimiwa Spika, sasa kama Zahanati haziwezi kujengwa zaidi ya sabini hizo kwa kweli itakuwa ni hatari kubwa na UKIMWI utaendelea kuzagaa. Naomba Waziri wa TAMISEMI au Naibu wake aje Mbeya nikampeleke kwenye zahanati ambazo bado wananchi wanasubiri ahadi ya Serikali kukamilisha zahanati hizo.

Mheshimiwa Spika, hela hazipo mpaka sasa hivi mpaka mwezi huu wa Kwanza au wa Pili ni asilimia 30 tu ya fedha ambazo zimekwenda kwenye Halmashauri tena za maendeleo, 30 *percent* sijui kama ni *forty* lakini kwangu ni *thirty percent,* hii hela haijakwenda kabisa, *thirty percent* ndiyo zimekwenda, *seventy percent* hakuna, tunategemea nini, kutakuwa na maendeleo nchi hii? Naomba suala hilo liangaliwe kwa makini zaidi. Hizi zahanati ambazo kwa kweli zinahitaji zikamilishwe, naomba Serikali iziangalie na Waziri aangalie kwa kweli zipangiwe bajeti.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya watu ambao wanaathirika zaidi na suala hili ni watu ambao wanaishi vijijini, watu wa mijini wana nafasi, hospitali zipo, lakini vijijini huko tunawatesa wale wananchi na wale wananchi ndiyo wanaipenda Serikali yao, ndiyo wanaichagua CCM, leo hii tunaacha wanakwenda wanavyokwenda.

Mheshimiwa Spika, naomba tuwaangalie watu hawa kwa sababu ni muhimu sana wana shida ya kila kitu, wana shida ya maji, zahanati, barabara, barabara hazipitiki kila mahali unaenda hakuna barabara, watu wanalala njiani, lakini huku mjini sisi tunatamba, tunatembea kwenye barabara za lami. Naomba Serikali iangalie watu wanaoishi maeneo ya vijijini wawahudumie, wapange bajeti ya kutosha ili na watu hao wafaidi matunda ya uhuru wa nchi yao. Kwa hiyo, hivyo ndivyo nilikuwa nafikiria ingekuwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naomba kwa TAMISEMI, kuna Vijiji vingi vilikuwa vimeomba viwe Vijiji na Kata na sehemu zingine kama kule kwangu kuna maeneo mengi ambayo walikataa hata kupiga kura, hawakwenda kwenye

kura kwa sababu wamenyimwa kupewa Kata au Vijiji. Kwa hiyo, hii naomba kwa sababu Waziri Mkuu aliahidi hapa kwamba atashughulikia….

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Nashukuru kwa kunipa nafasi sana.

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Agripina Buyogera atafuatiwa na Mheshimiwa Nyangwine halafu Mheshimiwa Sakaya!

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye Kamati hizi. Awali ya yote naomba niwapongeze Wenyeviti na Wabunge wa Kamati hizi kwa kazi nzuri waliyoifanya na kwa kweli mapendekezo yao ni ya msingi sana kama Serikali itatekeleza.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitoe ombi kwa Serikali kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini hasa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi. Kumekuwa na tatizo la wananchi kwa ajili ya mipaka, Wabunge wengi wamezungumza. Ni vizuri tatizo linapokuwa linazungumzwa na Wabunge Serikali ichukue hatua mapema. Naomba Serikali hususan TAMISEMI, vijiji ni mali ya Serikali na vinatambulika na vimesajiliwa, leo kuna mgogoro Mheshimiwa Waziri nimeshakwambia wa JKT pale Mtabira na vijiji vinavyozunguka eneo lile na hakuna mtu ambaye hajui kwamba yale yalikuwa ni makambi ya wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, baada wakimbizi kurejeshwa makwao ndiyo tumeweka jeshi. Sasa leo unakuta Mkuu wa Wilaya anaenda kufunga mafunzo ya kijeshi halafu wanatumia mafunzo yale kwenye hadhara kubwa wananchi wakiwa hapo anatangaza kwamba lile ni eneo la jeshi. Kati ya vijiji na lile Jeshi la JKT Mtabira, ni nani ameanza pale?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali hili lilichukue ndugu zangu, kwa sababu leo tunaona mauaji yanafanyika hapa na unajua jeshi siyo rafiki na kazi za wananchi. Jeshi limefundishwa lina kazi maalum na jeshi letu la Tanzania linaheshimika ulimwenguni kote, sasa leo inakuwaje wananchi waanze kugombana na jeshi letu? Kwa hiyo, naomba hili Serikali ichukue hatua za haraka kwenda kuonesha mipaka ili mpaka wa jeshi ujulikane, mpaka wa vijiji vinavyozunguka jeshi ujulikane. Naomba sana hilo.

Mheshimiwa Spika, la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri Mwanri anakumbuka niliwahi kwenda ofisi kwake kwa ajili ya Kitongoji cha Lugufu, watu wa maliasili wakiwa wanafyeka mazao, wakiwa wanawanyanyasha wananchi na hatimaye akampigia simu Mkurugenzi, zoezi lile wakalisitisha. Cha kushangaza kwenye uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa, bila sababu za kuridhisha kitongoji kile hakikushiriki kwenye uchaguzi. Maelezo yanasemekana kwamba wako kwenye hifadhi, kwa hiyo wanataka kuhamishwa. Naomba hili alifuatilie na kwa sababu ameshalifanyia kazi sina mashaka na yeye.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, naendelea na TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri kwanza nimpongeze kwa maamuzi yake ya kuwasimamisha wale Wakurugenzi kwa sababu ilikuwa hakuna namna na asingewasimamisha tena hapa tungemhoji maswali mengi. Vurugu zile za uchaguzi mimi nilifunga safari nikaenda TAMISEMI, watendaji wamenipokea vizuri sana pale, wamechukua hatua za kuwasilisha na Mkurugenzi wa Kasulu, lakini majibu waliyokuwa wanapewa mimi nikiwa ofisini yalikuwa hayaridhishi. Wanawaambia huku hamna tatizo ni tatizo dogo tunalishughulikia, Mkuu usiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, nimeondoka mimi hapa Dodoma naenda Kasulu, nakuta vijiji viwili, Kitema na Mkiheta vimefutwa vyote yaani kwamba wagombea wa NCCR wamekosea kujaza fomu vijiji vyote? Lakini baada ya kupigiwa simu huku wakakaa tena kikao kwamba Kamati sijui Kamati ya Rufaa ikakaa ikaamua kurudisha kijiji kimoja,

kingine kikaachwa na nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kasulu Vijijini vile vijiji vyote vilivyokuwa na matatizo, NCCR imeshinda hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Mheshimiwa Waziri awasiliane na wahusika hususan Waziri Mkuu watuletee Mkurugenzi haraka sana ili shughuli za maendeleo ziweze kuendelea vizuri katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu. Naamini hili atalitekeleza.

Mheshimiwa Spika, tangu nimeingia Bungeni nimekuwa nalalamika juu ya Kagera Nkanda, kila nikisimama hapa ninataja Kagera Nkanda. Hivi kwa nini Serikali haiwezi kutatua matatizo ya wananchi? Leo hii sasa Mgimwa yuko pale ananisikia, niliwahi kuuliza swali hapa na akanijibu kwamba Vijiji vya Kagera Nkanda vinanufaika na uwekezaji wa kitalu kilichopo Kagera Nkanda kwa kupata asilimia 25 kati ya fedha zinazopatikana.

Mheshimiwa Spika, naomba wakae wafuatilie hili, hizo fedha vijiji vyangu havijapata hata senti, lakini leo cha ajabu wananchi wako wanafyekewa mazao, yaani wamewaacha wakulima wakati Serikali inasema maisha bora kwa kila Mtanzania, wakulima wanalima mazao mahindi yamebeba, Watanzania wenzetu wanashika mapanga wanakwenda kufyeka mahindi. Wamekwenda wamechimba mihogo kwenye mashamba ya watu, wamewagawia Magereza hivi hii inaingia akilini kweli?

Mheshimiwa Spika, kama Bunge tunaisimamia Serikali na kuishauri naomba Serikali isikilize na haya ndiyo mambo yanayoleta vita. Juzi, Mheshimiwa Nyalandu hapa alikuwa analalamika kwamba kuna askari wetu wameuawa na wananchi wenye hasira, ni mambo kama haya! Leo mkulima anategemea alime, auze yale mazao, ndiyo alipe ada ya shule, asomeshe watoto wake, wewe unaingia shambani unafyeka mahindi. Naomba Serikali kelele za Kagera Nkanda, Vijiji vya Mviza, Kagera Nkanda, Katoto, naomba mviangalie kwa makini ili vurugu hizi ziishe.

Mheshimiwa Spika, tatizo ni mipaka, mwananchi wa kule anakwenda kulima akijua analima kwenye eneo lake la kijiji, lakini kesho ukishafika wakati wa kuvuna askari wa hifadhi wakifika wanasema uko kwenye hifadhi. Sasa hii mipaka tunaimba miaka mitano, huu ni mwaka wa mwisho wa uchaguzi. Kwa sababu ninavyoongea hivi wananchi wangu kule wananisikiliza, wanasema mama umewasilisha, umetimiza majukumu yako, tumeona mchawi wetu ni nani. Sasa kama kuna watu walikuwa wanafikiria wakiacha tu wananchi wakilalamika, ndiyo wanamwondoa Buyogera madarakani wamechemsha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikumbushe tena wachimbaji wa madini ya chokaa Makele. Kamati imetoa ushauri wake kwa kweli ule ushauri ni mzuri naomba msome ushauri ule waliotoa Kamati mkitekeleza hayo mtatusaidia sana na mtawasaidia Watanzania. Ndiyo maana niliwahi kusema humu Bungeni yapo maeneo ambayo hatuna sababu ya kuwa maskini, lakini Serikali imekataa kwa makusudi, kutuwekea miundombinu ya kuweza kututengenezea maisha bora, ni kwa nini?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najazia hayo, sasa naomba nihamie kwenye Katiba na Sheria. Nitachangia kidogo kwa sababu najua muda karibia unakwisha. Nakubaliana kabisa kabisa na mapendekezo ya Kamati kwamba bajeti ya Mahakama mhakikishe inaongezwa na inakwenda kwa wakati kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ukiangalia Wilaya zilizo nyingi….

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante ya pili, ahsante mama. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Nyangwine, halafu Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia katika mjadala huu unaohusu Kamati hizi tatu. Kwanza nianze kumpongeza Mwenyekiti mpya wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Mheshimiwa Rweikiza na mimi ni mjumbe katika Kamati hiyo, naamini kwamba tutampatia ushirikiano wa kutosha ili kuhakikisha kwamba sheria ya katika nchi yetu zinafuatwa na tunashauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, nianze moja kwa moja na mfuko wa *TASAF*. Huu mpango wa kunusuru kaya maskini nashauri elimu itolewe ili hata Waheshimiwa Wabunge waweze kuelewa na naamini kwamba elimu ikitolewa itaweza kusaidia, si kusaidia tu zile kaya maskini tu, hata kuwezesha miundombinu ya barabara katika hizo kaya maskini na hali kadhalika nashauri kwamba ikiwezekana hizo kaya maskini ziboreshewe makazi, yaani zijengewe nyumba za maisha au nyumba za gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika,Kuna nchi kama Mexico, Malaysia na China kwa wale Wajumbe wa Kamati ambao tuliambatana nao kwenda Mexico na wale ambao tulikwenda nao China tulishuhudia jinsi ambavyo mpango kama huu wa *TASAF* ulivyosaidia hizo familia na mwisho wa siku hizi familia ziki-*graduate* kutoka kwenye umaskini zinaonekana zina kitu chochote ambacho kinaonekana. Siyo kwamba tufanye miaka kumi au miaka mingapi, baadaye tunaacha hizi familia katika umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, naomba niongelee Tume ya Mipango. Kwanza nitoe pongezi kwamba Tume ya Mipango imejitahidi kupanga Mipango, lakini mpango mingine ambayo wakati fulani inatekelezeka na wakati fulani haitekelezeki. Napenda kushauri kwamba, Tume ya Mipango ihusishe Kilimo na Mifugo pamoja na Ardhi katika mpango wa Matokeo Makubwa Sasa.

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia wananchi wetu kutondokana na umaskini, bila kufanya hivyo, itafika mwaka 2025 bado tutakuwa katika lindi la umaskini na ule mpango

wa kufikia uchumi wa kati kama ilivyopendekezwa katika Mpango wa Maendeleo itakuwa bado ni ndoto. Kwa hiyo, nashauri kwa sababu hizi sekta mbili, kilimo na mifugo na ardhi zinahusu Watanzania wote tena karibu asilimia 80, nishauri kwamba ziingizwe katika mpango wa Matokeo Makubwa Sasa.

Mheshimiwa Spika, vile vile napendekeza MKURABITA wajitahidi sana kupima ardhi ya wanavijiji hasa katika Halmashauri zetu. Watoe hati za kimila ili hiyo ardhi itumike kama dhamana ya kuwezesha Watanzania kujivunia kitu ambacho watakuwanacho cha thamani ambayo ni ardhi.

Mheshimiwa Spika, nikumbushe kuhusu Mfuko wa Bunge. Ni aibu mpaka sasa hivi tunamaliza miaka mitano hatujajengewa Ofisi za Bunge katika Majimbo yetu, Majimbo yetu hayana Ofisi. Utakuta Waheshimiwa Wabunge tunafanya kazi mazingira magumu, lazima twende kuomba kwa Mkuu wa Wilaya ndiyo tupewe Ofisi. Nashauri kwamba ili kurudisha heshima ya Ubunge, ni vizuri Wabunge wajengewe Ofisi katika Majimbo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Hii Ofisi tangu tulipoingia katika Kamati hii tumetoa ushauri mkubwa sana kwamba, ikiwezekana hii Ofisi iwezeshwe na si kwamba iwezeshwe tu, zinunuliwe mashine za kisasa ili kuweza kuchapa nakala muhimu za Serikali na ambazo ni za siri. Hii itasaidia sana kudhibiti siri ambazo siyo muhimu sana zisambae mtaani. Ni aibu kwa Serikali kutumia nakala muhimu sana za Serikali, nakala za siri kwenda kuchapiwa mtaani Kariakoo. Nauliza kwamba, kununua *machine* moja ya rangi nne kwa Serikali tunashindwa nini ili kumwezesha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali aweze kufanya kazi yake kwa ufanisi?

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile naomba niungane na Mheshimiwa Ntunkamazina kuhusu kuhamia Dodoma. Kamati imefanya ziara na kuangalia hali halisi, ustawishaji wa Makao Makuu ya Dodoma, sasa hivi yapata miaka 42. Nashauri sana hii ni ndoto, kuhamia Dodoma ni ndoto kubwa

sana na jambo ambalo kwa kweli kutekelezeka ni ngumu sana. Kamati imeshauri kwamba, utashi wa kisiasa hasa wa viongozi unahitajika.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa tumeshauri kwa muda mrefu, mimi napendekeza na kwa kuwa Serikali inaendelea kutumia gharama kubwa, kujenga majengo makubwa, tena ya gharama kubwa katika Mji wa Dar es Salaam, nashauri tuachane na ndoto hizi za kuhamia Dodoma tubaki Dar es salaam tutangaze huu Mji wa Dodoma kama Kanda Maalum ya Vyuo Vikuu, hii itawezekana kabisa. Vile vile inawezekana ikawa Makao Mkuu ya Bunge, lakini Dodoma tutangaze kama ni Kanda Maalum ya Elimu ya Vyuo. Hilo nafikiri linawezekana kwa sababu tutatumia gharama kubwa sana kuendesha Serikali Dar es Salaam na Dodoma, lakini litakuwa ni jambo rahisi sana wakati Wabunge tutakapokuwa tunafanya Bunge mambo mengine yote yanafanyikia Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala kubwa la rushwa hasa katika Halmashauri zetu hasa katika Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya hasa katika Polisi na mengine kama suala la *Escrow* ambalo Mheshimiwa Ntukamazina amejadili hapa.

Mheshimiwa Spika, nianze na *Escrow*, kuna baadhi ya vyombo vya habari kama magazeti kama hili bado linataja. Kwa mfano, ukisoma gazeti hili linasema "Mgombea Urais achota bilioni moja *point* tatu za *Escrow*, Waziri Mwandamizi ajichotea bilioni mbili *point* sita". Nashauri kwamba TAKUKURU ifanye uchunguzi ili kuwabaini watu hawa ili wachukuliwe hatua. Itakuwa ni busara zaidi, kama wengine wamewajibishwa halafu wengine tunawaachia, kwa kweli hata Kamati yetu ambayo ni ya Katiba inayosimamia sheria ikiachia mambo kama hayo yanafanyika halafu vile vile hatuishauri Serikali, tutakuwa hatutendei haki nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Mahakama zetu hasa Mahakama za Mwanzo zimekithiri sana kwa rushwa na kwa kweli

Waheshimiwa Wabunge mnafahamu, Mahakimu katika Mahakama zetu za Mwanzo ni Miungu watu kule vijijini, wanawanyanyasa watu wetu, wanawanyanyasa wapiga kura wetu. Napendekeza kwamba, kwa kuwa Serikali imesikia na imeongeza hela katika Mfuko wa Mahakama, napendekeza kwamba, tuajiri Mahakimu wa kutosha ambao watakidhi haja za huko vijijini, lakini vile vile wale Mahakimu ambao wanapokea rushwa wachukuliwe hatua kali hata ikiwezekana wafukuzwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuongelea upungufu wa watumishi katika Halmashauri zetu. Tunajua kabisa kwamba, Halmashauri zetu ndizo ambazo zinapeleka mipango mingi ya maendeleo, lakini utakuta kabisa kwamba Halmashauri zetu hizi zina upungufu mkubwa wa watumishi. Nirejee katika Halmashauri zangu mbili, Halmashauri ya Wilaya ya Tarime na Halmashauri ya Mji wa Tarime. Halmashauri hizi zote mbili hazina Afisa Ardhi hata mmoja, ni aibu kwa sababu ukiangalia katika Halmashauri zetu hizi za Tanzania, Halmashauri ya Wilaya ya Tarime inaongoza kwa kulipa hela nyingi sana katika ardhi.

Mheshimiwa Spika, sasa inawezekana kabisa kwamba kukosekana kwa mtaalam wa ardhi hasa mtu anayehusika na mambo ya upimaji wa ardhi ni tatizo kubwa sana. Hili jambo linapelekea migogoro ya kila mara isiyokwisha kati ya wananchi wa Tarime na wananchi hata wa jirani wa Rorya na vile vile kati ya Kata na Kata au Kaya na Kaya. Napendekeza kwamba, kuanzia sasa hivi, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI achukue suala hili alifanyie kazi, nilishakwenda mpaka Ofisini kwake nikamweleza kuhusu tatizo hili tangu mwaka jana mpaka sasa hivi naona utekelezaji unasuasua. Kwa hiyo, naomba kusema kwamba nahitaji watumishi wa ardhi katika Halmashauri zangu zote mbili, Halmashauri ya Mji na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza kabisa kwamba, mipango mingi tunayoipanga kama hatutasimamia katika Halmashauri zetu, tutakuwa tunafanya kazi bure. Ni vizuri zaidi mipango ya maendeleo ifanyike kwa ufanisi, lakini vilevile

Wakuu wa Idara wengi katika Halmashauri zetu wanakaimu. Ni vizuri zaidi tuangalie namna gani na sasa hivi tuna vijana wengi waliosoma tuweze kuwaajiri katika Halmashauri zetu na tuwadhibiti na vile vile tukomeshe rushwa katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la UKIMWI na madawa ya kulevya kwa vijana. Naishauri Serikali ifanye jambo kubwa moja, tutunge sheria kali kuhusu madawa ya kulevya. Naamini kabisa kwamba, kizazi hiki kinaangamia kwa sababu ya tamaa za watu wachache ambao wanatumia vijana na vijana bila kujua la kufanya, wenyewe wanateseka wanakamatwa. Ukienda katika nchi kama China, ukienda Hong Kong ni aibu. Naamini Serikali itayafanyia kazi hayo…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Magdalena Sakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Maria Hewa na Mheshimiwa Said Mtanda na Mheshimiwa John Mnyika wajiandae!

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu na kwa dhati kabisa nipongeze taarifa zote tatu ambazo zimewasilishwa kwetu leo kwa ufasaha mkubwa. Ni kwa sababu ya muda tu lakini tungepata muda wa kutosha, tungeweza kuzichambua vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, nitajikita sana moja kwa moja kwenye taarifa zilizoko mbele yetu, nataka nianze na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia Kitabu cha Kamati ya Tawala za Mikoa kwenye ukurasa wa 16, nianze suala la hali ya makusanyo katika Halmashauri na Manispaa zetu. Kamati imeeleza vizuri sana kabisa. Kumekuwepo na tatizo

kubwa la makusanyo ndani ya Halmashauri na kila siku katika bajeti tunazungumza na leo nimekwenda kusoma taarifa ya Kamati hii ya mwaka jana. Yale yaliyoandikwa mwaka jana ya ushauri wa Kamati ndiyo hayo hayo yameandikwa mwaka huu na hakuna kilichofanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunalalamika hatuna fedha za miradi, lakini Kamati imekuwa inashauri na inaainisha kwenye taarifa yake, kuna upungufu mkubwa kwenye kukusanya mapato ya Halmashauri zetu kutokana na kukosekana kwa ufanisi, mikakati ya ukusanyaji mapato yatokanayo na vyanzo vilivyopo, tabia sugu ya udanganyifu katika makusanyo yanayopatikana, makisio ya chini ya bajeti, Halmashauri kutokuwa na *set* kamili ya sheria ndogondogo ya kukusanya vyanzo vya mapato, kuna masuala ya kuwa na vitabu bandia vya makusanyo.

Mheshimiwa Spika, ninachoshangaa, tunaposomewa taarifa hizi hapa Bungeni zinakuja kwa ajili ya kutufurahisha au tayari zikishasomwa ndani ya Bunge Serikali inaagizwa ikatekeleze. Haiwezekani kuendelea kulia kila siku miradi haitekelezwi kwa sababu hakuna pesa wakati vyanzo vipo tunashindwa kukusanya na kila siku taarifa zinakuja ni zile zile. Kuna udhaifu mkubwa sana kwenye kukusanya mapato. Vyanzo vya mapato ni vile vile, tunashauri vyanzo vibuniwe vipya, vyanzo ni vile vile, ubadhirifu ni ule ule, udanganyifu ni ule ule, wizi ni ule ule. Tutaendelea kulalamikia hapa Bungeni kwa miaka mingapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana, Kamati nimeangalia taarifa yake ya mwaka jana na ya mwaka huu pia wamesema, kwa miaka miwili mfululizo waliishauri TAMISEMI kuweka mikakati madhubuti ya kukusanya mapato ya majengo yaani *property tax* katika Miji, Manispaa, Majiji, halijafanyika mpaka leo. Sasa nashindwa kuelewa, tumekaa tunategemea wahisani, vyanzo vyetu vya ndani hatuwezi kukusanya, hii ni hatari kubwa.

Mheshimiwa Spika, lazima leo Bunge lako tutoe mapendekezo ya kuhakikisha vyanzo tulivyonavyo kwanza

viainishwe, TAMISEMI hawajaweza kuanisha vyanzo vya mapato vilivyoko kwenye Halmashauri zetu. Vingine vipo tu, ni ubadhirifu unaendelea, havijaainishwa, kwa hiyo, vianishwe, ifanywe tathmini, vikusanye mapato vizuri. Tuna uwezo wa kuwa na mapato ya ndani mazuri kabisa ya kutosha kuendesha miradi yetu, tatizo ni udhaifu wetu wa kukusanya.

Mheshimiwa Spika, kwenye utekelezaji wa miradi. Miradi mingi haitekelezwi, kiukweli tunatoka kwenye Halmashauri zetu tunaona. Ndiyo maana hata ukiangalia vitabu vyetu vya bajeti, ukiangalia ni *copy and paste*, miradi ya mwaka jana na mwaka juzi ndiyo hiyo hiyo ambayo inawekwa mwaka huu. Unakuta kitabu kikubwa kwa sababu miradi ile ile inaendelea kusogezwa mbele kwa sababu haitekelezwi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeeleza, zipo sababu mbalimbali za kutotekelezwa kwa miradi; kwanza fedha kuchelewa kutolewa au kutokutolewa kabisa. Serikali tumepanga mradi, Bunge limetenga fedha, haiendi kabisa au inakwenda kidogo. Leo ukizunguka kwenye Halmashauri zetu, leo karibu tunaingia kwenye *quarter* ya tatu, hivi sasa tunaingia *quarter* ya nne kumalizia miradi, wengine hata *quarter* ya kwanza hawajapata hata *single coin* unategemea kitu gani. Haya ni matatizo makubwa, ni shida kubwa, miradi yetu haitekelezwi kwa sababu Serikali dhaifu kutoa fedha, haitoi kabisa au inatoa kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine uzembe wa watendaji wa Halmashauri kufuatilia tathimni na ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji wa miradi. Kweli nao ni udhaifu mkubwa, unakuta miradi iko kwenye Halmashauri mpaka Kamati ya Bunge inakwenda kugundua kuna udhaifu, watendaji wako pale, hakuna anayefuatilia miradi iliyopo kule kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, tuna udhaifu mkubwa sana wa Watendaji wetu na ufuatiliaji hakuna na tunaendelea

kuwalea hao hao. Wasomi wakubwa wenye uwezo mzuri wako mitaani, hawana ajira, tunalea uzembe kwenye Halmashauri kwa sababu watu hawawezi kufanya kazi, hakuna ku-*deliver,* tunawakumbatia wakati watu wenye uwezo wa kufanya kazi wako mitaani na wamesoma vizuri na hawana mahali pa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana leo Bunge lako ni lazima tuhakikishe tunaiagiza TAMISEMI wawajibike kikamilifu kuhakikisha kwamba miradi ikishapangwa inatekelezwa kwa wakati. Tuna hasara kubwa kama Taifa, tunapopeleka mradi wa mwaka mmoja, miaka miwili, miaka mitatu, minne mitano fedha ile inaongezeka mara mbili mara tatu, mpaka na wale wasimamizi waelekezi tunawalipa mara mbili mara tatu, hiyo ni hasara kwa Taifa, Serikali haioni hilo!

Mheshimiwa Spika, suala lingine, ni miradi kutokuwa na ubora stahiki, nalo ni tatizo sugu. Unakuta mradi ni dhaifu, leo tunashuhudia barabara zinajengwa, haijakamilika huku nyuma ni mashimo, ajabu kabisa kabisa. Juzi tumekwenda Bunda kutembelea mradi wa maji, Kamati yetu ya Maji, tumekuta mradi ume-*cost* mabilioni ya hela, umezinduliwa mwaka jana mwezi wa Tatu mpaka leo maji hayajawahi kutoka, wananchi wanateseka, fedha imetumika *tank* lililotengenezwa maji yakiingia yanavuja, hakuna anayechukua hatua, hiyo ndiyo Serikali, hili ni tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna zabuni, zabuni zinatolewa kwa undugu, kwa uswahiba kwa urafiki, *ten percent,* tunawapa watu wasiokuwa na uwezo zabuni za miradi mikubwa, hili ni tatizo kubwa. Naomba Bunge lako Tukufu lihakikishe kwamba, angalau kwa miradi mikubwa kuwepo na vigezo kamili jinsi gani ya kutoa zabuni kwa sababu tukiachia tu Halmashauri tunaona kwamba kwa kiasi kikubwa wameshindwa.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye sheria. Nitazungumza suala ambalo limezungumzwa na wenzangu. TAKUKURU, tunacho chombo cha kusimamia rushwa ndani

ya nchi hii. Kwa miaka yote TAKUKURU inalia kwamba ipewe meno haipewi meno. Ukiangalia taarifa ya Kamati hapa, TAKUKURU makosa makubwa yote ni lazima wakaombe kibali kwa *DPP, DPP* ni hisani yake aamue uchunguzwe au usichunguzwe, apelekwe Mahakamani au asipelekwe. Leo tunaona kwenye Kamati ya Bunge inasema hapa kwamba:

"Aidha katika kipindi cha kuanzia Julai, 2014 mpaka Januari mwaka huu, majalada yaliyochunguzwa ni elfu tatu na kumi na nne ya rushwa, kati ya hayo TAKUKURU imefungua kesi 108 Mahakamani, mengine elfu tatu mia tano na ngapi hayajafunguliwa."

Mheshimiwa Spika, naomba sana, hatuwezi kuondoa rushwa na hii inatupa dhamira ya dhati kwamba, Serikali haina nia ya dhati ya kuondoa rushwa Tanzania. Ndiyo maana ukikuta waliofungwa Mahakamani kule ni wale dagaa wadogo wadogo tu, wale wakubwa wanatamba mitaani wala hawana shida. Leo watu wa *Escrow* wanatamba mitaani hawana shida, kaangalie aliyeiba kuku, aliyeiba elfu kumi anasota *lockup*, hili ni tatizo. Kwa nini Serikali haitaki kuja na sheria hapa, tubadilishe sheria ya kuanzisha TAKUKURU, tuipe meno iwe na uwezo wa kukamata, kuchunguza na kushtaki, kwa nini? kuna kigugumizi cha nini?

Mheshimiwa Spika, tunaomba leo Bunge hili litoe agizo kwa Serikali sheria ije hapa, hatuwezi kuendekeza rushwa. Najiuliza swali Serikali ilishawahi kufanya tathimni kuona namna gani rushwa inaharibu Taifa hili? Ilishawahi kufanya tathimini? Nina wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, ajali nyingi ndani ya nchi hii zinasababisha rushwa barabarani, watu wanapoteza maisha hospitalini kwa sababu ya rushwa. Leo rushwa inaingia Mahakamani, chombo cha kutoa haki pekee, rushwa imeingia, usipokuwa na hela utafungwa tu, mwenye hela hafungwi. Kila huduma ndani ya nchi hii ni rushwa, rushwa

imeoza, nchi imeoza, imenuka, rushwa ni kila mahali, lakini tunasema tunashughulikia rushwa kwa utaratibu gani? Kwa utaratibu wa kukamata dagaa au perege? Kambale wanacheza...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, naomba sana...

SPIKA: Tunaendelea, ahsante. Mheshimiwa Maria Hewa atafuatiwa na Mheshimiwa Said Mtannda na Mheshimiwa John Mnyika ajiandae!

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru umenipa nafasi hii ili niweze kuzungumza kidogo kutokana na uwasilishaji wa Kamati hizi tatu. Zote nazipongeza wamejitahidi na nadhani zitakuwa na maoni mazuri katika dakika ya mwisho, hongereni tu sana.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia kwangu nitajikita zaidi katika Kamati mbili; UKIMWI pamoja na suala zima la TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, nipende kuanza au na-*declare* tu kwamba, Kamati yangu ni ya UKIMWI na Madawa ya Kulevya.

Mheshimiwa Spika, siwatishi, lakini natamka ndani ya Bunge kwamba, UKIMWI, UKIMWI, narudia mara ya tatu UKIMWI upo na hauna dawa.

Mheshimiwa Spika, kwa vile nimetamka hivyo, nipende kuwaambia, kwamba ni afadhali wakati ndiyo janga la UKIMWI linangia nchini mwetu, watu tukastuka na tukajitahidi kujilinda na kuambukizwa na maambukizi haya ya UKIMWI, lakini hata hivyo, haikufanikiwa, binadamu wameambukizwa UKIMWI, lakini tumekwenda katika maisha

hayo, baadaye kumejitokeza madawa mbalimbali, kama vile *ARV*, watu wanazitumia dawa hizo na wakadhani sasa wamepata kitu cha kuwatia moyo kwamba, pamoja na kwamba ninao, nitaishi miaka kadhaa.

Mheshimiwa Spika, binadamu wameendelea kuishi katika mfumo huo, lakini wameishi katika mfumo wategemezi. Kwa maana ya wafadhili ndiyo wametuwezesha sisi kuwa na angalau na ahueni ya kusema hivyo kwamba, pamoja na kwamba UKIMWI upo, lakini wapo wafadhili, wanaoweza wakatu-*supply* madawa mbalimbali.

Ndugu zangu na Watanzania kabisa natamka, wafadhili wameanza kujitoa na wamejitoa. Sasa, aliyenao kapimwa na aliyenao, dawa hivi wafadhili kama wamejitoa, tunafanya nini na unajijua unao na ni afadhali ambaye hana, kwa kupima, maana yake wengine tunajifarijifariji tu, unajiona unenenene kidogo wala huugui ugui ovyo ovyo, kumbe ni mshindiliaji mzuri wa lishe, ukadhani huna.

Mheshimiwa Spika, kama yupo ambaye kapima, na anajiona kwamba yeye hana, kweli kwa kupitia vipimo na atulie. Kwa sababu wafadhili wamejitoa, *it means* hata hizo dawa za *ARV* hakuna sasa. Hata *NGOs* hizi ambazo zilikuwa ndizo wana mawasiliano na wafadhili hawa na zenyewe zitakufa, mwelewe hilo. Ninakoelekea katika mazungumzo yangu hata watu wa *TACAIDS*, hawana, watashika wapi, tutawalaumu bure, lakini ndiyo hivyo, walikuwa ndiyo kiungo kikubwa katika kutuweka sisi salama na wenyewe hawana.

Mheshimiwa Spika, Serikali, ndani ya Wizara ya Fedha, mwaka 2014/2015, walisema bilioni sita zitatoka, wakawatengea wafadhili hizi na sisi wakatutengea kama mapato yetu ya ndani, zitatoka mbili, na hizo mbili nazo ni za wafadhili, sisi sifuri, lakini wagonjwa ndiyo sisi, tunafanya nini!

Ndugu zangu, Mwenyekiti wangu wakati anasoma pale, amehimiza suala la kuanzishwa kwa Mfuko, naomba tusilipuuze hili! Watanzania sasa hakuna dawa za kutoka kwenye mifuko ya Wafadhili. *(Makofi)*

Naomba tulibebe kwa mikono miwili kabisa, hakuna kaya ambayo haijaguswa na tatizo hili, haipo. Naomba tuwe *serious* katika suala hili, mimi nimo ndani ya Kamati hiyo, hatari, hatari yaja, tena afadhali wakati UKIMWI unaingia, sasa tunao na hauna matibabu na huna hata ile bembeleza sasa ya *ARV*, tunafanya nini! Naomba mpokee wazo la kuanzisha mfuko Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Niwaombe kabisa, hata *NGOs* hizi zinakufa, nairudia hiyo. Nilikuwa napenda nilisisitize hilo ili tulione umuhimu na inawezekana hata na sisi tukianzisha, labda baadaye wanaweza wakafikiria jinsi gani wanaweza tena kutu-*support* kwa wale wenye nia njema, lakini hakuna sasa *support*, aliye na mgonjwa huko na Watanzania wananisikia, hapo ndipo. Kama hatutakuwa na elimu ya kuambizana kutulia, ni hapo sasa. Afadhali na akinamama Hewa sisi tumeshakua sasa, nakutulia, mlio vijana ni hapo sasa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kulihimiza hilo, napenda niongelee kidogo tu kwa ufupi kuhusu taarifa nyingine ya pili kama nilivyoisema. Mimi sitetei uhalifu katika ndani ya Halmashauri zetu. Mwenzangu Wenje pale nimemsikia amefoka sana kuhusu suala zima la Halmashauri yetu ya Mwanza. Imesemwa, kwa kweli imesemwa, wala hata simpingi, imesemwa.

Sasa katika hili, mimi ambacho kinanichanganya tu, hivi…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, ni ya kwanza.

SPIKA: Ya pili. Ahsante ya pili. Mheshimiwa Said Mtanda.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, ya pili, hapana, hapo umenidhulumu. *(Kicheko)*

SPIKA: Naomba tuendelee, Mheshimiwa Saidi Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Mnyika!

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa, uzima na uhai ili niweze kuzungumza machache kuhusiana na ripoti ya Kamati ya TAMISEMI na ripoti ya Kamati ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili niweze kupitia taarifa hizi ambazo zimewasilishwa na Wenyeviti wenzangu. Niwapongeze pia Dkt. Hamis Kigwangala, Mwenyekiti wa Kamati hii kwa kazi kubwa waliyoifanya. Pia nimpongeze pacha, dada yangu, mama yangu Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o, Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI kwa kazi kubwa na yeye ni mdau mkubwa kwa kweli wa masuala haya ya UKIMWI, nampongeza sana, anafanya kazi kubwa na nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa taarifa hii ya TAMISEMI. Kwanza nianze kwa kuonesha masikitiko yangu makubwa sana hasa kutokana na uchache wa fedha za Mfuko wa Barabara kwenye Halmashauri zetu. Fedha za Mfuko wa Barabara *(Roads Fund)* imekuwa ni tatizo kubwa na wananchi wa maeneo ya vijijini, barabara za vijijini ndizo barabara zinazotegemewa kwa ajili ya ukombozi wao kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014/2015, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi Vijijini, ilipangiwa fedha shilingi bilioni moja, milioni mia moja sitini na nane, lakini hadi leo tunapozungumza awamu ya kwanza na Mheshimiwa Waziri amenipa barua hii, halmashauri yangu imepokea shilingi milioni hamsini na tano, kwenye bilioni moja, milioni mia moja sitini na nane, halmashauri hadi leo imepokea shilingi milioni hamsini na tano.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa daraja la Mchinga peke yake, unagharimu shilingi milioni 380, mkandarasi amesimama kazi, hawezi kuendelea kwa sababu *certificates* zake nyingi hajalipwa, hali hii ni mbaya sana. Daraja lile la Mchinga litawanufaisha wananchi wa Tarafa nzima ya Mchinga, kutoka Mchinga hadi Kijiweni. Sasa Serikali ituambie ni lini sasa fedha hizo shilingi bilioni moja, zitapelwa ili kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa hii ya kamati ya TAMISEMI kwa kweli imenivutia sana, imenivutia kwa kuwa halmashauri yangu, baada ya kupata hii milioni hamsini na tano, tunajiuliza sasa, tunazipeleka kwenye ujenzi wa barabara gani! Mkandarasi anayedai shilingi milioni 300, unampaje shilingi milioni kumi? Pia barabara ile inayokwenda mpaka Nangaru, sasa hivi imefungwa na wananchi hawawezi kwenda kupata mahitaji yao Lindi. Tuliomba fedha shilingi milioni mia moja hamsini, milioni mia moja hamsini kwa barabara moja tu, tumepata fedha shilingi milioni hamsini na tano kwenye bilioni moja, mnataka kuwaambia nini wananchi wa pale.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Nangaru sasa wanalazimika kwenda wenyewe kuokota mawe ili kutengeneza barabara, mlipowafikisha ni pagumu na hatuwezi kuendelea na mtindo wa namna hii, kama hamna uwezo kwa nini mlibajeti! Wenzetu Waganda wakibajeti, kama wana milioni mia moja, wanabajeti hiyo hiyo wanakubaliana matumizi ya shilingi milioni mia moja. Kwa nini sisi tunawahadaa wananchi kwa kuwaeleza mambo yasiyotekelzeka?

Mheshimiwa Spika, hali hii haikubaliki na Serikali iende pale ikaone namna sasa hivi wananchi walivyo, kwenye misitu kutafuta mawe, ili barabara ya kwenda Nangaru, urefu wa kilimita 35 ipitike. Sasa Mbunge anaweka fedha ya Mfuko wa Mbunge milioni kumi, lakini barabara hiyo ni kukarabati baadhi ya maeneo, lakini barabara ile inahitaji shilingi milioni mia moja hamsini.

Mheshimiwa Spika, sasa hali hii ni mbaya na wakati huo huo, unamwambia mwananchi achangie mchango wa maabara, mnamchangisha shilingi elfu mbilimbili, nimesema wananchi wa pale hakuna kufanya hilo, kwanza Serikali ituangalie imalize tatizo lile kwa sababu huwezi kumchangisha mwananchi wakati huo huo anaokota mawe mwenyewe kwenye msitu, kuweza kukarabati barabara yake, utaratibu wa nchi gani huo! Haukubariki kabisa.

Mheshimiwa Spika, hilo la kwanza, lakini la pili, imeelezwa kwenye ripoti ya UKIMWI, ukatili wa kijinsia dhidi ya wananwake, ni suala ambalo ni kubwa sana na ukatili wa kijinsia siyo tu kuwapiga wanawake, hata kitendo cha kuwafanya wanawake waende kilomita 20 kutafuta maji, ni ukatili wa kijinsia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wanawake wa Mnang'ole, wanawake wa Dimba, wanafanyiwa ukatili wa kijinsia kwa sababu wanaamka usiku kwenda kutafuta maji kwenye mashimo, haiwezekani! Tumefanya juhusi kubwa sana, asilimia 85 ya tatizo la maji tumelimaliza, kwa kutumia juhudi zetu binafsi wenyewe, Mbunge kwa kutumia wafadhili wake, lakini iko haja ya Serikali kumaliza jambo hili.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Maji aliahidi kwenda pale, alipata msiba, ndugu yangu Amos Makala, nampa pole sana, lakini sasa kipindi cha maombolezo kimekwisha sasa turudi kazini, maana hata mimi nilipata msiba wa baba yangu, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kunifariji, mliniunga mkono, lakini nimerudi kazini ili kuendelea kuwatumikia wananchi wa Jimbo langu. Kwa hiyo, namwomba pia Mheshimiwa Makala kufanya ziara, Waziri wa TAMISEMI, kupita katika maeneo yale ya Mnang'ole, ya Dimba, Kilolambwani ili kuona tatizo la maji na kupatia ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Halmashauri zetu hazitenge asilimia tano kwa ajili ya akinamama, kwa ajili ya kuwakopesha ili wasiingie kwenye vitendo viovu

vitakavyowapelekea maambukizo ya UKIMWI, huo pia ni unyanyasaji wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, akinamama wa maeneo ya vijijini wananyanyaswa kijinsia kwa sababu haki yao ya asilimia tano na Serikali ipo, kwa nini haisimamii Halmashauri zetu kuweza kutenga asilimia tano. Ili vijana vijini waweze kupata mikopo ya gharama nafuu waweze kuendesha maisha yao kupitia kilimo kwa sababu ardhi ndiyo mkombozi wa wananchi wa kijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ripoti hii ukurasa wa 34 imeeleza mgogoro baina ya Halmashauri na Manispaa ya Lindi na wakazi wa eneo la Mmongo. Mgogoro huu ni wa muda mrefu, Kamati ya Bunge ya Kigwangalla imekwenda pale, tunachotaka sasa maamuzi ya Serikali yapi ili wananchi waweze kufahamu, hatua zilizochukuliwa ni zipi. Kama mgogoro umemalizwa kwa nini Serikali haitangazi bayana, kwamba mgogoro ule umekwisha na wananchi wale wanapata haki zao kama ilivyopendekezwa kwenye kamati ya Dkt. Kigwangalla.

Mheshimiwa Spika, nia yangu ni kutaka kuona Serikali inamaliza migogoro hii kwa wakati badala ya kuilea. Migogoro kila mahali, leo ukiamka *ESCROW*, kesho ukiamka *EPA*, kesho ukiamka hivi, kesho ukiamuka *UTT*, sijui *UTTI*, itakuwa nchi gani kila siku migogoro! Kwa hiyo, tunaomba TAMISEMI wamalize tatizo hili ili majibu sahihi na kwa wakati yapatikane kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Kitomanga, ilikuwa ni kitu cha afya, tumesema sasa Serikali imekubali na mimi Mbunge nawapongeza Serikali kwa kukubali kwamba kituo cha afya Kitomanga kipandishwe hadhi na kuwa hospitali ya Wilaya. Mkandarasi yuko pale, majengo yanaendelea kujengwa, korido zinajengwa, tumepeleka juzi akinamama pale kuangaliwa kansa ya matiti, kwa kazi kubwa tuliyoifanya, lakini sasa iko haja ya Serikali kutoa fedha ili kituo kile cha afya kijengwe katika hadhi ya hospitali kama tulivyokubaliana.

Juzi nimepita eneo la *site* hiyo hospitali ya Kitomanga na makazi yangu yako Kitomanga, nimeona mkandarasi amesimama kwa zaidi ya miezi mitatu, kwa sababu hajalipwa fedha. Kwa hiyo, kila unakopita, miradi yote imesimama.

Mheshimiwa Spika, lakini…

SPIKA: Aaa, ya kwanza vipi, wewe umesema sana, Mheshimiwa John Mnyika!

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Afadhali unishukuru tu. *(Kicheko)*

Nina tatizo la muda, msinione hivi.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nitaomba nianze kuchangia kwa taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, katika ukurasa wa 16, inahusu utendaji wa TAKUKURU, Kamati inasema, gharama nyingi za Serikali zimekuwa zikitumika katika kufanya uchunguzi wa tuhuma za rushwa, lakini majalada yanapowasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini, mengi yao hayatolewi vibali na kuachwa kwa kigezo cha kutokuwa na ushahidi wa kutosha, jambo linaloisababishia hasara Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo ya Kamati, pendekezo kubwa lililotolewa ni kwamba TAKUKURU sasa ipewe mamlaka ya kuweza si tu kuchunguza, bali pia kushtaki ikiwemo masuala yanayohusu rushwa kubwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono pendekezo hili la marekebisho ya sheria katika hatua ya baadaye, ningependa kupata maelezo ya Serikali, simwoni hapa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mpya, wala simwoni hapa Waziri wa Katiba na Sheria, lakini naamini Serikali ipo, wapo watakaosema kwa niaba yao. Naibu Waziri yupo, Serikali ipo na Kamati ipo.

Mheshimiwa Spika, kwanza Kamati itueleze, baada ya kupokea maelezo haya ya Serikali, kwamba TAKUKURU inachunguza, inabaini inaona kwamba yapo mashtaka a kupeleka Mahakamani ya ufisadi, lakini *DPP*, anasema hakuna ushahidi, mashtaka hayapelekwi Mahakamani, mashtaka hayo ya namna hiyo, ni mashtaka ambayo yanawahusu akina nani!

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, sababu hii imekuwa ikitolewa kila wakati, itakumbukwa kwenye kashfa ya *RADAR*, aliyekuwa akituhumiwa wakati huo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew Chenge, maelezo yaliyokuwa yakitolewa wakati huo, kwamba hakuna ushahidi, *DPP* hakuona sababu ya kupeleka Mahakamani. Matokeo yake watuhumiwa hawa wa kashfa za wakati huo, hawakupelekwa Mahakamani, wanaibuka leo kwenye kashfa zingine za namna hii!

Mheshimiwa Spika, tunapoletewa taarifa ya Kamati, ya ujumla ujumla, bila maelezo mahususi ni majalada yapi hasa hayo! Katika mazingira ya sasa ambapo kuna viongozi wa Serikali, wako Mahakamani kwa uzembe na kuisababishia hasara Serikali, kama akina Mramba, lakini viongozi wengine, ametoka Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliyepita Werema hapa, lakini inashangaza kwa nini mpaka leo hayuko Mahakamani kwa uzembe na kuisababishia hasara Serikali!

Mheshimiwa Spika, Kamati ikiendelea kutoa maelezo ya ujumla na Serikali isipotoa maelezo ya sababu za kina za kwa nini hasa TAKUKURU ikichunguza, majalada yakipelekwa kwa *DPP, DPP* anasema hakuna ushahidi na mambo yanaishia hapo. Jambo hili litaendelea hata baada ya kubadili sheria, kuipa mamlaka TAKUKURU iweze kushtaki, bado TAKUKURU itasema kuna mamlaka nyingine ya nchi inayoikataza TAKUKURU kwenda Mahakamani. Jambo hili mtandao wa *WikiLeaks* ulimnukuu Hosea akisema kuna mambo ambayo yeye anaamini angeyapeleka Mahakamani, lakini Ofisi ya Rais inamzuia.

Mheshimiwa Spika, sasa kunapotolewa taarifa za namna hii, huku kukiwa na taarifa kama hizi, ni wazi kwamba tunahitaji maelezo, si tu ya Waziri wa Sheria, ya Mwanasheria Mkuu ambaye hayupo, yeyote ambaye anamwakilisha maelezo haya yatolewe ili marekebisho ya sheria yasitibu tatizo upande mmoja lakini bado tatizo likabaki, ambayo ni nia ya dhati, dhamira ya dhati ya wenye mamlaka kuanzia Ofisi ya Rais mpaka wengine wenye mamlaka ya kuhakikisha kwamba hawaweki kizuizi kwa vyombo vya utawala vinapotaka kuchukua hatua dhidi ya watuhumiwa wa rushwa hata kama watu hao ni sehemu ya Serikali hiyo hiyo ambayo Rais anaiongoza. Kwa hiyo, hii la kwanza, kwamba maelezo ya ziada yatolewe.

Mheshimiwa Spika, la pili, Kamati imeeleza kwenye ukurasa wa 24 kwamba kati ya mambo ambayo Kamati inajivunia kwenye mafanikio kwenye utekelezaji wa majukumu yake ni masuala yanayohusiana na mafanikio ya mchakato wa Katiba mpya, mafanikio ya mchakato wa Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii tunayoijadili taarifa yake leo inaisimamia Ofisi ya Rais, inaisimamia Ofisi ya Waziri Mkuu katika maeneo yanayohusiana na mchakato huu. Ningependa kupata maelezo kutoka kwa Waziri wa Sheria na Katiba, kutoka kwa Kamati, Mheshimiwa Rais alikutana na viongozi wakuu wa vyama vya siasa kupitia *TCD*, akapokea maelezo ambayo hayakutokana tu na vyama vya upinzani bali pia yalitokana na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilichowakilishwa na Mheshimiwa Mangula na Mheshimiwa Kinana, kwamba kuna udhaifu katika mchakato wa mabadiliko ya Katiba, kuna mambo yanahitaji kurekebishwa. Rais akafikia makubaliano na viongozi wakuu wa vyama kwamba, mchakato huu sasa, Kura ya Maoni itasogezwa mbele itafanyika baadaye.

Katika mazingira ya namna hiyo na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ulikuwa ufanyike Februari. Kama vile nchi ina Rais zaidi ya mmoja, Waziri Mkuu Pinda akajitokeza akatangaza Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uharibifu wake

umeonekana. Sasa tumefikia kwenye kitanzi kingine, tunasema mafanikio ya mchakato wa Katiba. Sheria ilitaka kabla ya kufikia kura ya maoni Daftari kudumu la Wapiga Kura liwe limeboreshwa, na Serikali ikatangaza kwamba uandikishaji utafinyika upya.

Mheshimiwa Spika, kinachoendelea hivi sasa, pamoja na majibu ya Waziri Mkuu aliyoyajibu wakati anamjibu Kiongozi wa Upinzani Alhamisi iliyopita, kuna kizungumkuti kikubwa juu ya zoezi zima la uandikishaji, ambayo ni hatua mama kabla ya kuelekea kwenye Kura ya Maoni. Ni kwa nini sasa, kufuatia kizungumkuti hiki, zoezi likiwa limekwama, Serikali hii kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo kimsingi pamoja na taasisi nyingine inasimamia Tume ya Uchaguzi ikiwa haijatoa fedha, maandalizi yakiwa hayakamilika, wadau hawajashirikishwa, bado tunaambiwa zoezi hili linakwenda vizuri.

Ni kwa nini katika majumuisho ya Taarifa hii ya Katiba na Sheria Serikali isikubaliane sasa na makubaliano ya Rais na vyama vya siasa kwamba Kura ya Maoni ya Katiba mpya isogezwe mbele mpaka baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ili kama taifa kwanza tujielekeze katika kazi ya msingi ya kuboresha daftari?

Mheshimiwa Spika, zinahitaji bilioni 290, hazijatolewa mpaka hivi sasa tunavyozungumza. Leo na jana Tume iko Kusini ikitangaza kama vile uandikishaji unakaribia kuanza, lakini ukweli ni kwamba ndani ya Tume yenyewe kwa taarifa za ndani, kazi hii bado iko hovyo hovyo kweli kweli. Ni kwa nini tusichukue hatua kama taifa kabla ya madhara katika hatua ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, ni wazi, tukilinusuru taifa juu ya majanga yanayokuja mbele, kwenye Kura ya Maoni, kwenye Uchaguzi Mkuu, tutajipa nafasi ya kutosha ya kushughulikia masuala mengine ya maendeleo yanayotajwa kwenye taarifa nyingine, iwe ni taarifa ya TAMISEMI inayozungumzia miradi ya *DART*, iwe ni miradi ya maji, iwe ni miradi mingine ya maendeleo, katika hali tuliyonayo sasa kama taifa, nchi

imekwamba, imenasa katika kitanzi cha uchaguzi, imenasa katika kitanzi cha Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyote vile, kama Rais alikuwa mkweli kwa viongozi wakuu wa vyama, kama Rais hakutoa kauli ya uongo kupitia *TCD,* Serikali katika majumuisho itakiri udhaifu uliojitokeza na kusogeza mbele mchakato huu ili hatua za msingi ziweze kuchukuliwa. Na zaidi, Serikali itatoa maelezo hapa Bungeni, ni lini hasa, kwa ratiba, eneo kwa eneo uandikishaji wa wapigakura kwenye taifa letu utafanyika ili tulinusuru taifa na hatari inayokuja…

SPIKA: Haya, ahsante. Waheshimiwa, kuna watu nilikuwa niwape nafasi ya kuchangia, lakini muda nilionao hauwezekani. Kwa hiyo, naanza kuwaita Waheshimiwa Mawaziri. Tutaanza na Waziri wa Nchi, Utawala Bora, Mheshimiwa Mkuchika. Mna dakika kumi kumi tu, kwa hiyo mkijipanga hovyo hamtapata, muda hautoshi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Mheshimwia Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchagia taarifa ya mwaka ya shughuli ya Kamati ya Kudumu ya Katiba Sheria na Utawala, na kidogo ile ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika maeneo yaliyogusiwa rushwa na maadili ya viongozi.

Nianze kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Rweikiza kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati yetu. Napenda sana kushukuru ushirikiano tunaoupata Ofisi ya Rais Ikulu na Kamati hii katika utendaji kazi wa kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba Sheria na Utawala imetoa ushauri wa aina mbili kuhusu taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa; Moja inasema, kuipa mamlaka kamili ya kufungua mashitaka na kuyaendesha Mahakamani bila kuomba kibali cha Mkurugenzi wa Mashitaka Nchini.

Maoni ya pili, Kamati inasema, kutokana na kuongezeka kwa matukio ya rushwa nchini, Kamati imeona muda muafaka kwa nchi yetu kuanzisha chombo kingine

kipya kitakachodhughulikia makosa madogo madogo ya rushwa na kuwaachia TAKUKURU kushughulikia rushwa kubwa zenye athari kubwa za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia mambo yote mawili kwa pamoja kwa kusema hivi; ni kweli ziko nchi ambazo taasisi inayopambana na rushwa inapeleleza na kushitaki. Kwa hiyo hili linalopendelekezwa na Kamati hapa sio jambo jipya, linalopendekezwa na Kamati hapa sio jambo jipya, na nataka nitoe mifano. Nchi kama Uingereza, *Senior Fraud Office* ikishapeleleza haiombi kibali kwa Mwendesha Mashitaka, Uganda, Sierra Leone, Ethiopia na nchi nyingine nyingi.

Mheshimiwa Spika, sasa wanaopinga utaratibu huu wa kupeleza na kushitaki wanasema wenyewe kwa Kiingereza wanataka *checks and balance*. Yaani kwamba yule anayepelekeza, anayeshitaki asiwe yeye ndiye mtoa hukumu. Sasa mimi naona hapa ni upotoshwaji, kinachopendekezwa hapa si kwamba TAKUKURU ashitaki na kuhukumu. TAKUKURU ashitaki, kwa mujibu wa taratibu za nchi yetu mtoa haki, anayetafsiri sheria za nchi hii ni chombo cha Mahakama. Kwa hiyo, TAKUKURU wakipewa madaraka hayo maana yake ni kwamba watapeleleza, watashitaki.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijatoa majibu yetu kwa upande wa Serikali, moja kati ya Maazimio ya Bunge kuhusu sakata la Akaunti ya *Escrow* liliitaka Serikali kuleta hapa Bungeni marekebisho ya sheria ili kuipa TAKUKURU nguvu zaidi katika utendaji wake.

Aidha kwa mujibu wa Katiba inayopendekezwa ya Octoba, 2014 imetaja mambo mawili; Moja, nanukuu; "kwa madhumuni ya kudhibiti rushwa, kutakuwa na chombo ambacho kitakuwa na jukumu la kuzuia na kupambana na rushwa.

Pili, Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti kuhusu muundo, majukumu na mamlaka kinachorejewa katika ibara moja hapo juu."

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria iliyoanzisha TAKUKURU ni sheria ndogo sio sheria mama ya nchi ikilinganishwa na Katiba ambayo ni sheria mama, ni ushauri wetu kuwa tusubiri maamuzi ya *referendum* juu ya Katiba inayopendekezwa, kwa kuwa huwezi kubadili sheria ndogo leo halafu kesho ikaja sheria kubwa ambayo ile sheria ndogo ikawa inafanya tofauti; katika mazingi hayo sheria ndogo haiwezi kufanya kazi, unaheshimu sheria mama.

Kwa hiyo, ushauri wetu ni kwamba jambo hili tumelipokea, tunapendekeza tusubiri maamuzi ya wananchi kuhusu Katiba Inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; Katika Taarifa ya Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imependekezwa kwamba Serikali kwa kutumia vyombo vya Ulinzi na Usalama, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na nyingine zifanye uchunguzi na kuwachukulia hatua Madiwani wanaofanya biashara ya Halmashauri bila kuweka wazi maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kifungu cha 6(a), kinachohusu mgongano wa maslahi; ni marufuku kwa Diwani au kiongozi yeyote kufanya biashara na taasisi anayoiongoza.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Madiwani na Wabunge wenzangu kuacha mara moja, kabisa, kufanya biashara na kuzungumzia masuala yanayotuhusu bila kuweka wazi maslahi yetu, vinginevyo tutawachukulia hatua kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kuzungumzia, nani ana jukumu la kufuta rushwa nchi hii. Ni makosa makubwa kabisa kudhani kwamba Rais peke yake au Waziri Mkuu au Waziri wa Utawala Bora anaweza akafuta rushwa katika nchi hii. Vita ya Rushwa ni ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mimi namuheshimu sana kaka yangu Mheshimiwa Ntukamazina, namuheshimu sana. Vile alivyosema kwamba namuheshimu ni kweli namuheshimu, mkubwa kwangu, wakati anafanya kazi, mimi nasoma, nimekula kodi yake.

Sasa, lakini amezungumza kwamba, hivi Waziri wa Utawala Bora nchi inanuka. Waziri wa Utawala Bora ofisi iko Dar es Salaam, rushwa inaliwa Ngara, jimboni kwa Mbunge, nani atakuwa wa kwanza kujua, Ntukamazina au Mkuchika aliyeko Dar es Salaam? *(Kicheko)*

Mimi nasema hivi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ina kazi tatu; kupambana, lakini kuna *element* ya kuelimisha. Sisi katika Wizara ya Utawala Bora, mwaka wa jana tumefanya kazi nzuri sana, tumefanya semina kwa *RCC* karibu zote za nchi hii na Mabaraza ya Madiwani karibu yote. Mwaka huu tumejikita katika Mabaraza ya Wafanyakazi katika Wizara, mashirika ya umma, madhehebu ya dini, *scout* mahali popote, vyama vya siasa, mkitualika sisi tutakuja kutoa mada.

Mimi naomba ieleweke kwamba tukifanikiwa kuwaelimisha Watanzania madhara ya rushwa na kila Mtanzania akashiriki vita ya rushwa, nchi yetu itakuwa mahali pazuri pa kuishi na masuala ya rushwa yatakuwa yamepungua.

Rushwa, mimi nimezaliwa nimeikuta. Kengele ya kwanza! Kaka yangu Mhesimiwa Ntukamazina yeye mkatoliki mzuri tu, kitabu cha Kutoka Sura ya 28, kilitungwa mimi sijazaliwa wala babu yangu hajazaliwa, mle inaelezwa rushwa inapofusha macho. Waliomua Bwana Yesu, rushwa, alikwenda akawauliza ni nini mtakachonipa nami nitamsaliti kwenu. Imeelezwa mle, wakampimia vipande 30 vya fedha, akaenda akamsaliti.

Sasa, mimi nakuomba ndugu yangu, kaka yangu Mheshimiwa Ntukamazina na Watanzania wote mnaonisikiliza, kuna watu wanaitwa *whistle blowers*. Sisi tupeni taarifa, ukitupa taarifa mahala kuna mchezo wa

rushwa, ukiona vyombo vimezembea, hapo simama hapa sema kwa nguvu zako zote.

Mheshimiwa Spika, sitaki nipigiwe kengele ya pili. Mimi nashukuru sana, sana sana. Nawaomba Wabunge wenzangu humu ndani mtuunge mkono katika Wizara hii ya Utawala Bora, tushirikiane kuwaelimisha Watanzania waichukie rushwa ili wasaidie kutoa taarifa katika vyombo vinavyopambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Nakushukuru kwa kunipa dakika moja. Sasa nitamwita Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Mwandosya.

WAZIRI WA NCH,I OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nianze kwa kukipongeza chama changu, Chama Cha Mapinduzi kwa kutimiza miaka 38.

Mheshimiwa Spika, naupongeza sana uongozi wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Ruvuma kwa kufanikisha sherehe zilizofana na zilizotia fora.

Nilikuwa namsikiliza hapa Mheshimiwa Gekul juzi au jana anasema CCM imechoka. Lakini kama aliangalia, au aangalie tena kanda ya yale yaliyotokea Songea juzi, basi ajue kwamba CCM bado inatisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijielekeze moja kwa moja kwenye mapendekezo ya Kamati, na hii ni Kamati ya Katiba Sheria na Utawala Bora. Nitaanza maeneo yanayohusu *TASAF* kwa haraka haraka.

Moja, ni kwamba pendekezo la kwanza niseme tu kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha za kutosha katika bajeti ili kutunisha mfuko na tutakapoleta mapendekezo hapa kwa kweli yatakuwa ni mapendekezo ya Bunge hili na tutaomba mtukubalie tunapopendekeza, kwa sababu tumekubaliana na wadau wa mfuko huo kwamba tunaanza

kutenga kuanzia mwaka 2014/2015 kila mwaka shilingi bilioni 45 kwa ajili ya mfuko wa *TASAF*, kwa hiyo wote tuungane katike kulifanikisha hili.

Kuhusu kupatikana kwa kiwanja kwa ajili ya Makao Makuu ya *TASAF*, ningependa kusema kwamba taratibu karibu zinakamilika ili kiwanja ambacho kilikuwa kiwanja cha Kampuni ya Saruji kiweze kupatikana kwa ajili ya *TASAF* na hapo ndipo ambapo mpaka sasa Makao Makuu ya *TASAF* yalipo, kwa hiyo hili tutalifanikisha.

Kuhusu elimu kwa wananchi kuhusu vigezo mbalimbali vinavyotumika katika kuelewa au kufahamu kaya ambazo ni masikini sana ili ziweze zikafaidika katika mpango wa sasa, awamu ya sasa ya *TASAF* ningependa tu kusema kwamba ni mchakato shirikishi. Eneo linapotambuliwa kwamba sasa tunakwenda kufanya kazi basi tunakuwa na mikutano ya hadhara, na baada ya hapo katika mikutano hiyo ndipo vigezo vya kaya masikini vinawekwa na jamii yenyewe. *TASAF* inachokifanya katika mchakato huo kwa kweli ni kuwa wawezeshaji katika mlolongo mzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hivi ni vigezo vya wananchi wenyewe, wanasema katika eneo letu sisi tunajua kwamba kwa vigezo hivi tunavyovifahamu sisi ndizo kaya masikini. Na kwa kutumia vigezo hivyo wanachagua kaya zenyewe wananchi wenyewe, baada ya hapo wanaorodhesha. Wakishaorodhesha sasa kunakuwa na dodoso ambalo linasaidiwa kukamilishwa na hii timu ya wawezeshaji ili sasa kupata kaya masikini zaidi, masikini sana ambazo ndizo zinakuwa lengo la mpango huu wa *TASAF*.

Sasa uchambuzi wa kitaalam pamoja na kuchaguzi kaya hizi ambazo ni masikini sana, lakini baada ya hapo unarudi tena kwa jamii ambao wanakubaliana au hawakubaliani, au wanarekebisha uamuzi au kutambua zile kaya ambazo ni masikini sana. Na orodha hiyo ndiyo inayotumika katika mpango wa kutekeleza sasa kuzisaidia hizi kaya zilizo masikini.

Baada ya kumsikiliza ndugu yangu, mdogo wangu, Mbunge Mwenzangu wa Mbozi Magharibi, kuhusu *TASAF*, niseme tu inahudumia watu wote kwa usawa, kwa ushirikishi. Bila kujali dini, bila kujali vyama, kwa maana ya itikadi za vyama. Kwa hiyo, kwamba tunaweza kuahirisha kutekeleza mpango wa kitaifa ambao umo katika Ilani ya Uchaguzi, kwa sababu eti itaweza kubainika kwamba au kufikirika kwamba hizi fedha zinazokwenda kuhudumia wananchi zinakwenda kusaidia chama kimoja kwa kweli hii ni dhana potofu, na hatuwezi. Kwa hiyo, tutaendelea kutekeleza mpango huu wa *TASAF*.

Kulikuwa kuna mapendekezo kuhusu miundombinu katika makazi ya Rais, hasa Chamwino ambako Kamati ilitembelea. Niseme tu kwamba, ukarabati umeanza, Makazi ya Rais yenyewe tayari tumeishayakarabati. Linaloendelea ni kukarabai nyumba za wageni maarufu, na karibu tunakamilisha ukarabati huo. Kwa hiyo, Chamwino patabadilika, na ninaamii kabisa ndio kutakuwa kitovu cha Serikali pale.

Mheshimiwa Spika, kingine ni kuhusu mfumo wa maji: Rais Nyerere, Baba wa Taifa, aliamua kwamba haiwezikani kuwa na Ikulu ambayo iko tu haihusiani na kijiji ambacho imo. Kwa hiyo, mfumo wa maji wa Ikulu Chamwino ndio huo huo mfumo wa maji wa wananchi wa Chamwino. Kwa hiyo unapokarabati mfumo wa maji wa Ikulu, lazima uunganishe na ukarabati wa maji ya wananchi wa Chamwino ambao ni asilimia 49 tu wanaopata maji safi na salama.

Kwa maana hiyo, kupitia Wizara ya Maji, mpango unatekelezwa wa kukarabati, sasa hivi tumeishakamilisha bomba kuu kutoka Chamwino Ikulu mpaka Bwigiri, kilomita sita. Vile vile tunaweka bomba kuu jipya kutoka Chamwino Ikulu mpaka Msanga, ambako ni kama kilomita sita, tutazikamilisha mwishoni mwa mwezi Februari. Tunategemea tutanunua dira 770 za maji na viungo vyake ili kuwaunganisha kwa kuanzia wateja kama 300, halafu tunachimba visima viwili ili kuongezea uwezo wa maji siyo wa Ikulu tu, vile vile

kwa ajili ya wananchi wa Chamwino. Tumepanga kujenga matanki zaidi kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa Chamwino pamoja na Ikulu yenyewe.

Mheshimiwa Spika, sikutaka kuendelea zaidi, nadhani hii ilikuwa kengele ya kwanza. Lakini inatosha kabisa yale ambayo nilitaka kuyajibu. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Ukinipa muda mimi nashukuru maana nina tatizo hilo. Sasa nimuite Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia masuala machache sana , mengi atachangia Naibu wangu.

Kwanza, ningelipenda nichangie suala ambalo Mheshimwia Silinde alilizungumza na nimshukuru sana Mheshimiwa Agripina Buyogela kwamba amemjibu kwa namna moja au nyingine, suala la Wakurugenzi tuliowasimamisha.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba ni kweli walistahili kusimamishwa na wale waliovuliwa ukurugenzi walistahili. Kwa sababu kama ambavyo Mheshimiwa Agripina alikuja ofisini kwetu na tukauliza, tukapiga simu akisikia, walituhakikishia kwamba kila kitu kinakwenda vizuri na hakuna matatizo na walikuwa wanatushangaa taarifa hizo za kwamba mambo hayaendi vizuri tunazisikia wapi.

Sasa, inapokuja kwamba mtu ambaye amekuhakikishia kwamba mambo yako sawa na anakushangaa kwamba hizo taarifa unazompa hazina ukweli, kwa kweli inapoharibika anastahili kuchukuliwa hatua ambazo tumezichukua. Na sio kwamba tunawatisha ili uchaguzi mkuu unaokuja kwamba waogope kwa maana waisaidie CCM, waogope kwa maana watekeleze majukumu yao wanayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nilitaka nilchangie ni kuhusu suala la ugawaji wa Kata na Vijiji. Sio kila ombi linaloletwa linaweza likakubaliwa.

Mheshimiwa Spika, maombi mengine kwa kweli yalikuwa hayakidhi vigezo, na yale maeneo ambayo yalikuwa ni bahati mbaya kwamba hatukuwapa labda taarifa zilizoletwa kwetu zilikuwa siyo sahihi, tuliwaambia masuala ya kugawa Kata bado tunaendelea, na kwa upande wa vijiji tulisema ni mpaka uchaguzi upite, kwa sababu kwa mujibu wa kanuni zetu za uchaguzi, tunapaswa kuwapelekea vyama vya siasa, maeneo mapya ya uchaguzi, kwa maana vijiji, mitaa na vitongoji, siku 50 kabla ya uchaguzi. Kama tungegawa katikati zile siku 50 tusingelizifikia. Kwa hiyo, tuliwaomba wale wote maeneo ambayo tumekosa kuwapa Kata au Vijiji kwa makosa kwamba tutayapitia kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameahidi kwamba tutawezakuyapitia na tunaomba walete wale ambao wanaona kabisa kwamba wana sifa isipokuwa tulifanya makosa kuwaondoa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ningelipenda kulichangia ni lile linalohusu Mwanza, suala la kiwanja ambapo Mheshimiwa Wenje amelizungumzia. Amemsema Naibu wangu kwamba alikuwa dalali katika uuzaji wa kile kiwanja. Kwa kweli hiyo lugha kwanza nasikitika kwamba aliendelea nayo wakati akichangia mpaka mwisho.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu ni mimi niliyemtuma aende kusimamia, kwa sababu kulikuwa na masuala mengi sana yaliyokuwa yanaendana na suala zima la kiwanja pale Mwanza. Kwa kawaida Serikali haiuziani viwanja. Tulichofanya pale sisi ni kuisimia *BoT,* tena kwa mujibu wa wao wenyewe makubaliano ambapo walikuwa wanavutana. *BoT* walikuwa wanataka watoe shilingi bilioni 1.2. Naibu Waziri Mheshimiwa Mwanri ndiye aliyewalazimia mpaka ikafika shilingi bilioni 3.1.

Mimi nilitegemea Mheshimiwa Wenje, badala ya kumwita Naibu Waziri dalali, nadhani angemshukuru, kwa

sababau kimsingi, Serikali haiuziani wenyewe viwanja, inachofanya ni kutoa fidia kama kulikuwa kuna kitu pale kinachohitaji kufidiwa. Kwa hiyo ile pesa ilikuwa ni kwa ajili ya kurudishia miundombinu iliyoko pale.

Mheshimiwa Spika, na suala la kuzisaidia taasisi, hata *National Housing* wametuomba sisi tuwaombe Halmashauri iwape maeneo ambayo yapo kwa gharama nafuu au wanaweza wakayapata bure ili waweze kujenga nyumba ambazo zitakuwa za gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, na *BoT,* hatukuisaidia Mwanza tu, tumeisaidia Mtwara kupata kiwanja ambapo sasa hivi wanajenga jengo lao *BoT* kwa ajili ya Kanda ya Kusini. Kule Mtwara Benki Kuu wamechangia upimaji wa lile eneo shilingi milioni 3 tu. Sasa ninyi mmepata shilingi bilioni 3.1, Naibu Waziri anaitwa dalali, kule Mtwara sijui Meya aliyetusaidia sijui ataitwaje!

Mheshimiwa Spika, lakini sio hivyo tu, ili kuhakikisha kwamba Serikali haiuziani, hata jengo ambalo Chuo cha Watumishi wa Umma wanalitumia pale Mtwara, majengo mawili pamoja na viwanja vyake, Serikali nikiwa Utumishi, tuliiomba Ofisi ya Mheshimia Waziri Mkuu, yale majengo yalikuwa ya *PSRC,* badala ya kuwauzia wafanyabiashara, tuliomba na majengo yale tulipewa bure, hatukuziwa hata senti tano, wakati yale majengo yalikuwa sokoni, sisi tumeenda kuyatoa sokoni.

Mheshimiwa Spika, nilitaka niyatolee ufafanuzi masuala hayo machache na dakika zilizobaki napenda apewe Naibu wangu. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa mimi naomba nianze kwa kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Mheshimiwa Hawa Ghasia. Nataka nimwambie, baada ya kauli hii aliyoitoa hapa, kama kazi inauwa, mwaka huu nitakufa! Nitaendelea kukutii na nitaendelea kufanya kazi chini yako kwa uadilifu

mkubwa. Nakushukuru sana dada yangu kwamba umeliweka hili jambo vizuri, ningelisema mimi, watu wangefikiri kama najitetea hapa. Nilichofanya mimi ni kutii maelekezo yale na kuhakikisha kwamba tunasimamia maslahi ya Halmashauri ya Manispaa ya Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza hapa walikuwa wale mwanzo kabisa walioomba wachukue bure. Tukasema haiwezekani! Hiyo *shuttle* ambayo naambiwa nimefanya *shuttle* hapa, nilifanya shuttle ile kwa sababu nilijua kwamba kuna huduma zinazotolewa pale kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri ili waweze kutoa walau kitu kitakachosaidia kwenda kuweka huduma hizo mahali pengine. Zikapanda kutoka bilioni 1.2 mpaka 3.1, zikapanda! Kwa hiyo, tukafanya kazi ile kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niseme hapa na Mwenyezi Mungu ananisikia, sisemi uongo na wala sina *orientation* hiyo, *check record* yangu! Watu wengine wanafikiri kila mtu anaweza akakaa tu akafikiria tu kwamba nakwenda kuchukua. Sikufanya hivyo na siwezi kufanya hivyo. Kwa hiyo, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana na Mungu akubariki. *(Makofi)*

Ndugu yangu Mheshimiwa Wenje, ninachoweza kusema, mimi ni mfuasi wa Bwana Yesu, nakusamehe bure. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, yamesemwa mambo mengi hapa. Yamesemwa mambo mengi hapa, yamesemwa mambo mengi! Mheshimiwa Mfutakamba, tumekaa naye tumezungumza naye, na haya mapendekezo ambayo yamefanywa hapa, ni mapendekezo ambayo karibu asilimia 100 tunakubaliana naye, wala hatuna tatizo na haya mapendekezo ambayo yametolewa hapa.

Nataka tuseme hapa, kwamba yote haya ambayo wametushauri, sisi tunaona kwamba ni mambo ya msingi na kwa hiyo tutakwenda kuyafanyia kazi. Lakini, yako mambo ambayo tunafikiri kwamba kuna haja ya kusaidia

kidogo katika uelewa wetu. Kwa mfano, unapoanza na lile suala la kwanza la kujitegemea, tunafahamu kabisa kwamba bajeti yetu sisi asimilia 40 inatokana na *development partners,* na ndivyo inavyokwenda, hii fedha ya *Local Government Capital Development Grant* ni fedha ambayo inatoka kutoka kwa wahisani, na mhisani anapokuletea, wengine wanamuita mfadhili, mfadhili ni Mwenyezi Mungu tu, anapokuletea anakuletea kwa wakati wowote na saa yoyote anavyofikiri na *sometimes* asikuletee, na ndiyo maana miradi mingine unakuta inakuwa katika hali hii ambayo imezungumziwa hapa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimwia Mfutakamba na wenzake wamezungumzia suala la kujitegemea. Tunalichukua, ndiyo *orientation* yetu toka wakati wa Walimu tulikuwa tunazungumza suala la kujitegemea, tunaona kwamba ni hivyo. Na hili la vyanzo vya mapato tumeisha lifikiria tunaona kwamba ni jambo la msingi limezungumzwa hapa.

Mheshimiwa Spika, Waziri a Nchi, Ofisi ya Rais – Utawala Bora, Mheshimiwa George Mkuchika, amezungumzia hili suala la Madiwani, sina haja ya kulirudia tena, limeelezwa vizuri sana. Kwa hiyo, tunakubaliana naye kwamba huwezi ukawa na maslahi ndani ya Halmashauri kule halafu tena unatoka wewe mwenyewe unakuwa mkandarasi kule, hiyo ni un-*ethical* na hatukubaliani nayo.

Mheshimiwa Spika, la nne ambalo amelizungumza katika *bullet 4,* anazunguma habari ya *mult-model,* kwa maana ya Dar es Salaam. Dar es Salaam pale tumepeleka *DART* ile ya *Rapid Transport*. Anachosema anazungumza miaka 50, miaka 100 ijayo, anasema kwamba afikirie njia nyingine kuacha hilo kwa sababu Dar es Salaam inavyokua sasa hivi tunakwenda kwenye idadi ya watu milioni 4 mpaka milioni 5, tunakubaliana naye.

Amezungumzia habari ya kupitisha kwenye bahari, amezungumzia suala la *Metro* kupita chini, amezungumzia habari ya *Railways* na vitu vingine ambavyo *projectively*

kama mmesikiliza vizuri nilipokuwa najibu swali la *Metropolitan Development* kwa upande wa Dar es Salaam, ni miongoni mwa mambo hayo tunayokusudia kufanya katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo, hii tunakubaliana nao moja ka moja.

SPIKA: Sasa nitamuita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Uratibu na Bunge.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda mbali sana, naomba kwanza niwatoe hofu Watanzania wote na niwape taarifa rasmi kwamba, dawa hizi za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI zipo, wasiwe na hofu, na zinaendelea kutolewa, na bado *Global Fund* wanaendelea kutufadhili, lakini tunaendelea pia kushirikiana na Serikali ya Marekani kuhakikisha kwamba dawa hizi zinaendelea kutolewa.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza Watanzania wote wapate habari kwamba dawa hizi zipo na zitaendelea kutolewa na tatizo hilo la hizo dawa hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kwanza nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI pia na Kamati ya Katiba na Sheria kwa michango na mawazo mazuri waliyoyatoa pamoja na michango ya Waheshimiwa Wabunge waliyoitoa. Nianze na hili suala la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa takriban Watanzania 1,600,000, wanaishi na Virusi vya UKIMWI. Lakini kati yao hao 1,600,000, Watanzania 665,000, ndio walioanza kutumia dawa mpaka sasa hivi. Sasa hawa wengine bado hawajaanza kutumia dawa kutokana na sababu mbalimbali, wengine hawajapima, lakini wengine muda wa kutumia dawa bado haujafika.

Mheshimiwa Spika, kati ya hao ninaosema wana maambukizi, asilimia 60 ni wanawake na asilimia 40 ni wanaume. Kwa hiyo, unaona kwamba maambukizi haya ya vizuri hivi ni makubwa kwa wanawake zaidi ya wanaume. Lakini maambukizi haya yameendelea yakipungua kwa sababu ya juhudi za Serikali kupambana na tatizo la UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004 maambukizi yalikuwa ni 7%, lakini sasa hivi yameshuka mpaka 5.3% kwa mwaka 2011/2012. Hii ni juhudi kubwa iliyofanywa na Serikali, ingawa naomba pia Watanzania wajue maambukizi yaliyvyo sasa kwa wanawake wenye umri kati ya miaka 45 – 49 maambukizi ni 10.2% na kwa wanaume wenye umri wa miaka 45 – 49 maambukizi ni 6.7%.

Mheshimiwa Spika, bado naendelea kusema kwamba maambukizi kwa upande wa wanawake bado yanaedelea kuwa katika kiwango cha juu ukilinganisha na wanaume.

Mheshimiwa Spika, sasa ni lazima Serikali ipate ufumbuzi kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge, na mimi nasema michango yote na maswali yote tutayajibu kwa maandishi, muda ni mfupi.

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa imeamua kufanya yauatayo:-

Kwanza kabisa, ni kukubaliana na mapendekezo ya Kamati ya kuanzisha sheria ambayo itaunda mfuko wa kudhibiti UKIMWI katika nchi yetu ya Tanzania. Suala hili ni la muhimu sana, kwa kuwa kwa muda mrefu toka tumeanza mapambano haya Serikali ilikuwa ikiendelea kutegemea sana fedha ya wafadhili.

Mheshimiwa Spika, mfadhili atakapojitoa na tunafikiri kuanzia mwaka 2014 mpaka 2016 wafadhili wengi watakuwa wamejitoka tutakuwa kwenye matatizo makubwa. Naomba sheria hiyo tutakapoileta Bungeni, nadhani mwezi Machi, mtuunge mkono sasa tuanze kukusanya nguvu ya

ndani kuhakikisha tunadhibiti matatizo haya ya ugonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wabunge wengi wamechangia na Kamati zote zimechangia kuhusu tatizo la dawa ya kulevya. Tatizo hili kwa kweli ni kubwa na limekuwa likiendelea. Matumizi ya *heroine* na *cocaine* yanaendelea, lakini matumizi ya mirungi na matumizi ya bangi yamekuwa yakiendelea zaidi kuliko matumizi ya dawa hizo nyingine za kulevya. Hii ni shida kubwa.

Mheshimiwa Spika, Sheria za Kudhibiti Matumizi ya Dawa za Kulevya katika nchi ya Tanzania, zilianza toka miaka ya 1925 mpaka 1955. Lakini, unaona kwamba pamoja na juhudi hizo, bado tatizo limeendelea kuwa kubwa. Mwaka 1995 Serikali ilitunga sheria nyingine tena ya kudhibiti matumizi haya ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Kamati, nakubaliana na Wabunge, janga hili limendelea kuwa kubwa na linathari kubwa na hasa kwa viijana wetu watoto wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeona umuhimu na inakubaliana na Kamati. Ni muhimu sasa tulete sheria. Tutaleta sheria, na naomba tena Wabunge wakubali kutuunga mkono, mwezi Machi, 2015 tutaleta sheria nyingine ya kuona ni namna gani tunadhibiti tatizo hili la dawa za kulevya nchini.

Mheshimiwa Spika, tunachokwenda kufanya ni kufuta ile Sheria ambayo ilianzisha Tume mwaka 1995 na sasa tunaenda kuleta sheria ya kuanzisha mamlaka ya kudhibiti matatizo haya ya dawa za kulevya nchini. Sheria hiyo tunataka kuipa mamlaka, hiyo nguvu ya kuwakamata wote wanaoshughulika na dawa za kulevya, kuwapeleleza na vile vile kuwapekua. Sheria ya mwaka 1995 ilikuwa na upungufu mkubwa na hivyo tunaona kwamba ilikuwa haitusaidii kuwa na juhudi za kutosha za kupambana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Sheria ya mwaka 1995, yenyewe ilikuwa inabagua baadhi ya aina za dawa za kulevya kuingizwa kama ni dawa ambazo zinatakiwa zipigwe marufuku katika nchi yetu ya Tanzania. Pia Sheria ya mwaka 1995 yenyewe ilikuwa inatumia kigezo cha thamani ya dawa kama ndiyo kigezo cha kutoa dhamana na kushitaki na kutoa hukumu.

Mheshimiwa Spika, tumegundua kwamba badala ya kigezo hicho kusaidia mapambano, kilikuwa kinahamasisha zaidi. Mtu akisikia kuna mtu amekamatwa na dawa za milioni 30, badala ya kuleta ari ya kupambana, inahamasisha watu waendelee kufanya hiyo biashara ili waweze kujipatia kipato zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hiyo tutaibadilisha, sasa tutakuwa tunatoa dhamana na kutoa hukumu kwa kuzingatia wingi wa dawa unazokamatwa nazo na siyo thamani tena maana ilikuwa inapotosha ukweli.

Mheshimiwa Spika, suala la kuhamia Dodoma lipo palepale, azma ya Serikali ipo hapohapo, hatutaibadilisha, ni azma ya Serikali na itaendelea kuwa kama ilivyo. Tumeamua kuleta sheria, tutailea sheria ambayo iko kwenye mchakato ya kutambua Dodoma kuwa Makao Makuu ya Serikali na baada ya kufanya hivyo Dodoma kuiweka kuwa Makao Makuu, mchakato utaendelea wa kufanya azma hiyo itimie.

Mheshimiwa Spika, Serikali mpaka sasa imeendelea kupiga hatua. Kwa mfano, Wizara ya Fedha imeishajenga ofisi hapa Dodoma, *BoT* wameishajenga ofisi yao hapa, *TRA* na chama tawala, Chama Cha Mapinduzi kimeishaanza kujenga Makao Makuu jengo jipya, kubwa lenye thamani. Tunaonesha njia, dhamira ipo, tutatekeleza. Miundombinu tunaendelea kuiboresha lakini tunaendelea kujitathmini hatua hizo ili twende nazo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie na hili la mwisho. Sio kweli kwamba Mheshimiwa Rais amekuwa akisema uongo

katika mchakato wa Katiba, wanaosema maneno haya kwa kweli tunawaomba wamwombe radhi Mheshimiwa Rais wetu na hasa kama ni watu kutoka Upinzani, Mheshimiwa Rais amekuwa mvumilivu sana, amealika majadiliano mara chungu nzima Ikulu ili kupata muafaka katika jambo hili la Katiba.

Kwa hiyo, naomba sana wote kwa pamoja na hasa wenzetu wa Upinzani, Mheshimiwa Mnyika uheshimu heshima ya Mheshimiwa Rais kualika makundi mbalimbali Ikulu kupata ufumbuzi wa Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Katiba linaongozwa na sheria, haliongozwi na kitu kingine chochote. Tumetunga sheria hapa ndani ya Bunge, sheria hii ndiyo itakayotuongoza, tumefika wapi kwenye mchakato wa Kura za Maoni, tumefika wapi kwenye Daftari la Wapigakura, tumefika wapi katika kila hatua, tutaongozwa na sheria na hatutaongozwa na maneno hasa maneno ya Upinzani kama anavyosema Mheshimiwa Mnyika, tutaongozwa na sheria iliyotungwa ndani ya Bunge na sheria hiyo ndiyo itakayotupeleka mahali tu napotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Katika *report* ya Kamati kuna mambo mawili yanayohusu Ofisi ya Makamu wa Rais: Moja, ni jengo ambalo limejengwa nyuma ya makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais ambalo Wizara tulitakiwa kulifuatilia.

Mheshimiwa Spika, tumeiandikia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu jengo hili, na sio jengo hilo peke yake, lakini pia viwanja vyote vilivyopo nyuma ya jengo hilo na wamiliki

wake. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wamefanya kazi hiyo na tarehe 6 Februari, 2015 tumealikwa kwenye kikao cha kuzungumia mambo hayo. Kwa hiyo, tunalifanyia kazi na ni matumaini yetu kwamba tutalifikisha pazuri.

Pili, ni suala la uchakavu wa ujenzi katika jengo la Makamu wa Rais pamoja na ofisi pale Zanzibar. *Concern* ya Kamati ni kwamba kumetumika mbao badala ya *aluminium*, lakini nataka niseme kwamba ujenzi kule Zanzibar unatumia zaidi mbao kwa sababu ya hali ya hewa ya *humidity* pamoja na chumvi ya bahari.

Sasa, tatizo lililopo katika jengo lile ni kwamba, mbao zile zilipakwa *vanish* ambayo ni ya muda mrefu na imepigwa na jua, kwa hiyo inaonekana kupauka. Tutakachokifanya ni kuparua *vanish* yote na kuweka *vanish* mpya na jengo litarudi kwenye hali yake.

Mheshimiwa Spika, tunajitahidi kutunza jengo hili! Ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria!

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, na mimi nianze kwa kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, na mimi naomba niipongeze Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia na kuishauri Wizara yangu. Kamati hii kwa kiasi kikubwa imechangia ufanisi katika utendaji kazi wa Wizara katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mwenyekiti mpya wa Kamati Mheshimiwa Jasson Rweikiza kwa kuiongoza Kamati hii, na mimi napenda kuahidi ushirikiano,

mimi na Mheshimiwa Waziri na Viongozi wote wa taasisi zilizo chini ya Wizara katika utekelezaji wa majukumu yako.

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza taarifa ya Kamati kwa makini, nimesikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge wote kwa umakini na sasa napenda kuchangia hoja hii kwa kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilikuwa ni suala la ufinyu wa bajeti ya Mahakama. Kwa niaba ya Serikali, sisi tunatambua umuhimu wa Mahakama katika mfumo mzima wa utoaji haki na tunatambua kweli Mahakama zetu sasa hivi zinakabiliwa na tatizo la ufinyu wa bajeti, lakini kuanzia mwaka 2012 mpaka 2013 tumechukua hatua za makusudi za kuhakikisha kwamba Mahakama yetu inakuwa na fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2012/2013 bajeti ya Mahakama ilikuwa ni shilingi bilioni 102, mwaka 2013/2014 tuliongeza bajeti ya Mahakama hadi kufikia shilingi bilioni 160 na mwaka wa fedha 2014/2015 bajeti ya Mahakama imefikia shilingi bilioni 166. Huu ni mfano wa kwamba Serikali inatambua umuhimu wa Mahakama katika mfumo mzima wa utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba changamoto iliyokuwepo ni kwamba fedha hizi hazitolewi kwa wakati na hazitolewi zote. Kwa hiyo, sisi Wizara ya Katiba na Sheria tutaendelea kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha Hazina kuhakikisha kwamba fedha zinatolewa kwa wakati hasa fedha za ujenzi wa Mahakama.

Mheshimiwa Diana Chilolo amezungumzia ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Iramba, Mheshimiwa Agripina Buyogera na Mheshimiwa Mipaka wote wamezungumza ujenzi wa Mahakama. Kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana na wenzetu wa Hazina ili kuhakikisha kwamba fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama zinatolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ambayo imeongelewa pia na Kamati ni suala la upungufu wa rasilimali watu na ni kweli kama Serikali tunatambua kwamba upungufu wa rasilimali watu ni changamoto katika mfumo mzima wa utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nilieleze Bunge lako tukufu kwamba katika mwaka huu wa fedha Mahakama tayari imepata vibali vya ajira 1,057 kwa ajili ya kuajiri Mahakimu na watendaji wengine wa Mahakama.

Katika mwaka huu wa fedha tayari tumeishaajiri Mahakimu 103 na tayari pia tumeishaajiri watendaji wa Mahakama katika ngazi ya Mkoa kama Kamati ilivyoshauri katika mapandekezo yake kwamba tutekeleze sasa muundo wa Mahakama kwa mujibu wa Sheria ya Utawala wa Mahakama Namba 4 ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba tayari Mahakama imeishatangaza nafasi za watendaji wa Mahakama katika ngazi za Wilaya.

Naomba Waheshimiwa Wabunge muwaeleze wapigakura wenu, katika vyombo vya habari, magazeti ya jana zipo nafasi 80 kwa ajili ya maafisa utawala, zipo nafasi 80 kwa ajili ya maafisa utumishi. Hawa tutawapeleka katika Wilaya zote za Tanzania ili waweze kufanya kazi ya utendaji na Mahakimu na Majaji wafanye kazi za kusikiliza mashauri na kuendesha mashauri. Matangazo hayo yapo katika vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la vitendea kazi, napenda pia kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa mwaka huu wa fedha tayari tumeishanunua magari 137 na tumeishayasambaza katika Mikoa na Wilaya mbalimbali. Pia tumenunua pikipiki 230 kwa ajili ya kushughulikia shughuli za ukaguzi wa Mahakama katika Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imeongelea suala la mmomonyoko wa maadili hususani vitendo vya rushwa

miongoni mwa watendaji wa Mahakama na pia Mahakimu. Sisi kama Serikali, lakini Mahakama kupitia Wizara pia, tumeweza kutoa mafunzo kuhusu uzingatiaji wa maadili. Lakini pia naomba nilikumbushe Bunge lako tukufu na Watanzania wote kwamba Sheria ya Utawala wa Mahakama inataka kuanzishwa Kamati za Maadili za Mahakimu za Wilaya na Mikoa.

Kwa hiyo, tunaomba wananchi mtoe taarifa katika Kamati hizi, zipo katika ngazi za Wilaya na Mikoa kutoa taarifa kuhusu masuala mbalimbali ya ukiukwaji wa maadili kwa Majaji, Mahakimu na Watendaji wengine wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama kwa mfano, katika mwaka uliopita ilipokea mashauri 21, kati yao mashauri 6 Mahakimu walifukuzwa kazi na Mahakimu 15 walipewa onyo na kurudishwa kazini. Kwa hiyo, naomba nitoe rai kwa wananchi kutoa taarifa.

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo limeongelewa na Kamati ya Bunge nalo ni suala la TAKUKURU kupewa mamlaka kamili ya kuchunguza na kuendesha mashauri ya rushwa, Mheshimiwa Mkuchika ameliongelea vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe angalizo kwa Bunge lako tukufu, nakubaliana na hoja za Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna haja ya kupambana na rushwa na kuna haja ya kuijengea uwezo TAKUKURU, lakini mamlaka ya Mwendesha Mashitaka ni mamlaka ya kikatiba. Bunge lako lina dhamana na wajibu wa kuhakikisha kwamba hatuvunji Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutakapokuja kujadili mapendekezo, nitaleta mapendekezo kwamba pendekezo Namba 15 linalotaka kuipa TAKUKURU mamlaka kamili ya kuchunguza na kuendesha mashitaka litakuwa kidogo linakwenda kinyume na Katiba yetu ya nchi. Mheshimiwa Mkuchika amelieleza vizuri kwamba ni vizuri sasa tuangalie ni jinsi gani suala hili tutaweza kulifanyia kazi.

Ibara ya 59(b) ndiyo inasema Mkurugenzi wa Mashitaka atakuwa na uwezo wa kufungua, kuendesha na kusimamia mashitaka yote nchini. Kwa hiyo, tubadilishe hii Katiba kwanza ndipo tunaweza kufanya mambo mengine. Tubadilishe kipengele cha Katiba, lakini Mheshimiwa Mkuchika amelieleza vizuri kwamba labda tutazame mchakato huu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Mheshimwia Jenista Mhagama ameliongelea vizuri sana. Mheshimiwa Mnyika, anasema mchakato wa Katiba uliendeshwa kiholelaholela.

Mheshimiwa Spika, naomba nilieleze Bunge lako tukufu na Watanzania wote kwamba mchakato wa Katiba uliendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Sura ya 83 ya Sheria za Tanzania. Tulikaa hapa tukaijadili sheria ile na tukaipitisha.

Mheshimiwa Spika, sisi Serikali kwa upande wetu tunajua mchakato huu ulikwenda vizuri sana na sasa tupo katika hatua nyingine ya utekelezaji. Suala la kujadili lilishapitwa na wakati, sasa hivi tupo katika hatua nyingine ya utekelezaji. Namshukuru sana Mheshimiwa Jenista ameliweka vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na nawashukuru Wajumbe wote ambao mmechangia hoja hii. Tunawaahidi kwamba tunao mpango wa kujenga Mahakama zenu, upo hapa, tutawaeleza na tutaendelea kushirikiana nanyi katika kuhakikisha tunaimarisha mfumo wa utoaji haki katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28, nitaongeza muda baada ya kufika muda wa kuahirisha ile nusu saa niliyokuwa nayo. Kwa hiyo, namwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, dakika 15 na kila mtu anapewa dakika 15. Mheshimiwa Mwenyekiti!

MHE. JASSON S. LWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja ya Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala na napenda kusema kwamba katika michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, tumepata wachangiaji wa kuzungumza 14 na waliochangia kwa maandishi ni watano.

Mchangiaji Mheshimiwa Diana Chilolo amezungumzia suala la matatizo ya Mahakama, ufinyu wa bajeti, ambapo Mawaziri wamelijibu kwa kina. Lakini niseme kwamba kwa kweli Serikali inajitahidi kiasi cha kutosha kwamba bajeti imeongezwa kutoka shilingi bilioni 20 mwaka juzi hadi shilingi bilioni 166 sasa. Isipokuwa kwamba fedha hii haitoki kwa wakati, bajeti inaongezwa lakini fedha hiyo haitolewi. Kwa hiyo, sisi rai yetu kwenye Kamati ni kwamba fedha hiyo itolewe kama ilivyokuwa *budgeted*.

Mheshimiwa Spika, lakini pia amechangia kwamba Mahakama hazitoshi. Ni kweli tumesema kwenye maelezo tuliposoma taarifa yetu kwamba maeneo mengi Wilaya hazina Mahakama, Mahakama za Mwanzo hazitoshi na Mahakama Kuu hazitoshi. Ujenzi unaendelea, lakini tungeomba kasi hii iongezwe. Unakuta Hakimu wa Mahakama za Mwanzo ana Mahakama mbili au tatu anazozihudumia na umbali kati ya Mahakama moja hadi nyingine ni kilometa 30 au 40, kwa kweli hali hii inaleta adha kubwa sana kwa wananchi maana haki haipatikani kwa muda unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ntukamazina ameongea kwa kirefu kuhusu mambo mbalimbali yaliyomo kwenye taarifa yetu na hasa suala la rushwa. Jambo lililoongelewa kwenye Bunge lililopita, suala la *Account* ya *Escrow* na masuala mengine. Sisi tunasema, tunataka uchunguzi ufanywe kwa kina, wanaotajwatajwa wote wachunguzwe, wakibainika washitakiwe, kama wana hatia wafilisiwe na wapelekwe jela, siyo tu kukaa kimya. Tulimwita Mkurugenzi wa *PCCB* aje kwenye Kamati atuambie kwa nini mpaka leo ni kimya hatusikii kinachoendelea. Tangu Rais atoe maagizo yale ni

muda mrefu, lakini mpaka sasa hivi TAKUKURU wapo kimya, hatujui kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, amezungumzia *CDA* miaka 42 tangu ianze na kwa kweli Dodoma bado haijafikia hadhi ya kuwa Mji Mkuu wa nchi. Kwenye Kamati sisi tunasema kwamba kwa kweli kama sababu za kuhamia Dodoma hazipo tena, basi hili wazo lifutwe. Na sisi tunaunga mkono wazo la Mheshimiwa Ntukamazina, kama hakuna sababu na azma imekwisha, basi hilo wazo tuondokane nalo. Hawa walioanza baada ya sisi, Nigeria na wengine wamejifunza kwetu, wamehama kutoka Lagos kwenda Abuja, wamejifunza kwetu na leo wamehamia Abuja ndiyo Mji Mkuu, lakini sisi bado mpaka leo tunahangaika nao. Kwa hiyo, kwa kweli kuna haja ya kuliangalia upya jambo hili.

Amesema kuhusu MKURABITA, *TASAF* na kupima mashamba, ni jambo la muhimu sana. Tunapowaongelea hawa watu maskini sana wana mashamba, yakirasimishwa yakapata hati ni rahisi kwenda benki kukopa na kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Nyambari Nyangwine ameongelea mambo mengi, lakini ameongelea *TASAF* na Tume ya Mipango, yote yana umuhimu mkubwa. Lakini sisi tunasema *TASAF* inasaidia sana kupambana na umaskini katika kuwasaidia kaya maskini sana.

Mheshimiwa Spika, tunafikiri kwamba ingelikuwa ni vizuri kama kaya inapewa shilingi 138,000/= kwa miezi minne, hizi zingeunganishwa badala ya kaya moja zikawa kaya 20, wakapewa mafunzo watu hawa ingekuwa ni shilingi 3,000,000/=, wakapewa mafunzo ya mradi wakawa na mradi, hata mradi huu wa *TASAF* ukiisha wanaendelea kuwa na njia bora ya kujizalishia mali, kwa hiyo umaskini unakuwa umepigwa vita.

Amezungumzia ofisi za Wabunge, ni jambo la maana sana, kwa kweli Wabunge hatuna ofisi, inabidi sasa watu waje nyumbani, wananchi wakufuate nyumbani asubuhi

hujaamka wapate huduma, wanakosa huduma za lazima. Ni vizuri ofisi za Wabunge zikajengwa na mambo mengine ameongelea yeye pamoja na Wabunge wengine.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Silinde imejibiwa na Waheshimiwa Mawaziri, kuhusu Daftari la Kudumu.

Mheshimiwa Augustine Massele, amezungumzia mambo mbalimbali ambayo yamejibiwa na Waheshimiwa Mawaziri.

Mheshimiwa Sakaya amezungumzia suala la *PCCB* kuomba kibali kwa *DPP*. Mawaziri wamelijibu, lakini hili na mimi nisisitize kwamba na sisi tunafahamu kwamba Katiba inasemaje. Lakini jambo hili ni jambo la maana sana na la muhimu kutiliwa mkazo.

Mheshimiwa Spika, *PCCB* ilianza kama kikosi kidogo, ilikuwa inaitwa *Anti-Corruption Squad* miaka ya 70 au 60 mwishoni. Ilikuwa na watu wachache sana kama 20 au chini ya hapo, ilikuwa haina wanasheria, haina waendesha mashitaka, kulikuwa na mwanasheria mmoja Mzee Maftaha wanaomfahamu, alikuwa ndiye mwanasheria pekee *Anti-Corruption Squad*, isingewezekana watu hawa wakafanya mashitaka Mahakamani, ilibidi kesi ziendeshwe na *DPP*.

Mheshimiwa Spika, leo TAKUKURU ni chombo kikubwa sana na kina rasilimali watu wengi sana, kina vifaa vingi sana. Mwaka jana peke yake wameajiri watu 400. Inawezekana TAKUKURU inazidi Ofisi ya *DPP* kwa uwezo wa nguvukazi, kwa utaalamu na vifaa, inawezekana!

Sasa kwa nini waombe kibali kwa *DPP*? Kuna umuhimu gani? Kama wamepata mafaili 3,000 wameyachunguza, wamefungua mafaili 100 kwa kweli inaonesha kwamba kuna tatizo kubwa sana, kuna tatizo! Ni lazima mambo yabadilike. Tunafahamu Katiba na tunasema kwamba mchakato uanze kubadilisha utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Pindi Chana amechangia kwa maandishi, amezungumzia *TASAF* na ambayo tumeishaisemea. Lakini pia amezungumzia Mpigachapa wa Serikali kukarabati mitambo aliyo nayo ya uchapaji. Hili ni wazo zuri na tunasema kwamba apewe mitambo mipya kwa sababu kukarabati mitambo ya zamani ambayo imechoka inaweza isikidhi haja. Apewe mitambo mipya na ya kisasa maana kuna siri za Serikali humo ndani na kuna mambo mengi ya kufanya ambayo bila kuwa na mitambo ya kisasa kazi hii inaweza isifanyike kwa viwango.

Mheshimiwa Rebecca Mngodo amechangia kwa maandishi na yeye amezungumzia suala la TAKUKURU kupewa uwezo na meno. Hili ni jambo muhimu kwani rushwa ni sawa na makosa mengine. Kwa nini polisi wanapeleka watu mahakamani kwa wizi au makosa mengine, lakini linapokuja suala la rushwa ni lazima waombe kibali kwa Mkurugenzi wa Mashitaka.

Mheshimiwa Spika, rushwa na makosa mengine ya jinai yote ni ya jinai. Kwa hiyo, kama haiombi kibali kwa makosa mengine ya mauji, wizi na kadhalika, basi hata hili la rushwa lisiombewe kibali. Katiba iangaliwe upya tuanze mchakato wa kuirekebisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kesi kuchukua muda mrefu. Ni kweli kesi ikichukua muda mrefu wananchi wanapata taabu sana. Tunasema *justice delayed is justice denied!* Ni vizuri kesi zikachukua muda mfupi, zikaisha haraka.

Mheshimiwa Spika, Mahakama fedha iongezwe, *TASAF* elimu itolewe, tunakubaliana na mawazo ya Mheshimiwa Mngodo.

Mheshimiwa Vincent Nyerere amechangia kwa maandishi akasema kama kaya ambazo zimeonekana kuwa ni maskini sana zinapewa fedha na Serikali kupitia *TASAF,* kwa nini kaya hizo hizo zichangie tena maabara, afya na matibabu na michango mingine?

Mheshimiwa Spika, hili ni wazo la maana sana, kama hawa ni maskini sana watachangaje? Kwa kweli na mimi ninakubali kabisa kwamba, hawa watu wapewe msamaha *(exemption),* wasichangie mambo ya maabara, karo na mengine. Pale ambapo *TASAF* haipo maana haipo katika Mikoa au Wilaya zote, ipo katika baadhi ya maeneo, pale ambako haipo wale maskini sana waorodheshwe na wasamehewe michango hii ambayo kwa kweli hatuoni sababu ya mtu ambaye tayari ni maskini lakini tena anaambiwa achangie michango ambayo ni mikubwa.

Mheshimiwa Ritta Kabati amezungumzia nyumba za viongozi kama ile ya Makamu ya Rais, Tunguu na Waziri Mkuu, Dodoma. Amependekeza kwamba ujenzi ufanywe na Wakala wa Majengo wa Serikali *(TBA)* au Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*. Hilo ni wazo zuri lakini tukifanya hivi mimi ninafikiri tunarudi kwenye ukiritimba uliokuwepo zamani. Sasa hivi ni biashara huria, watu wanashindana kwa bei na viwango. Sheria zipo kama Mkandarasi au Mtaalamu wa Ushauri anaharibu kazi, sheria zipo zitumike kumbana. Pia amezungumzia *TASAF,* elimu, nimelisemea na Mawaziri wamelisemea.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria, wadau wapewe fursa ya kuchangia, hii inafanyika sana. Alhamisi tutaleta Muswada hapa, tumekaa Dar es Salaam na wadau zaidi ya 110; wamekuja Mashehe zaidi ya 40, Maaskofu nane na watu mbalimbali zaidi ya 50. Wamechangia, wametoa mawazo yao na kwa kweli wana uelewa wa kutosha na sisi tunazidi kuwafafanulia. Kwa hiyo, wadau kwa kweli wanashirikishwa vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jitu Soni amezungumzia ujenzi wa Mahakama ambalo tumelisemea. Pia amesema TAKUKURU itoe elimu na iongeze kasi. Wanatoa elimu, wana vipindi kwenye redio na televisheni. Mimi ninasema tu waongeze kasi ili kusudi watu waelewe ubaya wa rushwa na namna ya kupambana nao kwa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, kibali cha *DPP* na yeye ameungana na sisi kwamba kwa kweli kiondolewe. Hivyo ndivyo ilivyo katika nchi nyingine, ametaja Mheshimiwa Waziri Uganda, Uingereza na sehemu nyingine, kusudi tuweze kupambana na rushwa kwa kasi ambayo inaridhisha.

Mheshimiwa Spika, amependekeza fedha ya Mahakama iwe *ring fenced*, yaani isitumike kwenye mambo mengine ambayo hayakukusudiwa. Ni jambo la maana sana, kama kuna fedha imetolewa isibadilishwe matumizi na vyanzo vingine viainishwe ili vitumiwe kwenye kazi ambayo imekusudiwa. Kama nilivyosema kwa kweli kesi ikichelewa sana siyo vizuri. Pia amependekeza Mahakama zipewe vifaa kama *photocopy* na vifaa vingine. Hilo nalo ni jambo la maana kwa sababu mtu anapewa labda hukumu ya jela miezi sita, anakata rufaa, kuja kupata nakala ya hukumu ni miezi minne, kuja kupeleka rufaa mahakamani miezi mingine minne, anakuta hata kifungo kimeisha.

Kwa hiyo, huyo ni kwamba amenyimwa haki ya kukata rufaa na kusikilizwa kabla adhabu yake haijaisha.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dakika 15 nilizopewa nimeona hazitoshi nimeona nichangie kwa kujibu hayo machache ambayo nimeweza kusema. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ninaomba usome *statement* ile ya kuwasilisha Muswada wako. Kuna yale maneno ambayo yako kwenye *Order Paper* na yanatakiwa kusomwa ili sisi tuhoji. Haya mpe hayo.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaomba kwamba sasa Bunge lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kama tulivyoiwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa maneno hayapo hivyo, umeyasoma sawa sawa?

MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Ninaomba kutoa hoja.

SPIKA: Hujasema pamoja na maoni na mapenekezo, hujamaliza.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo. *(Kicheko)*

MHE. GODBLESS B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, ninaafiki!

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo imetolewa na sasa nitawahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala katika kipindi cha Januari 2014 hadi Januari, 2015 ilipitishwa na Bunge pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo)

SPIKA: Sasa nitamuita Mwenyekiti wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa fursa hii ili kutoa mawasilisho ya mwisho kuhusu Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Niwashukuru Waheshimiwa wachangiaji wote, sita wamechangia kwa maandishi na 16 wamechangia kwa kuongea.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninapenda kuongeza katika mapendekezo tuliyotoa na hili Mheshimiwa Mtanda

pia ameliongelea kuhusu mgogoro baina ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi na wakazi wa eneo la Mmongo Mabano, Kata ya Rasibura. Hili ni suala ambalo lilikuwa na tatizo baina Mfuko wa Dhamana ya Uwekezaji *(UTT)* na wenye maeneo yale Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda tu kusisitiza kwamba wale ambao malipo yametolewa na wameona kuwa wamepunjwa, tunaomba mamlaka isimamie hili suala, makadirio yafanyike tena ili wenye maeneo ya ufukweni *(beach plots)* waweze kulipwa stahiki na haki zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, ihakikishe inatekeleza kwa ukamilifu maazimio yote yanayotakiwa na Kamati na Taarifa za Utekelezaji wa maazimio hayo ziwasilishwe mbele ya Kamati kabla ya Bunge la Bajeti la mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala ambayo yamezungumzwa na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunataka kusisitiza tu kwamba bajeti ziweze kuwa za kujitegemea kiasi ambacho miradi yote ya maendeleo ihakikishe fedha za ndani zinakuwa *budgeted* katika umbile la bajeti na kama kutakuwa na fedha za ziada tutafute kwenye *concessions loans* kwa sababu tukiendelea kutegemea wahisani, hii itatuletea matatizo.

Aidha, pia katika suala la kupunguza matumizi ya Serikali tunashauri liwe jukumu la Serikali ndiyo mwajiri na ijibadilishe kwa vitendo vya uasilia kuwa ni mwezeshaji, mtunga sera na mwangalizi wa namna bora ya kutia chachu ukuaji wa uchumi kwenye sekta zinazotoa ajira kwa wingi kama kwenye kilimo, viwanda vyenye *backward* na *forward linkages* na kilimo na biashara ambayo itahusisha biashara ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, pia tulikuwa tunasisitiza kwamba Serikali ipunguze ukubwa wa majukumu yake kwa kupunguza idadi ya Wizara kama ikiwezekana.

Tume ya Wakala mbalimbali kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kama semina, warsha, makongamano na kupanga bajeti, kuandaa mipango ya maendeleo ambayo utekelezaji wake utakuwa rahisi kutokana na matumizi ya manunuzi, labda yale magari makubwa yenye *engine cc* zaidi ya 3000 kama mashangingi yawe ni marufuku na kupunguza matumizi ya mafuta ya magari.

Mheshimiwa Spika, haya tunafikiri gharama kama hizi zikipunguzwa Serikali inaweza kuwa na fedha za kutosha kupeleka kwenye maendeleo ya wananchi hasa waliopo vijijini.

Mheshimiwa Spika, nimepata mapendekezo kutoka kwa Mheshimiwa Jitu Soni akipendekeza utaratibu wa kukusanya mapato kwa njia ya elektroniki. Ninafikiri hili ni suala zuri, TAMISEMI ijaribu kuangalia ni jinsi gani inaweza kufanya utaratibu huo.

Mheshimiwa Sylvester Maselle Mabumba, amependekeza suala moja ambalo silikubali kwamba hatuwezi kulijadili suala la UDA. Kwa hiyo, hilo sitaweza kulijadili, lakini na yeye amependekeza tu sheria ndogo ndogo TAMISEMI izisimamie ili tuweze kuongeza mapato kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Agripina Buyogera, amezungumzia tatizo kubwa la vile vijiji ambavyo havikupata fursa ya kupiga kura, lakini pia amezungumzia masuala ya sheria katika kupata huduma mbalimbali kupitia TAMISEMI. Pia kwenye sehemu ya uwindaji ya Kagera Nkenda, hili suala amelizungumzia na ninafikiri TAMISEMI iliangalie ni jinsi gani hili linaweza kushughulikiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Moshi Kakoso amezungumzia suala la upungufu wa huduma katika maeneo ya Mpanda Vijijini, suala la maji pamoja na huduma za madaktari na wauguzi. Hili suala liko hata katika maeneo ya Igalula kule ambako kuna sehemu ambazo hospitali hazipati dawa na waganga

ni wachache pale Igalula Barazani. Tusaidiwe kikamilifu na TAMISEMI katika hilo, ili huduma hizi ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, liko suala la karibu shilingi bilioni kumi ambayo ni asilimia tano ya *own sources*, lakini Halmashauri nyingi hazipeleki hizi asilimia tano kwa vijana na asilimia tano kwa wanawake. Hii iko kisheria, ni lazima TAMISEMI isimamie kikamilifu kuhakikisha kwamba asilimia tano zinaenda kuwasaidia vijana na asilimia tano ziwasaidie akina mama katika miradi yao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yale 20 tuliyotoa ningeomba sasa Bunge lizingatie mapendekezo ya Kamati pamoja na maoni ya mapendekezo 20 ya jumla tuliyoleta yanayopatikana ndani ya taarifa ya Kamati hii. Ninaomba kutoa hoja.

SPIKA: Nyie hamjui ile *statement* yetu? Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inasema nini ili kila mtu ajue?

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Masuala ya TAMISEMI, pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, ninaafiki!

SPIKA: Hoja hiyo mmeiamua. Kila mtu ana ile karatasi ambayo imeandikwa Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015, mapendekezo ya Kamati. Tunakwenda ukurasa kwa ukurasa, ukifika ukurasa huo anayetaka kusema atasema.

Haya tuko ukurasa wa kwanza, Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru …

SPIKA: Hatuondoki kwenye mapendekezo ya Kamati maana ndiyo kazi yao.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo dogo lakini muhimu kwenye pendekezo namba tatu. Kamati inapendekeza kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kwa kushirikiana na vyombo vya usalama itoe elimu na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kutunza na kulinda miundombinu ya mradi wa mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam.

Sasa baada ya maneno "Kamati inapendekezo kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kwa kushirikiana na…" kabla ya maneno "vyombo vya usalama" yaongezwe maneno "Manispaa za Jiji la Dar es Salaam" kwa sababu kumekuwa na tatizo hili la kutokuwa na ushirikishwaji wa karibu. Kama tunazungumza kuhusu elimu kwa wananchi na kadhalika, Manispaa ni muhimu zikahusishwa.

Mheshimiwa Spika, nina amini hili pendekezo litakubalika tu kwa sababu ni dogo lakini muhimu.

SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti mweyewe yuko wapi? Mheshimiwa Waziri ninadhani halina tatizo, kwani ninaona ameboresha hilo. Kwa hiyo tunaenda ukurasa wa pili, Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, jambo hilo hilo kwenye azimio namba nne. Kamati inapendekeza kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kwa kushirikiana na…, kabla ya maneno "Wizara husika za kisekta" yaongezwe maneno "Manispaa za Jiji la Dar es Salaam" kwa sababu ukiondoa mpango huu kuna mpango kabambe wa Jiji la

Dar es Salaam *master plan*. Kwa vyovyote vile mipango hii ni lazima ihuianishwe, kwa hiyo kushirikisha manispaa kama *planning authority* ni jambo la msingi. Ninaomba hili nalo liongezwe kwenye sehemu hiyo.

SPIKA: Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, hilo mimi sina matatizo nalo, isipokuwa nilitaka tu kuomba ufafanuzi kwa Mwenyekiti wa Kamati katika hilo pendekezo (a); Usafiri wa mabasi yaendayo juu ya maji. Kidogo kwa uelewa wangu na katika nchi nilizotembelea ni sehemu moja tu nimelikuta basi linaloweza kupita majini na linatumiwa na watalii.

Mheshimiwa Spika, labda angetuelewesha hayo mabasi, ili tuweke kitu ambacho kwa kweli kinaeleweka. Nilitaka tu atufafanulie kwani mabasi yanayokwenda juu ya maji tangu nimezaliwa nimewahi kuliona moja tu tena Dubai ambako wanatumia watalii. Labda kama alikuwa anamaanisha vivuko kama *ferry boats* zile, pantoni au sijui, kwa hiyo nilitaka tu ufafanuzi maana tusikubali kitu ambacho hatukiwezi.

SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui!

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, mabasi hayo sasa hivi yako mengi tu kule Ulaya. Yako pale Rotterdam na yanafanyakazi vizuri tu, tena yanachukua *passengers*. Kwa hiyo, tunaweza kutoa basi kama hilo kutoka Posta ya Zamani pale watu wanaingia tu kama vile wanavyoingia kwenye *Azam Marine,* halafu wanaweza kwenda mpaka Bagamoyo bila tatizo lolote.

Haya ni mabasi mazuri na yako *comfortable* na mimi nimeyapanda yale. Mheshimiwa Waziri asiwe na wasiwasi, teknolojia hii ipo vizuri na ni rafiki na iko salama, na gharama

zake sidhani kama ni kubwa sana. Basi hili linaenda kwenye maji tu, ni kama kununua boti tu, ni mabasi mazuri yale.

SPIKA: Waheshimiwa kila kitu ni wakati, hivi wakati ndiyo huu?

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, enhe, wakati ndiyo huu, naam! *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hapana, hili tuliache Kamati itaendelea kulifanyia kazi siku zijazo. Hili tuliondoe, mtaendelea kulifanyia kazi ninyi wenyewe kwa sababu bado mna kazi na Wizara hii.

Haya ukurasa wa pili ile alilosema Mnyika limeingia ukurasa wa tatu Mheshimiwa Silinde.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ukurasa wa tatu pendekezo namba 11. Pendekezo hili linasema Kamati inaishauri Serikali Kuu kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ihakikisha kuwa fedha za matumizi ya kawaida na fedha za miradi ya maendeleo zinawasilishwa kwa Serikali za Mitaa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sasa hoja yangu ambayo ninataka kurekebisha ni kwamba huu wakati ndiyo imekuwa ni tatizo unaweza kuambiwa wakati ikawa ni mwaka mpya wa Bajeti, sasa mimi nilichotaka kuongeza ni kwamba na zisipowasilishwa taarifa itolewe katika Halmashauri husika ili watu tujue. Kwa sababu siku zote TAMISEMI wameshindwa kuleta fedha na hawaleti sababu ni kwa nini wameshindwa kuleta fedha hizo.

SPIKA: Ninadhani ni *implied* liko ndani ya humu kama ukisema kwa wakati, wakati kama siyo wenyewe ni lazima taarifa itatolewa. Tunaendelea ukurasa wa nne, Mheshimiwa Wenje.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, katika pendekezo la namba 18 hapo ninapendekeza mwishoni hapo tuongeze maneno yafuatayo; kwamba na wakandarasi watakaofanya kazi chini ya kiwango wanyang'anywe leseni zao za kazi.

SPIKA: Mimi ninadhani halina ugomvi Mheshimiwa Waziri TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, mimi sidhani kama kuna matatizo kwa sababu kama katika Halmashauri Mkandarasi amefanya vile isivyotakiwa na kama Halmashauri inamlazimisha afanye na ana kaidi mara nyingi huwa wanashitaki Bodi ya Wakandarasi. Kwa hiyo, kwenye Bodi kule ndiko ambako wengine kwa kweli huwa wanawafutia. Kwa hiyo tuseme kuwa taarifa ipelekwe Bodi ya Wakandarasi.

SPIKA: Ulisemaje Wenje? Kusema kwamba taarifa ipelekwe katika Bodi ya Wakandarasi.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, ninasema sawa.

SPIKA: Tunaanza ukurasa wa tano Mheshimiwa Wenje.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa tano mimi nilileta mapendekezo ya kuongeza maneno hapo chini kwamba tuongeze namba 21 itakayosomeka kwamba ili kupata suluhisho la kudumu la kuondokana na rushwa na ubadhirifu wa mali za umma, Kamati inaishauri Serikali itekeleze ushauri wa ukaguzi maalumu uliofanywa na CAG na pia taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwenye Halmashauri ya Jiji la Mwanza ya kuwachukulia hatua za kinidhamu ikiwamo kuwafukuza kazi na kuwafungulia mashtaka watendaji wote wa Serikali waliosababisha hasara katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Spika, hili pendekezo nilileta kwa sababu ukisoma taarifa ya *CAG* kuna tatizo katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwenye ujenzi wa kliniki ya Halmashauri ambayo imejengwa chini ya kiwango na kuna matatizo mengi pia hapo. Lakini pia taarifa ya *LAAC* pia walisema na taarifa ya Kamati ya TAMISEMI yaani Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika ukurasa wao wa 28 pia wamezungumzia hili jambo kwa makini na kuna taarifa kuwa Mheshimiwa Waziri Hawa Ghasia kuna baadhi ya watendaji hawa ambao amekwisha wachukulia hatua lakini ninashangaa aliyekuwa Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza Bwana Wilson Kabwe aliyesababisha hasara hizi zote katika Jiji la Mwanza amehamishiwa katika Jiji la Dar es Salaam na hajachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, hata aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Manunuzi Bwana Tito bado amebaki palepale katika Jiji la Mwanza. Kwa hiyo, ninaleta mapendekezo haya ili kuitaka Serikali kupitia Wizara waweze kuchukua hatua kutokana na hizi taarifa za *CAG* zilizoletwa hapa pamoja na taarifa ya *LAAC,* pamoja na Taarifa ya Kamati hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili waweze kuchukua hatua dhidi ya huyu mtu anayeitwa Kabwe aliyesababishia Jiji la Mwanza hasara.

Mheshimiwa Spika, haya ni mapendekezo yangu.

SPIKA: Mapendekezo yako ninayakataa *right away* kwa sababu sisi hatuwezi kutumika hapa kufukuza watu au kufanya nini. Taarifa hii inaafikiwa?

(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kufikiwa)

(Hapa haikurekodiwa)

SPIKA: Usogee hapa na una dakika 15.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O – MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru wote waliochangia hoja ya Kamati

yetu. Kwa utafiti wa haraka haraka hoja ya Kamato yetu mwaka huu imepata wachangiaji wengi kuliko mwaka jana na hii ina maana kwamba tatizo tulilokuwa tunaliongelea ni kubwa na linagusa hisia za Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika hoja hii imepata wachangiaji tisa, wachangiaji wanne wamechangia kwa maandishi na wachangiaji watano wamechangia kwa kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya ufinyu wa muda kwanza ninaomba kuzungumzia hoja ambayo imechangiwa na wachangiaji wengi na hoja ya Mfuko wa UKIMWI kuwa na rasilimali endelevu. Hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Diana Chilolo ambaye ni Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Annastella Mallac…

SPIKA: Eleza tu habari ya kuchangia wanajua wenyewe walichangia na *Hansard* ipo.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O – MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI: Mheshimiwa Spika, sawa.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ni muhimu kwa sababu tunazungumzia mfuko endelevu. Nawaomba Wabunge wenzangu na Watanzania waelewe kwamba mtu yoyote anayetumia dawa za kupunguza makali ya virusi ya UKIMWI, atazitumia dawa hizi kwa maisha yake yote hata kama ataishi miaka 100 au miaka 60, 70, 80 na kila siku bila ya kupumzika.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo ni lazima nchi iwe na utaratibu wa kuwa na rasilimali za kuendeleza hapo ambapo wafadhili watakuwa hawapo ili kulinda maisha ya Watanzania, hiyo ndiyo hoja ambayo imezungumziwa kwa urefu kabisa na wachangiaji wengi kwamba tunahitaji kuwa mfuko endelevu, Mfuko wa UKIMWI na mimi ninaishukuru Serikali na kuipongeza kwamba imeleta hoja hii, Muswada tayari na ninaomba kuendelea kuwaomba Wabunge wenzangu utakapofika Muswada huu tuupitishe na kwa kweli

vitafutwe vyanzo vya mapato vya kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana.

Mheshimiwa Spika, tunapoongea sasa hivi siyo kwamba watu wote wanaohitaji dawa wako kwenye dawa ni kwa sababu wananchi wengi vijijini hawajafikiwa na hakuna vifaa tiba na wakati mwingine vi-*agency* havipatikani na hata vipimo inabidi waende mbali hospitali za Mikoa, Hospitali za Wilaya tunataka wapate vipimo pale pale katika maeneo yao kama ni kwenye kituo cha afya au zahanati au huduma za mkoba na huduma hizi zitawezekana tu kama tutakuwa na rasilimali za nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili suala ni muhimu na ninaomba kwa kweli litiliwe mkazo na umuhimu unaostahili na nitashangaa pale nitakapoona Serikali itakapokuja wakati tunaleta Muswada na kusema kuwa vyanzo vya mapato havipo, hapo Waheshimiwa Wabunge wenzangu tusikubali, tunaomba vyanzo vya mapato vya kupata fedha za mfuko huu ziweze kuainishwa mapema kabla ya Muswada huu haujafika hapa Bungeni.

Suala lingine lililozungumziwa kwa kina na wachangiaji ni suala zima la dawa za kulevya na kwa kweli wameipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ili tuweze kuwa na sheria yenye meno. Tatizo hili limekuwa sugu na tumeeleza kwenye maelezo ya Kamati kwamba kwa sababu ya udhaifu wa sheria tuliyokuwa nayo watu ambao siyo waaminifu na wafanyabiashara wa dawa za kulevya wameutumia mwanya huo, kwa hiyo, sheria itakayokuja tuna uhakika kwamba itakuwa na meno na itaweza kukidhi matakwa ambayo yamekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, tumeeleza katika taarifa yetu kwamba tayari Muswada umeshapita kwenye Kamati na tuna uhakika kwamba Waheshimiwa Wabunge kwa sababu mmelizungumza kwa uchungu mkubwa mtakuwa tayari kuunga mkono wa hoja hii itakapokuwa imeletwa na Serikali mbele yetu na kuweza kusaidia kupambana na tatizo hili

ambalo ni angamizo kubwa la vijana wetu ambao ndiyo nguvu kazi na tegemeo la Taifa hili.

Suala lingine lililozungumziwa ni bajeti finyu kwa ajili ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI, Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya lakini pia tumeona kuwa fedha hazijapelekwa kwenye Halmashauri. Hili limechangiwa na Wajumbe karibu wote na kwa kweli kama kweli tuna dhamira ya dhati na utashi wa kisiasa, iweje fedha zinazotengwa huko Wizara ya Fedha - Hazina wanapoona wana upungufu wa fedha wanachukua fedha za UKIMWI ndiyo wanapeleka sehemu nyingine na wanawaacha Watanzania wakiwa hawana fedha wakijua ni maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tuchezee maisha ya Watanzania kama kwweli tumedhamiria tujue kwamba tatizo la UKIMWI ni tatizo la uchumi, ni tatizo kubwa sana. Tunapoacha kuwahudumia hawa ina maana kwamba na uchumi wa nchi yetu unashuka. Mimi ninaomba kuanzia leo tudhamirie humu Bungeni na tuazimie kwamba hizi fedha ziwekwe zuio kama zinavyowekewa fedha za barabara, fedha za *REA* na fedha za maji ili kuhakikisha kwamba tunalinda kizazi kijacho na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanaoumia ni wanawake na watoto na wengi wao hawajapata huduma mpaka sasa hivi tunapozungumza wakiwemo wanawake na watoto wa Jimbo lako la Njombe Kusini. Tukiweza kuainisha haya ina maana kwamba fedha zinafika.

Mheshimiwa Spika, huu ni ugonjwa, kwa nini miezi sita fedha isipelekwe hata senti tano huku tukijua kwamba tunahudumia wagonjwa, hivi ugonjwa unasubiri?

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba wanatakiwa wapate huduma, elimu inatakiwa itolewe. Sasa hivi tumetoka katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa wamechaguliwa viongozi wapya kwenye vijiji, kwenye mitaa na vitongoji hawana elimu yoyote tunategemea hao watapata elimu kama fedha hazipelekwi?

Mheshimiwa Spika, tunategemea Tume ya Kudhibiti UKIMWI itafanya kazi, tunategemea Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya itafanya kazi wakati hata fedha walizopangiwa hawapati. Tutoe azimio kabisa kuwa iwe ni mwiko kabisa fedha za UKIMWI na fedha za Dawa za Kulevya kutopelekwa huko zinakostahili kwenda tutakuwa tumewatendea haki Watanzania.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililozungumzwa ni suala la lishe na limezungumzwa kwa kina kabisa kwamba tunakabiliwa na tatizo na inawezekana hatulioni. Hata sisi hapa tuna tatizo la lishe, tatizo la lishe siyo utapiamlo tu hata afya iliyozidi nayo ni utapiamlo. Tuna uzito uliozidi ambao nao ni tatizo la lishe, msifikiri tatizo la lishe ni tatizo tu la uzito pungufu au kuwa na udumavu, ni tatizo kubwa na kwa kweli Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma imetuelezea kabisa kuwa imefanya utafiti na watumishi wengi wamepima na wengi wameonekana kuwa wana tatizo la lishe iliyozidi ambayo ni uzito mkubwa, *pressure* na magonjwa ambayo hayaambukizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vijijini huko tatizo ni kubwa kwenye jamii kwa kuwa na udumavu na huu udumavu mtoto akidumaa katika siku 1,000 za maisha yake atadumaa milele na hata darasani hataweza kitu.

Mheshimiwa Spika, asilimia 42 ya watoto wote wa Tanzania wamedumaa, hivi tunafikiri kuwa na viongozi gani katika kizazi kijacho kama hatutalitilia mkazo suala la lishe na ninaomba kikundi cha lishe humu Bungeni siku ya Alhamisi kinazindua Ilani ya Masuala ya Lishe ambayo yataingizwa katika vyama vyote vya siasa wakati wa uchaguzi ili litiliwe umuhimu unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina uhakika kabisa kwa vile liko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Jenista, Waziri aliyeko sasa ni mwanachama mwanzilishi wa masuala ya lishe nina uhakika atasimama kidete kuhakikisha ya kwamba lishe inaimarishwa, lishe kwa wanawake, lishe kwa vijana na watoto wetu.

Suala lingine lililozungumzwa ni ukatili wa kijinsia. Mheshimiwa Saidi Mtanda amezungumza kwamba kuna uhusiano na huduma za maji ndiyo ukatili wa kijinsia pia una mahusiano na maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Akina mama wanaamka usiku na wasichana kwenda kuchota maji wanabakwa huko na wengine wanaambukizwa virusi vya UKIMWI, huo siyo ukatili?

Kwa hiyo, ukatili anaouzungumza ni kweli na ninakubaliana uko wa kupigwa, lakini pia upo ukatili ambao wanaambukizwa kwa sababu ya vitendo vinavyotokana na matatizo yaliyopo maji hayapo, wanafanya kazi zilizozidi lakini Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inapewa fedha kiduchu, haiwezi kufanya chochote na ndiyo ilitakiwa isimamie masuala yote ya wanawake na watoto, hili nalo ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, suala la mikopo tumezungumza katika Kamati yetu kwamba mikopo ya vijana na wanawake iongezwe kwenye Halmashauri, tutilie mkazo ile 10%, hatuelewi na ndiyo hilo nililolisema kwa sababu wanaona hilo siyo tatizo wanaweka fedha kwenye mambo mengine wanafikiri hili siyo la muhimu kumbe hili ndiyo muhimu kwa kizazi kijacho.

Mheshimiwa Spika, tunaongeza watu walioambukizwa virusi vya UKIMWI kwa sababu ya matatizo kama haya yanayojitokeza tumeona pia hata fedha tulizopanga kwenye Benki ya Wanawake zilizotengwa kwenye bajeti hazijaenda zote, labda zingeenda zingeweza pia kusaidai kuondokana na matatizo haya ya ukatili wa kijinsia saa nyingine ni kwasababu za kiuchumi wanawake na wasichana wanapata manyanyaso.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililozungumzwa limezungumzwa ni la mila potofu na hizo mila potofu zimeelezwa kwamba na zenyewe zinachangia kwa kiasi kikubwa kwa maambukizi ya virusi vya UKIMWI na zote hizi ni kweli kabisa kuwa zipo mila ambazo zimepitwa na wakati kwa baadhi ya makabila, na ninakubaliana kabisa na mtoa

hoja kwamba kama hatutazizungumza itakuwa pia ni tatizo na yote haya ikiwemo mila potofu yamezungumzwa na Mheshimiwa AnnaStella Mallac yatazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, mila hizi zinatofautiana makabila kwa makabila, hebu tufanye utafiti na tuone kila kabila lina mila gani potofu ambazo zimepitwa a wakati zinaongeza maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi ni sala la elimu kwa vijana. Hili limezungumzwa na Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Sarah Msafiri na Mheshimiwa Jitu Soni ya kwamba kama hatutatoa elimu kwa vijana kizazi kijacho kitaangamia na Kamati imeliona na imeliandika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililozungumzwa limezungumzwa na Mheshimiwa Ritta Kabati kuhusu Mkoa wa Iringa ambao tumeutaja kwamba ni kati ya Mikoa yenye maambukizi makubwa lakini pia ni Mkoa ambao umekosa rasilimali. Ninaungana na ninamshukuru Mheshimiwa Ritta kwa kuungana na Kamati kwamba kwa kweli Mikoa hii ikiwamo Njombe na Mbeya inatakiwa kupata rasilimali.

Lakini Kamati imeandika kwamba imekubaliana na maoni ya wadau wa maendeleo na wameshauri kwamba fedha nyingi zimpelekwa mahala ambapo kuna tatizo kubwa na kwenye tatizo kubwa siyo kwa Mkoa mzima katika Mkoa wataangalia ni Wilaya gani yenye matatizo makubwa na kwenye Wilaya pia wataangalia ni kijiji gani au ni kata gani. Tukipunguza maambukizi katika Mikoa hii au katika vijiji vinavyohusika, au Kata zinazohusika tutakuwa tumeshusha maambukizi ya virusi kwa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana kabisa na kupongeza wadau na kwenye taarifa yetu tumesema kwamba Kamati pia iliweza kukutana na Ujumbe wa Benki ya Dunia, Mfuko wa Dunia wa UKIMWI na Kifua Kikuu na pia Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID) na walizungumzia suala hili la kuweza kuangalia uchangiaji wa rasilimali, lakini

Kamati imekubali kuwa *Global Fund* imefanya kazi kubwa kuweza kutoa fedha.

Kwa hiyo, tunakubaliana kuwa fedha kweli zipo, lakini ni za kununua dawa na tunapongeza njia ambayo inatumika ya kununua dawa moja kwa moja imeiwezesha Serikali kuweza kununua dawa nyingi kupitia *Global Fund,* lakini hoja tunayoizungumza Kamati ni kwamba tunataka Mfuko Endelevu utachangiwa na watu wengi na siyo utakaotegemea fedha za Serikali peke yake, utakaowezesha kupatikana kwa huduma kama tutakuwa na Mfuko huo hatutapigizana kelele hapa kwa Bajeti ndogo ya Serikali, tutakuwa na mfuko wa ziada ninaendelea kukazia kwa ajili ya huu mfuko. Kwa hiyo hata fedha za *Global Fund* zikichelewa tutajua kuwa tuna fedha zetu.

Mheshimiwa Spika, *system* ya namna hii tulielezwa kuwa imetumika Zimbabwe ninarudia kwa sababu ya suala hili imetumika Zimbawe wameweza kuhakikisha kuwa wana fedha za kutosha, wameweza kununua vifaa tiba vinavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, kuwa na mfuko huu pia itanunua vifaa tiba ambavyo vitatibu magonjwa ambata ambayo wagonjwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI wanayapata, hizi ni dawa za magonjwa ya kawaida tu. Kwa hiyo, ina maana mfuko huu utasadia pia kutoa huduma za afya kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wenzangu wamezungumzia pia masuala ya mafunzo kwa watumishi hasa watumishi wa Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya kwamba wajengewe uwezo na mimi nakubaliana kabisa kwamba ipo haja ya kujengewa uwezo. Lakini pia kama tulivyosema, wamezungumzia suala la kuweza kuongeza rasilimali.

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Kengele ya pili hiyo.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O – MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI: Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba sasa Bunge lako lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015 iliyopitishwa na Bunge)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Twende *page* kwa *page*. Ukurasa wa kwanza, ukurasa wa pili Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Kwenye pendekezo namba mbili, Mwenyekiti wa Kamati amezungumza kwa uchungu sana juu ya kutokutolewa kwa fedha zilizotengwa na Serikali kwa ajili ya UKIMWI ambapo fedha za wahisani kati ya bilioni 137 mpaka Januari zilikuwa zimetolewa bilioni mbili tu na fedha za ndani kati ya bilioni kumi, mpaka sasa hazijatoka hata shilingi moja.

Sasa mwisho wa pendekezo hili Kamati inaliomba Bunge hili lipate maelezo kutoka Serikalini sababu ya kutokupeleka fedha hizi zilizotengwa hata kwenye Mikoa yenye maambukizi makubwa kama Njombe, Iringa, Mbeya na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, naamini pendekezo hili la Kamati lilikuwa muafaka wakati Kamati inasoma taarifa yake ili Serikali itoe maelezo. Katika hatua ya sasa ambapo Serikali imekwishatoa maelezo na bado Mwenyekiti katika

kuhitimisha ameonyesha ipo haja ya fedha kupelekwa. Napendekeza kwamba sehemu hii ya pendekezo ibadilike, badala ya maneno hayo niliyoyasema isomeke; "Kamati inapendekeza fedha zipelekwe kwa wakati hasa katika Mikoa yenye maambuzi makubwa kama Njombe, Iringa, Mbeya na Dar es Salaam ama maneno mengine yoyote ambayo bado yataweka pendekezo lenye kuhitaji bado Serikali ipeleke fedha badala ya pendekezo lililopo sasa la Serikali kutoa maelezo ambalo limekwishapitwa na wakati.

SPIKA: Mheshimiwa Mnyika hizi Kamati ndiyo maana tumasema mapendekezo bado wenyewe wanaweza kutaka Serikali ieleze, kwa nini haifanyi hivyo kwa sababu si lazima, inawezekana ku-*fit* hata hii, bado kwamba Serikali itoe maelezo. Sasa hivyo ndivyo inavyosema.

Ukurasa wa tatu, ukurasa wa nne kuna mtu? Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, ukurasa wa nne.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, naomba nianze tena kwa kuishukuru na kuipongeza Kamati, kwa jinsi kwa kweli inavyojali na kuzingatia masuala haya ya UKIMWI nchini.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la tisa linasema Kamati inatambua mchango mkubwa wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwani amefanya mambo mengi mazuri ya kuigwa katika suala hili la kupambana na UKIMWI ikiwa ni pamoja na kuwaongoza Watanzania kupima ili kujua afya zao.

Mheshimiwa Spika, lakini pale imeendelea kujitokeza kwa Mheshimiwa Rais kupima kulichangia na kuhamasisha wananchi wengi kupima na kuondoa unyanyapaa miongoni mwa jamii. Kutokana na hilo Kamati inapendekeza kwamba, ile siku aliyopima Mheshimiwa Rais, iwe ni siku ya upimaji wa UKIMWI nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali tunaishukuru sana Kamati kwa kuipa hadhi siku hiyo, na tunaiunga mkono sana Kamati. Lakini sentensi ile inaishia na kwamba lakini pia iwe ni kumbukumbu ya kuhamasisha Watanzania wajue afya zao, haina neno.

Mheshimiwa Spika, lakini kuifanya siku hiyo iwe ni siku ya uzinduzi na muendelezo wa siku ya UKIMWI duniani ambayo kilele chake kuwa tarehe 1 ya mwezi wa kumi na mbili kila mwaka, sisi kama Serikali tulikuwa tunafikiri kwamba kipengele hiko kiachwe kwa sababu, kuingiza tena maadhimisho ya shughuli ambayo yatakuja tena kuadhimishwa kitaifa tarehe moja mwezi wa kumi na mbili, inaweza ikawa ni gharama zaidi kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI, ni bora kuishia pale kwa kuthamini siku hiyo, kufanya ndiyo siku ya kupima na mambo hayo yote itakuwa ni kawaida na wananchi watahamasishwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuiweka kama ndiyo siku ya uzinduzi wa maadhimisho ya siku ya UKIMWI ambayo yatakuja tena kufanyika tarehe moja, Desemba, nadhani inaweza ikawa ni mzigo mkubwa sana kwa Tume yetu na kwa Serikali kwa ujumla wake.

SPIKA: Mwenyekiti wa Kamati!

MHE. LEDIANA M. MANG'ONG'O- MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa aliyokubali ya Kamati, lakini nafikiri aidha ni Kiswahili ndiyo hakieleweki. Lengo la Kamati tunasema hivi, hiyo siku sio siku ambayo itakusanya watu, naanzia hiyo tarehe 14 sio siku ya kukusanya watu, ni siku ambayo watu wote wanakwenda kupima kwenye sehemu zao kokote walipo. Halafu itakuwa ni muendelezo na taarifa kamili ya shughuli za upimaji, watu waliojua afya zao na nini itakwenda kuelezwa siku ya UKIMWI Duniani.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Rwanda inaadhimisha maadhimisho kuanzia mwezi wa sita, inakwenda kujumuisha

mwezi wa kumi na mbili. Kwa hiyo, muda wote huu, unakuwa ni shughuli mbalimbali zinafanyika, zinafikia watu wengi.

Mheshimiwa Spika, kwanza sikubaliani kama Kamati kuhusiana na siku ya UKIMWI Duniani inavyoendeshwa, kwa sababu ikiendeshwa inakusanya watu wachache tu pale, watu wa vijijni huko ndani hawafikiwi na ndiyo maana Kamati tukaona kwamba iende hivyo, ikifika Desemba ndiyo kinakuwa kilele maadhimisho yanaendelea vilevile. Kama *de-agencies* zitakuwepo, wananchi wanaendelea kupima kama kawaida, hilo ndiyo lilikuwa lengo la Kamati. Halina maana kwamba tarehe 17 ile ifanyike halafu iwe ni kubwa kama ile.

Mheshimiwa Spika, hizi siku zipo hata kwenye nchi nyingine. Nchi kama ya Marekani ina siku ya kutoa elimu kwa wanawake, kuna siku iliyotengwa ya kutoa elimu kitaifa kwa vijana, ina siku iliyotengwa kitaifa kwa watu kujua afya zao na mwisho inakuwepo siku ya UKIMWI Duniani. Sasa sisi wenye maambukizi makubwa kama hatufanyi hivyo tutakuja kusahau, watakuja viongozi wengine UKIMWI sio kipaumbele, tutasahaulika na hatujui dunia hii yatazuka mambo gani mengine.

SPIKA: Naona mnasema kitu sawasawa, ile sikukuu ya duniani inajulikana. Nadhani kubwa ambayo ilikuwa haina kazi ni ile ya tarehe 14. Mimi nadhani ukiondoa ile ya duniani kutakuwa hakuna tatizo, yatakuwa mambo hayo hayo, kwa sababu haya mambo ni ya kuyafanyia kazi.

MHE. LEDIANA M. MANG'ONG'O- MWENYEKITI WA KAMATI YA UKIMWI: Mheshimiwa Spika, nakubali tuiondoe.

SPIKA: Tunaondoa ile sikukuu ya duniani ni *obvious.* Sasa hii ambayo haikuwa *obvious* ilikuwa ni ile ya tarehe 14. Siku ya kupima na maandalizi mengine ya utendaji yataendelea.

Ukurasa wa tano.....aah, Mheshimiwa Sabreena sikukuona, ukurasa wa nne!

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nilikuwa bado kwenye ukurasa wa nne kwenye pendekezo namba kumi. Linasema "kwa baadhi ya maeneo ambayo Kamati imetembelea, kumekuwa kuna malalamiko kwamba kuna watu wanaambukiza UKIMWI wenzao kwa makusudi. Kamati inashauri kuwa ibuniwe mbinu nzuri ya kuelimisha watu ambao wameathirika ili wasiendelee kuwaambukiza wenzao kwa mkusudi, bali wawe na mioyo ya imani, upendo na huruma kwa kutokufanya tendo la ngono bila kinga, akijua kufanya hivyo kutamuathiri mwingine."

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu nilikuwa nashauri watu wanaofanya hivyo kwa makusudi, hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa, kwa sababu kumuambukiza mtu UKIMWI kwa makusudi ni kosa kisheria.

SPIKA: Ipo sheria inayosema unavyosema.

Haya tunaenda ukurasa wa 5, 6, 7, 8, 9 na wa 10. Mheshimiwa Mnyika kwanza.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 10, juu ya pendekezo namba 23, kwamba hakuna Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI na kwamba kamati itataarifiwa sera hiyo tayari imeshawasilishwa, imeshapitiwa na Sekretariati ya Baraza la Mawaziri, inasubiri tu kupitishwa na kikao cha pamoja baina ya Makatibu Wakuu wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, sasa mwishoni, hata hivyo, Kamati inashauri kwamba Serikali iharakishe mchakato wa uundaji wa Sera hiyo ya Taifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya, hasa ikizingatiwa sera ndiyo huitangulia kuweka misingi ya uundaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwenye pendekezo namba 22 ambalo limekwishapitishwa tayari, inaonekana kama Muswada umeshawasilishwa, Kamati imemaliza kazi yake na inatarajia mkutano ujao wa Bunge Muswada huo utaletwa Bungeni.

Sasa ili kuhakikisha kwamba Muswada utaletwa vilevile sera ikiwa tayari, napendekeza kwamba sehemu hiyo ya mwisho isomeke; "hivyo Kamati inashauri kwamba Serikali iharakishe mchakato wa uundaji wa sera hiyo ya Taifa ya kupambana na dawa za kulevya kabla ya kupitishwa kwa Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya, kwa sababu ilivyo hivi sasa imetoa *option,* Muswada unaweza kuendelea bila sera na Muswada upo kwenye hatua ya mbele. Kwa kuwa sera tayari rasimu ipo na ipo katika hatua za mwisho, basi iwekwe hiyo *condition*, isaidie kuharakisha hiyo sera kukamilika ili tukiletewa sheria tuwe tumeshafikiri kuhusu sera vilevile ili iongoze utungaji wa sheria. Nashukuru.

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa hiyo namba 23, lakini ilikuwa ni marekebisho tu machache kwamba inasema hiyo Rasimu ya Sera ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya imeshapitishwa na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, inasubiri kupitishwa kikao cha pamoja baina ya Makatibu Wakuu na Baraza la Mawaziri. Nadhani hatuna kikao cha namna hii, labda inasubiri kupita katika kikao cha Makatibu Wakuu ili iende katika Baraza la Mawaziri, yaani *NTC* halafu iende kwenye Baraza la Mawaziri.

Nadhani labda inasubiri kupitishwa katika kikao cha Makatibu Wakuu na baadaye iende Baraza la Mawaziri. Hakuna kikao cha pamoja cha Makatibu Wakuu na Mawaziri kwa maana ya kutunga sera.

SPIKA: Mapendekezo yote mawili mimi siyaoni kama kuna tatizo. Kwa hiyo, taarifa hii inaafikiwa.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

SPIKA: Kwa hiyo, taarifa hii pia imepita. Kwa hiyo, niwashukuru Wenyeviti kwa kazi mliyofanya. Lakini kwa muda ujao mapendekezo yenu yawe *specific,* yamekuwa tu

yamejaa maneno mengi, halafu huoni mapendekezo yako wapi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naona mmepata *order paper* hii *(supplementary order paper)* ambayo inahusu Mkutano wa 18, Kikao cha Saba, tarehe tatu, Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa muda mrefu shughuli za Bunge zimekuwa zikifanywa Spika na Naibu Spika na Mwenyekiti Mheshimiwa Zungu. Hali hiyo imewafanya viongozi hawa kufanya kazi kwa muda mrefu bila kupata muda wa kupumzika na kutokana na uchache wao ikizingatiwa kuwa nafasi mbili zilikuwa wazi kufuatia Mheshimiwa Jenista Mhagama kuteuliwa kuna Naibu Waziri na pia Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib kutoweza kufanya kazi ya Wenyekiti kwa sababu maalum.

Waheshimiwa Wabunge, ni kwa sababu hiyo na kwa mujibu wa Kanuni ya 7(2) ya Kanuni zetu, Kamati ya Uongozi pamoja na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu leo imefanya kikao ili kupendekeza majina ya Wabunge yatakayowasilishwa Bungeni ili yathibitishwe kuwa Wenyeviti wa Bunge.

Kutokana na utamuduni wetu wa siku za nyuma, katika kikao hicho Kamati ya Uongozi imependekeza majina mawili kujaza nafasi za nasibu mbili zilizo wazi ili Bunge liweze kuyathibitisha.

Waheshimiwa Wabunge, waliopendekezwa ni kama ifuatavyo; Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge amependekezwa, hili linazingatia kuwa na Mwenyekiti aliyetoka upande wa Zanzibar, hususan kutokana na nafasi iliyokuwa ya Mheshimiwa Dkt. Muhammed Seif Khatib. *(Makofi)*

Halafu Mheshimiwa Lediana Mang'ong'o, Mbunge amependekezwa kuzingatia kuziba nafasi aliyoiacha Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama. *(Makofi)*

Hivyo basi nawasilisha majina hayo kwenu ili kwa kufuata utaratibu wetu pale inapotokea majina yanayopendekezwa, ni sawa na nafasi zilizopo huwa tunathibitisha na kuwachagua kwa kupita bila kupingwa.

Sasa nitawahoji ili mthibitishe mapendekezo ya Kamati ya Uongozi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kidawa hatukujui simama huko ulipo na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o simama ulipo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, haya ndiyo majina ambayo Kamati ya Uongozi iliyapitia na kutoa mapendekezo kwenu, sasa nawahoji.

(Majina ya Wenyeviti wa Bunge kuthibitishwa na Bunge)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo Wenyeviti wetu wapya ni Mheshimiwa Kidawa na Mheshimiwa Mng'ong'o. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Baada ya kusema hivyo, kesho ni siku ya sheria ambayo huadhimishwa kila mwaka, kwa hiyo, kutokana na mihimili yote mitatu tunashiriki.

Kwa hiyo, mimi kesho asubuhi nitakwenda, Mwenyekiti ataendelea na shughuli za kesho. Kwa hiyo, nawatakieni jioni njema, ahsante kwa kazi kubwa mliyoifanya.

(Saa 2.15 Usiku Bunge lilihairishwa hadi siku ya Jumatano, Tarehe 4 Februari, 2015 saa Tatu Asubuhi)